

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Thelathini na Sita – Tarehe 24 Mei, 2018

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

NDG. ATHUMAN HUSSEIN - KATIBU MEZANI:

HATI ZA KWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA NISHATI:-

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

MHE. HAMIDA M. ABDALLAH (K.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA NISHATI NA MADINI):-

Taarifa ya Kamati ya Nishati na Madini kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Hamida. Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani sioni. Tunawashukuru kwa kutapatia nusu saa ya bure, Katibu.

NDG. ATUMAN HUSSEIN - KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Tunaanza na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Omari Abdallah Kigoda, Mbunge wa Handeni, uliza swali lako tafadhalii.

Na. 307

**Asilimia Tano ya Mapato ya Halmashauri kwa ajili ya
Vijana na akina Mama**

MHE. OMARI A. KIGODA aliuliza:-

Je, ni kwa kiasi gani Serikali inasimamia suala la asilimia 10 ya mapato ya Halmashauri kwa ajili ya vijana na akina mama?

SPIKA: Jamani hili swali Waheshimiwa Mawaziri wamejibu sana, basi tuendelee kulijibu. Naomba Waheshimiwa Wabunge wote sasa mlsikilize tusilione tena swali hili la asilimia 10.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA
SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Omari Abdallah Kigoda, Mbunge wa Handeni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuhakikisha halmashauri zote nchini zinatenga asilimia 10 ya mapato yake kwa ajili ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Katika Mwaka wa Fedha 2016/2017, jumla ya shilingi bilioni 56.8 zilitengwa na halmashauri zote nchini na jumla ya shilingi

bilioni 17.5 sawa na asilimia 31 zilitolewa kwa vikundi nya wanawake na vijana. Katika mwaka wa fedha 2017/2018 jumla ya shilingi bilioni 61.6 zilitengwa na hadi kufikia Februari, 2018 jumla ya shilingi bilioni 15.6 sawa na asilimia 27 zilikuwa zimetolewa, ambapo jumla ya vikundi 8,672 nya wanawake na vijana vilipatiwa mikopo. Katika mwaka wa fedha 2018/2019, shilingi bilioni 53.8 zimetengwa kwa ajili ya Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu wenyewe Ulemavu katika halmashauri zote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuongeza uwajibikaji katika kutenga na kupeleka fedha za Mfuko wa Wanawake na Vijana kwa vikundi husika, Serikali itaweka utaratibu katika Sheria ya Fedha (*Finance Bill*) ya mwaka 2018/2019 utakaohakikisha kwamba halmashauri zote zinatekeleza kikamilifu agizo hilo. (*Makofu*)

SPIKA: Mheshimiwa muuliza swali, Mheshimiwa Omari.

MHE. OMARI A. KIGODA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya halmashauri bado zinalalamikiwa kwamba utekelezaji huu ni mdogo au wakati mwingine haufanyiki kabisa. Je, malalamiko haya yanapotokea katika baadhi ya halmashauri, hawa vijana, walemvu na akina mama, ni wapi wanapaswa waende kulalamika ili kuhakikisha utaratibu huu unafanyika? Ahsante sana.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, sisi ndiyo Madiwani, sasa tukintaka Waziri asimamie jambo letu wenye, Mheshimiwa Waziri, majibu tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Omari Abdallah Kigoda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema hapo awali, ni kweli kwamba hatua ya kwanza kabisa ya kusemewa ni kwa Mheshimiwa Diwani, lakini vilevile kuititia Baraza la Madiwani ambazo ndicho kikao cha kwanza kabisa kuhoji kuhusu mgawanyo wa fedha ambazo zimetengwa kwa ajili ya mikopo ya vijana na wanawake.

Mheshimiwa Spika, lakini katika ukaguzi ambao wamekuwa wakiufanya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali amekuwa akionesha kwamba halmashauri ambazo hazitengi fedha kikamilifu kama ambavyo mapato ya ndani yanaonesha zimekuwa zinaandikiwa madeni. Kwa hiyo, uwajibikaji unaanzia hapo na hatua hizi tutaendelea kuzifuatilia. Kama nilivyosema katika jibu la msingi kwamba tunatarajia kuweka kipengele kwenye sheria ambacho kitalazimisha sasa kila halmashauri itengete asilimia 10 ya mapato yake ya ndani na itoe fedha hizo kwa ajili ya vikundi vya vijana na wanawake. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Sannda nilikuona na Mheshimiwa Mchungaji Msigwa.

MHE. EDWIN M. SANNDA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati huu ni llani yetu ya Chama cha Mapinduzi, ni sera, sheria na kule kwenye halmashauri zetu lisipotekelezwa ni hoja ya ukaguzi lakini bado kuna changamoto za utekelezaji. Je, ni lini sasa Serikali itatoa waraka mkali kabisa ambao utaelekeza halmashauri zote zitekeleze na zisipotekeleza ziweze kuwjibishwa?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Jafo majibu tafadhali.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la rafiki yangu Mbunge wa Kondoa Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, jambo hili tumelitolea maelezo hapa mara kadhaa na hata tukifanya rejea wakati nawasilisha bajeti yetu ya mwaka wa fedha 2018/2019 tulisema wazi kwamba katika ajenda hii ya mikopo ya akina mama na vijana sasa suala hili linakuwa si la hiari tena. Nimesema wazi mara kadhaa kwamba jamani fedha hizi hazifiki Hazina zinaishia katika halmashauri zetu. Jukumu letu kubwa sisi kuhakikisha tunasimamia katika Kamati za Fedha ili fedha hizi ziweze kufika kwa vijana na akina mama, hilo ndilo jambo la msingi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ndio maana katika *Finance Bill* ya mwaka huu tumeleta kifungu maalum kwa ajili ya *enforcement* ya jambo hilo. Ni imani yangu kwamba baada ya Sheria hiyo ya Fedha kufika hapa, Wakurugenzi wote, lakini niwatake Madiwani wote na Wabunge wote katika halmashauri zetu tuweze kuwa imara kuhakikisha utaratibu wa fedha hizi ambazo zinatengwa na katika bajeti ni lazima zitengwe, ziweze kuwafikia vijana na akina mama wetu. Kwa hiyo, hili ni jambo letu sisi sote na si jambo la mtu mmoja na kwa vile sheria inakuja nadhani hapa itakuwa hakuna suala la *negotiation*, tutakwenda kwa mujibu wa sheria itakavyotuongoza. (*Makof*)

SPIKA: Mchungaji nimeshakutaja. Uliza swali lako tafadhali.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Manispaa ya Iringa ni moja ya Manispaa ambazo zinatekeleza kwa ukamilifu na kwa uaminifu suala hili la asilimia 10 kwa vijana na akina mama. Na kwa kuwa Serikali imekuwa ikichelewa wakati fulani kuleta pesa zinazotoka Serikali Kuu kwa ajili ya maendeleo, Wizara haioni ni muhimu sasa kuziona halmashauri kama Manispaa ya Iringa ambazo zinafanya vizuri ili ziwape kipaumbele kupeleka hela za kimaendeleo kwa sababu zinatekeleza wajibu wake?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, majibu tafadhali.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la rafiki yangu, Mheshimiwa Mchungaji Msigwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba nikiri wazi kuna manispaa nydingi sana zafanya vizuri hapa nchini kwetu katika miradi mbalimbali ya maendeleo. Miongoni mwa manispaa inayofanya vizuri vilevile ni Manispaa ya Kinondoni ukiachana na Iringa na juzi juzi waliweza kutoa fedha zaidi ya shilingi bilioni 2 kwa ajili ya mikopo ya akina mama na vijana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini katika suala zima la upelekaji wa fedha za maendeleo tumejipanga na ndiyo maana hapa katikati unaona jinsi tunavyojitahidi kwa kadri iwezekanavyo na tuna matarajio kwamba kabla mwaka huu wa fedha haujafika, si Halmashauri ya Iringa peke yake isipokuwa manispaa zote na halmashauri zote kuhakikisha zinapata fedha na *especially*kwa ajili ya kwenda kukamilisha yale majengo yetu ya hospitali na madarasa. Tunawasiliana na wenzetu wa Hazina ikibidi tutatumia *force account* kuhakikisha kiwango kikubwa cha fedha kinapatikana katika halmashauri zetu ili miradi hii ya maendeleo iweze kutekelezeka katika eneo yetu.

SPIKA: Mbunge mzoefu, Mheshimiwa Lubeleje na Mheshimiwa Cecilia Paresso.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hii asilimia 10 ya vijana na akina mama hii ni *revolving fund*, mtu anakopa, anarejesha. Nataka kumuuliza Mheshimiwa Waziri, hawa

tunaowakopesha, je, wanarejesha na kama hawarejeshi, wanachukuliwa hatua gani? (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo la Senator Lubeleje.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Lubeleje, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba fedha hizi wanapokopeshwa vikundi vya vijana na wanawake wanatakiwa kurejesha na mratibu mkuu wa marejesho ni Afisa Maendeleo ya Jamii katika halmashauri husika. Kwa hiyo, kama kuna sehemu hawarejeshi kabisa, huo utakuwa ni udhaifu mkubwa sana wa kikazi wa huyo Afisa Maendeleo ya Jamii pamoja na Kamati yake ya Mikopo ya Halmashauri. Wito ambao tunautoa ni kwamba ni lazima wanaokopeshwa warejeshe, vinginevyo hatua zitachukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo zuri kabisa ambalo amelifanya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI wakati anawasilisha hotuba ya bajeti ni kutoa tangazo kwamba kuanzia mwakani atafuta au amefuta riba kwenye mikopo ya wanawake na vijana. Kwa hiyo, hiyo iwe kichocheo cha mwananchi ye yeyote atakayekopeshwa mikopo hiyo arudishe fedha kama alizokopa bila riba. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Cecilia Paresto, swali la mwisho hapo.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kumekuwa na Mifuko mingi ya Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi, mingine iko Ofisi ya Waziri Mkuu na mingine iko TAMISEMI; na kwa kuwa sheria/takwa hili la kutaka kutengwe asilimia 10 kwenye Serikali za Mitaa, muda mwingi katika ripoti za CAGimeonekana ufanisi ni hafifu, kama kweli mna lengo la kuwawezesha wananchi

kiuchumi, kwa nini msifikirie kuunganisha mifuko hii uwe mfuko mmoja ili kuwepo na ufanisi?

SPIKA: Ushauri huo, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, majibu tafadhali.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Spika, naomba nitoe majibu ya nyongeza kwenye swali la msingi sana aliloliuliza Mheshimiwa Parezzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa ndani ya Serikali tumeanza kutafakari na kuona ni kwa kiasi gani tunaweza kuitazama kwa kina mifuko hii yote takriban kama 16 ama 19 hivi tuliyonayo, tukaiunganisha na kuipunguza ikajenga nguvu kubwa zaidi na ikawa na *impact* kubwa zaidi kwa Watanzania wengi na hasa wale ambao wako vijiji. Kwa hiyo, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba kazi hii imeshaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu inaishughulikia vizuri na baada ya muda mfupi nadhani tunaweza tukaja na sheria ya kuunganisha baadhi ya mifuko na kuibakiza michache ambayo itakuwa na *impact* kubwa kwa maendeleo ya Watanzania. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana kwa kuchukua ushauri huo. Tunaendelea na Wizara ya Mifugo, swali litaulizwa na Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma.

Na. 308

Tatizo la Uvuvi Haramu

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA aliuliza:-

Tatizo la uvuvi haramu bado linaendelea licha ya jitihada za Serikali kuchoma nyavu za uvuvi zisizopendekezwa:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kukomesha uvuvi haramu zaidi ya kuchukua hatua hiyo ya kuchoma nyavu?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara imepewaa jukumu la kulinda, kusimamia, kuhifadhi na kuendeleza rasilimali za uvuvi nchini kwa mujibu wa Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya Mwaka 2003 na Kanuni za Uvuvi za Mwaka 2009. Katika kutekeleza jukumu hili, Serikali imekuwa ikifanya jitihada kudhibiti vitendo vya uvuvi haramu kwa kufanya doria za mara kwa mara pamoja na kufanya operesheni mbalimbali ikiwemo Operesheni Sangara ya mwaka huu wa 2018, Operesheni Jodari na za Kikosi Kazi cha Kitaifa, kwa maana ya *Mult (Multi-Agency Task Team - MATT)* cha kuzuia uharibifu wa mazingira ili kulinda rasilimali za uvuvi kwa manufaa ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inayo mikakati mbalimbali ya kupambana na uvuvi haramu. Mikakati hiyo ni pamoja na: Kuimarisha ushirikishwaji wa jamii katika kusimamia na kulinda rasilimali za uvuvi kupitia halmashauri, Serikali za Vijiji na Vikundi vya Usimamizi Shirikishi (*BMU's*); kuendelea kutoa elimu kuhusu athari za uvuvi haramu kwa mazingira, jamii na kiuchumi; kufanya maboresho ya sheria ili kuwa na sheria kali dhidi ya uvuvi haramu hasa uvuvi wa kutumia mabomu/ milipuko, ikiwa ni pamoja na kuweka kipengele cha kuonesha uvuvi haramu ni sawa na uhujumu uchumi; na kuimarisha Mashirikiano ya Kikanda na Kimataifa kwa kushirikiana na nchi mbalimbali zikiwemo nchi za *SADC* katika kuzuia uvuvi uisoratibowiwa na usioripotiwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara inahamasisha ufugaji wa samaki ili kupunguza nguvu ya uvuvi kwenye maji ya asili.

Aidha, naomba Waheshimiwa Wabunge wote watusaidie katika kuwaelimisha wananchi kuachana na vitendo vya uvuvi haramu na kushiriki katika kulinda rasilimali za nchi yetu. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, swalii nyongeza.

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri lakini nina maswali mawili mafupi.

Mheshimiwa Spika, swalii la kwanza, kwa kuwa wavuvi wana-*complain* kuwa hawapati elimu ya uvuvi ambao unatakiwa na wanaopaswa kusimamia ni Afisa Ugani lakini mara kwa mara hawafanyi hivyo. Je, Serikali Inafanyakaje kusudi kuwapatia elimu ili hawa wavuvi waweze kuelewa ni nyavu zippi zinazotakiwa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, kwa kuwa ufungaji wa samaki kwa kutumia mabwawa au *fish ponds* wananchi wameitikia kwa nguvu lakini bado hawajapatiwa elimu sawasawa. Je, Serikali ina mkakati gani wa kutoa elimu hii ya ufungaji wa samaki wa mabwawa ili kupunguza utapiamlo pamoja na kuinua kipato na kuhamasisha wananchi wa mikoa yote waweze kufuga ukiwepo na Mkoa wangu wa Morogoro maana hata wanawake wanaweza wakafuga kwa mabwawa? Ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa. Majibu ya swalii hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Abdallah Ulega.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ya kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma na nichukue fursa hii kumpongeza sana kwa ufulilaji na umakini wake katika kuona sekta hii ya uvuvi na kilimo zinasonga mbele.

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza anataka kujua namna ambavyo sisi Serikali tumejipanga katika kuwasaidia wananchi wetu katika kupata elimu ya kujua ipi ni nyavu halali na ipi isiyokuwa nyavu halali, hasa ikizingatiwa kwamba Maafisa Ugani wetu hawafanyi kazi yao ipasavyo. Nataka nimhakikishe tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imejipanga vyema na ndiyo maana katika mabadiliko na maboresho ya sheria ambayo tunakwenda nayo katika mwaka huu, katika jambo moja kubwa tutakalolifanya ni pamoja na kuhakikisha tunaziboresha *BMUs* zetu, kwa sababu *BMUs* ni mali ya wananchi wenyewe na zinachaguliwa na wananchi wenyewe. Tuna hakika kwamba kwa kufanya hivyo tutakuwa tumewafikia wananchi, wapeane elimu waweze kujua.

Mheshimiwa Spika, lazima niseme ukweli kwamba bahati nzuri nyavu zinazotumika ni chache. Kwa mfano, nyavu ya dagaa kwa upande wa ziwani inafahamika wazi kwamba ni nyavu inayotakiwa kuwa na jicho lisilozidi au lisilopungua milimita nane. Kwa hivyo, mtu anapokwenda akanunua nyavu inayoshuka chini ya ukubwa wa milimita nane hilo jambo tayari amevunja sheria. Kwa upande wa bahrini, inafahamika wazi kwamba ni nyavu isiyopungua ukubwa wa milimita 10. Kwa hivyo, kwa wavuvi ambao hiyo ndiyo shughuli mara nyangi wamekuwa wakifahamu.

Mheshimiwa Spika, swali la pili anataka juu ya mkakati wetu kama Serikali. Naomba nimhakikishie habari njema kabisa kwamba sisi kama Serikali katika moja ya jambo kubwa tunalokwenda kulifanya sasa ni kuhakikisha vituo vyetu vyote vya uzalishaji wa vifaranga vya samaki nchi nzima, Kituo kama kile cha Morogoro pale Kingolwira na vingine vya Luhira kule Songea na Mwaipula kule Tabora vyote tunakwenda kuviboresha ili tuweze kuzalisha vifaranga vya kutosha na hatimaye wafugaji wetu waweze kuvipata.

Mheshimiwa Spika, lakini lingine ni kuhakikisha tunakwenda sambamba na wenzetu wa Wizara ya Fedha kwa sababu tumeshapeleka mapendeleko yetu ya kupunguza tozo na kodi mbalimbali ambazo ndizo

zimekuwa kikwazo katika uwekezaji kwenye eneo hili la ufgaji wa samaki. Naomba tu Mheshimiwa Mbunge na wadau wengine wote waendelee kujipanga kuhakikisha kwamba huko iko fursa ya kuendeleza sekta hii ya uvuvi.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Hili swali lina wapambe wengi, Mheshimiwa Ester Bulaya na Mheshimiwa Hawa Ghasia.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa Wabunge wenzangu watakulaliana na mimi kwamba hakuna mtu anayeunga mkono uvuvi haramu na sisi tunaotoka Kanda ya Ziwa tumekua kutokana na samaki. Kitu ambacho tunahoji ni namna gani hii operesheni watu wasiowatakla mema wananchi wetu wanavyoindesha.

Mheshimiwa Spika, nilimwambia Waziri Jimboni kwa Mheshimiwa Kangi watu walienda kuvunja mafriji (*fridges*) ma-frizer (*freezers*) na kuwakamata wale watu na kuchukua pesa zao kinyume na utaratibu. Hivi navyoongea jimboni kwangu juzi Polisi wamewavamia akina mama na kuwapiga mabomu wakishirikiana na Mkuu wa Wilaya. Swali langu, hivi ni kweli operesheni yenu inalenga kunyanyasa watu na mnatoa tamko gani kwa watu ambao wanafanya vitu vya namna hii? (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante kwa swali limeeleweka. Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Abdallah Ulega.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ester Bulaya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza natoa shukrani kubwa sana kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuwa Bunge zima limetuunga mkono juu ya suala linalohusu uvuvi haramu,

kwa sababu uvuvi haramu ni uharibifu wa maliasili za nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, swalı lake linahusu ni kwa nini watu wanaotekeleza jukumu hili la operesheni dhidi ya uvuvi haramu wananyanya wa nanchi. Kwa heshima kubwa na taadhima nataka niseme kwamba tunachokifanya tunakiita kwa kifupi Operesheni Uvuvi Haramu, lakini sisi tunakwenda mbele zaidi na kupambana na biashara haramu ya mazao yanayotokana na uvuvi.

Mheshimiwa Spika, kesi anayoisema Mheshimiwa Ester Bulaya ni maalum, kwamba kuna tatizo la wananchi katika jimbo lake au jimbo la Mheshimiwa Kangi Lugola wamenyanyaswa katika mafriji yao. Naomba nimhakikishie kwamba Serikali ipo kuanzia katika ngazi za Wilaya, sisi tuko tayari kupokea malalamiko yote yanayohusu *specific cases* na kuyashughulikia.

Mheshimiwa Spika, nataka nimwambie tumewatuma kufanya kazi ya kudhibiti uvuvi haramu na biashara haramu ya mazao ya uvuvi na siyo kuwanyanya watu. Kwa hivyo, kama ipo kesi maalumu inayohusu mtendaji wetu amenyanya mtu, sisi tuko tayari kupokea kesi hiyo, kuichukulia hatua na hata kumchukulia hatua Mtendaji ye yote atakayethibitika kwamba amefanya vitendo vya uvunjifu wa maadili kwa kuwaonea Watanzania.

SPIKA: Tumesikia uzoefu wa Ziwa Viktoria, twende baharini, Mheshimiwa Hawa Ghasia.

MHE. HAWA A. GHASIA: Mheshimiwa Spika, nashukuru na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swalı la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, napenda kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa nini tusitumie uzoefu ambao tuliuapata katika mradi wa *MACEP* ambapo zoezi la kuzuia uvuvi haramu lilikuwa linaenda sambamba na kuwawezesha wavuvi wetu kwa vifaa na zana bora ili waondokane na uvuvi haramu?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ya kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Hawa Ghasia, kwamba kwa nini tusitumie uzoefu tulioupata katika mradi wa *MACEP*. Mradi wa *MACEP* ulikuwa ni mradi maalum uliofadhiliwa na Benki ya Dunia. Mradi ule ulikuwa unahusianisha vipengele vingi ikiwemo kuwawezesha wavuvi wetu ikiwa ni pamoja na kujenga miundombinu ya uvuvi katika Ukanda wa Pwani.

Mheshimiwa Spika, tunao Mradi unaoitwa SWIOFish hivi sasa ambaa pia upo kwenye Ukanda wa Pwani. Moja ya jambo ambalo unafanya ni pamoja na kuwawezesha wavuvi, kuwafanya *capacity building* kwa maana ya uwezo wao wa pamoja wa kijamii, lakini vilevile na kujenga miundombinu. Kwa hivyo, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mradi huu upo katika hatua za kati na katika hatua zake za mwisho nina imani tutafika katika hii hatua ambayo yeeye ameipendekeza hapa.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Sware swalii la mwisho eneo hilo.

MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, Wizara imekuwa ikidhibiti nyavu haramu kwa kuzichoma, lakini tunajua kwamba uchomaji wa nyavu hizi za *plastic* huleta madhara makubwa sana kwa afya za binadamu kwa sababu uchomaji wa *plastic* huachilia sumu kali sana aina ya *dioxin* ambayo inaweza ikaleta madhara makubwa sana kwenye ini, figo, moyo na magonjwa mengine kwa binaadamu. Kwa nini Serikali isitafute mikakati mingine mahsusii inayotunza mazingira katika kudhibiti hizi nyavu haramu? (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Abdallah Ulega, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvu, majibu ya swalii hilo tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kujibu swalii la nyongeza la Mwalimu wangu Mheshimiwa Dkt. Semesi Sware ambaye amenifundisha, pamoja na mengine Sheria za Uvuvu za Mwaka 2003, Na.22 pale Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika Sheria ya Uvuvu inaeleza wazi kwamba ukikamata nyavu haramu ni kuteketeza. Sasa katika uteketezaji ndiyo yeye anasema tutafute njia nyingine siyo ile ya kuchoma moto kwa sababu ukichoma moto ule moshi unakwenda kuathiri wanaadamu. Mimi nadhani tutalichukua jambo lake hili na tutalifanyia mkakati mzuri wa kuhakikisha wakati tunachoma basi ule moshi usiende kuathiri watu wengine wanaozunguka jamii ile. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Tunahamla Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Neema William Mgaya atauliza swalii lake.

Na. 309

Tatizo la Maji Jimbo la Wanging'ombe

MHE. NEEMA W. MGAYA aliuliza:-

Tatizo la maji katika Jimbo la Wanging'ombe limekuwa sugu kwa sasa:-

Je, ni lini Serikali itatatua tatizo hilo?

SPIKA: Majibu ya swalii hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Aweso, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Neema William Mgaya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kubabiliana na tatizo la maji katika Jimbo la Wanging'ombe ambapo katika mwaka wa fedha 2017/2018, Halmashauri ya Wanging'ombe imetengewa jumla ya shilingi bilioni 4.7 na mpaka Machi, 2018, Serikali impeleka jumla ya shilingi bilioni 1.8. Kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji na Usafi wa Mazingira, Halmashauri ya Wanging'ombe imekamilisha miradi katika Vijiji vya Wangama, Mtama, Masaulwa, Isimike, Igenge na Idenyimembe na wananchi wanapata huduma ya maji. Miradi mingine katika vijiji tisa ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, kwa mpango wa muda mrefu, Serikali kupitia fedha za mkopo wa masharti nafuu kutoka Benki ya *Exim* ya India itatekeleza mradi wa kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji katika maeneo yanayopata huduma ya maji kutoka mradi wa kitaifa wa Wanging'ombe pamoja na Mji wa Igwachanya. Kazi zinazotarajiwa kutekelezwa ni pamoja na ukarabati wa chanzo cha Mbukwa na Mtitafu; ulazaji wa bomba kuu katika chanzo cha Mbukwa umbali wa kilomita 112; ukarabati wa matanki 59; kulaza bomba kuu kutoka chanzo cha Mtitafu umbali wa kilimita 15; ujenzi wa tanki la ujazo wa lita 200,000 katika eneo la Igwachanya; na ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji. Utekelezaji wa mradi huo unatarajiwa kuanza mwaka wa fedha 2018/2019.

SPIKA: Mheshimiwa Neema Mgaya, swali la nyongeza.

MHE. NEEMA W. MGAYA: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Nina maswali mawili ya nyongeza kwa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, Serikali imejenga Mradi wa Maji wa Kibena Howard lakini mpaka hivi sasa mradi ule bado haujaanza kutoa maji. Je, ni lini Serikali itahakikisha mradi huu unaanza kutoa maji ili wananchi wa Kibena na Hospitali ya Mkoa wa Kibena ili iweze kupata huduma hii ya maji?

Mheshimiwa Spika, lakini swalii langu la pili, ni lini Serikali itaanza kutekeleza Mradi wa Maji Tarafa ya Matamba, Wilaya ya Makete?

SPIKA: Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Waziri wa Maji amesimama, tafadhalii Mheshimiwa.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mradi wa Kibena umekamilika tatizo ambalo lipo ni umeme na tulishaagiza walete *quotation* kutoka *TANESCO* tuwalipe ili waunge umeme na wananchi wa Kibena waendelee kupata maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, lakini kuhusiana na suala la Matamba, nilitembelea Matamba na nikatoa maelekezo. Nishukuru kwamba Mheshimiwa Mbunge ameleta makadirio yale na katika mwaka ujao wa fedha tutatekeleza mradi mkubwa ili wananchi wa eneo la Matamba waweze kupata huduma ya maji safi na salama kwa kukarabati mradi uliokuwepo ambao ulikuwa na bomba dogo sasa tutaweka bomba kubwa ili maji yaweze kupatikana kwa wingi.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Maji, unaona watu waliosimama walivyo wengi, nashindwa nani apewe sasa nani asipate nafasi. Mheshimiwa Silinde na Mheshimiwa Flatei nimewaona.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na uzuri umeona idadi ya Wabunge waliosimama hii ni kuashiria kwamba maji ni tatizo.

Mheshimiwa Spika, mimi tu niulize swalii dogo ambalo litaambatana na ushauri. Moja ya sababu inayopelekea kuwepo kwa tatizo kubwa la maji ni kwa sababu Serikali hajakita maji kama moja ya kipaumbele chake. Ni kwa nini sasa Serikali isikubali maji kuwa moja ya vile vipaumbele vitatu

vikubwa vya Taifa, kwamba tutenge bajeti walau asilimia 20 kwa kuhakikisha tunatatua tatizo la maji nchi nzima? Kwa nini msikubaliane na jambo hilo ili tuondoe tatizo hili nchi nzima? Ahsante. (*Makof*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Isack Aloyce Kamwelwe.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali dogo la Mheshimiwa Silinde, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilishaweka kipaumbele kuhusiana na utekelezaji wa miradi ya maji safi na salama. Ilianza mwaka 2006/2007 ambapo tulianza programu ya utekelezaji wa miradi ya maji nchini na ndiyo tulipoweka mikakati ya kujenga miradi 1,810 na hadi leo tumeshatekeleza miradi 1,468.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika mkakati huo tume-*ring fence*, tumeweka fedha Sh.50 zinatolewa katika kila lita ya mafuta. Huo ni mkakati maalumu kuonyesha kwamba sasa Serikali imeshaona suala la maji ni la kipaumbele na ndiyo maana kutoka kwenye huo mfuko kila mwaka tunatengewa shilingi bilioni 158.5. Ninyi Waheshimiwa Wabunge mmeendelea kusema kwamba fedha hiyo iongezwe ili iweze kutumika kwenye miradi. Kwa hiyo, Serikali tayari ilishaweka kipaumbele cha maji na tutahakikisha wananchi wanapata maji safi na salama.

SPIKA: Nilishakutaja Mheshimiwa Flatei na upande wa CUF utauliza swali linalofuata.

MHE. FLATEI G. MASSAY: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa muda wa kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, tatizo sugu linaloonekana kwenye swali la msingi la Wanging'ombe linafanana kabisa na tatizo sugu la kukosekana maji Mbulu Vijijini. Kwa kuwa Mheshimiwa

Waziri amefika katika Jimbo langu, kwanza namshukuru, lakini sasa tumesaini Mkataba na *DDCA* wa kuchimba visima sita (6), tangu Januari mpaka leo hawaonekani na hawakuchimba visima vile. Waziri atatusaidiaje sasa *DDCA* waje kuchimba visima ambavyo tumeingia nao mkataba na Halmashauri yangu Jimbo la Mbulu Vijiijini? (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya majibu ya swali hilo, Mheshimiwa wa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Eng. Kamwelwe tafadhali, *DDCA* wameingia mitini.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Massay kwa jinsi anavyoshughulikia Jimbo lake. Nilishawahidi kufika kule na ni kweli kwamba *DDCA* wamesaini mkataba wa visima sita. Kwa sababu hili suala ni la kiutendaji, mimi na yeze baada ya Bunge leo tuwasiliane ili tuweze kuwaliza *DDCA* kwa nini hawajapeleka mitambo kwenda kuchimba.

SPIKA: Nilishakubalia uliza swali la nyongeza Mheshimiwa.

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Tatizo la miundombinu hii ya maji halipo tu Wanging'ombe lipo pia pale Temeke ambako miundombinu ya maji taka pale Kurasini imekufa kabisa na sasa hivi mazingira yale kwa kweli yanatia kinyaa kwa sababu vinyesi vinatapakaa nje. Wizara ilisema kwamba wanataka wajenge mitambo ya kisasa ya kuchakata taka na nimeona wameanza kulipa fidia japo kidogo kidogo sana. Sasa kwa sababu jambo hili ni la hatari linaweza kusababisha magonjwa mlipuko pale, Wizara ina mpango gani wa kuanza kujenga mitambo hiyo mipya haraka?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Eng. Kamwelwe, tafadhali.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekit, kwanza nimshukuru amekiri kwamba na fidia tumeanza kulipa na tumeshapata fedha kutoka Serikali ya Korea Dola milioni 90. Kwa hiyo, wakati wowote tunatangaza tenda tuanze utekelezaji wa mradi huo. Hata hivyo, katika kipindi kuna miradi midogo midogo tunayotekeleza ili kuhakikisha kwamba suala la kipindupindu haliwakuti wananchi.

SPIKA: Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge na Wizara ya Fedha na Mipango, swali la Mheshimiwa Dkt. Suleiman Ally Yussuf, kwa niaba yake Mheshimiwa Masoud Abdallah.

Na. 310

Akaunti ya Pamoja ya Muungano

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM (K.n.y. MHE. DKT. SULEIMAN ALLY YUSSUF aliuliza:-

Serikali iliunda Akaunti ya Pamoja ya Fedha kwa mujibu wa Ibara 133 ya Katiba kupitia Sheria Na.15 ya Mwaka 1984 ili kila upande usimamie uchumi wake na uchumi wa Muungano usimamiwe na chombo cha Muungano:-

(a) Je, ni kwa nini miaka 33 sasa Akaunti hiyo haijafanya kazi yake?

(b) Je, gharama kiasi gani imetumika kuanzisha taasisi ambayo haina faida yoyote?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Kijaji, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Suleiman Ally Yussuf, Mbunge wa Magogoni, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatambua uwepo wa Akaunti ya Pamoja ya Fedha pamoja na Tume ya Pamoja ya Fedha. Ibara ya 133 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imebainisha sharti la kutungwa kwa sheria itakayoweka utaratibu wa uendeshaji wa Tume ya Pamoja ya Fedha pamoja na Akaunti ya Pamoja ya Fedha. Ili kutekeleza sharti hilo la kikatiba, Bunge lako Tukufu lilitunga Sheria ya Tume ya Pamoja ya Fedha ya Mwaka 1996 (*The Joint Finance Commission Act, 1996*) na hivyo kuwezesha kuanza kazi kwa Tume ya Pamoja ya Fedha mwaka 2003.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa uendeshaji wa Akaunti ya Pamoja ya Fedha umependekezwa kwenye ripoti ya mapendekezo ya vigezo vyta kugawana mapato na kuchangia gharama za muungano iliyoandalishi na Tume ya Pamoja ya Fedha mwaka 2006. Hata hivyo, akaunti ya pamoja ya fedha haijanza kufanya kazi kwa kuwa majadiliano kati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu mapendekezo ya Tume hayajakamilika.

(b) Mheshimiwa Spika, tangu kuzinduliwa kwake mwaka 2003 Tume ya Pamoja ya Fedha imekuwa ikiidhinishiwa bajeti yake na Bunge lako Tukufu kuititia bajeti ya Fungu 10, chini ya Wizara ya Fedha na Mipango. Katika kipindi cha kuanzia mwaka wa fedha 2003/2004 hadi 2017/2018, Tume imeidhinishiwa bajeti ya Sh.31,971,490,663 kwa ajili ya uendeshaji na utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, aidha, si kweli kwamba Tume ya Pamoja ya Fedha haina faida yoyote. Katika kutekeleza majukumu yake ya msingi, Tume imefanya stadi sita tangu kuanzishwa kwake kwa lengo la kutoa mapendekezo na ushauri katika eneo la uhusiano wa kifedha kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Pia, Tume ya Pamoja ya Fedha imeandaa rasimu ya Mwongozo wa Uendeshaji wa Akaunti ya Fedha ya Pamoja ambao unatarajiwa kutekelezwa mara majadiliano ya pande mbili za Muungano yatakapokamilika.

SPIKA: Mheshimiwa Masoud Abdallah, swalii la nyongeza.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Spika, nakushukuru lakini nasikitika na majibu haya kwani ni majibu yale yale ya muda mrefu ambayo yamekuwa yakinolewa hapa Bungeni na imekuwa kidogo hayaleti taswira nzuri kwa pande mbili za Muungano. Nina maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, katika majibu yake anasema kwamba Tume ya Pamoja haijaanza kufanya kazi kwa kuwa majadiliano kati ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu mapendekezo ya Tume hayajakamilika. Miaka yote hiyo mapendekezo wanajadiliana kati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, sasa mpewe muda gani? Mtuambie wananchi wanataka kusikia leo, mpewe muda gani mtawezza kukamilisha hayo mapendekezo? Ni miaka 33 ya Tume lakini tangu mapendekezo mwaka 2003 ni miaka kadhaa sasa, lakini hakuna kitu na wakati huo mnaendelea kutumia bilioni 31 *point*; mtuambie mnataka muda gani hasa, nusu karne au karne moja?

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, majibu ya Serikali yanasesma kwa makini sana, Tume ya Pamoja ya Fedha imeandaa rasimu ya Mwongozo wa uendeshaji wa Akaunti ya Fedha ya Pamoja ambao unatarajiwa kutekelezwa mara baada ya majadiliano ya pande mbili za Muungano yatakapokamilika. Wameandaa rasimu sasa, miaka yote hiyo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri atuambie maeneo machache ya rasimu hiyo, maana hakuna anayeamini tunaona ni kiini macho, kizungumkuti, tuambie hayo maeneo machache.

SPIKA: Mheshimiwa Masoud, mwisho wa siku uliza swalii basi bwana.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Spika, maeneo machache ya rasimu yaliyotayarishwa ni yapi? Kwa sababu tayari wameshaanda rasimu lakini hakuna anayeamini, tunaona haya ni majibu tu ya kizungumkuti, kiini macho, kusadikika, tuambie hilo.

SPIKA: Ahsante sana. Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri Fedha, niliona Naibu Waziri Muungano anataka kusaidia, Mheshimiwa Kangi Lugola, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA): Mheshimiwa Spika, napenda kuongezea majibu ambayo yamejibiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri. Majibu ambayo sisi kama Serikali tunaamini yalikuwa ni majibu mazuri, majibu yanayojitosheleza, lakini kwa kiu ya Mheshimiwa Masoud anasema bado Serikali haina dhamira ya kuhakikisha kwamba hiyo Akaunti ya Fedha ya Pamoja inaanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti yetu ambayo ilipitishwa na Bunge hili, Serikali kupitia Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, aliliarifu Bunge lako Tukufu kwamba mwezi wa Aprili, tarehe 22, Kamati ya Pamoja ambayo inahusu Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na ya Muungano watacaa kwa ajili ya kuchambua mapendekezo ambayo yametoka kwenye Tume ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya Mheshimiwa Rais wa nchi yetu ilikuwa ahudhurie Mkutano wa *Commonwealth* kule London, Uingereza, lakini akawa amemtuma Mheshimiwa Makamu wa Rais ambaye ndiye Mwenyekiti wa hicho kikao cha Kamati ya Pamoja, kwa hiyo, matokeo yake kikao kile hakikufanyika. Aliporudi wakati kikao kile kilikuwa kimeandaliwa tena, akatumwa na Mheshimiwa Rais kwenda kwenye Mkutano wa *SADC*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba yale yote aliyojasema tuko katika hatua nzuri. Mapendekezo yalishawasilishwa kwenye

ile Kamati, ni uchambuzi tu ambao ukishafanyika yale maeneo ambayo alikuwa anasema ni maeneo gani yataweza kufanyiwa kazi na Mheshimiwa Mbunge atayafahamu.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Khatib, swali la nyongeza.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Jambo hili ni la muda mrefu na limekuwa likijitokeza kila mara. Si aibu wala si ajabu kwa lile linalotushinda tukawa wakweli na tukafanya lingine tunaloliweza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, haikuwa aibu kumuondo Rais wa Zanzibar kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hilo limefanyika; na hili la Akaunti ya Pamoja kama linatushinda ni kwa nini lisiondolewe na tukatafuta njia nyingine au utaratibu utakaotuwezesha kuliendesha jambo hili katika mustakabali huo, badala ya kuendelea kuvunja Katiba kwa kutotimiza takwa hili la kikatiba? Ahsante.

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Khatib, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, masuala ya Muungano na zile changamoto zake tulishasema hapa Bungeni, changamoto zile 15 ambazo tulikuwanazo tayari 11 zimeshapatiwa ufumbuzi tumebakii na nne tu. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hii Akaunti ya Fedha ya Pamoja anayoizungumzia tusipokuwa makini na jambo hili, tusipokuwa na maridhiano, tunaweza tukaingia kwenye matatizo ambayo yatasababisha Watanzania kuanza

kusema kwamba, afadhali hata hiyo Akaunti tusingekuwanayo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tuko kwenye uendeshaji wa gari, tunapokuta kuna kibao kimeandikwa hapa uendeshe *speed* 50 au 80 na sisi hatuna budi kufanya hivyo. Katika jambo hili kuna umakini mkubwa ambao unatakiwa.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Khatib Serikali ina dhamira ya dhati na wala hatuna kigugumizi na hatuna sababu yoyote ya kuuaibisha Muungano kwa sababu tulishaungana, haya mambo mengine yote haya tutayashughulikia vizuri. Atupe nafasi kwa sababu tunesema kile kikao kitafanyika, asiwe na haraka. Ahsante sana.

SPIKA: Tunaenda Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Mheshimiwa Emmanuel Adamson Mwakasaka, Mbunge wa Wanyamwezi wa Tabora Mjini.

MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA: Mheshimiwa Spika, asante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la msingi, lakini nakuomba kabla sijaauliza hili swali niombe jambo moja ambalo limejitokeza kutohana na swali hili. Hili swali nilikuwa nimepewa barua litajibiwa kesho lakini leo nimelikuta hapa. Sasa sisi ni wawakilishi wa wananchi na maswali mengi tunayouliza yanahusiana na wao na Mbunge unakuwa umewajulisha kwamba siku fulani swali hili litajibiwa na kumbe lile swali...

SPIKA: Mheshimiwa sasa unaanza kuomba Mwongozo.

MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA: Mheshimiwa Spika, naomba nitumie hii nafasi...

SPIKA: Twende kwenye swali moja kwa moja, hayo mengine tutayatatua baadaye.

MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA: Mheshimiwa Spika, ahsante.

Na. 311

Ajali za Bodaboda Zinazosababishwa na Askari Polisi

MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA aliuliza:-

Kumekuwa na ajali nyingi zinazotokana na vitendo vya baadhi ya Askari Polisi maarufu kama *PT* kuwakamata waendesha bodaboda wakiwa kwenye mwendo huku wakiwa wamebeba abiria. Hali hiyo hupelekea waendesha bodaboda na abiria kupata ajali mara kwa mara:-

Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha kuwa ajali za kizembe zinazosababishwa na baadhi ya Askari Polisi zinakomeshwa?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, tafadhali.

WAZIRI WA MAMBO NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka, Mbunge wa Tabora Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa tafiti mbalimbali zilizofanywa na Jeshi la Polisi, ajali za barabarani husababishwa na vyanzo vikuu vitatu ambavyo ni vyanzo vya kibinadamu ambavyo husababisha ajali kwa asilimia 76, vyanzo vya kiufundi ambavyo vinasababisha ajali kwa asilimia 16 na vyanzo vya kimazingira ambavyo vinasababisha ajali kwa asilimia 8. Ni katika vyanzo vya kibinadamu ndivyo tunakuta kuna uzembe amba pia uko wa namna nyingi.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya vijana wetu waendesha pikipiki bado wana uelewa mdogo kuhusu sheria

za usalama barabarani na wengine pikipiki zao zina mapungufu mengi ambayo huwafanya kutokujiamini wanapoendesha. Kutokana na sababu hizi na nyinginezo, waendesha pikipiki hujihisi wana makosa wakati wote wawapo barabarani na hivyo huwa na hofu ya kukamatwa na Askari Polisi.

Mheshimiwa Spika, ni wajibu wa Askari Polisi kuhakikisha kuwa sheria zinafuatwa na si kuvunjwa. Waendesha pikipiki wanapaswa kutambua hilo na wao kutimiza wajibu wao wa kufuata sheria. Hali ya kutambua kuwa wana makosa ndio huwafanya kukimbia askari hata kama askari hana lengo la kuwakamata, hivyo husababisha ajali za kizembe bila sababu.

Mheshimiwa Spika, ili kuepukana na ajali za kizembe, Serikali kupitia Jeshi la Polisi itaendelea kutoa elimu kwa waendesha pikipiki ili kuwajengea uelewa wa sheria za usalama barabarani. Elimu hii itasaidia kuondokana na dhana potofu iliyojengeka mionganoni mwa waendesha pikipiki na wapanda pikipiki kutokutii sheria ama kusababisha vyanzo vyta ajali barabarani kwa kuwakimbia Askari Polisi kwa hofu ya kukamatwa, hata kama hawana makosa.

Mheshiiwa Spika, aidha, natumia fursa hii pia kulielekeza Jeshi la Polisi nchini kutumia muda wao vizuri katika kuwaelimisha waendesha pikipiki kufuata sheria za usalama barabarani kwa ajili ya usalama wao na watumiaji wengine wa barabara.

SPIKA: Mheshimiwa Mwakasaka swali la nyongeza.

MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kwa kuwa hawa baadhi ya maaskari wetu ambao wamekuwa wakiwakamata hawa bodaboda wakiwa kwenye mwendo na kuwasababishia ajali ambapo wengine wamepata

ulemau mkubwa na hata kusababisha kifo. Sijui Serikali pale inapokuwa imethibitisha kwamba uzembe ulikuwa ni wa askari na yakatokea madhara kwa muendesha bodaboda, sijui huwa wanakuwa na mpango gani wa kuwapa fidia hawa waendesha bodaboda? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Iakini swalii langu la pili, kuna malalamiko mengi ya waendesha bodaboda kwamba mara nyingi wanapokuwa wamekamatwa huwa wanabadilishiwa mashtaka wanapofika kituoni. Sasa kwa kuwa hatuna *CCTV camera* za kuangalia hasa yule wa bodaboda alikamatwa kwa kosa gani, je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha kwamba kosa lile alilokamatiwa yule mhusika ndilo analoshtakiwa nalo? (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, tafadhalli.

WAZIRI WA MAMBO NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa kuleta swalii hili kwa sababu ni kweli ni jambo ambalo linajitokeza katika baadhi ya maeneo na linaleta malalamiko.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba maisha ya vijana wetu yakipotea hayana fidia ya kusema umeweza kufidia maisha. Kwa hiyo, jambo ambalo tunafanya kama Wizara kwa kweli sisi kiutawala tunaelekeza utaratibu wa kiustaarabu wa ukamataji wa vijana hawa ili isisababishe ajali ambazo zinapoteza maisha kwa vijana wetu. Pia, tumeendelea kuwaelezea vijana wetu kwa sababu wamekuwa na uongozi kwenye vituo vyao kuhakikisha kwamba nao wanatoa ushirikiano, kwa wale ambaao wamefanya makosa ni haki yao kufika kwenye adhabu ili kuweza kupunguza makosa hayo yanayojitokeza.

Mheshimiwa Spika, kuhusu yale ya kubambika kesi hilo ni kosa la kimaadili na sisi kama Wizara wale wote wanaofanya haya kwa wananchi wanachukuliwa hatua kwa mujibu wa utaratibu wa ufanyaji kazi wa Jeshi la Polisi.

SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Adadi Rajab, Mbunge wa Muheza, uliza swali lako tafadhali.

MHE. ADADI M. RAJAB: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kunipa nafasi ya kuuliza swali moja kuhusiana na bodaboda hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na mapendekezo ya kuleta mabadiliko ya baadhi ya sheria za usalama barabarani, ikiwepo bodaboda. Kwa sababu, takwimu zinaonesha kwamba vifo vinavyosababishwa na ajali barabarani bodaboda zinaongoza. Chama cha Wabunge kimetoa mapendekezo ya kuleta hapa Bungeni mabadiliko ya sheria hiyo. Ni lini Wizara au Serikali italeta mabadiliko hayo ili yaweze kufanyiwa kazi ili kupunguza hizi ajali za barabarani, hususan, bodaboda?

SPIKA: Majibu ya swali hilo la nyongeza zuri sana, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, tafadhali.

WAZIRI WA MAMBO NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Adadi Rajab kwa swali zuri la nyongeza na yeye ni *dictionary* yetu kwenye Wizara kwa sababu ana kumbukumbu nzuri ya masuala ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba jambo hilo analolisemea limeshapita ngazi ya Wizara na liko ngazi ya vikao vya Makatibu Wakuu na baada ya hapo litapitia Baraza na tutaleta Bungeni kwa ajili ya ukamilishwaji wa hatua hiyo anayoiomba Mheshimiwa Mbunge.

SPIKA: Mheshimiwa Goodluck Mlinga ananiambia yeye ni muendesha bodaboda siku moja moja na Mheshimiwa Waitara. Mheshimiwa Goodluck Mlinga.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mheshimiwa Waziri wakati akijibu hoja zangu za kuhusu *fine* kwa madereva wa bodaboda alikiri kweli haiwezekani bodaboda anabeba abiria mmoja, anatozwa

fine Sh.30,000 wakati basi linalobeba abiria 60 *fine* ni ile ile Sh.30,000. Tunaomba atuhakikishie katika hayo mabadiliko ya sheria, je, hii sheria ya *fine*kwa ajili ya madereva bodaboda itakuwepo? Ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, tafadhalii.

WAZIRI WA MAMBO NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, nimempata vizuri mwakilishi na msemaji/mtetezi wa vijana, Mheshimiwa Mlinga. Niseme tu suala la *fine* sheria yake inapitishwa na Bunge kuititia *Finance Bill* ambayo itakuja kwenye mapendekezo ya Wizara ya Fedha. Sisi kama Wizara tumependekeza hivyo hivyo kwamba kwa kweli, ni vyema *fine* ya bodaboda itofautishwe na *fine* ya mabasi na *coaster* kwa sababu *fine* ya bodaboda kuwa sawasawa na ya magari makubwa yanayobeba abiria wengi ndiyo inayosababisha bodaboda nyingi zinarundikana kwenye vituo vya polisi kwa kushindwa kulipia *fine* zile. Kwa hiyo, tuliona ni vyema ikawa *fine* inayoweza kulipika ili kuweza kuwa na mantiki ile ya kutoa onyo badala ya kuwa chanzo cha fedha.

SPIKA: Mheshimiwa Waitara, wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Martha Mlata.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Ni kweli kwamba kuna tatizo kubwa sana la ajira katika nchi hii hasa kwa vijana na vijana wengi wamejiajiri kuititia njia ya bodaboda na nyingi wamekopeshwa kwa mikataba mbalimbali na watu wenye fedha zao. Ukitunguka katika vituo vya polisi nchi hii, hata hapa Dodoma, bodaboda zimejaa kila mahali.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri anakiri kwamba *fine* ni kubwa kweli kweli, kwa hiyo, kuna kesi nyingi za vijana hawa na wenye bodaboda zao wanawadai fedha. Ni nini kauli ya Serikali na hasa Mheshimiwa Waziri, kuondoa bodaboda katika vituo vya polisi, kwa maana ya kupunguza gharama, ili vijana hawa waendelee kujiajiri na wapunguze

kesi ambazo wameshtakiwa na watu wenye bodaboda zao ambao wamefunga nao mikataba? Ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo la nyongeza, Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

WAZIRI WA MAMBO NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, sikumpata vizuri babu yangu, Mheshimiwa Mwita, Wanyiramba tulishaondoka siku nyingi Mara, kwa hiyo, lafudhi kidogo imenishinda.

Mheshimiwa Spika, lakini ambacho tunafanya, moja, tunatoa elimu kuweza kuhakikisha kwamba wanafuata taratibu, kwa sababu kwa kweli maisha ya vijana wetu wengi sana yanakatika kutokana na wao kutokuzingatia taratibu za kujifunza maana bodaboda ni vyombo vya moto kama vyombo vingine na vimeduwa vikisababisha sana ajali. Kwa hiyo, tumeweka mkazo sana kwenye kutoa elimu lakini hata wao tumewelekeza sana kuhakikisha kwamba nao wanaliongelea jambo hili kama moja ya jambo la hatari ambalo linasababisha madhara haya.

Mheshimiwa Spika, lakini kuhusu kupunguza mishtuko hiyo pamoja na bodaboda nyingi kwenye vituo vya polisi, hilo tumeelekeza moja kwenye hili la upande wa *fine*, lakini la pili tumeelekeza hata kiutawala tu kwamba, kuwe na utaratibu wa kuwaandikisha na kuwaruhusu wawe na hivyo vifaa vyao ili waweze kulipa baada ya muda ambao wataweza kupewa. Nchi nyingine ambazo zimeendelea taratibu zote za mambo ya *fine* za usalama barabarani wanafanya kuandikisha na kumpa muda mtu aliyekutwa na kosa wa kufanya malipo hayo punde atakapokuwa ameshaanza kufanya kazi na hicho chombo chake.

Mheshimiwa Spika, utaratibu ambao umekuwa unatumika muda huu ni wa kushikilia bodaboda hiyo na kusema mpaka atakapokuwa amelipa ndipo atakapewa. Tumeelekeza tu zile bodaboda ambazo zinatakiwa kutumika kama sehemu ya ushahidi, kwa mfano, kwenye makosa makubwa kama ya madawa ya kulevyta, mambo ya uhalifu

wa kutumia silaha, hivyo ndivyo ambavyo tunaweza tukashikilia kwa sababu makosa yake kwa kweli haturuhusu yaendelee kufanyika kwa kutumia bodaboda hizo.

SPIKA: Mheshimiwa Martha Mlata swali la mwisho kabisa.

MHE. MARTH M. MLATA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa hivi karibuni Serikali imewaondoa madereva wengi ambaao ni wazoefu kwa sababu wao ni darasa la saba na kuwaajiri vijana wadogo kwa sababu wao wana-*qualify* ama kidato cha nne na kuendelea, lakini bila uzoefu na tumeshuhudia sasa ajali zimeanza kuwamaliza viongozi wetu. Serikali haioni sasa hilo ni bomu kubwa sana inatengeneza kwa ajira za vijana ambaao hawana uzoefu kwa kuwamaliza watu? Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu ya swali la dada yako. Kijana anaajiriwa leo kesho anamwendesha Waziri. (*Makofi*)

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana dada yangu Mheshimiwa Martha Mlata kwa swali nzuri na swali lenye mantiki. Nachoweza kusema tu ni kwamba Idara yetu ya Usalama Barabarani itaendelea kufuatilia masuala ya uzoefu kuhusu uendeshaji wa vyombo hivi vya moto. Hata kwenye swali la msingi tulipotoka kwenye upande wa bodaboda ndivyo vitu ambavyo tumeendelea kuwasitizia kwamba mtu anajifunza ndani ya robo saa na baada ya hapo anabeba watu watatu kwenye pikipiki yake. Kwa maana hiyo hata upande wa magari tutaendelea kuongea na wenzetu kwa upande wa magari haya ya Serikali ambayo ameyaongelea, wawze kuzingatia suala la uzoefu wa anayeendesha gari hiyo pamoja na mwendo ambaao anatakiwa kuendesha gari hiyo.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru, *session* ya kwanza ya maswali tuishie hapo, tuendelee na utambulisho.

Waheshimiwa Wabunge, kama navyowaambieni siku zote yaani mnazungumza kwa sauti kweli kweli humu ndani, kunakuwa kama kilabuni vile. Tupunguze sana sauti tunapokuwa tunaongea maana tuko wengi sana karibu mia nne, kwa hiyo, inakuwa shida kidogo.

Wageni walioko katika Jukwaa la Spika ni 118 wa Mheshimiwa Dkt. Merdad Kalemani, Waziri wa Nishati amba ni Katibu Mkuu - Dkt. Hamisi Mwinyimvua, karibu sana Katibu Mkuu. (*Makofi*)

Vilevile tunao Wenyeviti wa Bodi; Mwenyekiti wa Bodi ya *TANESCO* - Ndugu Alexander Kyaruzi; Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya *TPDC* - Jaji Mstaafu Josephat Mackanja; Mwenyekiti wa Bodi ya *REA* - Dkt. Gidion Kaunda; Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya *PURA* - Ndugu Beng'l Issa; Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya *PBPA* - Dkt. Henry Chau; na Mwenyekiti wa Bodi ya *EWURA* - Prof. Jamidu Katima. Karibuni sana Wenyeviti wa Bodi Mbalimbali. (*Makofi*)

Pia karibuni sana Wakuu wa Idara na Vitengo vyta Wizara wote mlioko hapa na Wakuu wa Taasisi tunao Mkurugenzi Mkuu wa *TANESCO* - Dkt. Tito Mwinuka; Kaimu Mkurugenzi Mkuu *REA* - Eng. Amos Maganga; Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa *TPDC* - Eng. Kapuulya Musomba; Kaimu Meneja Mkuu *TGDC* - Eng. Kato Kabaka; Mkurugenzi Mkuu *PURA* - Eng. Charles Sangweni; na Kaimu Mtendaji Mkuu *PBPA* - Ndugu Erasto Simon. Mheshimiwa Waziri Makaimu wengi sana huko inakuwaje? (*Makofi*)

Pia wapo wageni 18 wa Mheshimiwa Waziri wa Nishati, amba ni ndugu na jamaa zake kutoka kule Chato Mkoani Geita, wakiongozwa na Ndugu Shabani Ntande, Mkuu wa Wilaya ya Chato. Wale wageni wa kutoka Chato wako wapi? Ooooh, karibuni sana Dodoma, ninyi Wasukuma hapa ni Jiji mwende taratibu msije mkagongwa na bodaboda. (*Makofi/Kicheko*)

Wageni wengine wa Mheshimiwa Waziri ni Madiwani wa Kata na Viti Maalum kutoka Halmashauri ya Chato. Waheshimiwa Madiwani, karibuni sana. (*Makof*)

Pia ipo familia ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, ni Ndugu Vaileti Kalemani, mke wa Mheshimiwa Waziri. Karibu sana shemeji yetu. Wasukuma nao kumbe wana macho wanajua kuchagua. Yupo pia mtoto wa Mheshimiwa Kalemani, Ndugu Theresia Kalemani, karibu sana mwanetu, karibu sana Theresia. (*Makof/Kicheko*)

Wapo wageni sita wa Mheshimiwa Naibu Spika ambaao ni marafiki zake kutoka Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Ndugu Kitu Mwila ambaye ni Kada wa CCM aliyekuwa Katibu wa CCM, Tawi la Mpakani B Kijitonyama. Karibuni sana. (*Makof*)

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, wageni wanne wa Mheshimiwa Subira Mgatu, Naibu Waziri wa Nishati na Mheshimiwa Hawa Ghasia ambaao ni viongozi wa Umoja wa Wahitimu wa Shule ya Sekondari ya Ndanda (UWAISEDA) kutoka Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Mwenyekiti wa Umoja huo Ndugu Yohana Kasawala. Karibuni sana. (*Makof*)

Wageni wawili wa Mheshimiwa Jumaa Aweso, Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, ambaao ni ndugu zake kutoka Mkoani Morogoro. Karibuni sana. (*Makof*)

Wageni watatu wa Mheshimiwa Rashid Shangazi ambaao ni Watafiti wa Shirika la Haki Rasilimali kutoka Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Mratibu wa Shirika hilo, Ndugu Rachel Chagonja. Wako pale karibuni sana. (*Makof*)

Wageni watano wa Mheshimiwa Stanslaus Mabula ambaao ni wafanyakazi wa Kampuni ya *CRRC Zhuzhou Locomotive Company*, popote pale mlipo naomba msimame, wageni wetu kutoka China, Karibuni sana Bungeni. (*Makof*)

Wageni wa Mheshimiwa Joshua Nassari ambaye ni Ndugu Lightness Richard kutoka Asasi ya *The Green Icon* inayojihusisha na mazingira iliyopo Wilayani Arumeru Mkoani Arusha. Hawapo.

WABUNGE FULANI: Wapo.

SPIKA: Oooh, nimeambiwa wapo. Karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni 72 wa Mheshimiwa Flatei Massay ambao ni Chama cha Wanafunzi kutoka Mkoa wa Arusha na Manyara wakiongozwa na Ndugu Zawadiel Batolomayo. Karibuni sana wageni wetu. (*Makofi*)

Mgeni mwingine wa Mheshimiwa Massay ni Diwani wa Mbulu, Mheshimiwa Peter Tarimo. Karibu sana Mheshimiwa Peter. (*Makofi*)

Wageni sita wa Mheshimiwa Hamidu Bobali ambao ni wapiga kura wake kutoka Mchinga Mkoa wa Lindi wakiongozwa na Ndugu Hamza Nyagula. Karibuni sana Wamachinga kutoka Mchinga. (*Makofi*)

Wageni 12 wa Mheshimiwa Abdallah Chikota ambao ni Wanachuo kutoka Chuo Kikuu cha St. John wanaotokea Mkoani Mtwara wakiongozwa na Ndugu Yustus John. St. John, wale pale ahsanteni sana. (*Makofi*)

Wageni 26 wa Mheshimiwa Ester Mahawe ambao ni Wajasiriamali kutoka Wilaya ya Babati, Mkoani Manyara wakiongozwa na Ndugu Agape Kiwelu. Wale pale, oooh, mmependeza kweli. Karibuni sana wageni wetu kutoka Babati. (*Makofi*)

Wageni 36 wa Mheshimiwa Cosato Chumi ambao ni Wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma wanaotokea Mafinga, Mkoani Iringa wakiongozwa na Ndugu Christina Donatusi. Karibuni sana, wako pale. (*Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa Seif Gulamali ambaye ni Mpiga kura wake kutoka Manonga, Mkoa wa Tabora, Ndugu Mustafa Kisimba. Yule kule, karibu sana. (*Makof!*)

Mgeni wa Mheshimiwa Ritta Kabati ambaye ni ndugu yake kutoka Mkoani Iringa, Ndugu Josiah Kifunge. Karibu sana Josiah. (*Makof!*)

Wageni 16 wa Mheshimiwa Dkt. Rashid Chuachua ambao ni Umoja wa Wanachuo wa Vyuo Vikuu vya Dodoma kutoka Mikoa ya Lindi na Mtwara (UTWALISO) wakiongozwa na Ndugu Kenneth Songa. Karibuni popote pale mlipo, wako pale. (*Makof!*)

Wageni walitembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ni Waandishi wa Habari 28 ambao ni Muungano wa Klabu za Waandishi wa Habari nchini *UTPC* kutoka Wanachama wa Muungano wa nchi nzima wakiongozwa na Ndugu Victor Maleko. Karibuni sana. (*Makof!*)

Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane hili ni tangazo muhimu, Mwenyekiti wa *TWPG* Mheshimiwa Margaret Sitta, anawatangazieni Waheshimiwa Wabunge kwamba *TWPG* imeandaa hafla ya uchangiaji fedha itakayofanyika hapa Dodoma mwishoni mwa mwezi Juni yaani mwishoni wa mwezi ujao kwa ajili ya ujenzi wa vyoo vya mfano katika majimbo yenu yote 264.

Kwa kuwa shughuli hiyo ya uchangiaji fedha itawahuisha Waheshimiwa Wabunge wenyewe na Mgeni Rasmi anatarajiwa kuwa mmoja kati ya viongozi wakuu wa nchi yetu, hivyo kumeandaliwa burudani mbalimbali siku hiyo ikiwemo maonesho mitindo, *fashion show* ambaye wahusika wake watakuwa ni Wabunge wenyewe, tutawaona Waheshimiwa Wabunge wakiwa katika aina mbalimbali ya *fashion*. Kutakuwa na michezo ya vichekesho (*comedy*), kutakuwa na Wabunge watakaoimba na tumeambiwa kuna waimbaji wazuri sana humu ndani, wakiongozwa na Mheshimiwa King. (*Makof!*)

Pia kutakuwa na mashindano ya kucheza muziki katika kunakshi siku hiyo ikiwa ni sehemu ya kuchangisha fedha hizo na kutakuwa na mambo mengi. Mwanamitindo maarufu hapa nchini Hadija Mwanamboka atatoa mafunzo hapa Bungeni kwa ajili ya kuwafundisha Wabunge miondoko ya jukwaani ya mitindo (*catwalk*). Ile lazima ufanye mazoezi vinginevyo unaweza kukuta Waheshimiwa wanapiga mieleka halafu ikawa ni hatari tena. (*Makofi/Kicheko*)

Hivyo basi, Waheshimiwa Wabunge wote wanawake na wanaume tunaombwa kushiriki katika burudani hizo. *TWPG* wanaendelea kujandaa na wanawaomba mtoe kila aina ya ushirikiano. Kuna fomu maalum ambayo itatolewa ili tuweze kujaza kuona ni maeneo gani ambayo tungependa kushiriki katika kunakshi siku hiyo. Fomu hiyo ipo katika jengo kuu pale mapokezi unaweza ukaipata na kuanza kujaza ni eneo gani ambalo unadhani utasidia katika kuchangamsha siku hiyo na kuifanya iwe siku bora. Tunafanya taratibu kwamba onyesho hilo tutatafuta baadhi ya vituo vya televisheni ambavyo litalionesha *live* nchi nzima. Kwa hiyo, itakuwa ni hafla nzuri sana. (*Makofi*)

MHE. NAPE MOSES NNAUYE: Hoja ya kuahirisha shughuli za Bunge.

MWONGOZO WA SPIKA

SPIKA: Katibu nitajie majina.

NDG. ATHUMAN HUSSEIN – KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Lubeleje, Mheshimiwa Nassari, Mheshimiwa Matiko na Mheshimiwa Nape.

SPIKA: Haya. Tuanze na Mheshimiwa Seneta Lubeleje.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Spika, swali namba 311 linalohusu bodaboda ni suala nyeti na linatugusa Wabunge wote. Juzi Kamati yetu ya Utawala na Serikali za Mitaa tulifanya ziara Kanda ya Ziwa, kila Kituo cha Polisi unakuta pikipiki nyingi zimelala tu pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi sikatai kwamba wale wana makosa lakini kama wana makosa wapigwe *fine*, kama hawana *fine* wapelekwe mahakamani kuliko kulundika pikipiki kwenye vituo vya polisi na ile ni ajira ya vijana wetu. Naomba kauli ya Serikali pamoja na kwamba Mheshimiwa Waziri juzi alisema bodaboda zote ambazo zipo kwenye vituo vya polisi ziondolewe lakini bado hazijaondolewa. Naomba kauli ya Serikali kama wale vijana wana makosa wafikishwe mahakamani lakini kama wamelipa *fine* kwa nini pikipiki ziozee kwenye vituo vya polisi? (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Lubeleje, naamini Serikali imesikia, sidhani kama kuna haja Mheshimiwa Waziri kuongea yaani ni ukweli uliowazi kabisa labda ufanye sensa Mheshimiwa Waziri, waambie Ma-RPC wakutumie ni pikipiki ngapi ziko vituo vya polisi. Hapa tu Dodoma penyewe ziko 300, sijui 400 hapo mkoani hapo yaani ni rasilimali kubwa sana ambayo tumei-ground, hata Serikali yenewe inakosa pesa, ni nyingi mno sijui zinaweza zikawa ngapi. Sasa hili lilitakiwa liangaliwe kipeke yake, labda kama una cha kusema Mheshimiwa Waziri. (*Makofii*)

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, nakubaliana na hoja ya Mheshimiwa Mbunge na jambo hili takribani mwezi mmoja uliopita nilielekeza kwamba pikipiki zote ambazo zina makosa madogo ambazo hazina masuala ya ushahidi wa mahakamani warejeshewe wale watu kwa sharti la kwamba kama amepewa *fine* na anatakiwa kulipa apewe pikipiki ile akatumie kutafuta fedha himzo za kuweza kulipa hiyo *fine* aliopewa.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo kwa swali hili ambalo Mheshimiwa Lubeleje amelileta hata Mheshimiwa Flatei alikuja hapa akiniambia hili jambo ulilojibu kwake sasa hivi kuna jambo linaendelea. Nitumie tu fursa hii kuelekeza tena kwamba pikipiki zote ambazo ziko vituo vya polisi ambazo si za ushahidi kwenye makosa makubwa ya matumizi ya silaha ama madawa ya kulevyaa na vinginevyo ambavyo ni vitu vya usalama barabarani ambapo

wameshapewa *fine* warejeshewe wenye pikipiki hizo ili wakatafuta hizo *fine* wapewe muda ambao watatakiwa kulipa *fine* hizo. Nielekeze kwamba jambo hilo lifanyike leo na mimi nitapita kufanya hizo sensa ambazo umeelekeza. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Nassari.

MHE. JOSHUA S. NASSARI: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Mionganoni mwa shughuli ambazo zilifanyika jana ndani ya Bunge letu ilikuwa ni pamoja na kutoa taarifa kwa wawakilishi wetu ambao wamefanikiwa kuchaguliwa kwenye *Forum* ya Kimataifa ya Bunge la Afrika (*PAP*).

Mheshimiwa Spika, hapa nyuma kidogo uwakilishi wetu wa chombo kama Bunge kwenye *Forum* za Kimataifa kwa mfano kwenye Bunge la Jumuiya ya Madola (*Commonwealth*) ama kwenye Bunge la Afrika (*PAP*) na *Forum* nyiningine nydingi na kama *SADC*, uwakilishi wetu kama Bunge la Tanzania kwa kweli umekuwa hafifu kidogo kwa siku za nyuma tukubali. Sasa ningeomba mwongozo wako tu kwamba wewe kama kiongozi wa mhimili ambaye tunamshukuru Mungu kwamba umerudi na uko hapa sasa tunataka kujua ni kwa nini sisi tumeendelea kuwa nyuma kwenye ushiriki wetu kwenye hizi *forum* za Kimataifa, lakini pia utoe *commitment* yako kama Spika na Kiongozi wa Mhimili huu.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu jana tunashereheke, kina Mheshimiwa Masele wamepokelewa na Rais Ikulu lakini ushiriki wao kwenye hizi *forum* kwa mfano *South Africa* wamekuwa wanakwenda kwa gharama zao, wanajilipia ndege kwa gharama zao na wamekwenda kufanya kampeni kwa gharama zao. Mataifa mengine kama Cameroon na sehemu nyiningine wametuma *delegation* kabisa ya nguvu kutoka kwa Rais, kutoka kwa Bunge kwenda kutafuta hii nafasi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi ningetaka tu mwongozo wako na *commitment* ili sasa Bunge letu liweze kushiriki

kikamilifu kwenye hizi *forum*. Nilikuwa London mwaka juzi tukawa tunalamikiwa na Afrika Meneja wa *Commonwealth*, mimi nimekutana naye *in person* akanambia Bunge letu limekuwa halina ushiriki, limekuwa ni hafifu, wamekuwa hawapeleki watu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tunaomba *commitment* yako kama Spika ili watu waweze kushiriki. Kwa sababu mimi illifika hatua nikatumiwa *email* naombwa kushiriki kuliwakilisha Bunge eti nikuombe wewe ruhusa kwa sababu tayari niko kule hakuna *implication* za kibajeti na nini, lakini nikaona hapana huu si utaratibu kwa sababu tuna wawakilishi ambaao tumewachagua hapa ndani. Sasa naomba *commitment* yako, nashukuru sana. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Esther Matiko.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Mimi naomba mwongozo kwa mujibu wa Kanuni 99(3) lakini pia Kanuni ya 103(1) mpaka (11).

Mheshimiwa Spika, natambua kabisa kwamba Bunge ambalo linakaa Aprili mpaka Juni ni *session* ni muhimu sana kwa mustakabali wa maendeleo ya nchi yetu kwa maana Wabunge tunakaa kuweza kuitisha bajeti za maendeleo na matumizi mengine. Jana ukialangalia kwenye *Order Paper* ilikuwa ni Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Nimejaribu kuitia *Order Paper* yote na kwa kuzingatia umuhimu wa Wizara hii kwamba ndiyo taswira ya nchi yetu kimataifa, *ina-judge* ni vipi Tanzania ina mahusiano na nchi zingine na mambo mengine mengi.

Mheshimiwa Spika, nimesimama kuomba mwongozo wako kwa sababu kwenye *Order Paper* ya jana shughuli zilizokuwepo ilikuwa ni maswali na baadaye hoja ya Wizara hii. Tunavyojua sasa hivi wakati wa Bunge la Kumi tulikuwa tunachangia dakika 15, tukazirudisha na kwenye Kanuni tukaandika dakika 10 ambazo kwa kweli bado ni chache lakini ni kwa nini nimesimama, jana tumejadili vizuri wame-

table Mawaziri na Kamati, wakajadili Wabunge kama kawaida. Imefika saa saba aliyejkuwa amekalia Kiti akaongeza nusu saa na kwa kawaida sasa hivi ikifika saa saba tunaahirisha Bunge tunaenda tunarudi saa 10.00, Waziri ana-*wind up* na baadaye tunaingia kwenye Kamati ya Matumizi mpaka saa 12.00 ambapo ukiingia kwenye Kamati ya Matumizi kuna hoja ambazo zilikuwa hazijajibowi kimsingi zinaenda kujibowi pale kwenye masuala ya sera mbalimbali ili Waziri atoe ufanuzi mzuri na wenye hoja na wenye kukidhi na kama haukidhi Bunge linaamua kama ambavyo limefanya wakati wa Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, jana tumeahirisha Bunge saa 7.30, aliyejkuwa amekalia Kiti aliweza kutoa dakika tano tu kwa Naibu Waziri ku-*wind up* na dakika 10 tu kwa Waziri ku-*wind up*. Hili Bunge mimi nina miaka minane sijawahi kuona hiki kitu. Baada ya hapa tukaingia kwenye *guillotine* bila hata kupititia kifungu chochote kuweza kupata ufanuzi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sisi tuko hapa Dodoma tunatumia fedha za walipa kodi maskini tunaahirisha Bunge saa 7.30 kwenye *Order Paper* haja-indicate kuna kazi yoyote maalum ya Bunge kwenda kufanya tunaenda kulala majumbani na mahotelini. Tunatumia fedha za walipa kodi maskini, *this is not right*. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako sisi ni mhimilli ambao unatakiwa kuvisimamia na kuishauri Serikali hasa kipindi hiki cha bajeti. Kwa nini tunakubali kutumia fedha za walipa kodi maskini ambazo posho zetu wengine ni sawasawa na mshahara wa walimu ambao hata wanakopwa na hawalipwi.

Mheshimiwa Spika, huo ndiyo mwongozo naouomba.

SPIKA: Mheshimiwa Nape.

MHE. NAPE M. NNAUYE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nasimama kwa Kanuni ya 47 na 48, nataka kutoa hoja ya kuahirisha shughuli za Bunge ili kujadili jambo la dharura.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa wakati tunapitisha Bajeti ya Wizara ya Kilimo hapa ndani nilikamata shilingi kwa hoja ya fedha za *Export Levy*. Kiti chako kwa busara kiliagiza twende kukutana na Kamati ya Bunge ya Bajeti kwa ajili ya kulijadili jambo hilo na kulitafutia ufumbuzi. Bahati mbaya tumekutana zaidi ya mara mbili na wenzetu wa Wizara ya Fedha, Waziri wa Fedha, Naibu wake, Katibu Mkuu, Manaibu, Kamishna wa Bajeti na wengine wote walikuwa *busy* na shughuli zingine hawakuweza kuhudhuria vikao hivyo.

Mheshimiwa Spika, hivi tunavyozungumza jambo la dharura ni kwamba kuna ugonjwa unaitwa mnyauko fusari, unamaliza zao la korosho na korosho inakauka. La pili, bei ya *sulphur* ambayo ilitakiwa kuuzwa kwa Sh.16,000 kama fedha za *Export Levy* zingetolewa sasa mfuko mmoja umefika Sh.75,000. Hakuna namna ambayo wakulima wa korosho watanunua mfuko huu. Fedha hizi zimeshikiliwa na Serikali siyo fedha zao ni fedha za wakulima wa korosho na hii ni kwa mujibu wa sheria si hisani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, msimu wa kupulizia korosho ni sasa, ugonjwa unaendelea kutafuna zao la korosho na kwa kuwa korosho inalimwa katika mikoa 17 sasa ni zaidi ya nusu ya nchi, naaminini hilli jambo ni kubwa, ni la dharura. Naomba huruma yako na Bunge hili, busara yako na Bunge hili tulijadili jambo hili tuokoe zao la korosho. Pia zao hili ndilo lilihofanya vizuri katika msimu uliopita katika mauzo ya mazao nje ya nchi yetu. Serikali kuendelea kukamata fedha hii nadhani ni kuhujumu zao hili lakini ni kuhujumu uchumi na mapato ya nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba busara na huruma yako tulio koe zao la korosho baada ya jaribio la kwenda kwenye

kikao cha Kamati ya Bajeti kushindwa, niliahidi nitarudisha hapa tumeshindwana nairudisha hapa tulizungumze.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, tupe mrejesho wa kikao chako ambacho tulikuwa tumeomba kwamba mkutane na Serikali kwenye Kamati ya Bajeti.

MHE. HAWA A. GHASIA – MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI: Mheshimiwa Spika, ni kweli hili suala lililetwa katika Kamati ya Bajeti na tulipata fursa ya kukutana na mtoa hoja pamoja na Wabunge ambao walikuwa na maslahi na hoja hili. Pia tulipata fursa ya kukutana na Waziri wa Kilimo na Watendaji kutoka Bodi ya Korosho na Kituo cha Utafiti cha Naliendele na kikao chetu cha mwisho kilikuwa jana.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuipitia hii hoja na kuangalia Kanuni ambayo inataka hoja zitoke ndani ya Bunge na kwenda katika Kamati ya Bajeti tukaikuta inakosa sifa ya kuja kwenye Kamati yetu kwa sababu kifungu ambacho tulikuwa tunakizungumzia, pesa ambazo tunazizungumzia hazikuwa mionganoni mwa vifungu ambavyo tulikuwa tunavizungumzia. Hata ukienda kuangalia katika bajeti ya Wizara ya Kilimo hizo fedha hata ya mwaka jana hutaziona kwa sababu kwa mujibu wa ile sheria asilimia 65 ya pesa zile (*Export Levy*) zinaenda katika Mfuko wa Kuendeleza Korosho ambao sasa hivi majukumu yake yamepelekwa katika Bodi ya Korosho na asilimia 35 ya *Export Levy* inaenda Mfuko Mkuu. Sheria ile ni ya Bunge ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na haijabadilishwa, kwa hiyo, kamati imeshindwa kuendelea kujadili suala lile na tumelirudisha katika Ofisi yako ili uweze kulitolea maamuzi mengine.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Spika, nimesikiliza hoja iliyowasilishwa mbele ya Bunge lako na Mheshimiwa Nape, nimesikiliza ushauri uliotolewa na Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti na nilikuwa naendelea kupitia Kanuni yetu ya Bunge, Kanuni ya 105 ambacho kilitumika katika kushughulikia hoja hii ilipojitokeza wakati wa bajeti ya Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, kama maudhui ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti yanastahiki kuchukuliwa na Kiti chako, kwa hiyo, ni wajibu wetu kama Serikali sasa kurudi katika utaratibu utakaotuelekeza na si kuendelea na *Budget Committee* kwa haraka ile ambayo utakayotuelekeza ili sasa jambo hili tuweze kulimaliza kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, wakati tunaendelea kuhangaika na jambo hili katika siku hizi chache ambazo tulikuwa tunasimamia, pamoja na maelekezo ya sheria ya mgawanyo wa fedha zile kati ya Serikali na Bodi ya Korosho lakini Serikali ilikuwa imeshaagizwa kuhakikisha inatoa shilingi bilioni 10 za haraka ziweze kuanza kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo ambayo ninayo na niliyopewa na Waziri wa Fedha na niliagiza niletewe uthibitisho, fedha hizo za mwanzo zilishapelekwa. Hata hivyo, liko jambo mahsus ambalo linahitaji kujadiliwa kwa kina baina ya Serikali na Bunge kwa niaba ya wananchi ili kuhakikisha tatizo hilo linatatuliwa kwa haraka na wakulima wa korosho na zao la korosho linaendelea kuwa ni zao linalotegemewa katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

SPIKA: Mheshimiwa Zitto, wa mwisho kwenye eneo hilo.

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Spika, tuna tatizo kubwa sana sasa hivi la Serikali kudharau sheria ambazo zimetungwa na Bunge. Suala la *Export Levy* ya korosho si pekee ambalo Serikali inaa gizwa na sheria kwamba *TRA* wakusanye, wapeleke sehemu fulani Mfuko Mkuu wa Hazina na sehemu fulani iende kwenye chombo husika na Serikali haipeleki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wiki hii nimebahati kuhuduria vikao vya Kamati ya Bajeti. Kulikuwa kuna mjadala mkubwa sana kuhusiana na fedha ya reli (*Railways Development Levy*) ambao *TRA* inakusanya, inazipeleka zote Mfuko Mkuu wa Hazina na Serikali haitoi kabisa kwenda kwenye *Railways Development Levy* (*RAHCO*) kama sheria ambavyo inataka.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tuna tatizo la msingi hapa, kwa sababu iwapo *TRA* ingekuwa inazipeleka fedha za *Export Levy* ya korosho moja kwa moja kule ambako kunatakiwa, matatizo ambayo Mheshimiwa Nape anayazungumza sasa wala yasingekuwepo, wala tusingepoteza muda leo kujadiliana. Kwa hiyo, kuna tatizo la uvunjifu wa sheria ambayo sasa imekuwa ni kawaida ya Serikali ya Awamu ya Tano kufanya mambo bila kuzingatia sheria hata kidogo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa naomba kama jinsi ambavyo Mheshimiwa Nape ameomba, kwa dharura ambayo inatakiwa jambo hili litazamwe na litazamwe kwa muktadha wa uvunjifu wa sheria wa masuala yote yanayohusiana na mambo ya mapato ili Bunge lako liielekeze Serikali kufuata sheria za nchi ambazo kila mmoja wetu ameapa kuzilinda na kuzitetea. (*Makofii*)

SPIKA: Nawashukuruni wote kwa miongozo ambayo mmeiomba. Nianze na hili ambalo tumemaliza nalo. Ningemba Mheshimiwa Nape na Waheshimiwa Wabunge hili mtuachie Meza kwa sasa ili Mheshimiwa Waziri Mkuu mwenyewe akirudi niweze ku-*engage* naye tuone tunakwendaje. Kama hatutaona njia basi tutalirudisha kwenu

ili tuweze kuona Bunge hili linasema nini kuhusu jambo hili. Hili ni moja ya mambo yanasisitisha sana, sana. (*Makofi*)

Waziri wetu wa Kilimo alipoenda mara ya mwisho kwenye Kamati ya Bajeti imebidi atoe machozi, amelia kama mtoto mdogo. Mtu analaumiwa wala si mkosaji. Wizara ya Fedha kuna mambo yanaendelea huko sasa sisi tunakuwa hatujui, kwa hiyo, tunawaona kama nyie ni wabaya. Kwa sababu hawa watu ni hela zao, hivi kwa nini ukae na hela ya mtu awe anakuomba, anakupigia magoti, anakulambalamba na hela ni yake? (*Makofi*)

Hapo tulipofika ni mbali sana. Sasa Waheshimiwa Mawaziri wawe wanalia kweli kwenye Kamati za Bunge, hapana. Wizara ya Fedha hebu m jitathmini. Mnawafanya wanakuwa *very miserable*, hawawezi kusema kwa sababu ya uwajibikaji wa pamoja. Kwa hiyo, anapigwa na Wabunge anagumia tu. Sasa sisi wote tunadhani Waziri mbaya, hapa katikati tulikuwa tunapambana na Waziri wa Nishati hela ya REA, kumbe ni hawahawa walikuwa wameshika hela ya REA ndio maana miradi ilikuwa imesimama na kadhalika. (*Makofi*)

Kwa hiyo, huenda kuna shida Wizara ya Fedha, kwa sababu sisi hatujui tunawaoneni wabaya kwa sababu ni hela za wenyewe wala si hela za hii bajeti ambayo tunalongelea sisi. Haya ni makato ya wakulima wa korosho, ni hela zao. Kwa hiyo, tuachieni Mheshimiwa Waziri Mkuu akirudi *tu-rub shoulders* halafu tutarudi kwenu. Kwa kweli ni jambo ambalo linasikitisha na naomba muanze kulifanyia kazi haraka, kwa sababu mambo ya kilimo yanaenda na msimu. Kama msimu wa kupuliza *sulphur* umepita ina maana mwaka huo zao zima lime-crush, unaona. Kwa hiyo, lazima na utoaji fedha uende kwa msimu, huwezi kushika dokezo, oh, dokezo sijui limefanyaje, sijui likoje likoje halafu inachukua mwezi haiwezekani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Esther Matiko mwongozo wako kuhusu jana ni kwamba Mheshimiwa Naibu Spika alipokuwa hapa

katika mjadala ule alipata ushauri kutoka upande wa CCM kwamba hakukuwa na mchangiaji kwenye mambo ya vifungu, hakuna wa kukamata shilingi wala nini lakini pia upande wenu taarifa iliyokuja ni kwamba hapakuwa na mtu ambaye alikuwa anataka kushika kifungu chochote.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa
Wabunge waliongea bila mpangilio)*

SPIKA: Aah, viongozi wenu walileta maandishi au mnataka mpaka tutajane majina jamani.

WABUNGE FULANI: Taja.

SPIKA: Kwa hiyo, tuheshimu viongozi wetu, Mheshimiwa Selasini alituambia hapa kwamba tusonge mbele. Kwa hiyo, ni uendeshaji mzuri tu, ni *consultation* zilifanyika. Labda wengine hamkujua kinachoendelea lakini mambo yako salama. (*Makofii*)

Mheshimiwa Nassari anazungumzia habari ya ushiriki wetu katika mikutano ya nje. Tumekuwa tukijitahidi kushiriki kutegemea na bajeti yetu ilivyo na hali halisi ilivyo. Nimewahi kujibu na nijibu tena leo na jibu hili wala siyo kwamba lina nia mbaya, sera yetu imekuwa ni kupunguza safari za nje, tumezipunguza kwa zaidi ya asilimia 90 na nimeeleza mara kwa mara kwa nini safari hizo zimepungua. Ndiyo mtazamo wa nchi, ndiyo mwelekeo wa nchi, hata Mkuu wetu wa Nchi ye ye mwenyewe ni mfano wa kutokusafiri nje. (*Makofii*)

Sasa kundi ambalo ndio limebakia la kusafiri nje angalau ni *IPU* ambalo lina Wabunge sita (6); *SADC-PF* yenye Wabunge watano (5); *PAP* yenye Wabunge wanenye (4) kwa sasa; *ACP* ambayo ina Wabunge watatu (3) wanaoshiriki huko; na *CPA* approximately watano (5) na tukiaweka hata wale wa *Great Lakes* wasiozidi watano (5) ukiwajumlisha

wote hawa wanakaribia 30 na Bunge hili lina Wabunge 393. Ukiiondoa hawa 30 wanabakia Wabunge 363 ambao kwa miaka 5 hawatasafiri kwenda popote labda vile visafari tunavyopataga, tunauliza mtu bwana pana kasafari hapa hakina chochote unasemaje, ukatembee kidogo, vile ambavyo havihuishi fedha ya Serikali ndiyo tumekuwa tukiokota mmoja mmoja, wengine mnakataa. Kuna wakati hapa tulipata safari ya kwenda China Wabunge 20, wanafika *airport* pale karibu Wabunge sita, saba wala hawapo wanasema Spika safari zako za njaa hatuendi sisi. (*Makofii/ Kicheko*)

Sasa panapokuwa na Wabunge 30 katika 393 halafu hawa 30 kila wakati wanatushughulisha kujibu kuhusu kwa nini wao hawasafiri, hapo ndipo huwa naona kama ni *very unfair*. Tutakuwa tunashughullika nao ofisi huko, tunaelezana ikiwezekana wanaenda na kadhalika lakini wasifanye kama wanastahili sana, hapo ndipo penye tofauti, inategemea na mambo kadhaa mfano bajeti yetu na mambo mengine.

Kwa hiyo, bajeti yetu ikiruhusu wataenda, inapokuwa kidogo imebana na mambo mengine kidogo hayajakaa sawa, kikao hiki mnakosa, kikao kinachokuja mnakwenda, hivyo hivyo ndivyo tunavyoenda. Kwa hiyo, ukiwa katika kundi la wenzako wote ambao hawaendi kokote lakini wewe angalau unasafiri kidogo halafu ninyi tena ndiyo wa kuuliza maswali kila kukicha inakuwa haipendezi. Hayo mambo tuyamalize *administratively*, inakuwa inapendeza namna hiyo zaidi. Kwa hiyo, tutaendelea tu kusafiri hao wachache kutegemeana na hali halisi na mambo yalivyo hapa Mezani.

Sasa nimkaribishe Mheshimiwa Najma ili tuweze kuendelea na hoja inayofuatia.

Hapa Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Katibu tuendelee.

NDG. ATHUMAN HUSSEIN – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali
kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 - Wizara ya Nishati**

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Nishati, karibu.
(*Makofî*)

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuwasilisha hoja katika Bunge lako Tukufu, naomba hotuba yangu yote iliyomo kwenye kitabu cha bajeti iingie kwenye *Hansard* pamoja na taarifa ambayo nawasilisha mbele ya Bunge lako Tukufuna maandishi mengine yatakayohitajika kwa ajili ya zaida, kwa ajili ya Bunge lako Tukufu basi yaweze kuingia kwenye *Hansard* kama taarifa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji ya mwaka 2017/2018 na kuitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati na taasisi zilizopo chini yake kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu. Vilevile namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwawezesha Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutekeleza kazi zao za Kibunge kwa kushirikiana na mimi katika Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee nitumie fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. John

Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miongozo makini wanayonipa ili kuhakikisha kuwa azma ya Tanzania kuwa nchi ya viwanda inafikiwa. Ni wazi kwamba viongozi wetu hawa wamekuwa mstari wa mbele katika kutoa maelekezo yenye lengo la kuhakikisha kwamba umeme wa kutosha, wa uhakika, unaotabirika na wenye gharama nafuu unazalishwa ili kuchochaea ukuaji wa viwanda hapa nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Ally Mohamed Shein, Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuiongoza vyema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Nampongeza pia Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa usimamizi thabiti wa shughuli za Serikali ndani na nje ya Bunge lako Tukufu. Ni imani yangu kwamba kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu, viongozi wetu hawa kitaifa wataendelea kuwa chachu ya uhamasishaji wa shughuli za maendeleo hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kunateua kuiongoza Wizara ya Nishati. Uteuzi huo umenipa fursa ya kutoa mchango wangu katika kusimamia sekta hii muhimu kwa malengo ya Taifa letu. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Rais na Watanzania wote kuwa nitasimamia shughuli za Wizara hii kwa nguvu na akili zangu zote, kwa ubunifu na welevu mkubwa ili kuhakikisha kwamba sekta hii inadhihirisha kuwa ndiyo injini kuu katika kujenga uchumi wa viwanda wa Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nampongeza Mheshimiwa Subira Khamis Mgusu, Mbunge wa Viti Maalum kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Nishati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakupongeza wewe mwenyewe, Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, Wenyeviti wa Kamati pamoja na Wenyeviti wa taasisi mbalimbali zinazosimamia shughuli hizi za Bunge. Nampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Luka Kitandula, kwa kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Nishati na Madini. Pia nampongeza Mheshimiwa Mariam Ditopile Mzuzuri, kwa kuteuliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo. Aidha, nawapongeza na kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kwa kupokea Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 na pia kuitisha Mapato na Matumizi ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na upya wake Kamati hiyo Imekuwa ikitoa mchango na ushauri unaolenga kuboresha utendaji wa Wizara kwa maslahi mapana ya Taifa letu, hususan katika kuhakikisha kuwa umeme wa uhakika unazalishwa na wananchi wengi zaidi wanafikiwa na huduma hiyo hapa nchini. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa Wizara ya Nishati itaendelea kupokea ushauri na mapendekezo ya Kamati hiyo na Kamati nydingine za Bunge ili kuhakikisha kuwa Wizara inatekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuwapongeza, Mheshimiwa Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, Mbunge wa Jimbo la Songea Mjini, Mheshimiwa Justin Joseph Monko, Mbunge wa Jimbo la Singida Kaskazini, Mheshimiwa Dkt. Steven Lemomo Kiruswa, Mbunge wa Jimbo la Longido, Mheshimiwa Maulid Mtulia, Mbunge wa Jimbo la Kinondoni na Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel, Mbunge wa Jimbo la Siha kwa kuchaguliwa kwao kwa kishindo kuwa Wawakilishi wa wananchi katika majimbo yao. Hakika ni heshima kubwa walijopewa na wananchi na nawaombea kila la kheri katika kutekeleza jukumu lao hilo la uwakilishi katika Bunge letu Tukufu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii pia kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole kwako wewe binafsi, Naibu Spika na Bunge lako Tukufu na kwa familia ya aliyekuwa Mbunge wa Songea Mjini, Mheshimiwa Leonidas Gama kwa kuondokewa na mpendwa wetu huyo. Tunamwomba Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi, amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, naomba sasa kuwasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Shughuli za Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2017/2018 ulijielekeza katika maeneo makuu yafuatayo: Kuimarisha uzalishaji, usafirishaji na kuongeza kasi ya usambazaji wa umeme nchini; kufanikisha utekelezaji wa mradi mkubwa wa ujenzi wa bomba la mafuta ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania); kuendeleza miradi ya nishati jadidifu; kuwezesha uwekaji wa miundombinu ya usambazaji wa gesi asilia katika viwanda mbalimbali na matumizi ya majumbani pamoja na kufanikisha utekelezaji wa mradi wa kusindika gesi asilia (*LNG*); kuvutia uwekezaji katika Sekta ya Nishati, hususan kwenye uzalishaji wa umeme na utafutaji wa mafuta na gesi asilia. Sambamba na hayo, ni kuendelea kutekeleza agizo la Serikali la kuhamia Dodoma na kuwajengea uwezo wananchi hasa wafanyakazi wa Wizara katika fani za umeme, mafuta, gesi asilia na nishati jadidifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 iliyokuwa Wizara ya Nishati na Madini (Fungu 58) iliidhinishiwa na Bunge lako Tukufu jumla ya shilingi bilioni 998.34. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 945.89 sawa na asilimia 94.7 ya bajeti yote zilitengwa kwa ajili ya sekta ya nishati. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 916.84 sawa na asilimia 96.9 ni fedha za maendeleo na shilingi bilioni 29.04 sawa na asilimia 3.1 ni fedha za matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, fedha za maendeleo zilizotengwa, shilingi

bilioni 748.60 sawa na asilimia 81.7 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 168.24 sawa na asilimia 18.3 ni fedha za nje. Kwa upande wa Bajeti ya Matumizi ya Kawaida, shilingi bilioni 14.92 sawa na asilimia 1.6 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (*OC*) na shilingi bilioni 14.12 sawa na asilimia 1.5 ya bajeti yote ni mishahara ya wafanyakazi wa Wizara ya Nishati na taasisi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Aprili, 2018, Wizara ya Nishati kupitia (Fungu 58) ilikuwa imepokea jumla ya shilingi bilioni 446.50 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Sekta ya Nishati. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 424.91 sawa na asilimia 95.2 zilikuwa ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambapo fedha za ndani ni shilingi bilioni 413.09 sawa na asilimia 79.2 na shilingi bilioni 11.82 sawa na asilimia 2.8 ni fedha za nje. Aidha, kiasi kilichobaki cha shilingi bilioni 21.58 sawa na asilimila 4.8 zilikuwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi cha mwaka 2017/2018 iliyokuwa Wizara ya Nishati na Madini ilipanga kukusanya jumla ya shilingi bilioni 532.83 kutokana na mapato yanayohusu Sekta ya Nishati. Mapato hayo yanatokana na vyanzo mbalimbali vikiwemo shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi asilia; mauzo ya gesi asilia; mauzo ya nyaraka za zabuni; tozo ya umeme na stakabadhi nyinginezo. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Aprili, 2018, Wizara ilikuwa imekusanya jumla ya shilingi bilioni 280.27 sawa na asilimia 53. Wizara itaendelea na juhudzi za kukusanya mapato ili kufikia lengo lililowekwa kwa kipindi cha mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio yaliyopatikana kwa Mwaka 2017/2018. Mafanikio 23 yalipatikana kutokana na Sekta ya Nishati kwa kipindi cha mwaka 2017/2018 ambayo ni pamoja na yafuatayo:-

(i) Kuendelea na utekelezaji wa Mradi Kabambe wa Kupeleka Umeme Vijijini kupitia *REA* Awamu ya Tatu ambapo hadi mwezi Mei, 2018 kazi zilizokamilika ni pamoja na ujenzi wa kilomita 985 za njia ya msongo wa kilovoti 33,

ujenzi wa kilomita 1,870.37 za njia ya usambazaji umeme wa msongo wa kilovoti 0.4 na ufungaji wa transforma 751, hizi zote zikiwa na uwezo tofauti. Kazi nyingine iliyofanyika ni pamoja na kuunganisha vijiji 545 vimeunganishwa na kuwashwa umeme na wateja 14,817 tayari wameunganishiwa umeme. Hata hivyo, jumla ya vijiji 502 vimejengwa miundombinu ambavyo pia vinasubiri kuwashwa na vitawashwa wakati wowote kuanzia sasa.

(ii) Kukamilika kwa upelekaji umeme katika Makao Makuu ya Wilaya ya Tanganyika na Halmashauri ya Wilaya ya Bumbuli pamoja na kufanya Makao Makuu ya Wilaya zote nchini kupatiwa umeme wa uhakika.

(iii) Kukamilika kwa asilimia 100 kwa Mradi wa ORIO katika Miji ya Ngara, Biharamulo, Mpanda pamoja na Inyonga; hivi sasa inapata umeme wa uhakika.

(iv) Serikali imesitisha matumizi ya mitambo ya kukodi ya binafsi ya kuzalisha umeme kwa kutumia mafuta mazito katika kuzalisha umeme hasa katika makampuni ya Aggrekona IPTL na kuokoa wastani wa jumla ya shilingi bilioni 11.46 kwa mwezi. (*Makofi*)

(v) Kukamilisha ujenzi wa mradi mpya wa Kinyerezi II na kuingiza katika Gridi ya Taifa umeme wa megawatt 168 mwezi Aprili, 2018.

(vi) Kukamilika kwa mradi mpya wa Kinyerezi II na ukarabati wa mitambo ya kuzalisha umeme ya Kihansi, Kidatu, Mtera na *New Pangani Falls* kumeongeza uhakika wa upatikanaji umeme katika Gridi ya Taifa na kuwa na ziada ya umeme wa wastani wa megawatt 280 kwa siku na kuondokana na mgao wa umeme.

(vii) Kukamilika kwa ukarabati wa mitambo ya kuzalisha umeme Mtwara pamoja na kuongeza mitambo mipyä miwili mipyä ya uwezo wa megawatt nne na hivyo

kuongeza uhakika wa upatikanaji wa umeme katika Mikoa ya Lindi na Mtwara. (*Makofi*)

(viii) Kukamilika kwa asilimia 100 kwa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kilovoti 132 yenye urefu wa kilomita 80 kutoka Mtwara hadi Mahumbika (Lindi) pamoja na vituo vya kupoza umeme vya Mtwara na Mahumbika.

(ix) Kukamilika kwa asilimia 95 kwa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kilovoti 220 kutoka Makambako hadi Songea.

(x) Kukamilika kwa ujenzi wa vituo vipyta vya kupoza umeme vya Mbagala, Kipawa, Gongolamboto na Mbura hati Mkoani Dar es Salaam. (*Makofi*)

(xi) Kukamilika kwa ujenzi wa vituo vya kupoza umeme vya Njiro, Mount Meru, Sakina, Unga Ltd, *Kilitex* na Thembi Mkoani Arusha. (*Makofi*)

(xii) Kukamilika kwa ujenzi wa vituo vya kupoza umeme vya Bomambazi na *Trade School* vya Kilimanjaro.

(xiii) Kukamilika kwa ukarabati wa vituo vya kupoza umeme vya Mikocheni, Oysterbay, City Centre, Gongolamboto, Kariakoo, Mbagala, Chang'ombe, Kipawa na Ubungo Mkoani Dar es Salaam. (*Makofi*)

(xiv) Kuunganishwa kwa Mikoa ya Lindi na Mtwara katika Gridi ya Taifa kutokana na kukamilisha ujenzi wa njia ya msongo wa kilovoti 33 kutoka Mbagala, Mkuranga, Ikwiriri, Somanga Fungu, Lindi, Nangurukuru, Kiranjeranje, Mtomkavu, Changarawe hadi Mtwara yenye urefu wa kilomita 451. (*Makofi*)

(xv) Kuunganishwa kwa Wilaya za Ngara na Biharamulo katika Gridi ya Taifa kutokana na kukamilika kwa ujenzi wa njia ya msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilomita 70 na hivyo kupunguza gharama za matumizi ya

mafuta kwa wastani wa shilingi bilioni 3.5 kwa mwaka. Pia kukamilika kwa ujenzi wa njia hizi kumewezesha kuunganisha nchi yetu katika Gridi ya Taifa kutoka Mtwara mpakani mwa Msumbiji hadi Ngara mpakani mwa Rwanda na Burundi. (*Makofi*)

(xvi) Kusitisha uingizaji wa vifaa vya ujenzi wa miundombinu ya umeme ikiwemo nguzo, transforma, nyaya na mita za LUKU kutoka nje ya nchi na hivyo kulipunguzia gharama kubwa Shirika la Umeme Nchini (*TANESCO*) na kuokoa wastani wa shilingi bilioni 162.57 kwa mwaka. (*Makofi*)

(xvii) Kuanza maandalizi ya ujenzi na utekelezaji wa mradi mkubwa wa kuzalisha umeme wa maji wa maporomoko ya Mto Rufiji *megawatt* 2,100.

(xviii) Kuunganishiwa umeme wateja wapya 201,046 na kufanya jumla ya wateja waliounganishiwa umeme hadi mwezi Mei, 2018 kufikia 2,226,036 kutoka 2,024,990 mwaka 2016.

(xix) Kukamilika kwa maandalizi ya utekelezaji wa Mradi wa Kusafirisha Mafuta Ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania).

(xx) Kukamilika kwa ujenzi na kuanza kutumika kwa Bandari ya Mtwara kupokea mafuta na hivyo kufanya Tanzania sasa kuwa na Bandari tatu za kupokea mafuta zikiwemo Dar es Salaam na Tanga. (*Makofi*)

(xi) Kuanza utekelezwaji wa mpango wa kusambaza gesi asilia majumbani na katika magari katika Mikoa ya Dar es Salaam na Mtwara. (*Makofi*)

(xxii) Kuongezeka kwa gesi asilia iliyogunduliwa kutoka futi za ujazo trilioni 57.25 mwaka 2016/2017 na kufikia futi za ujazo trilioni 57.54 mwaka 2017/2018 kutokana na ugunduzi wa kitalu cha Ruvuma cha futi za ujazo bilioni 466 kutoka futi za ujazo bilioni 178.

(xxiii) Shirika la Umeme nchini TANESCO, kupitia Kampuni yake Tanzu ya kutengeneza nguzo za zege, imeanza taratibu za manunuza ya nguzo za zege zitakazoanza kutumika mwezi Julai, 2018. Aidha, mafanikio mengine makubwa ni TANESCO imeanza maandalizi ya kujenga njia ya kusafirisha umeme kwa Mkoa wa Kigoma ili kuuingiza Mkoa wa Kigoma katika gridi ya Taifa na kuunganisha na kituo cha kuzalisha umeme cha Urambo, Kaliua na Uvinza. Mradi huu utakamilika mwezi Machi, 2019.

Mheshimiwa Spika, mafaniko hayo yanatokana na utekelezaji thabiti wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2015 - 2020 chini ya uongozi makini wa Serikali ya Awamu ya Tano. Ilani hiyo imejielekeza katika kufikia uchumi wa viwanda ifikapo mwaka 2020 ambapo Sekta ya Nishati ndiyo injini kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mafanikio hayo, naomba sasa nitoe Taarifa ya Mpango wa Bajeti wa Mwaka 2018/2019. Maeneo ya kipaumbele ya Wizara ya Nishati kwa mwaka 2018/2019 ni pamoja na kuongeza uzalishaji wa umeme kwa kutekeleza miradi mikubwa ya kuzalisha umeme ikiwemo mradi wa kuzalisha umeme katika Mto Rufiji wa megawati 2,100 na miradi ya kuzalisha umeme kwa kutumia gesi asilia ya Kinyerezi I - *Extension* ya megawati 185, Somanga Fungu megawati 330 pamoja na Mtware megawati 300; kuimarishe mifumo ya usafirishaji wa umeme mkubwa nchini; kuendelea na utekelezaji wa Awamu ya Tatu ya Mradi Kabambe wa Kusambaza Umeme Vijijini (*REA III*); na kuendelea na utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania). Mambo mengine yatakayotekelezwa ni kuimarishe shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi asilia; kuendeleza miradi ya nishati jadidifu (jotoardhi, upepo na umeme-jua na mambo mengine) na kuendelea kuwajengea uwezo watumishi wa Wizara na taasisi zilizo chini ya Wizara ya Sekta ya Nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya upatikanaji wa umeme nchini. Mahitaji ya umeme nchini yameendelea

kuongezeka kutokana na kukua na kuongezeka kwa shughuli za viwanda na hasa kiuchumi zinazohitaji nishati ya umeme katika uzalishaji. Katika mwaka 2017/2018, uwezo wa mitambo ya kuzalisha umeme umeongezeka kutoka megawati 1,450 mwaka 2016/2017 na kufikia megawati 1,517.47 mwezi Mei, 2018 sawa na ongezeko la asilimia 4.7. Ongezeko hilo limetokana na kukamilika kwa mitambo sita ya kuzalisha umeme ya Kinyerezi II ambayo hadi sasa inazalisha jumla ya megawati 168. Ongezeko hilo limewezesha kuwa na umeme wa ziada wa wastani wa megawati 280 ambapo matumizi ya juu ya umeme yamefikia wastani wa megawati 1,051 kwa siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2018/2019, Serikali itaendelea na utekelezaji wa mradi wa kuzalisha umeme megawati 2,100 kutoka katika Maporomoko ya Mto Rufiji. Kazi zitakazofanyika ni pamoja na ujenzi wa kambi ya ofisi za wafanyakazi; ujenzi wa bwawa (*main dam and spillways*) na ujenzi wa njia kuu za kupitisha maji (*tunnels*). Fedha za maendeleo za ndani shilingi bilioni 700 zimetengwa kwa ajili ya kuanza kutekeleza kazi hizo. Utekelezaji wa shughuli za ujenzi wa mradi unatarajiwa kuanza mwezi Julai, 2018 kwa mkandarasi kuanza kazi za awali kwa miezi mitatu na kufuatiwa na ujenzi wa miundombinu ya mradi huu unaotarajiwa kukamilika katika kipindi cha miezi 36.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na manufaa makubwa ya jumla ya kuongeza uzalishaji wa umeme mwaka 2018 wa megawati 2,100 katika Gridi ya Taifa itaanza baada ya Mradi kukamilika, manufaa mengine ya mradi huu ni pamoja na mambo yafuatayo:-

(i) Kuvutia utalii na hivyo kuongeza fedha za kigeni. Shughuli za majini zitaongezeka kama vile michezo ya majini na visima zaidi ya 10 ndani ya bwawa vitatengenezwa pamoja na mazalia ya samaki, pia mazalia wa mamba wataongezeka, mazalia wa viboko wataongezeka na hivyo kuvutia watalii. Aidha, tuta la kuzuia maji litakalojengwa katika Mradi huu wa Mto Rufiji litakuwa

na urefu sawa na ghorofa 45 kwenda juu na upana wa kilometra moja litakalovutia utalii wa *site seeing* hivyo litawezza kutumika hata katika fungate za maharusi.

(ii) Kutunza maji katika bwawa la mradi yenyewe uwezo wa kumwagilia hekta 250,000 hivyo kukuza shughuli za umwagiliaji.

(iii) Kutoa huduma za kijamii katika maeneo yanayozunguka mradi katika maeneo na vijiji vinavyozunguka mradi ikiwa ni pamoja na kuruhusiwa kufanya uvuvi dhibitivu (*controlled fishing*), hasa samaki watakapoongezeka na kufikia saizi ya kutosha katika bwawa kubwa. Bwawa kubwa litakuwa na kilometra za mraba 914.

(iv) Kusambaza umeme katika vijiji vipatavyo 46 vya jirani katika Wilaya zikiwemo Morogoro Vijijini, Kibiti, Rufiji, Ulanga, Malinyi pamoja na Mlimba. Mradi huu hautaathiri wananchi kwa kuwaondoa au kuwahamisha katika makazi yao. (*Makofi*)

(v) DAWASA wameshaanza kufanya utafiti mahali watakapochukua maji kwa ajili ya matumizi ya majumbani kwa watu wa Mikoa ya Pwani na Dar es Salaam. Katika mikoa hii, maji hayo yatapita katika Vijiji vya Wilaya za Rufiji, Kibiti, Mkuranga, Temeke hadi Kigamboni na hivyo kuingia katika mfumo ya maji wa Jiji la Dar es Salaam. (*Makofi*)

(vi) Mradi utatoa ajira ya watu 10,000 wakati wa ujenzi wa mradi na takriban watu 1,000 wakati wa uendelezaji hasa katika taasisi za maliasilli, ujenzi wa miundombinu ya umeme, ikiwemo pamoja na uvuvi.

(vii) Mradi huu utatoa huduma za kijamii (*Cooperate Social Responsibility – CSR*) kwa kuchangia katika ujenzi wa shule, vituo vya afya na viwanja vya michezo katika wilaya zinazozunguka eneo la mradi ikiwamo Wilaya ya Malinyi, Ulanga, Morogoro Vijijini, Kibiti, Rufiji, Mlimba na maeneo mengine ya jirani. *TANESCO* hutoa takribani shilingi

bilioni 150 kwa mwaka, kati ya hizo shilingi bilion 66 huelekezwa katika *CSR*za miradi ya kuzalisha umeme wa maji.

(viii) Mradi utakapokamilika utazalisha *unit* za umeme kilowati 6,200 kwa siku zitakazouzwa kwa wateja na kuliingizia Shirika la Umeme Nchini *TANESCO* shilingi triliioni 1.6 kwa mwaka.

(ix) Kulingana na usanifu wa mradi huu, mradi unatarajiwa kudumu kwa zaidi ya miaka 80 toka utakapokamilika na kuanza kutumika ambapo miradi mingine ya Kihansi, Mtera inaonesha uhai wake ni angalau miaka 50.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mpango wa Kutunza Mazingira, *TANESCO* itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kutunza mazingira kwa ajili ya athari za kijamii zinazoweza kutokea kutokana na shughuli za mradi huu kama ambavyo itaaishwa katika Ripoti ya Mazingira (*Environmental Impact Assessment*) ambayo itazalisha mpango mkakati na hatua za juu ya namna ya kutunza mazingira na kuhakikisha kwamba utunzaji wa mazingira unakuwa endelevu. Jambo hili linakamilishwa pia na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira ambapo wakati wowote *EIA certificate* itaweza kutolewa. Aidha, *TANESCO* hutoa fedha takribani shilingi milioni 436 kwa mwaka kwa ajili ya utunzaji wa mazingira katika miradi ya kuzalisha umeme wa maji. Utaratibu huu upo pia katika miradi ya Kihansi wenye vyura adimu duniani ambapo *TANESCO* huchangia wastani milioni 200 kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miradi wa *Kinyerezi Extension*. Kazi zilizofanyika katika mradi huu kwa mwaka 2017/18 ni pamoa na kukamilisha ujenzi wa misingi ya kusimika mitambo ya kuzalisha umeme na transfoma; ujenzi wa misingi ya kituo cha kupoza umeme; na ujenzi wa njia ya msongo wa kilovoti 220 inayounganisha mtambo wa *Kinyerezi / Extension* na *Kinyerezi II* na kuunganishwa katika Gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2018/2019 kazi ya usimikaji wa mitambo pamoja na ukamilishaji wa ujenzi wa kituo cha kupoza umeme zitafanya kwa gharama ya shilingi bilioni 164, zikiwa ni fedha za ndani. Ujenzi wa mradi ulianza mwezi Novemba, 2016 na unatarajija kukamilika mwezi Januari, 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Mradi wa Rufiji – megawati 2,100. Lengo la kutekeleza mradi huu ni kuzalisha umeme wa jumla ya megawati 2,100 kwa kutumia maji (*Hydro Power Plant*) katika Bonde la Mto Rufiji. Utekelezwaji wa mradi huu mkubwa nchini ni kichocheo muhimu katika kuwezesha Tanzania kufikia azma yake ya kuwa nchi ya uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025. Katika kipindi cha mwaka 2017/2018 hatua iliyofikiwa ni pamoja na kufanya uchambuzi wa zabuni (*tender evaluation*) zilizowasilishwa na wakandarasi wallooniesha nia ya kutekeleza mradi huu. Aidha, ujenzi wa njia ya msongo wa kilovoti 33 kutoka eneo la Dakawa kwa ajili ya kupeleka umeme utakaotumiwa na mkandarasi wakati wa ujenzi wa mradi ulianza mwezi Novemba, 2017 na unatarajija kukamilika Julai, 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Kinyerezi II – megawati 240. Uzalishaji umeme katika mradi huu ulizinduliwa rasmi na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, tarehe 03 Aprili, 2018. Hadi sasa mitambo sita ya *gas turbines* imefungwa na inazalisha umeme wa jumla ya megawati 168 zilizoingizwa katika Gridi ya Taifa. Ufungaji wa mitambo miwili yenye uwezo wa kuzalisha megawati 80.4 kwa kutumia mvuke (*steam turbines*) unatarajija kukamilika mwezi Juni, 2018. Shughuli zote hizi za mradi zinatarajija kukamilika ifikapo mwezi Septemba, 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Somanga Fungu. Mradi huu unahu ujenzi wa mitambo ya kuzalisha umeme wa megawati 330 kwa kutumia gesi asilia katika eneo la Somanga Fungu, Mkoani Lindi. Aidha, mradi huu unahu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa kilovoti 400 umbali wa kilomita 198.2 kutoka Somanga Fungu hadi Kinyerezi.

Upembuzi yakinifu wa mradi umekamilika na taratibu za kumpata mkandarasi mwenye uwezo wa kitaalam na fedha kwa kushindanishwa chini ya utaratibu wa *EPC plus Financing* zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2018/2019, kazi zilizopangwa kufanyika ni pamoja na: Kukamilisha taratibu za kumpata mkandarasi na fedha za kutekeleza mradi; kumpata Mshauri Mwelekezi wa usimamizi wa mradi; na kuanza utekelezaji wa mradi. Jumla ya shilingi bilioni 4.5 fedha za ndani na fedha za nje zimetengwa ili kutekeleza kazi hizo. Ujenzi wa mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Septemba, 2018 na kukamilika ifikapo mwezi Septemba, 2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Mtwara – megawati 300. Mradi huu unahu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa megawati 300 kwa kutumia gesi asilia Mkoani Mtwara. Mradi utahusu pia ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa kilovoti 400 umbali wa kilometra 253 kutoka Mtwara hadi Somanga Fungu. Utekelezaji wa mradi huu utaimarisha upatikanaji wa umeme katika Mikoa ya Lindi na Mtwara. Katika mwaka 2017/2018, kazi zilizotekelawa ni pamoja na kuanza upembuzi yakinifu chini ya ufadhili wa JICA mwezi Julai, 2017 ambao unatarajiwa kukamilika mwezi Agosti, 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2018/2019, kazi zilizopangwa kufanyika ni pamoja na kukamilisha upembuzi yakinifu wa mradi; kumtafuta Mshauri Mwelekezi; na kumpata Mkandarasi. Jumla ya shilingi bilioni 3.7 zinakadiriwa kutumika kuwalipa fidia wananchi watakaopisha mradi. Aidha, katika mwaka 2018/2019 fedha za nje shilingi bilioni 4 zimetengwa ili kutekeleza shughuli za mradi huu. Ujenzi wa mradi unatarajiwa kuanza mwezi Novemba, 2018 na kukamilika mwezi Juni, 2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi mingine mikubwa ya kuzalisha umeme. Miradi mingine ya kuzalisha umeme iliyopo katika hatua mbalimbali za utekelezaji ni pamoja na Mradi wa Kakono – megawati 87; Mradi wa Rusumo – megawati

80; Mradi wa Murongo/Kikagati – megawati 14; Mradi wa Malagarasi – megawati 45; Mradi wa Ruhuji – megawati 358; Miradi ya Kinyerezi III – megawati 600; Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa kutumia Makaa ya Mawe Kiwira – megawati 200; Mradi wa Umeme Unaotokana na Nishati ya Jua katika Mkoa wa Shinyanga – megawati 150; Mradi wa Umeme wa Upopo Singida – megawati 100; na Miradi ya Kuzalisha Umeme kutokana na Nishati Jadidifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa njia za kusafirisha umeme. Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme, kazi zilizotekelezwa katika mradi huu kwa kipindi cha mwaka 2017/18, kwa upande wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kilovoti 220, ni kukamilika kwa usanifu, utengenezaji, usafirishaji wa vifaa na ujenzi wa misingi ya nguzo. Kwa upande wa ujenzi wa vituo vya kupoza umeme maeneo yaliyokamilishwa ni pamoja na Makambako, Madaba na Songea, usafirishaji wa vifaa na ujenzi wa misingi umekamilika. Hadi kufikia mwezi Mei, 2018 ujenzi wa miundombinu ya usambazaji umeme kwenye vijiji 32 kati ya 120 umekamilika na jumla ya wateja 1,500 kati ya 22,000 wameunganishiwa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla hadi kufikia mwezi Mei, 2018 ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme kilovoti 220 kutoka Makambako – Songea umefikia asilimia 95; ujenzi wa Vituo viwilli vipyta vya Kupoza Umeme vya Madaba na Songea umefikia asilimia 76; na usambazaji umeme umefika asilimia 68.5 kwa Mikoa ya Ruvuma na Njombe. Kazi zitakazofanyika mwaka 2018/2019 ni kukamilisha ujenzi wa vituo vya kupoza umeme; ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 220; na uunganishaji wa wateja. Jumla ya shilingi bilioni 13 zimetengwa katika mwaka 2018/2019 ili kutekeleza kazi hizo. Aidha, kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 7 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 6 ni fedha za nje. Mradi huu ulianza mwezi Desemba, 2016 na unatarajiwा kukamilika mwezi Septemba, 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya kusafirisha umeme. Kazi zilizofanyika katika mradi huu kwa kipindi cha mwaka

2017/2018 ni pamoja na mkandarasi kufanya *detailed survey* ya njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 400 kutoka Singida hadi Namanga; kufanya usanifu wa majaribio ya nguzo na vifaa vingine vitakavyotumika katika ujenzi. Aidha, kufanya utafiti wa udongo katika njia ya umeme lakini pia Serikali kukamilisha uhakiki wa malipo ya fidia kwa wananchi watakaopisha mradi. Jumla ya shilingi bilioni 68.31 zinakadirwa kutumika kuwalipa wananchi fidia. Vilevile, taratibu za kumpata mkandarasi atakayesambaza umeme katika vijiji 21 vinavyopitiwa na mradi huu zinaendelea. Kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 wananchi watakaopisha ujenzi wa mradi watalipwa fidia zao kati ya mwezi Mei na Juni, 2018 na wakandarasi kuendelea na shughuli za ujenzi wa mradi. Jumla ya shilingi bilioni 15 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza kazi hizo. Utekelezaji wa mradi huu ulianza mwezi Machi, 2017 na unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi mingine ya kusafirisha umeme. Miradi mingine ya kusafirisha umeme iliyopo katika hatua mbalimbali za utekelezaji ni pamoja na: Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa *kV 400* kutoka Rufiji – Chalinze – Dodoma yenye urefu wa kilomita 512; mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa kilovoti 400 kutoka Somanga Fungu – Kinyerezi yenye urefu wa kilomita 198; Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa kilovoti 400 kutoka Iringa – Mbeya – Tunduma – Sumbawanga – Mpanda – Kigoma – Nyakanazi, mradi huu una urefu wa kilomita 1,372 na mradi wa Njia ya Umeme wa Msongo wa kilovoti 220 kutoka Bulyanhulu – Geita wenye urefu wa kilomita 55.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Njia ya Umeme wa Msongo wa kilovoti 220 na kutoka Geita – Nyakanazi wenye urefu wa kilometra 133; Mradi wa Njia za Kusafirisha Umeme wa Msongo wa kilovoti 400 na kilovoti 220 wa *North – East Grid*; lakini pia Msongo wa kilovoti 400 kutoka Mtwara - Somanga Fungu wenye urefu wa kilometra 253; mradi wa Njia ya Umeme wa Msongo wa kilovoti 220 kutoka Rusumo – Nyakanazi yenye urefu wa kilometra 98.2; na Mradi wa Njia

ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa kilovoti 400 kutoka Masaka (Uganda) hadi Mwanza (Tanzania).

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi mingine ya kusambaza umeme vijiji. Katika mwaka 2017/2018, Serikali kupitia Wakala wa umeme Vijiji (*REA*) imeendelea kukamilisha utekelezaji wa Mradi Kabambe wa Kusambaza Umeme Vijiji Awamu ya II (*REA II*) kwa kumalizia kazi na kuongeza kazi kwa vijiji vilivyorukwa na kuwaunganisha wateja. Hadi kufikia Desemba, 2017 mradi huo ulikuwa umekamilika kwa asilimia 99 kwa kufikisha miundombinu ya umeme katika vijiji 2,598 kati ya 2,697 sawa na asilimia 96.3 na hivyo kuwezesha kuwaunganishia umeme jumla ya wateja 178,641 ambao ni sawa na asilimia 71.46 ya matarajio ya awali ya wateja 250,000. Zoezi la kuunganisha wateja ni endelevu kulingana na wateja wanavyolipia na hivyo kazi zinaendelea kufanywa na Shirika la Umeme Nchini (*TANESCO*). Uunganishwaji wa wateja hao umechangia ongezeko la upatikanaji wa huduma za umeme vijiji (*accessibility*). Hivi sasa upelekaji wa umeme vijiji umefikia asilimia 49.5 mwaka 2017 kutoka asilimia 20.23 mwaka 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa mradi huu uliokuwa umesimama katika Mikoa ya Kilimanjaro na Singida kutokana na Mkandarasi wa awali, Kampuni ya *Spencon Services Ltd* kushindwa kuukamilisha kazi hizo, sasa kazi hizo zinaendelea. Mradi huo unatekelezwa na Kampuni za Kitanzania za *Njarita Contractors* na *Octopus* kwa Mkoa wa Kilimanjaro pamoja na *Dynamic Services* kwa Mkoa wa Singida. Kazi zitakazofanyika katika mwaka 2018/2019 ni kukamilisha mradi katika Mikoa ya Kilimanjaro na Singida; kumalizia marekebisho madogomadogo (*snags*) yaliyojitokeza wakati wa ujenzi. *TANESCO* itaendelea kuwaunganisha wateja kadri wanavyolipia. Mradi katika Mikoa hii ya Kilimanjaro na Singida unatarajiwa kukamilika mwezi Agosti 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi Kabambe wa Usambazaji Umeme Vijiji *Turnkey III*, REA Awamu ya Tatu. Mradi wa Kusambaza Umeme Vijiji Awamu ya Tatu

unalenga kufikisha umeme katika vijiji 7,873 ambavyo hadi kufikia mwezi Juni, 2016 vilikuwa havijafikishiwa miundombinu ya umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika kipindi cha kuanzia mwezi Februari hadi Mei, 2018 jumla ya vijiji 545 kati ya 7,873 vilivyobaki tayari vimeunganishiwa umeme na hivyo kubaki vijiji 7,328 vinavyoendelea kuunganishiwa umeme hivi sasa. Kazi zinazofanyika ni pamoja na kujenga miundombinu ya kusambaza umeme na kufunga transfoma katika maeneo mbalimbali ikiwemo taasisi za umma, miradi ya maji na shughuli nyingine za kiuchumi. Hata hivyo, mradi huu unalenga kufikisha umeme katika vitongoji vya vijiji vyote hapa nchini, ambavyo pia havijafikiwa na miundombinu ya umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha mradi huu unapitia pia katika mradi wa *Densification* ambapo unapeleka umeme katika vitongoji ambavyo havijafikishiwa umeme katika miradi iliyotanguliwa. Kazi zingine zinazofanyika ni pamoja na ujenzi miundombinu ya usambazaji na ufungaji wa transfoma pamoja na kuunganisha wateja katika Gridi ya Taifa. Hadi sasa yapo maeneo ambayo yapo kwenye visiwa na katika maeneo ya bahari ambapo vitapelekewa umeme kwa mpango wa *solar*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa mradi huu upo katika Awamu Tatu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, awamu ya kwanza ni Mradi wa Usambazaji Umeme katika Maeneo ambayo yamefikiwa na Miundombinu ya Umeme (*Densification*). Mradi huu unahusisha kuongeza wigo wa usambazaji umeme katika vijiji, vitongoji na maeneo ambayo yana miundombinu ya umeme lakini yamerukwa katika vijiji vitongoji vyake. Katika mradi huu jumla ya vijiji 4,395 vimeshawashwa umeme na kuunganisha wateja. Mradi utatekelezwa katika mikoa yote ya Tanzania Bara na utahusisha ujenzi wa kilomita 18,625 za umeme wa msongo wa KV 33; lakini kilomita 35,614 za msongo wa KV 0.4; pamoja na ufungaji wa transfoma 13,622. Pamoja na kazi hizo,

kazi zitakazofanyika ni kuunganishaji wateja wa awali 992,373 kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2016/2017 hadi mwaka 2020/2021. Malengo ya kuunganisha wateja ni 300,000 katika utekelezaji wa mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu unatekelezwa kwa awamu ambapo Awamu ya Kwanza yaani (*Densification – Round I*) ilianza mwezi Aprili, 2017 katika Mikoa nane ya Pwani, Tanga, Arusha, Iringa, Njombe, Mbeya, Songwe na Mara na hadi kufikia mwezi Mei, 2018 imekamilika kwa asilimia 98. Katika Awamu hii jumla ya vijiji 300,000 kati ya vijiji 350,000 sawa na asilimia 98.3 vimepatiwa umeme pamoja na kuunganishiwa umeme wateja 12,084. Aidha, kati ya wateja hao wateja waliolengwa kuunganishwa ni 53,000. Gharama ya utekelezaji wa miradi hii ni shilingi bilioni 62. Aidha, Mradi wa *Densification – Round II* utahusisha vitongoji vilivyomo katika vijiji 4,090 vilivyosalia ambavyo vinakadiriwa kugharimu jumla ya shilingi bilioni 1,938. Awamu hii itaanza kutekelezwa mwezi Julai, 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Kusambaza Umeme Vijiini Awamu ya III (*Grid Extension*). Mradi huu unatekelezwa katika vijiji 3,553 kwa Mikoa yote ya Tanzania Bara na unahusisha ujenzi wa takriban kilomita 15,600. Hii ni pamoja na kujenga miundombinu ya KV 33,000; pamoja na kilomita 16,420 za njia ya msongo wa Kilometra 16,420 wa KV 0.4; na ufungaji wa transfoma 6,740. Mradi huu unatarajia kuunganishaji wateja wa awali 300,000. Aidha, maombi ya vijiji 1,541 vilivyorukwa yamepelekwa katika hatua za kupitishwa ili itakaporidhiwa kupitia Bunge lako Tukufu basi marekebisho yaweze kufanyika na kuongeza vijiji hivi ili kufanya upelekaji umeme vijiini kukamilika. Ongezeko hilo litafanya jumla ya vijiji vitakavyopelekewa umeme katika Mzunguko huu wa Kwanza kufikia 5,100 na kubaki na vijiji 2,773 vitakavyofikishiwa umeme katika Mzunguko wa Pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi huu wa REA Awamu ya Tatu, mzunguko wa pili utaanza mwezi Julai, 2019 na kukamilika 2020/2021. Hivyo kupelekea sasa vijiji vyote vya Tanzania Bara kufikiwa na miundombinu ya umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi Mei, 2018 katika kipindi cha miezi mitatu (3) ya ujenzi baada ya kukamilika kwa kipindi cha miezi mitatu (3) ya uhakiki wa vijiji na miezi mitatu (3) mingine ya uingizaji wa vifaa na maandalizi ya ujenzi, jumla ya vijiji 502 vimejengwa miundombinu ya umeme ikiwa ni pamoja na kusimikwa nguzo na kufungwa transfoma katika Mikoa yote ya Tanzania Bara isipokuwa Mikoa ya Kigoma na Katavi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa taarifa katika Bunge lako Tukufu kuwa Mkandarasi *M/s CCCE - ETERN-HEI Consortium* aliyePATIKANA kwa ajili ya kutekeleza mradi wa REA Awamu ya III katika vijiji vilivyobaki kwa Mkoa wa Kigoma ataanza kazi rasmi tarehe 1 Juni, 2018 yaani mwaka huu baada ya taratibu zote kukamilika. Kwa upande wa Mkoa wa Katavi taratibu za kumpata mkandarasi zitakamilika iflikapo tarehe 15 Juni, 2018. Shughuli za utekelezaji wa mradi wa REA III katika Mkoa wa Katavi pia zitaanza mwezi Juni mara baada ya mkandarasi kupatikana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji 502 vilivyotajwa hapo juu vinatarajiwa kuwashwa umeme hivi karibuni. Mbali na vijiji hivyo vilivyojengwa miundombinu hadi kufikia Mei 2018 yaani mwaka huu, vijiji vingine 545 vimewashwa umeme sawa na vijiji 182 kwa wastani ambao ni asilimia 92 ya lengo la kuwashwa umeme vijiji 197 kwa mwezi. Pia, katika vijiji vilivyowashwa umeme wateja 15,073 wameunganishwa umeme sawa na asilimia 90 ya lengo la kuwaunganishia umeme wananchi yaani wateja 16,666 kwa mwezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miradi ya Kusambaza Umeme katika maeneo ya pembezoni. Mradi huu unahusisha usambazaji wa umeme katika vijiji 121 vilivyopo pembezoni mwa mkuza wa Mradi wa kusafirisha umeme wa msongo wa KV 400 kutoka Iringa hadi Shinyanga. Katika mradi huu, wateja 25,000 wa awali wanatarajiwa kuunganishiwa umeme. Mradi huu pia unahusisha upanuzi wa kituo cha kupoza umeme cha Mtera. Hadi kufikia Mei, 2018, jumla ya vijiji 25 vimefikiwa na kuunganishiwa umeme ambapo wateja 861 pia wameunganishiwa umeme. Kwa upande wa upanuzi wa

kituo cha kupoza umeme cha Mtera usanifu unatarajiwa kukamilika ndani ya mwezi wa Mei, yaani mwezi huu 2018. Shughuli za ujenzi wa kituo zitaanza Julai, 2018 na kukamilika Machi, 2019. Mradi huu utagharimu Shilingi bilioni 57 ambazo ni msaada kutoka Serikali za Sweden na Norway.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uendelezaji wa Nishati Jadidifu (*Off-Grid Renewable Projects*). Mradi wa Uendelezaji wa Nishati Jadidifu umegawanyika katika makundi mawili ambapo Kundila Kwanza linahusisha usambazaji wa umeme vijiji ni kwa maeneo yaliyopo nje ya gridi kwa mfumo wa Malipo kwa Matokeo yaani (*Results Based Financing Project*). Katika Kundila hili, mikataba ya miradi 22 yenye uwezo wa kuzalisha jumla ya MW 24.2 zitasambazwa katika vijiji 139 na kuunganisha wateja 33,939 ambayo pia imeshasainiwa na waendelezaji wako tayari kuanza kazi. Maeneo hayo ni pamoja na maeneo ya Mikoa ya Iringa, Njombe, Tanga, Dodoma, Singida, Lindi, Mtwara, Tabora, Mwanza, Geita pamoja na Kagera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kundila Pili la Mradi huu linahusu kufunga mifumo ya umeme-juu yaani (*solar PV systems*) katika Taasisi za Umma zikiwemo shule za sekondari, vituo vya afya, zahanati zilizopo mbali na maeneo ya mradi pamoja na maeneo ya masoko. Aidha, mradi huu utaenda katika maeneo ya taasisi ambazo pia ziko mbali na eneo la Gridi. Mradi unatekelezwa katika Wilaya nane (8) za Biharamulo, Bukombe, Chato, Sikonge, Kasulu, Kibondo, Tunduru pamoja na Namtumbo. Hadi kufikia Mei, 2018 utekelezaji wa mradi ulifikia asilimia 92 na unatarajiwa kukamilika Juni, 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Usambazaji Umeme katika Vijiji vilivyopo Pembezoni mwa Miji yaani (*Peri-Urban Electrification Program*). Mradi huu unalenga kusambaza umeme katika vijiji vilivyopo pembezoni mwa miji ili kuboresha huduma za kijamii na kuhamasisha ujenzi wa viwanda vidogo. Aidha, Wakala wa Nishati Vijiji umekamilisha usanifu wa mradi wa majaribio utakaotekelzwa katika Mikoa wa Pwani kwa Wilaya ya Kigamboni na Mkoani Dar es Salaam. Mradi

huu utavinufaisha vijiji na vitongoji takribani 250 na kuwaunga wateja wa awali 37,000. Mradi huu unafadhiliwa na Serikali ya Norway kwa gharama ya shilingi billioni 83. Mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Aprili, 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Aprili, 2018, *REA* ilikuwa imepokea jumla ya shilingi billioni 313.5 kati ya shilingi billioni 469 zilizopangwa kwa mwaka 2017/2018, hii ni sawa na asilimia 67 ya bajeti. Aidha, katika mwaka wa fedha 2018 fedha zilizotengwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya Usambazaji Umeme Vijijini ni jumla ya shilingi billioni 412.08. Kati ya fedha hizo, shilingi billioni 375.38 ni fedha za ndani na shilingi billioni 36.70 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ndogo ya mafuta na gesi asilia. Kazi za utafutaji wa mafuta na gesi asilia zinaendelea ambapo jumla ya kampuni nane (8) zinafanya utafutaji wa mafuta na gesi asilia kuititia mikataba kumi na moja (11) ya Uzalishaji na Ugawanaji Mapato (*Production Sharing Agreement*). Mwaka 2017/2018 uhakiki wa gesi asilia uliofanywa na (*TPDC*) kwa kushirikiana na Kampuni ya Ndovu Resources umeongeza kiasi cha gesi asilia kufikia futi za ujazo billioni 466 kutoka futi za ujazo billioni 178 mwaka 2016/2017 katika kitalu cha Ruvuma. Hadi kufikia sasa kiasi cha gesi asilia kilichogunduliwa nchini ni futi za ujazo triliioni 57.54.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni za *Heritage Rukwa Tanzania Limited* na Swala Oil na Gesi Tanzania zinaendelea na maandalizi ya kuchoronga visima vya utafutaji mafuta katika vitalu vya Rukwa Kusini pamoja na Kilosa-Kilombero sawia. Aidha, Kampuni ya *Ndovu Resources* imeendelea na maandalizi ya Mpango wa Uendelezaji wa gesi asilia iliyo gunduliwa katika eneo la Ntorya - Mtwara. Vilevile, Kampuni ya Dodsal Hydrocarbons imeendelea na uchukuaji wa *data* za mitetemo (*seismic data*) katika Kitalu cha Ruvu ili kuhakiki ukubwa wa mashapo ya gesi asilia iliyo gunduliwa hivi karibuni. Kwa upande mwingine, Kampuni ya *Pan African Energy* na *Maurel et Prom* zimeendelea na uzalishaji wa gesi asilia katika Vitalu vya Songo Songo na Mnazi Bay kwa wastani wa futi za ujazo milioni 95 na milioni 80 kwa siku sawia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2017/2018, *TPDC* imepitia na kuhakiki michoro (*Design Drawings*) ya awali iliyowasilishwa na mkandarasi kwa ajili ya kuunganisha gesi asilia katika viwanda vya *Lodhia Steel*, *Knauf Gypsum* na *Bakhressa Food Products* vilivyoko Mkuranga. Mkandarasi wa ujenzi wa bomba la kusambaza gesi asilia katika viwanda vya *Coca-Cola Kwanza Limited* na *BIDCO Industry* vilivyoko eneo hilo bado wanaendelea na kazi hiyo na imeanza Aprili, 2018. Awamu ya kwanza ya ujenzi wa miundombinu ya kupeleka gesi asilia katika viwanda vya *Dangote Cement* Tanzania Limited kilichopo Mtwara ilikamilika Septemba, 2017. Hivi sasa Kampuni ya Dangote inaendelea na maandalizi ya awali ya utumiaji wa gesi asilia (*Testing and Commissioning*). Napenda kutumia nafasi hii kuiagiza kampuni ya Dangote kuanza kutumia gesi kuanzia sasa kwa sababu maandalizi ya kupelekewa gesi yameshakamilika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2018/2019, *TPDC* itakamilisha majadiliano na kuingia mikataba ya kusambaza gesi asilia katika kiwanda cha *Knauf Gypsum* kilichopo Mkuranga Mkoani Pwani. Vilevile, *TPDC* itafanya majadiliano na wateja wapya wa viwanda walioonesha nia ya kuunganishiwa gesi asilia wakiwemo *LN Future Building Materials* pamoja na *Kings Alluminium* ya Mkuranga-Pwani pamoja na MM-1 *Intergrated Steel* kilichopo Mikocheni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usambazaji wa gesi majumbani. Hadi sasa jumla ya nyumba 70 zilizopo maeneo ya Mikocheni, Dar es Salaam ziliunganishwa na miundombinu ya gesi asilia. Katika mwaka 2017/2018, miundombinu ya kuunganisha gesi asilia majumbani imeanza kutandazwa katika Jiji la Dar es Salaam. Maeneo yanayoanza kupelekewa gesi majumbani kupitia Mradi huu ambaao umeanza mwezi Aprili, 2018 ni pamoja na Ubungo, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Mlalakua, Makongo Juu, Changanyikeni, Survey, Sinza, Shekilango, Mwenge, Viwanda vya Coca Cola, maeneo ya Mikocheni pamoja na Manzese. Mradi huu ni endelevu kutegemeana na mahitaji yatakavyokuwa yanajitokeza katika maeneo husika. Zaidi ya wateja wa awali

1,000 wanatarajiwa kufikiwa na mradi huu na kuanza kutumia gesi majumbani kuanzia mwezi uliopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi mwingine unaofanyiwa maandalizi utakaoteklezwa na mradi huu katika Mkoa wa Mtwara ambapo usambazaji wa gesi asilia majumbani utaanza katika maeneo Magereza, Magomeni, Ufukoni, Ligula, Hospitali Kuu ya Mkoa, Chuo cha Ualimu katika Manispaa ya Mtwara, Mtwara Girls pamoja na VETA. Kazi inayofanyika kwa sasa ni ukamilishaji wa taratibu za kuunganisha bomba lenye msukumo mdogo (*low pressure*) kwa ajili ya kupeleka gesi majumbani kwa wananchi wa Mtwara. Kazi hizi zinakamiliika Juni, 2018 na kazi ya usambazaji wa gesi asilia itaanza mwanzoni mwa Julai, 2018 ambapo wateja wa awali wanatarajiwa kuwa zaidi ya 580. Kazi hii itakuwa endelevu na itafanywa na GASCO (kampuni Tanzu ya TPDC).

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengine yataendelea kusambaziwa gesi asilia baadaye ikiwemo ni pamoja na Mikoa ya Mtwara na Lindi itaanza pia katika Mikoa ya pembezoni pamoja na mikoa mengine kwa Tanzania Bara. Mradi huu utaanza kutekelezwa Julai, 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bei ya gesi majumbani. Bei ya gesi majumbani itakuwa na punguzo la asilimia 40 ya bei za mtungi wa gesi wa kawaida inayouzwa hivi sasa kutoka nchini za nje. Hivyo basi, bei katika mtungi ambao gharama yake ni 55,000 kwa sasa itakuwa takribani Sh.25,000 hadi Sh.30,000. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2018/2019, *TPDC* inatarajia kuweka miundombinu itakayowezesha zaidi ya nyumba 2,000 kuunganishiwa gesi asilia pamoja na kusambaza gesi asilia katika Migahawa ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Soko la Feri Jijini Dar es Salaam, Kampuni ya Usimamizi wa Mabasi ya Dar es Salaam (*UDART*) pamoja na maeneo ya Kigamboni. Ili kuwezesha unganishwaji wa wateja hao, uchambuzi wa kifedha pamoja na Tathmini ya Athari

za Mazingira (*Environmental and Social Impact Assessment-ES/A*) utaendelea kufanyika. Fedha za ndani za *TPDC* shilingi bilioni 20.9 zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuchakata na kusindika gesi asilia. Mradi wa *LNG* unalenga kusindika gesi asilia iliyogunduliwa katika kina kirefu cha Bandari ili iweze kutumika ndani na kusafirishwa kuuzwa nje ya nchi. Katika mwaka 2017/2018 kazi zilizofanyika ni pamoja na marudio ya ukamilishaji wa tathmini ya eneo pamoja na kukamilisha utafiti wa kihandisi. Maeneo mengine ni kufanya majadiliano (*HGA*) kati ya Serikali na wawekezaji. Katika mwaka 2018/2019, kazi itazotekelawa ni pamoja na Usanifu wa Awali yaani (*Pre-FEED*) kwa ajili ya ujenzi wa *LNG*. *HGA* inaendelea kujadiliwa na itaenda kukamilika mwisho wa mwaka ujao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, falda zinazotarajiwa kutokana na mradi huo ni pamoja na kuongezeka kwa mapato ya Serikali kupitia mauzo ya gesi asilia katika soko la kimataifa; upatikanaji wa nishati ya uhakika kwa ajili ya matumizi ya ndani na kusafirisha nje; upatikanaji wa ajira kwa wazawa; ukuaji wa Miji ya Lindi na Mtwara ikiwa ni pamoja na upanuzi wa bandari na uwanja wa ndege; na upatikanaji wa malighafi wa viwanda kama vile mbolea, plastiki pamoja na *petrochemicals*. Fedha za ndani shilingi bilioni 6.5 zimetengwa kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kwa ajili ya kazi hizo za ujenzi wa mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bomba la kusafirisha mafuta ghafi. Hatua za awali za utekelezaji wa mradi huu zilianza Januari, 2018. Kazi zilizotekelawa kwa upande wa Tanzania ni pamoja na Usanifu wa Kihandisi wa Mradi wa FEED pamoja na kuridhiwa kwa Mkataba wa *Intergovernmental Agreement (IGA)*. Pia Wabunge waliridhia mkataba wa IGA kati ya Serikali ya Tanzania na Uganda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi zingine zinazofanyika ni pamoja na utafiti wa *Geological, Geotechnical* pamoja na kazi zingine za kihandisi. Hivi sasa majadiliano ya *HGA* nayo yanaendelea ambayo yatakamilika mwezi Mei, 2018. Kazi

zilizopangwa kutekelezwa wa mwaka 2018 ni pamoja na kukamilisha majadiliano HGA na SHA; kukamilisha usanifu wa kina kihandisi lakini kuwalipa fidia wananchi watakaopisha mradi pamoja na kazi nyingine za usanifu. Kiasi cha shilingi bilioni 54.2 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bomba hili la mafuta litapita katika vijiji 180, Wilaya 24 na Mikoa minane ya Kagera, Geita Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara na hatimaye Tanga. Ujenzi wa mradi huu unatajiwa kuanza mwezi Juni, 2018 na kukamilika mwaka 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mafanikio yaliyopatikana kwa kuanza kutumika kwa Bandari ya Tanga kupokea mafuta kwa ajili ya matumizi ya Mikoa wa Tanga, Kilimanjaro na Arusha, hivi sasa Serikali itaanza kutumia Bandari ya Mtwara kupokea mafuta kwa ajili ya matumizi ya Mikoa ya Lindi na Mtwara. Maeneo mengine yatakayonufaika na mradi huu ni pamoja na Ruvuma Njombe, Songwe, Rukwa pamoja na Katavi. Bandari ya Mtwara itaanza rasmi kupokea mafuta kwa kutumia mfumo wa uigizaji kwa pamoja mwezi Juni, 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, meli ya kwanza itaanza kushusha mafuta tani 10,000 ya petroli na dizeli ambapo miundombinu iliyopo kwa sasa ina uwezo wa kutunza mafuta lita milioni 26. Aidha, mahitaji ya mafuta kwa mikoa ya Ukanda huo kwa sasa ni lita milioni 12 hadi 15 tu. Utaratibu wa kupanga bei ya mafuta yatakayoingizwa kuititia Bandari ya Mtwara utazingatia pia utaratibu unaotumika katika Bandari ya Tanga. Kutokana na sababu hiyo, wananchi wa Mtwara na mikoa jirani wataanza kununua mafuta kwa bei ya chini sawa na Dar es Salaam. Hata hivyo, kutokana na kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi katika maeneo hayo, Serikali inawakaribisha wawekezaji waje kuwekeza zaidi katika Mikoa ya Lindi na Mtwara kwa sababu upatikanaji na usuhajji wa mafuta unapatikana katika ukanda huo. Kuanza kutumika kwa Bandari ya Mtwara katika kupakua mafuta, kumeifanya Tanzania kuwa na Bandari tatu za kushusha mafuta kwa

mfumo wa kuagiza kwa pamoja ambazo ni Dar es Salaam, Tanga pamoja na Mtwara zenyewe uwezo wa kupakua mafuta jumla ya litu milioni 300 hadi milioni 450 kwa siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo ya rasilimali. Katika kuongeza tija na motisha kwa watumishi wa Wizara, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara iliwapandisha madaraja jumla ya watumishi 10 katika kada mbalimbali. Katika kipindi cha mwaka 2018/2019, Wizara inatarajia kuwapandisha madaraja watumishi 100 ambaao wamepata sifa za kitaaluma na wenye utendaji mzuri wa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Wizara pamoja na taasisi zake inatarajia kuajiri jumla ya watumishi 207 katika kada mbalimbali. Kati ya watumishi hao, watumishi 43 wataajiriwa na Wizara, 116 *TPDC* na 48 *PURA*. Kwa mwaka 2017/2018, watumishi 16 walihudhuria mafunzo ya muda mrefu nje ya nchi. Kadhalika Watanzania 22 walipata ufadhili wa masomo nchini China. Katika mwaka 2018/2019, watanzania 22 watapatiwa ufadhili wa masomo kutoka Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhusiano wa Kimataifa. Kwa niaba ya Serikali, napenda kutambua mchango wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB*), Benki ya Dunia, Exim Bank, Benki ya Ushirikiano wa Japan, Benki ya *Unicredit*, *Economic Development Fund*, Mfuko wa Uendelezaji wa Geothermal, *GRMF*, *JICA*, Ufaransa, Norway, Uingereza, *SIDA*, Umoja wa Ulaya, *USAID* (Marekani). Kwa kipindi cha mwaka 2018/2019 Serikali kupitia Wizara ya Nishati itaendelea kushirikiana na washirika hawa pamoja na wengine katika uendelezaji wa sekta hii muhimu kwa ukuaji wa uchumi wa nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani. Kipekee namshukuru kwa dharti Mheshimiwa Subira Khamis Mgusu, Mbunge wa Viti Maalum na Naibu Waziri wa Nishati kwa namna anavyonisaidia katika kusimamia Sekta hii ya Nishati. Hakika tangu ameteuliwa kuwa Naibu Waziri wangu amekuwa na mchango mkubwa katika kusimamia sekta hii

ambayo ina mchango mkubwa sana katika ukuaji wa uchumi wa nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi bora wa sekta hii nchini unategemea sana ushirikiano unaotolewa na watendaji mbalimbali wa Wizara. Hivyo basi, naomba nitumie nafasi hii kumshukuru sana Katibu Mkuu wangu, Dkt. Hamisi Hassan Mwinyimvua, akisaidiana na wataalam wengine. Nawashukuru na kuwapongeza Wakuu wa Idara na Vitengo pamoja na watumishi wote wa Wizara kwa ushirikiano wanaonipatia kuniwezesha kusimamia shughuli hizi muhimu kwa ajili ya mustakabali wa Taifa letu. Ni matumaini yangu kuwa ushirikiano utazidi kuimarika na hivyo kusukuma gurudumu na kujenga uchumi wa viwanda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kuwashukuru Wenyeviti na Wajumbe wa Bodi zote, Wakuu wa Taasisi na watumishi wote wa taasisi zilizo chini ya Wizara yangu kwa ushirikiano wanaonipatia. Hakika Mwenyezi Mungu atawalipa. Ni wazi kuwa ushirikiano huo umekuwa chachu katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, naipongeza wananchi wa Jimbo la Chato kwa uvumilivu wao hasa napokosekana katika shughuli za Kijimbo. Nawaomba sana wananchi wa Chato tuendelee kuungana, jukumu letu ni moja, napokuwa sipo Jimboni ni kwa sababu ya mstakabali wa Jimbo na Taifa kwa ujumla. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima ya pekee, naipongeza sana familia yangu ikiongozwa na mpendwa wangu Vaileti Kalemani kwa ustahimilivu wao wanaonipa ikiwa ni pamoja na watoto. Mbali ya kunikosa katika majukumu ya kifamilia lakini natambua wanajua natekeleza majukumu ya Kitaifa. Mwenyezi Mungu atawalipeni kwa nyoyo hizo za uvumilivu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hitimisho. Kwa heshima ya pekee, naomba Bunge lako Tukufu sasa likubali kuitisha Makadirio ya Jumla ya Sh.1,692,286,014,000 kwa ajili ya

matumizi ya Wizara ya Nishati na Taasisi zake. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama ifuatavyo:-

(i) Sh.1,665,141,000,000 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, Sh.1,489,741,000,000 ni fedha za ndani na Sh.175,400,000,000 ni fedha za nje.

(ii) Sh.27,145,014,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, Sh.15,025,821,000 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na Sh.12,119,193,000 ni kwa ajili ya Mishahara (P.E) ya watumishi wa Wizara na Taasisi zilizo chini yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tena nitoe shukrani zangu za dhati kwako wewe na kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza, kunishauri na kunelekeza. Nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge shukrani hizo mpokee kwa sababu zinawastahili. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba hii pia inapatikana katika Tovuti ya Wizara kwa anuani ya www.nishati.go.tz. Vilevile, hotuba hii ina vielelezo mbalimbali kwa ajili ya ufanuzi wa masuala muhimu yanayohusu Sekta ya Nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba maelezo ambayo nimeyatoa hapa na yale mengine ambayo nimeweka mezani yote yaingie katika *Hansard*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa naomba kutoa hoja. (*Makof*)

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Kalemani, hoja imeungwa mkono.

**HOTUBA YA WAZIRI WA NISHATI MHE. DKT. MEDARD
MATOGOLO CHANANJA KALEMANI (MB.),
AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA
MATUMIZI YA WIZARA YA NISHATI KWA MWAKA 2018/
19 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

A. UTANGULIZI

1. *Mheshimiwa Spika*, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji ya Mwaka 2017/18 na kuitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati na Taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka 2018/19.

2. *Mheshimiwa Spika*, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu. Vilevile, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwawezesha Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutekeleza kazi zao za Kibunge na kushiriki Mkutano huu wa 11 wa Bunge lako Tukufu.

3. *Mheshimiwa Spika*, kwa namna ya pekee nitumie fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mhe. Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miongozo makini wanayonipatia ili kuhakikisha kuwa azma ya Tanzania kuwa nchi ya viwanda inafikiwa. Ni wazi kuwa viongozi wetu hawa wamekuwa mstari wa mbele katika kutoa maelekezo yenye lengo la kuhakikisha kuwa umeme wa kutosha, wa uhakika, unaotabirika na wa gharama nafuu unazalishwa ili kuchochaea ukuaji wa viwanda hapa nchini. Nampongeza Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuiongoza vyema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

4. ***Mheshimiwa Spika***, nampongeza pia Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa usimamizi thabiti wa shughuli za Serikali ndani na nje ya Bunge lako Tukufu. Ni imani yangu kuwa kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu, Viongozi wetu hawa wa Kitaifa wataendelea kuwa chachu ya uhamasishaji wa shughuli za maendeleo nchini.

5. ***Mheshimiwa Spika***, nitumie fursa hii pia kumshukuru Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kunitfea kuiongoza Wizara ya Nishati. Uteuzi huo umenipa fursa ya kutoa mchango wangu katika kuisimamia Sekta hii muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu. Napenda kumhakikisha Mhe. Rais na Watanzania kuwa nitasimamia shughuli za Wizara hii kwa nguvu zangu zote, akili zangu zote, ubunifu na weledi mkubwa ili kuhakikisha kuwa Sekta ya Nishati inadhihirisha kuwa ndiyo injini kuu katika kujenga uchumi wa viwanda wa Taifa letu. Vilevile, nampongeza Mhe. Subira Khamis Mgusu, Mbunge wa Viti Maalum kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Nishati.

6. ***Mheshimiwa Spika***, napenda nikupongeze wewe binafsi, Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge, Wenyeviti wote wa Kamati mbalimbali za Kudumu pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge lako Tukufu kwa uongozi wenu mahiri katika kuliongoza Bunge hili na Kamati zake. Kwa namna ya pekee nampongeza Mhe. Dustan Luka Kitandula (Mb.), kwa kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini na Mhe. Mariam Ditopile Mzuzuri (Mb.), kwa kuteuliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo. Aidha, nawapongeza na kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kwa kupokea Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Mwaka 2017/18 na Makadirio ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2018/19.

7. ***Mheshimiwa Spika***, pamoja na upya wa Kamati hiyo, imekuwa ikitoa michango na ushauri unaolenga kuboresha utendaji wa Wizara kwa maslahi ya Taifa, hususan

katika kuhakikisha kuwa umeme wa uhakika unazalishwa na wananchi wengi zaidi wanafikiwa na huduma hiyo hapa nchini. Napenda kulihakikisha Bunge lako Tukufu kuwa Wizara ya Nishati itaendelea kupokea ushauri na mapendekezo ya Kamati hiyo na Kamati nydingine za Bunge katika kuhakikisha kuwa Wizara inatekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

8. ***Mheshimiwa Spika***, naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuwapongeza, Mhe. Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, Mbunge wa Jimbo la Songea Mjini; Mhe. Justin Joseph Monko, Mbunge wa Jimbo la Singida Kaskazini; Mhe. Dkt. Stephen Lemono Kisurwa, Mbunge wa Jimbo la Longido; Mhe. Maulid Mtulia, Mbunge wa Jimbo la Kinondoni; na Mhe. Dkt. Godwin Mollel, Mbunge wa Jimbo la Siha kwa kuchaguliwa kwao kwa kishindo kuwa Wawakilishi wa wananchi katika Majimbo yao. Hakika ni heshima kubwa waliyopewa na wananchi na nawaombea kila la heri katika kutekeleza jukumu lao hilo la uwakilishi katika Bunge letu Tukufu.

9. ***Mheshimiwa Spika***, nitumie fursa hii pia kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole kwako wewe binafsi, Naibu Spika, Bunge lako Tukufu na kwa familia ya aliyekuwa Mbunge wa Songea Mjini, Mheshimiwa Leonidas Gama kwa kuondokewa na mpendwa wetu huyo. Tunamwomba Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi, Amina.

10. ***Mheshimiwa Spika***, baada ya utangulizi huo, naomba sasa kuwasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Shughuli za Wizara ya Nishati kwa Mwaka 2017/18 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2018/19.

B. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA WIZARA YA NISHATI KWA MWAKA 2017/18

11. ***Mheshimiwa Spika***, utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2017/18 ulijielekeza katika maeneo yafuatayo: kuimarisha uzalishaji, usafirishaji na kuongeza kasi ya usambazaji wa umeme nchini; kufanikisha

utekelezaji wa Mradi mkubwa wa Ujenzi wa Bomba la Mafuta ghafi kutoka Kabaale (Uganda) hadi Bandari ya Tanga (Tanzania); kuendeleza miradi ya nishati jadidifu kama vile umeme-jua, maporomoko ya maji, jotoardhi na tungamotaka; kuwezesha uwekaji wa miundombinu ya usambazaji wa gesi asilia katika viwanda mbalimbali na matumizi ya majumbani pamoja na kufanikisha utekelezaji wa Mradi wa kusindika gesi asilia (*Liquefied Natural Gas - LNG*); kuvutia uwekezaji katika Sekta ya Nishati, hususan katika uzalishaji wa umeme kupitia vyanzo mbalimbali vilivyopo; utafutaji wa mafuta na gesi asilia; na kuwezesha Taasisi zilizopo chini ya Wizara ya Nishati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

12. ***Mheshimiwa Spika***, maeneo mengine ni: kuendelea kutekeleza agizo la Serikali la kuhamia Dodoma; kuwajengea uwezo Watumishi wa Wizara katika fani za umeme, mafuta, gesi asilia na nishati jadidifu; kuendelea kuweka mazingira wezeshi kwa wananchi kunufaika na rasilimali za mafuta na gesi asilia; kuelimisha umma na kuboresha mawasiliano kati ya Wizara na wadau mbalimbali kuhusu masuala ya Nishati. Wizara ilijielekeza pia katika kusimamia, kufuatilia na kuboresha Sera, Sheria, Mikakati na Miongozo mbalimbali ili kuboresha ufanisi na tija katika Sekta ya Nishati.

13. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2017/18 iliyokuwa Wizara ya Nishati na Madini (Fungu 58) iliidhinishiwa na Bunge Jumla ya **Shilingi bilioni 998.34**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 945.89** sawa na **asilimia 94.7** ya bajeti yote zilitengwa kwa ajili ya Sekta ya Nishati. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 916.84** sawa na **asilimia 96.9** ni fedha za Maendeleo na **Shilingi bilioni 29.04** sawa na **asilimia 3.1** ni fedha za Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha za Maendeleo zilizotengwa, **Shilingi bilioni 748.60** sawa na **asilimia 81.7** ni fedha za ndani na **Shilingi bilioni 168.24** sawa na **asilimia 18.3** ni fedha za nje. Kwa upande wa Bajeti ya Matumizi ya Kawaida, **Shilingi bilioni 14.92** sawa na **asilimia 1.6** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (O.C) na **Shilingi bilioni 14.12** sawa

na **asilimia 1.5** ya bajeti yote ni Mishahara ya Watumishi wa Wizara ya Nishati na Taasisi zake.

14. ***Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Aprili, 2018 Wizara ya Nishati kupitia (Fungu 58) ilikuwa imepokea Jumla ya **Shilingi bilioni 446.50** kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Sekta ya Nishati. Kati ya fedha hizo **Shilingi bilioni 424.91** sawa na **asilimia 95.2** zilikuwa ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambapo fedha za ndani ni **Shilingi bilioni 413.09** sawa na **asilimia 97.2** na **Shilingi bilioni 11.82** sawa na **asilimia 2.8** ni fedha za nje. Aidha, kiasi kilichobaki cha **Shilingi bilioni 21.58** sawa na **asilimia 4.8** zilikuwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

15. ***Mheshimiwa Spika***, kwa kipindi cha mwaka 2017/18 iliyokuwa Wizara ya Nishati na Madini ilipanga kukusanya Jumla ya **Shilingi bilioni 532.83** kutokana na mapato yanayohusu Sekta ya Nishati. Mapato hayo yanatokana na vyanzo mbalimbali vikiwemo: Shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi asilia; Mauzo ya gesi asilia; Mauzo ya Nyaraka za Zabuni; Tozo ya umeme na Stakabadhi nyinginezo. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Aprili, 2018 Wizara ilikuwa imekusanya Jumla ya **Shilingi bilioni 280.27** sawa na **asilimia 53**. Wizara itaendelea na juhudzi za kukusanya mapato ili kufikia lengo liliowekwa kwa kipindi cha mwaka 2017/18.

Mafanikio yaliyopatikana kwa Mwaka 2017/18

16. ***Mheshimiwa Spika***, mafanikio yaliyopatikana katika Sekta ya Nishati kwa kipindi cha mwaka 2017/18 ni pamoja na:

(i) Kuendelea na utekelezaji wa Mradi Kabambe wa Kupeleka Umeme Vijiji kupitia REA Awamu ya Tatu ambapo hadi mwezi Mei, 2018 kazi zilizokamilika ni pamoja na ujenzi wa kilomita 985 za njia ya msongo wa KV 33, ujenzi wa kilomita 1,870.37 za njia ya usambazaji umeme wa msongo wa KV 0.4 na ufungaji wa transfoma 751 zenyе ukubwa tofauti. Jumla ya vijiji 518 vimeunganishwa na kuwashwa umeme na

wateja 14,817 wameunganishiwa umeme na Jumla ya vijiji 420 vimejengwa miundombinu ya umeme na vinatarajiwa kuwashwa hivi karibuni;

(ii) Kukamilika kwa upelekaji umeme katika Makao Makuu ya Wilaya ya Tanganyika na Halmashauri ya Wilaya ya Bumbuli na kufanya Makao Makuu ya Wilaya zote nchini kuwa yamepelekewa umeme;

(iii) Kukamilika kwa **asilimia 100** kwa Mradi wa ORIO katika Miji ya Ngara, Biharamulo na Mpanda ambapo kwa sasa miji hiyo inapata umeme wa uhakika;

(iv) Kusitisha matumizi ya mitambo ya kukodi ya binafsi ya kuzalisha umeme kwa kutumia mafuta mazito katika kuzalisha umeme ikiwemo ya Aggreko na IPTL na kuokoa wastani wa jumla ya **Shilingi bilioni 11.46** kwa mwezi;

(v) Kukamilisha ujenzi wa Mradi mpya wa Kinyerezi II na kuingiza katika Gridi ya Taifa umeme wa **MW 168** mwezi Aprili, 2018;

(vi) Kukamilika kwa Mradi mpya wa Kinyerezi II na ukarabati wa mitambo ya kuzalisha umeme ya Kihansi, Kidatu, Mtera, New Pangani Falls na Ubungo II kumeongeza uhakika wa upatikanaji umeme katika Gridi ya Taifa na kuwa na ziada ya umeme wa wastani wa **MW 280** kwa siku na kuondokana na mgao wa umeme;

(vii) Kukamilika kwa ukarabati wa mitambo ya kuzalisha umeme Mtwara pamoja na kuongeza mitambo mpya miwili (2) yenye uwezo wa **MW 4** na hivyo kuongeza uhakika wa upatikanaji wa umeme katika Mikoa ya Lindi na Mtwara;

(viii) Kukamilika kwa **asilimia 100** kwa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa KV 132 yenye urefu wa

kilomita 80 kutoka Mtwara hadi Mahumbika (Lindi) pamoja na vituo vya kupoza umeme vya Mtwara na Mahumbika;

(ix) Kukamilika kwa **asilimia 95** kwa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa **kV 220** kutoka Makambako hadi Songea;

(x) Kukamilika kwa ujenzi wa vituo vipyta vya kupoza umeme vya Mbagala, Kipawa, Gongolamboto na Mburahati Mkoani Dar es Salaam;

(xi) Kukamilika kwa ujenzi wa vituo vya kupoza umeme vya Njiro B, Mount Meru, Sakina, Unga Ltd, Kiltex na Thembi Mkoani Arusha;

(xii) Kukamilika kwa ujenzi wa vituo vya kupoza umeme vya Bomambuzi na Trade School Mkoani Kilimanjaro;

(xiii) Kukamilika kwa ukarabati wa vituo vya kupoza umeme vya Mikocheni, Oysterbay, City Centre, Gongolamboto, Kariakoo, Mbagala, Chang'ombe, Kipawa na Ubungo Mkoani Dar es Salaam;

(xiv) Kuunganishwa kwa Mikoa ya Lindi na Mtwara katika Gridi ya Taifa kutokana na kukamilisha ujenzi wa njia ya msongo wa KV 33 kutoka Mbagala kupitia Mkuranga, Ikwiriri, Somanga Fungu, Lindi hadi Mtwara yenye urefu wa kilomita 451;

(xv) Kuunganishwa kwa Wilaya za Ngara na Biharamulo katika Gridi ya Taifa kutokana na kukamilika kwa ujenzi wa njia ya msongo wa KV 33 yenye urefu wa kilomita 70 na hivyo kupunguza gharama za matumizi ya mafuta kwa wastani wa **Shilingi bilioni 3.5** kwa mwaka. Kukamilika kwa ujenzi wa njia hizi kumeweza kuunganisha nchi yetu katika Gridi ya Taifa kutoka Mtwara mpakani mwa Msumbiji hadi Ngara mpakani mwa Rwanda na Burundi;

(xvi) Kusitisha uingizaji wa vifaa vyatya ujenzi wa miundombinu ya umeme ikiwemo nguzo, transfoma, nyaya na mita za LUKU ndani ya nchi na hivyo kulipunguzia gharama kubwa Shirika la Umeme Nchini, TANESCO na kuokoa wastani wa **Shilingi bilioni 162.57** kwa mwaka;

(xvii) Kuanza maandalizi ya ujenzi na utekelezaji wa Mradi mkubwa wa kuzalisha umeme wa maji wa maporomoko ya Mto Rufiji MW 2100;

(xviii) Kuunganishiwa umeme wateja wapya 201,046 na kufanya jumla ya wateja walionganishiwa umeme hadi mwezi Mei, 2018 kufikia 2,226,036;

(xix) Kukamilika maandalizi ya utekelezaji wa Mradi wa Kusafirisha Mafuta Ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania);

(xx) Kukamilika kwa ujenzi na kuanza kutumika kwa Bandari ya Mtwara kupokea mafuta hivyo kufanya Tanzania kuwa na Bandari tatu (3) za kupokea mafuta zikiwemo Dar es Salaam na Tanga;

(xi) Kuanza utekelezwaji wa Mpango wa Kusambaza Gesi Asilia Majumbani katika Mikoa ya Dar es Salaam na Mtwara; na

(xxii) Kuongezeka kwa gesi asilia iliyogunduliwa kutoka Futi za Ujazo Trilioni 57.25 mwaka 2016/17 na kufikia Futi za Ujazo Trilioni 57.54 mwaka 2017/18 kutokana na ugunduzi wa kitalu cha Ruvuma cha Futi za Ujazo Bilioni 466 kutoka Futi za Ujazo Bilioni 178.

17. ***Mheshimiwa Spika***, mafanikio hayo yametokana na utekelezaji thabiti wa llani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2015 - 2020 chini ya Uongozi makini wa Serikali ya Awamu ya Tano. llani hiyo imejielekeza katika kufikia uchumi wa viwanda ifikapo mwaka 2020 ambao Sekta ya Nishati ndiyo injini.

**C. MPANGO NA BAJETI YA WIZARA YA NISHATI
KWA MWAKA 2018/19.**

18. ***Mheshimiwa Spika***, maeneo ya kipaumbele ya Wizara ya Nishati kwa kipindi cha mwaka 2018/19 ni pamoja na: kuongeza uzalishaji wa umeme kwa kutekeleza miradi mikubwa ikiwemo: Mradi wa kuzalisha umeme katika Mto Rufiji MW 2,100 uliopo wilayani Rufiji na miradi ya kuzalisha umeme kwa kutumia gesi asilia ya Kinyerezi I - *Extension MW 185; Kinyerezi II MW 240; Somanga Fungu MW 330 Mkoani Lindi;* pamoja na MW 300 Mkoani Mtwara; kuimarishe mifumo ya usafirishaji wa umeme mkubwa nchini; kuendelea na utekelezaji wa Awamu ya Tatu ya Mradi Kabambe wa Kusambaza Umeme Vijijini (REA III); kuendelea na utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Bomba la kusafirisha Mafuta Ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania); kuimarishe shughuli za utafutajji wa mafuta na gesi asilia; na kuendeleza miradi ya nishati jadidifu (jotoardhi, upepo na umeme-jua). Wizara imejielekeza katika kutekeleza maeneo mengine ya kipaumbele yakiwemo: kuendelea kuwajengea uwezo watumishi wa Wizara na Taasisi zilizo chini yake katika kusimamia Sekta ya Nishati; kuboresha mazingira ya ofisi kwa watumishi wa Wizara na Taasisi zake ili kutoa huduma bora zaidi; na kuendelea kuelimisha umma na kuboresha mawasiliano na wadau mbalimbali kuhusu masuala ya nishati.

19. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/19, Wizara imepangiwa kukusanya Jumla ya **Shilingi bilioni 394.45**. Kati ya makusanyo hayo, **Shilingi bilioni 394.44** zitakusanya kupitia shughuli za mafuta na gesi asilia na **Shilingi milioni 10.00** zitakusanya kupitia shughuli za utawala.

**D. SEKTA NDOGO YA UMEME
HALI YA UPATIKANAJI WA UMEME NCHINI**

20. ***Mheshimiwa Spika***, katika kutimiza azma ya Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa viwanda na kufikia malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa ya Mwaka 2025, Serikali kupitia Wizara ya Nishati imelenga kuzalisha umeme

MW 5,000 ifikapo mwaka 2020 na kufikisha **MW 10,000** ifikapo mwaka 2025. Aidha, mahitaji ya umeme nchini yameendelea kuongezeka kutokana na kukua na kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi zinazohitaji nishati ya umeme wa kutosha, wa uhakika, unaotabirika na wa gharama nafuu katika uzalishaji.

21. ***Mheshimiwa Spika***, umeme uliozalishwa nchini uliongezeka kutoka **GWh 7,092** mwaka 2016 na kufikia **GWh 7,114** mwaka 2017 sawa na ongezeko la **asilimia 0.3**. Aidha, katika mwaka 2017/18 uwezo wa mitambo ya kuzalisha umeme (*Installed capacity*) iliyopo nchini umeongezeka kutoka **MW 1,450** mwaka 2016/17 na kufikia **MW 1,517.47** mwezi Mei, 2018 sawa na ongezeko la **asilimia 4.7**. Ongezeko hilo limetokana na kukamilika kwa mitambo sita (6) ya kuzalisha umeme ya Kinyerezi II ambayo hadi sasa inazalisha Jumla ya **MW 168**. Kati ya **MW 1,517.47** zilizounganishwa katika Gridi ya Taifa ni **MW 1,435.56** na zillizopo nje ya Gridi ya Taifa ni **MW 81.91 (Kielelezo Na.1 na Na.2)**. Ongezeko hili limewezesha kuwa na umeme wa ziada wa wastani wa **MW 280** ambapo matumizi ya juu ya umeme yamefikia wastani wa **MW 1,051** kwa siku.

MIRADI YA KUZALISHA UMEME

Ujenzi wa Mradi wa Rufiji (Rufiji Hydro Power Project) – MW 2,100

22. ***Mheshimiwa Spika***, lengo la kutekeleza Mradi huu ni kuzalisha umeme wa Jumla ya **MW 2,100** kwa kutumia maji (*Hydro Power Plant*) katika Bonde la Mto Rufiji. Utekelezwaji wa Mradi huu mkubwa nchini ni kichocheo muhimu katika kuwezesha Tanzania kufikia azma yake ya kuwa nchi ya uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025. Katika kipindi cha mwaka 2017/18 hatua iliyofikiwa ni pamoja na kufanya uchambuzi wa zabuni (*tender evaluation*) zilizowasilishwa na Wakandarasi walioonesha nia ya kutekeleza Mradi huu. Aidha, ujenzi wa njia ya msongo wa **kV 33** kutoka eneo la Dakawa kwa ajili ya kupeleka umeme utakaotumiwa na Mkandarasi wakati wa ujenzi wa Mradi ulianza mwezi

Novemba, 2017 na unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Julai, 2018.

23. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka 2018/19 Serikali itaendelea na utekelezaji wa Mradi huu ambapo kazi zitakazofanyika ni pamoja na: ujenzi wa kambi na ofisi za wafanyakazi; ujenzi wa bwawa (*main dam and spillways*); na ujenzi wa njia kuu za kupitisha maji (*tunnels*). Fedha za maendeleo za ndani **Shilingi bilioni 700** zimetengwa katika mwaka 2018/19 kwa ajili ya kuanza kutekeleza kazi hizo. Utekelezaji wa shughuli za ujenzi wa Mradi unatarajiwa kuanza mwezi Julai, 2018 kwa Mkandarasi kuanza kazi za awali kwa miezi mitatu (3) na kufuatiwa na ujenzi wa miundombinu ya Mradi unaotarajiwa kukamilika katika kipindi cha miezi 36.

Mradi wa Kinyerezi I Extension - MW 185

24. ***Mheshimiwa Spika***, Mradi huu unahusu upanuzi wa kituo cha kuzalisha umeme cha Kinyerezi I kwa kuongeza mitambo itakayozalisha **MW 185** na kufanya kituo hicho ambacho kwa sasa kinazalisha umeme wa **MW 150** kuzalisha jumla ya **MW 335**. Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania kwa **asilimia 100** kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 188** sawa na takriban **Shilingi bilioni 434**. Katika mwaka 2017/18 kazi zilizokamilika ni pamoja na: ujenzi wa misingi ya kusimika mitambo ya kuzalisha umeme na transfoma; ujenzi wa misingi ya kituo cha kupoza umeme; na ujenzi wa njia ya msongo wa **KV 220** inayounganisha mtambo wa Kinyerezi I Extension na Kinyerezi II na kuunganishwa katika Gridi ya Taifa.

25. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka 2018/19 kazi ya usimikaji wa mitambo pamoja na ukamilishaji wa ujenzi wa kituo cha kupoza umeme zitafanyika kwa gharama ya **Shilingi bilioni 164** zikiwa ni fedha za ndani. Ujenzi wa Mradi ulianza mwezi Novemba, 2016 na unatarajiwa kukamilika mwezi Januari, 2019.

Mradi wa Kinyerezi II - MW 240

26. *Mheshimiwa Spika*, Mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia gesi asilia wa Kinyerezi II unatarajiwa kuongeza Jumla ya **MW 240** katika Gridi ya Taifa. Uzalishaji umeme katika Mradi huu ulizinduliwa rasmi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli tarehe 03 Aprili, 2018. Hadi sasa mitambo sita (6) ya *gas turbines* imefungwa na inazalisha umeme wa jumla ya **MW 168** zilizoingizwa katika Gridi ya Taifa. Ufungaji wa mitambo miwili (2) yenye uwezo wa kuzalisha Jumla ya **MW 80.4** kwa kutumia mvuke (*steam turbines*) unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2018. Gharama za kutekeleza Mradi huu ni **Dola za Marekani milioni 344** sawa na takriban **Shilingi bilioni 794.12**. Asilimia 15 ya gharama za Mradi huu ni fedha za ndani na **asilimia 85** ni mkopo wa masharti nafuu kutoka benki za *Japan Bank for International Cooperation (JBIC)* na *Sumitomo Mitsui Banking Corporation (SMBC)* za Japan.

Mradi wa Somanga Fungu - MW 330

27. *Mheshimiwa Spika*, Mradi huu unahuusu ujenzi wa mitambo ya kuzalisha umeme wa **MW 330** kwa kutumia gesi asilia. Aidha, Mradi unahuusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa **kV 400** umbali wa kilomita 198.2 kutoka Somanga Fungu hadi Kinyerezi. Mradi huu utamiliikiwa na Serikali kupitia TANESCO kwa asilimia 100. Gharama za Mradi zinakadiriwa kuwa **Dola za Marekani milioni 396** sawa na takriban **Shilingi bilioni 914.16**. Upembizi Yakinifu wa Mradi umekamilika na taratibu za kumpata Mkandarasi mwenye uwezo wa kitaalam na fedha kwa kushindanishwa chini ya utaratibu wa *EPC plus Financing* zinaendelea.

28. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka 2018/19 kazi zilizopangwa kufanyika ni pamoja na: kukamilisha taratibu za kumpata Mkandarasi na fedha za kutekeleza Mradi; kumpata Mshauri Mwelekezi wa usimamizi wa Mradi; na kuanza utekelezaji wa Mradi. **Shilingi bilioni 4.5** fedha za nje zimetengwa ili kutekeleza kazi hizo. Ujenzi wa Mradi huu

unatarajiwa kuanza mwezi Septemba, 2018 na kukamilika ifikapo mwezi Septemba, 2021.

Mradi wa Mtwara MW 300

29. *Mheshimiwa Spika*, Mradi wa Mtwara unahu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa **MW 300** kwa kutumia gesi asilia na ujenzi wa kituo cha kupoza umeme. Mradi utahusu pia ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa KV 400 umbali wa kilomita 253 kutoka Mtwara hadi Somanga Fungu. Utekelezaji wa Mradi huu utaimarisha upatikanaji wa umeme katika mikoa ya Lindi na Mtwara. Mradi huu unatarajiwa kugharimu **Dola za Marekani milioni 360** sawa na takriban **Shilingi bilioni 831** na utamiliwa na Serikali kuititia TANESCO kwa asilimia 100. Katika mwaka 2017/18 kazi zilizotekelizwa ni pamoja na kuanza Upembuzi Yakinifu chini ya ufadhili wa JICA mwezi Julai, 2017 ambao unatarajiwa kukamilika mwezi Agosti, 2018.

30. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2018/19 kazi zilizopangwa kufanyika ni pamoja na: kukamilisha Upembuzi Yakinifu wa Mradi; kumtafuta Mshauri Mwelekezi; na kuandaa nyaraka za zabuni kwa ajili ya kumpata Mkandarasi. Jumla ya **Shilingi bilioni 3.7** zinakadiriwa kutumika kuwalipa fidia wananchi watakaopisha Mradi. Katika mwaka 2018/19 fedha za nje **Shilingi bilioni 4** zimetengwa ili kutekeleza shughuli za Mradi huu. Ujenzi wa Mradi unatarajiwa kuanza mwezi Novemba, 2018 na kukamilika mwezi Juni, 2021.

Mradi wa Kakono – MW 87

31. *Mheshimiwa Spika*, Mradi huu unahu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa **MW 87** kwa kutumia maji ya Mto Kagera na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa **KV 132** yenye urefu wa kilomita 38.8 kutoka Kakono hadi Kyaka. Gharama za ujenzi wa Mradi ni **Dola za Marekani milioni 379.4** sawa na takriban **Shilingi bilioni 875.84**. Kazi iliyofanyika katika mwaka 2017/18 ni kupima na kutathmini eneo la Mradi ambapo taarifa kuhusu alama za mipaka na tathmini ya eneo la ujenzi wa kituo cha kuzalisha

umeme pamoja na njia ya kusafirisha umeme imekamilika. Aidha, Mshauri Mwelekezi (Kampuni ya *Studio Pietrangeli* kutoka Italia) kwa ajili ya kusimamia utekelezaji wa Mradi ameshapatikana.

32. ***Mheshimiwa Spika***, kwa mwaka 2018/19, kazi zitakazofanyika ni pamoja na: kuwalipa fidia wananchi watakaopisha Mradi; kumpata Mtaalam Mshauri kwa ajili ya kufanya utafiti zaidi wa kijolojia na haidrolojia; na kutayarisha zabuni kwa ajili ya Mkandarasi wa ujenzi wa kituo na miundombinu ya kusafirisha umeme. Jumla ya **Shilingi bilioni 4.05** zimetengwa kwa ajili ya shughuli hizo. Kati ya fedha hizo **Shilingi bilioni 2** ni fedha za ndani na **Shilingi bilioni 2.05** ni fedha za nje. Mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Machi, 2019 na kukamilika ifikapo mwezi Novemba, 2021.

Mradi wa Rusumo - MW 80

33. ***Mheshimiwa Spika***, Mradi huu unahuusu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa **MW 80** kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Kagera ambapo umeme huo utagawanywa kwa usawa kati ya nchi za Tanzania, Rwanda na Burundi. Mradi unahuishisha pia ujenzi wa njia za kusafirisha umeme wa msongo wa **kV 220** kutoka Rusumo hadi kituo cha kusafirishia umeme kwa kila nchi. Kwa upande wa Tanzania umeme utasafirishwa hadi Nyakanazi. Katika kipindi cha mwaka 2017/18, kazi zilizofanyika ni kuanza ujenzi wa: bwawa la kuhifadhia maji; njia za kupitisha maji (*intake tunnel*); eneo la kusimika mitambo (*power house*); barabara za kuingia eneo la Mradi; pamoja na ofisi na nyumba za wafanyakazi.

34. ***Mheshimiwa Spika***, kazi zilizopangwa kufanyika mwaka 2018/19 ni: kukamilisha ujenzi wa kambi ya kudumu ya wafanyakazi; kukamilisha miundombinu ya barabara za kuingia eneo la Mradi; na kuendelea na ujenzi wa bwawa la kuhifadhia maji; njia za kupitisha maji (*intake tunnel*); na eneo la kusimika mitambo (*power house*). Fedha za nje **Shilingi bilioni 3** zimetengwa katika mwaka 2018/19 kwa ajili ya Mradi huu. Utekelezaji wa Mradi ulianza mwezi

Machi, 2017 na unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Februari, 2021.

Mradi wa Murongo/Kikagati - MW 14

35. *Mheshimiwa Spika*, Mradi huu unahusu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa **MW 14** kwa kutumia maji ya Mto Kagera zitakazogawanya kwa usawa katika nchi ya Tanzania na Uganda. Mradi pia utahusisha ujenzi wa njia za kusafirisha umeme wa msongo wa **KV 33** yenye urefu wa kilomita 0.7 kutoka Kikagati (Uganda) hadi Murongo (Tanzania). Mradi huu unatekelezwa na mwekezaji binafsi, Kampuni ya Kikagati Power Company Ltd (KPCL) iliyoasajiliwa nchini Uganda ambapo umeme utakaozalishwa utauzwa kwa Kampuni za Uganda Electricity Transmission Company Ltd (UETCL) na Tanzania Electricity Supply Company Ltd (TANESCO). Mradi utagharimu **Dola za Marekani milioni 58** sawa na takriban **Shilingi bilioni 133.89**.

36. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka 2017/18 kazi zilizofanyika ni pamoja na: kusainiwa kwa Mkataba wa Ugawanaji wa Umeme kwa Usawa (*Power Sharing and Sales Agreement*) katika UETCL na TANESCO; kusainiwa kwa Mkataba wa Kuuziana Umeme (*Power Purchase Agreement*) katika kampuni ya KPCL na UETCL; kukamilika kwa malipo ya fidia kwa wananchi wanaopisha Mradi; na kuanza kutekelezwa kwa kazi za awali za ujenzi ikiwemo kambi ya wafanyakazi na barabara za kuingia kwenye eneo la Mradi (*access road*). Kazi zitakazotekeliza kwa mwaka 2018/19 ni pamoja na: kukamilisha ujenzi wa kambi ya kudumu ya wafanyakazi na miundombinu ya barabara za kuingia eneo la Mradi; na kuanza ujenzi wa bwawa (*main dam and spillways*) na njia kuu za kupitisha maji (*tunnels*). Mradi huu ulianza mwezi Novemba, 2017 na unatarajiwa kukamilika mwezi Oktoba, 2020.

Mradi wa Malagarasi – MW 45

37. *Mheshimiwa Spika*, Mradi huu unahusu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa **MW 45** kwa kutumia

maporomoko ya maji ya Mto Malagarasi Mkoani Kigoma na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa **KV 132** yenyeye urefu wa kilomita 53 kutoka Malagarasi hadi Kidahwe-Kigoma. Gharama za utekelezaji wa Mradi ni **Dola za Marekani milioni 149.5** sawa na takriban **Shilingi bilioni 345.12**. Katika mwaka 2017/18 kazi zilizofanyika ni pamoja na: uboreshaji wa tathmini ya athari za jamii na mazingira (ESIA) na tathmini ya fidia kwa wananchi watakaopisha Mradi; upimaji na uthamini wa eneo la Mradi wa njia ya kusafirisha umeme umeanza; na Mshauri Mwelekezi (Kampuni ya *Studio Pietrangeli* kutoka Italia) kwa ajili ya kusimamia utekelezaji wa Mradi amepatikana.

38. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/19, kazi zilizopangwa kufanyika ni pamoja na: kukamilisha Upembuzi Yakinifu wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa **KV 132**; kumpata Mkandarasi; na kukamilisha upimaji na uthamini wa eneo la Mradi na njia ya kusafirisha umeme. Jumla ya **Shilingi bilioni 7.8** zinakadiriwa kutumika kuwalipa fidia wananchi watakaopisha Mradi. Katika mwaka 2018/19 **Shilingi bilioni 4.3** zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Mradi. Kati ya fedha hizo **Shilingi bilioni 1.5** ni fedha za ndani na **Shilingi bilioni 2.8** ni fedha za nje. Shughuli za ujenzi wa Mradi huu zinatarajiwaa kuanza mwezi Machi, 2019 na kukamilika ifikapo mwezi Juni, 2021.

Mradi wa Ruhudji - MW 358

39. ***Mheshimiwa Spika***, Mradi huu unahu unahusu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa **MW 358** kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Ruhudji. Mradi utahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa **KV 400** yenyeye urefu wa kilomita 170 kutoka Ruhudji Mkoani Njombe hadi kituo cha kupoza umeme cha Kisada Mkoani Iringa. Kazi zilizofanyika hadi sasa ni pamoja na Serikali kuwasilisha maombi ya ufadhili wa Mradi kwa Benki ya Dunia na kufanyika kwa zoezi la uhakiki wa kiwango cha maji katika Mto Ruhudji ili kujua kiwango halisi cha umeme kinachowezza

kuzalishwa. Utekelezaji wa Mradi huu unakadiriwa kugharimu **Dola za Marekani milioni 460.6** sawa na takriban **Shilingi trillioni 1.06**. Katika kipindi cha mwaka 2018/19 Serikali itaendelea na majadiliano na wafadhili ili kuwezesha upatikanaji wa fedha za kutekeleza Mradi. Mradi huu unatarajija kuanza kujengwa katika kipindi cha mwaka 2018/19 baada ya fedha kupatikana na unatarajija kukamilika mwaka 2020/21.

Miradi ya Kinyerezi III - MW 600

40. ***Mheshimiwa Spika***, Mradi huu utahusisha ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme kwa kutumia gesi asilia **MW 600** katika awamu mbili (2) za **MW 300** kwa kila awamu katika eneo la Kinyerezi - Dar es salaam. Kazi zilizopangwa kutekelezwa katika mwaka 2018/19 ni pamoja na: kukamilisha Upembizi Yakinifu; na kumpata Mkandarasi mwenye uwezo wa kitaalam na fedha kwa kushindanishwa chini ya utaratibu wa *EPC plus Financing*. Utekelezaji wa mradi huu unatarajija kuanza mwezi Novemba, 2018 na kukamilika mwezi Desemba, 2021.

Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa kutumia Makaa ya Mawe Kiwira – MW 200

41. ***Mheshimiwa Spika***, Mradi huu unahusu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme kwa kutumia makaa ya mawe chenye uwezo wa **MW 200** katika eneo la Kiwira na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa **KV 220** yenye urefu wa kilomita 100 kutoka Kiwira hadi Uyole-Mbeya. Gharama za kutekeleza Mradi zinakadiriwa kuwa **Dola za Marekani milioni 320** sawa na takriban **Shilingi bilioni 738.72**. Katika mwaka 2018/19 TANESCO na STAMICO watakamilisha Makubaliano ya Awali (*Memorandum of Understanding - MoU*) ya kuuziana makaa ya mawe na taratibu za kumpata Mkandarasi mwenye teknolojia na uwezo wa kutekeleza Mradi na kuanza shughuli za ujenzi baada ya kukamilisha Upembizi Yakinifu. Mradi huu unatarajija kuanza mwezi Oktoba, 2019 na kukamilika mwezi Aprili, 2022.

Ukarabati wa Mitambo katika Kituo cha Kufua Umeme cha Hale (*Hale Hydro Power Plant*)

42. ***Mheshimiwa Spika***, Mradi huu unahu unahusu ukarabati wa mitambo na ujenzi wa miundombinu ya kuzalisha umeme katika Kituo cha Hale ili kuwezesha kituo hicho kuzalisha umeme kwa kiwango cha uwezo wake wa **MW 21** kutoka **MW 10.5** zinazozalishwa sasa. Makadirio ya gharama za Mradi huu ni **SEK milioni 200** sawa na takriban **Shilingi bilioni 50.98** ambapo **asilimia 60** ya gharama hizo ni msaada kutoka Serikali ya Sweden kupitia Shirika lake la Maendeleo la Kimataifa (Sida) na **asilimia 40** ni mchango wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika kipindi cha mwaka 2017/18 kazi zilizofanyika ni pamoja na kukamilika kwa: usanifu (*design*) wa Mradi; uandaaji wa Mpango Kazi; *pre-qualification* ya Wakandarasi. Zabuni zitafunguliwa mwezi Juni, 2018. Kwa mwaka 2018/19 Mkandarasi ataanza kazi ya ukarabati wa mitambo ambapo jumla ya **Shilingi bilioni 6.7** fedha za nje zimetengwa. Mradi unatarajiwa kuanza mwezi Oktoba, 2018 na kukamilika mwezi Novemba, 2021.

Mradi wa Umeme Unaotokana na Nishati ya Jua katika Mkoa wa Shinyanga – MW 150

43. ***Mheshimiwa Spika***, Mradi huu unahu unahusu ujenzi wa kituo cha kufua umeme-jua **MW 150** katika eneo la Ibadakuli Wilayani Kishapu Mkoani Shinyanga. Mradi huu unatarajiwa kutekelezwa na Serikali kupitia TANESCO kwa ufadhilli wa Taasisi ya Maendeleo ya Ufaransa (AFD). Katika kuendeleza Mradi huu AFD imetoa msaada wa **Euro 520,130** sawa na takriban **Shilingi bilioni 1.3** kwa ajili ya kuwezesha na kukamilisha zoezi la Upembusi Yakinifu utakaojumuisha tathmini ya kitaalam, kiuchumi na mazingira. Kazi zilizofanyika katika mwaka 2017/18 ni pamoja na: kukamilisha tathmini ya fidia kwa wananchi watakaopisha Mradi pamoja na kupatikana kwa Mshauri Mwelekezi ambaye ameanza kazi ya Upembusi Yakinifu unaotarajiwa kukamilika mwezi Septemba, 2018. Jumla ya **Shilingi bilioni 1.3** zinakadiriwa kutumika kuwalipa fidia wananchi watakaopisha Mradi.

Katika mwaka 2018/19 kazi zilizopangwa kufanyika ni pamoja na: kulipa fidia wananchi watakaopisha Mradi; kukamilisha taratibu za ufadhilli wa Mradi; na kuanza utekelezaji wa Mradi. Mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Januari, 2019 na kukamilika mwezi Desemba, 2020.

Mradi wa Umeme wa Upopo Singida – *Wind East Africa (WEA) MW 100*

44. ***Mheshimiwa Spika***, Mradi huu ni wa kuzalisha umeme wa **MW 100** unaotokana na nishati ya upopo katika eneo la Kisaki na Utaho Mkoani Singida. Mradi utatekelezwa kwa ubia kati ya Kampuni ya *Six Telecoms* (Tanzania), *International Finance Corporation - IFC* (Marekani) na Aldwych International (Uingereza). Gharama za Mradi huu zinakadiriwa kuwa **Dola za Marekani milioni 285** sawa na takriban **Shilingi bilionti 657.92**. Kwa mwaka 2017/18 majadiliano ya Mkataba wa Kibashara (PPA) kati ya TANESCO na Kampuni ya Wind East Africa (WEA) yakokatika hatua za mwisho. Katika mwaka 2018/19 kazi zilizopangwa kufanyika ni pamoja na kukamilisha majadiliano ya PPA na kuanza utekelezaji wa Mradi. Ujenzi wa Mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Oktoba, 2018 na kukamilika mwezi Desemba, 2020.

UJENZI WA NJIA ZA KUSAFIRISHA UMEME

Mradi wa njia ya Umeme wa Msongo wa KV 220 kutoka Makambako hadi Songea na Usambazaji wa Umeme Vijiji kwa Mikoa ya Njombe na Ruvuma

45. ***Mheshimiwa Spika***, lengo la Mradi ni kujenga njia ya umeme wa msongo wa **KV 220** yenye urefu wa kilomita 250 kutoka Makambako hadi Songea kupitia Madaba. Kazi nyingine zinazohusu Mradi ni: ujenzi wa vituo vipyta viwili (2) vya kupoza umeme vya Madaba na Songea mjini; upanuzi wa kituo cha kupoza umeme cha Makambako; utandazaji wa nyaya za mawasiliano; ujenzi wa njia za kusambaza umeme wa msongo wa **KV 33** wenye urefu wa kilomita 900; na kuunganisha wateja wa awali 22,700 katika Vijiji 120 vya

Wilaya za Makambako, Njombe na Ludewa katika Mkoa wa Njombe; na Songea Vijiji, Songea Mjini, Namtumbo na Mbinga katika Mkoa wa Ruvuma.

46. ***Mheshimiwa Spika***, kazi zilizotekelezwa kwa mwaka 2017/18 kwa upande wa njia ya kusafirisha umeme **KV 220** Makambako hadi Songea ni kukamilika kwa usanifu, utengenezaji, usafirishaji wa vifaa na ujenzi wa misingi ya nguzo. Kwa upande wa ujenzi wa vituo vya kupoza umeme vyenye uwezo wa KV 220/33 vya Makambako, Madaba na Songea, usafirishaji wa vifaa na ujenzi wa misingi umekamilika. Hadi kufikia mwezi Mei, 2018 ujenzi wa miundombinu ya usambazaji umeme kwenye vijiji 32 kati ya 120 umekamilika na jumla ya wateja 1,500 kati ya 22,000 wameunganishiwa umeme.

47. ***Mheshimiwa Spika***, kwa ujumla hadi kufikia mwezi Mei, 2018 ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme **KV 220** kutoka Makambako – Songea umefikia **asilimia 95**; Ujenzi wa vituo viwili (2) vipyta vya kupoza umeme vya Madaba na Songea umefikia **asilimia 76**; na usambazaji umeme umefika **asilimia 68.5** kwa Mikoa ya Ruvuma na Njombe. Kazi zilizopangwa kufanyika mwaka 2018/19 ni kukamilisha: ujenzi wa vituo vya kupoza umeme; ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa **KV 220**; na uunganishaji wa wateja. Jumla ya **Shilingi bilioni 13** zimetengwa katika mwaka 2018/19 ili kutekeleza kazi hizo. Kati ya fedha hizo **Shilingi bilioni 7** ni fedha za ndani na **Shilingi bilioni 6** ni fedha za nje. Mradi huu ulianza mwezi Desemba, 2016 na unatarajiwa kukamilika mwezi Septemba, 2018.

Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa KV 400 kutoka Iringa - Shinyanga (Backbone – Awamu ya Pili)

48. ***Mheshimiwa Spika***, Mradi huu unahu sukuongeza uwezo (*upgrade*) wa vituo vya kupoza umeme kutoka **KV 220** hadi **KV 400** katika mijji ya Iringa, Dodoma, Singida na Shinyanga. Gharama ya Mradi ni **Dola za Marekani Milioni 120** sawa na takriban **Shilingi bilioni 277.02**

zinazotokana na mikopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya Jumuiya ya Ulaya (EIB) na Serikali ya Japan kupitia Shirika lake la Maendeleo la Kimataifa (JICA). Katika kipindi cha mwaka 2017/18 Mkandarasi atakayefanya kazi katika vituo vya kupoza umeme vya Dodoma na Singida amepatikana na tayari ameanza kazi. Katika mwaka 2018/19 kazi zilizopangwa kufanyika ni: kumpata Mkandarasi kwa ajili ya vituo vya Iringa na Shinyanga na kuendelea na utekelezaji wa Mradi. Mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Septemba, 2018 na kukamilika mwezi Juni, 2020.

Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa KV 400 kutoka Masaka - Mwanza

49. *Mheshimiwa Spika*, Mradi huu unahuusu ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa **KV 400** kutoka Masaka nchini Uganda hadi Mwanza - Tanzania na upanuzi wa vituo vya kupoza umeme wa KV 400/220 katika maeneo ya Kyaka na Rusumo/Nyakanazi. Kazi zilizofanyika kwa mwaka 2017/18 ni kukamilika kwa majadiliano ya Mkataba kati ya TANESCO na Mshauri Mwelekezi Kampuni ya Norconsult kutoka Norway atakayedurusu Upembuzi Yakinifu wa Mradi. Upembuzi Yakinifu huo unatarajiwa kuanza mwezi Oktoba, 2018 na kukamilika mwezi Novemba, 2019. Katika mwaka 2018/19 **Shilingi bilioni 2.5** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kazi hiyo.

Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa KV 400, Iringa - Mbeya – Tunduma - Sumbawanga – Mpanda - Kigoma – Nyakanazi (*North West Grid*)

50. *Mheshimiwa Spika*, Mradi unahuisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa KV 400 kutoka Iringa - Mbeya – Tunduma - Sumbawanga – Mpanda - Kigoma – Nyakanazi yenye urefu wa kilomita 1,372. Mradi huu utawezesha kuunganisha umeme maeneo ya Magharibi na Kaskazini-Magharibi mwa Tanzania katika Gridi ya Taifa na kuondoa matumizi ya mitambo ya mafuta (*diesel*) katika maeneo hayo na kuwafikishia umeme wananchi wengi.

51. ***Mheshimiwa Spika***, Benki ya Dunia imeonesha nia ya kufadhili ujenzi wa vituo vya kupoza umeme na njia ya kusafirisha umeme kutoka Iringa – Mbeya – Tunduma – Sumbawanga – Kigoma yenyе urefu wa kilomita 612 inayounganisha Zambia na Tanzania. Mradi utagharimu **Dola za Marekani milioni 455** sawa na takriban **Shilingi trillioni 1.05**. Sehemu hii ya Mradi itaunganisha Mradi wa *North-West grid* kV 400 unaoanzia Sumbawanga – Mpanda – Kigoma – Nyakanazi yenyе urefu wa kilomita 760. Serikali ya Korea Kusini kupitia Mfuko wake wa Maendeleo (EDCF) imeonesha nia ya kufadhili ujenzi wa vituo vya kupoza umeme katika maeneo ya Kigoma na Nyakanazi kwa **Dola za Marekani milioni 40.5** sawa na takriban **Shilingi bilioni 93.49** na AfDB imeonesha nia ya kufadhili ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Nyakanazi hadi Kigoma yenyе urefu wa kilomita 280 kwa **Dola za Marekani milioni 93.5** sawa na takriban **Shilingi bilioni 215.84**.

52. ***Mheshimiwa Spika***, kazi zilizofanyika katika kipindi cha mwaka 2017/18 ni pamoja na: kupima na kufanya tathmini ya maeneo kwa ajili ya kujenga vituo vya kupoza umeme vya Kigoma, Mpanda, Sumbawanga na Tunduma; kukamilisha uandaaji wa taarifa za fidia kwa wananchi watakaopisha Mradi kutoka Kigoma hadi Nyakanazi; na kuendelea na majadiliano na wafadhili wa Mradi ambao ni Benki ya Dunia, AfDB na EDCF. Jumla ya **Shilingi bilioni 25.5** zinakadirisha kuwa zitatumika kulipa fidia wananchi watakaopisha Mradi katika maeneo ya Iringa - Mbeya; Mbeya – Tunduma - Sumbawanga; na Kigoma - Nyakanazi.

53. ***Mheshimiwa Spika***, kazi zilizopangwa kufanyika mwaka 2018/19 ni: ulipaji wa fidia kwa wananchi watakaopisha Mradi; kukamilisha majadiliano na wafadhili wa Mradi; kuwapata wakandarasi wa ujenzi; na kuanza utekelezaji wa Mradi. Jumla ya **Shilingi bilioni 33.2** zimetengwa kwa ajili ya kazi hizo. Katи ya fedha hizo **Shilingi bilioni 31** ni fedha za ndani na **Shilingi bilioni 2.2** ni fedha za nje. Mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Desemba, 2018 na kukamilika mwezi Agosti, 2021.

Mradi wa Njia za Kusafirisha Umeme wa Msongo wa kV 400 na kV 220, North – East Grid

54. ***Mheshimiwa Spika***, lengo la Mradi huu ni kusafirisha umeme utakaozalishwa katika kituo cha Kinyerezi, Dar es Salaam kwenda katika Mikoa ya Arusha na Tanga ambapo njia zilizopo kwa sasa zimezidiwa na mahitaji makubwa ya umeme. Mradi huu utagharimu **Dola za Marekani milioni 692.7** sawa na takriban **Shilingi trillioni 1.59**. Kati ya gharama hiyo, **asilimia 85** ni mkopo kutoka Benki ya Exim ya China na **asilimia 15** ni mchango wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania. Katika kipindi cha mwaka 2017/18 kazi zilizofanyika ni pamoja na: kukamilisha upimaji na tathmini ya mali za wananchi watakaopisha Mradi kwa kipande cha kutoka Kinyerezi - Kiluvya - Chalinze hadi Segera. Fidia kwa kipande cha Kinyerezi – Chalinze inatarajiwa kulipwa wakati wowote kuanzia sasa na maandalizi ya ulipaji fidia kwa kipande cha kuanzia Chalinze hadi Segera yanaendelea. Kwa mwaka 2018/19 jumla ya **Shilingi bilioni 47.8** zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi. Kati ya fedha hizo **Shilingi bilioni 34.8** ni fedha za ndani na **Shilingi bilioni 13** fedha za nje.

Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa kV 400 kutoka Somanga Fungu - Kinyerezi

55. ***Mheshimiwa Spika***, Mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa **kV 400** kutoka Somanga Fungu Mkoani Lindi hadi Kinyerezi, Dar es Salaam wenye urefu wa kilomita 198 na kujenga kituo cha kupoza umeme cha Somanga Fungu. Mradi huu utaunganisha na kusafirisha umeme unaotarajiwa kuzalishwa katika maeneo ya Somanga Fungu na Mtwara hadi Kinyerezi Dar es Salaam. Gharama za Mradi ni **Dola za Marekani milioni 150** sawa na takriban **Shilingi bilioni 346.27**.

56. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka 2017/18 kazi zilizofanyika ni pamoja na: kuendelea na ulipaji wa fidia kwa wananchi wanaopisha Mradi ambapo hadi

kufikia mwezi Aprili, 2018 jumla ya **Shilingi bilioni 49.5** zimelipwa kwa wananchi 2,487 kati ya 3,901. Aidha, Mshauri Mwelekezi (Kampuni ya *Byucksan Power Limited* ya Korea Kusini) kwa ajili ya kudurusu Upembuzi Yakinifu ameanza kazi mwezi Desemba, 2017 na anatarajia kukamilisha mwezi Julai, 2018. Kazi zilizopangwa kufanyika kwa mwaka 2018/19 ni: kukamilisha malipo ya fidia kwa wananchi waliobaki na kudurusu Upembuzi Yakinifu. Jumla ya **Shilingi bilioni 23.5** zimetengwa kutekeleza kazi hizo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 22** ni fedha za ndani na **Shilingi bilioni 1.5** ni fedha za nje. Shughuli za ujenzi zinatarajiwaa kuanza mwezi Agosti, 2019 na kukamilika mwezi Machi, 2020.

Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa kV 400 kutoka Rufiji – Chalinze – Dodoma

57. ***Mheshimiwa Spika***, Mradi huu unahu unahusu ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa **kV 400** yenye urefu wa kilomita 512 kutoka Rufiji kuitia Chalinze Mkoani Pwani hadi Dodoma na upanuzi wa vituo vya kupoza umeme wa kV 400/ 220 katika Mji wa Chalinze na Jiji la Dodoma. Gharama za Mradi zinakadiriwa kuwa **Dola za Marekani milioni 276.36** sawa na takriban **Shilingi bilioni 637.97**.

58. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka 2017/18 kazi zilizofanyika ni: Upembuzi Yakinifu kwa kipande cha kutoka Chalinze hadi Dodoma; na Upembuzi Yakinifu wa Awali (*Pre-feasibility Study*) kutoka Rufiji hadi Chalinze. Pia, maandalizi ya kumpata Mshauri Mwelekezi kwa ajili ya kufanya mapitio ya Upembuzi Yakinifu kwa eneo la Rufiji hadi Chalinze yameanza. Kazi zilizopangwa kufanyika kwa mwaka 2018/19 ni: kufanya Upembuzi Yakinifu; kuweka mipaka na kufanya tathmini ya njia ya kusafirishia umeme kutoka Rufiji hadi Chalinze; na kukamilisha malipo ya fidia kwa wananchi watakaopisha Mradi. Fedha za ndani **Shilingi bilioni 39** zimetengwa kwa ajili ya kazi hizo. Mradi huu unatarajiwaa kuanza mwezi Desemba, 2018 na kukamilika mwezi Desemba, 2020.

Mradi wa Njia ya Umeme wa Msongo wa kV 220 kutoka Bulyanhulu – Geita

59. *Mheshimiwa Spika*, Mradi huu unahu ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa **kV 220** yenye urefu wa kilomita 55 kutoka Bulyanhulu hadi Geita; ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Geita; upanuzi wa Kituo cha kupoza umeme cha Bulyanhulu; usambazaji wa umeme katika vijiji nane (8) vitakavyopitiwa na Mradi (kilomita 115) ambapo wateja wapya 1,500 wataunganishiwa umeme. Gharama za Mradi huu ni **Dola za Marekani milioni 23** sawa na takriban **Shilingi bilioni 53.09**.

60. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka 2017/18 kazi zilizofanyika ni pamoja na: kukamilika uhakiki wa fidia kwa wananchi watakaopisha Mradi pamoja na kuwapata Wakandarasi watakaotekeleza Mradi. Jumla ya **Shilingi bilioni 2** zinakadirisha kutumika kuwalipa fidia wananchi watakaopisha Mradi. Kwa mwaka 2018/19 **Shilingi bilioni 5** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa Mradi. Mradi unatarajiwa kuanza mwezi Agosti, 2018 na kukamilika mwezi Aprili, 2020.

Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa kV 220 ya Geita – Nyakanazi na Usambazaji wa Umeme katika Vijiji vitakavyopitiwa na Mradi

61. *Mheshimiwa Spika*, Mradi huu unahu ujenzi wa njia ya **kV 220** (km 133), kituo cha kupoza umeme Nyakanazi na kusambaza umeme katika vijiji 32 vinavyopitiwa na Mradi. Gharama za utekelezaji wa Mradi huu ni **EIRO milioni 45** sawa na takriban **Shilingi bilioni 113.31**. Mradi huu unafadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (KfW), Taasisi ya Maendeleo ya Ufaransa (AFD), Umoja wa Ulaya (EU) na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

62. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka 2017/18 kazi zilizofanyika ni: kufanya tathmini na uhakiki wa mali zitakazoathiriwa na Mradi; kumpata Mkandarasi atakayejenga njia ya kusafirisha umeme; kujenga vituo vya

kupoza umeme; na usambazaji wa umeme vijijini. Jumla ya **Shilingi bilioni 5.79** zinakadiriwa kutumika kuwalipa fidia wananchi watakaopisha Mradi. Kazi zilizopangwa kufanyika katika kipindi cha mwaka 2018/19 ni kuwalipa fidia wananchi na kuanza utekelezaji wa Mradi. Fedha za nje **Shilingi bilioni 1.6** zimetengwa kwa ajili ya shughuli za Mradi. Mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Julai, 2018 na kukamilika mwezi Desemba, 2019.

Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa KV 400 kutoka Singida - Arusha – Namanga

63. *Mheshimiwa Spika*, Mradi huu unahu ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa **KV 400** kutoka Singida hadi Namanga kuititia Arusha yenyе urefu wa kilomita 414. Mradi umegawanyika katika maeneo matano (5) ya utekelezaji ambayo ni: Singida - Babati (km150); Babati - Arusha (km150); Arusha – Namanga (km114); ujenzi na upanuzi wa vituo vya kupoza umeme (*Substations*) na usambazaji wa umeme katika vijiji 21 vitakavyopitiwa na Mradi. Gharama za Mradi huu ni **Dola za Marekani milioni 258.82** sawa na takriban **Shilingi bilioni 597.48** ambapo **asilimia 83** ya fedha hizo zitatolewa na wafadhili (AfDB na JICA). Aidha, Serikali ya Tanzania itachangia **Dola za Marekani milioni 43.89** sawa na takriban **Shilingi bilioni 101.32** ambazo ni **asilimia 17** ya gharama za Mradi.

64. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka 2017/18 kazi zilizofanyika ni pamoja na: Mkandarasi kufanya *detailed survey* ya njia ya umeme wa msongo wa **KV 400** kutoka Singida hadi Namanga; kusanifu na kufanya majaribio ya nguzo na vifaa vingine vitakavyotumika katika ujenzi; kufanya utafiti wa udongo katika njia ya umeme; na Serikali kukamilisha uhakiki wa malipo ya fidia kwa wananchi watakaopisha Mradi. Jumla ya **Shilingi bilioni 68.31** zinakadiriwa kutumika kuwalipa fidia wananchi. Kazi nyiningine zilizotekelawa ni kufanya malipo ya awali (*advance payment*) kwa Wakandarasi wote wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme na kumpata Mkandarasi wa kujenga kituo kipyä cha kupoza umeme cha Kisongo Mkoani Arusha.

Vilevile, taratibu za kumpata Mkandarasi atakayesambaza umeme katika vijiji 21 vinavyopitiwa na Mradi zinaendelea.

65. *Mheshimiwa Spika*, kazi zilizopangwa kufanyika mwaka 2018/19 ni Serikali kuwalipa fidia wananchi watakaopisha ujenzi wa Mradi na Wakandarasi kuendelea na shughuli za ujenzi wa Mradi. **Shilingi bilioni 15** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza kazi hizo. Utekelezaji wa Mradi huu ulianza mwezi Machi, 2017 na unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2019.

Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa KV 400 kutoka Mtwara - Somanga Fungu

66. *Mheshimiwa Spika*, Mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa **KV 400** yenye urefu wa kilomita 253 kutoka Mtwara hadi Somanga Fungu na ujenzi wa kituo cha kupoza umeme katika Manispaa ya Mtwara. Katika kipindi cha mwaka 2017/18 kazi zilizotekelawa ni kufanya Upembuzi Yakinifu ulioanza mwezi Julai, 2017 na unatarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2018 pamoja na tathmini ya athari za mazingira.

67. *Mheshimiwa Spika*, kazi zilizopangwa kutekelezwaw kwa mwaka 2018/19 ni kukamilisha: Upembuzi Yakinifu; Taarifa ya Athari za Mazingira; taratibu za ufadhili wa Mradi; uwekaji wa alama za mipaka na kutathmini mali za wananchi watakaopisha eneo la Mradi; utafutaji wa Mshauri Mwelekezi kwa ajili ya kusimamia utekelezaji wa Mradi; na upatikanaji wa Mkandarasi wa ujenzi. Mradi huu utafadhiliwa na Serikali ya Japan kupitia Shirika lake la JICA na unakadirisha kugharimu **Dola za Marekani milioni 231.1** sawa na takriban **Shilingi bilioni 533.49**. Fedha za nje **Shilingi bilioni 2** zimetengwa katika mwaka 2018/19 kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi. Mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Desemba, 2018 na kukamilika mwezi Machi, 2021.

Mradi wa Rusumo – Nyakanazi kV 220

68. ***Mheshimiwa Spika***, Mradi unahuusu ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa **kV 220** yenyeye urefu wa kilomita 98.2 kutoka Rusumo hadi Nyakanazi. Gharama za Mradi ni **Dola za Marekani milioni 35** sawa na takriban **Shilingi bilioni 80.79**. Katika kipindi cha mwaka 2017/18 kazi zilizotekelozwa ni pamoja na kukamilisha: usanifu wa Mradi; uandaaji wa taarifa ya mpango wa mazingira; utangazaji wa zabuni kwa ajili ya kumpata Mkandarasi; na uhakiki wa fidia kwa wananchi watakaopisha Mradi. Jumla ya **Shilingi bilioni 5.19** zinakadiriwa kutumika kuwalipa fidia wananchi watakaopisha Mradi. Kwa mwaka 2018/19 kazi zilizopangwa kufanyika ni: kukamilisha maandalizi ya mkatuba wa ujenzi na kumpata Mkandarasi wa Mradi; kuwalipa fidia wananchi; na kuanza ujenzi wa Mradi. Fedha za nje **Shilingi bilioni 5** zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi. Mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Julai, 2018 na kukamilika mwezi Julai, 2019.

MIRADI YA KUBORESHA NJIA ZA KUSAMBAZA UMEME

Mradi wa Kuboresha Vituo 10 vya Kupoza Umeme

69. ***Mheshimiwa Spika***, Mradi huu unahuusu ujenzi na uboreshaji wa vituo 10 vya kupoza umeme ambavyo ni Mlandizi, Chalinze, Mufindi, Mwakibete, Zuzu, Tabora, Nyakato, Musoma, Kibeta na Same. Vilevile, Mradi unalenga kuboresha Mfumo wa Usimamizi na Upatikanaji wa *Data (Supervisory Control and Data Acquisition - SCADA/Energy Management System -EMS)* pamoja na kuunga waya wa mawasiliano (*optic fiber*) wenye urefu wa jumla ya kilomita 1,345 kwa vituo vya Kanda ya Kusini Magharibi, Kanda ya Ziwa na maeneo ya Kondoa, Babati, Mbulu na Karatu ambayo hayana *optic fiber*. Gharama za Mradi zinakadiriwa kuwa **Euro milioni 53** sawa na takriban **Shilingi bilioni 133.45** na unafadhiliwa na Taasisi ya Maendeleo ya Ufaransa (AFD). Katika kipindi cha mwaka 2017/18 kazi iliyofanyika ni kumpata Mshauri Mwelekezi kwa ajili ya kusimamia utekelezaji wa Mradi na anatarajiwa kuanza kazi mwezi Julai, 2018.

70. ***Mheshimiwa Spika***, kazi zilizopangwa kufanyika mwaka 2018/19 ni pamoja na: kukamilisha durusu ya wigo wa kazi (*Scope of Work*); kufanya tathmini ya athari kwa jamii na mazingira (ESIA); kuandaa michoro (*Conceptual Design*); kuwapata Wakandarasi; na kuanza utekelezaji wa Mradi. Mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2020.

Mradi wa TEDAP wa kuboresha njia za usambazaji umeme (*Distribution*) katika mikoa ya Dar es Salaam, Arusha na Kilimanjaro

71. ***Mheshimiwa Spika***, kwa kipindi cha mwaka 2017/18 ufungaji wa vifaa vyta kuongozea na kulinda mitambo (*control and protection*) pamoja na transfoma umekamilika katika vituo vyote 19 na vituo 18 vimewashwa na vinatumika. Aidha, ujenzi wa njia za msongo wa KV 33 na 11 katika Mikoa ya Dar es Salaam, Arusha na Kilimanjaro umekamilika kwa **asilimia 100**. Kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa mwaka 2018/19 ni: kukamilisha kazi zilizobaki katika njia ya msongo wa KV 132 ya Mbagala kwenda Kurasini pamoja na kituo cha kupoza umeme cha Kurasini. Fedha za nje **Shilingi bilioni 6.4** zimetengwa katika mwaka 2018/19 kwa ajili ya malipo ya Mkandarasi. Kazi hizo zinatarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2018.

Mradi wa Kuboresha Mfumo wa Usambazaji Umeme katika Jiji la Dodoma chini ya Ufadhilli wa JICA

72. ***Mheshimiwa Spika***, Mradi huu utahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa KV 132 kutoka Zuzu kwenda Msalato na kutoka Zuzu kwenda Kikombo pamoja na ujenzi wa vituo viwili (2) vipyta vyta kupoza umeme katika maeneo ya Msalato na Kikombo Mkoani Dodoma. Kazi nyingine ni ujenzi wa njia za kusambaza umeme wa msongo wa KV 33 katika Jiji la Dodoma. Lengo la mradi huu ni kuijandaa na ongezeko la mahitaji ya umeme yanayokadiriwa kufikia **MW 200** ifikapo mwaka 2020 kutoka mahitaji ya juu ya sasa ya **MW 28** kutokana na Serikali kuhamishia shughuli zake Makao Makuu Jijini Dodoma. Katika kipindi cha mwaka 2017/18 kazi zilizofanyika ni pamoja na

Serikali kuwasilisha maombi ya ufadhili wa Mradi kwa Serikali ya Japan kupitia Shirika lake la Maendeleo la JICA. Kazi zilizopangwa kwa mwaka 2018/19 ni kukamilisha taratibu za ufadhili wa Mradi na kuanza utekelezaji. Mradi unatarajiwa kukamilika mwaka 2020/21.

**Mradi wa Usambazaji Umeme kwa Maeneo ya Mijini
(Urban Electrification Program)**

73. ***Mheshimiwa Spika***, Mradi huu unahusu kuongeza kasi ya kuunganisha wateja mijini na kupanua miundombinu ya usambazaji umeme ili kuhamasisha ujenzi wa viwanda na kufikisha umeme katika makazi na maeneo ya huduma za jamii. Kwa mwaka 2017/18 Serikali iliwasilisha maombi katika Benki ya AfDB kwa ajili ya ufadhili wa Mradi ambapo Benki hiyo imempata Mshauri Mwelekezi kwa ajili ya kuandaa Mpango Kabambe wa Usambazaji Umeme (*Distribution Master Plan*) katika mikoa minne (4) ya Dodoma, Mbeya, Arusha na Mwanza. Kazi hiyo itakapokamilika itaiwezesha AfDB kupata makadirio ya fedha zinazohitajika kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi katika mikoa husika. Kazi ya kuandaa Mpango huo inatarajiwa kufanyika katika mwaka 2018/19.

74. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali pia imewasilisha maombi Benki ya Dunia kwa ajili ya ufadhili wa Mradi katika mikoa mingine iliyobaki ya Tanzania. Bara Katika mwaka 2018/19 Benki ya Dunia itamtafuta Mshauri Mwelekezi atakayefanya Upembuzi Yakinifu ili kuainisha maeneo ya mijini yanayohitaji umeme katika mikoa hiyo. Upembuzi Yakinifu unatarajiwa kuanza mwezi Septemba, 2018 na kukamilika mwezi Septemba, 2019 ambapo fedha za nje **Shilingi bilioni 7** zimetengwa kwa ajili ya kazi hiyo.

MIRADI YA KUSAMBAZA UMEME VIJIJINI

Mradi Kabambe wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Pili (*Turnkey Phase II*)

75. ***Mheshimiwa Spika***, Mradi huu ulihusisha ujenzi wa vituo sita (6) vya kuongeza msongo wa umeme (KV 11/

33) katika miji ya Kigoma, Kasulu, Kibondo, Ngara, Mbinga na Tunduru; ujenzi wa kilomita 17,740 za njia ya msongo wa KV 33; ujenzi wa kilomita 10,970 za njia za usambazaji umeme wa msongo wa KV 0.4/0.23; ufungaji wa transfoma 4,100 za ukubwa tofauti; na uunganishaji wa wateja wa awali 250,000.

76. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2017/18 Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA) imeendelea kukamilisha utekelezaji wa Mradi Kabambe wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Pili (REA II) kwa kumalizia kazi za nyongeza (*additional scope*) na kuunganisha wateja. Hadi kufikia mwezi Desemba, 2017 Mradi huo ulikuwa umekamilika kwa **asilimia 99** kwa kufikisha miundombinu ya umeme katika vijiji 2,598 kati ya 2,697 sawa na **asilimia 96.3** na hivyo kuwezesha kuwaunganishia umeme jumla ya wateja 178,641 ambaao ni sawa na **asilimia 71.46** ya matarajio ya awali ya wateja 250,000. Zoezi la kuunganisha wateja ni endelevu kulingana na wateja wanavyolipia na kazi hiyo itaendelea kufanywa na Shirika la Umeme Nchini (TANESCO). Uunganishwaji wa wateja hao umechangia ongezeko la upatikanaji wa huduma za umeme vijijini (*access*) kufikia **asilimia 49.5**.

77. ***Mheshimiwa Spika***, utekelezaji wa Mradi huu uliokuwa umesimama katika Mikoa ya Kilimanjaro na Singida kutokana na Mkandarasi wa awali Kampuni ya Spencon Services Ltd kushindwa kuukamilisha kwa sasa unaendelea. Mradi huo unatekelezwa na Kampuni za Kitanzania za Njarita Contractors na Octopus Engineering kwa Mkoa wa Kilimanjaro na JV EMEC Engineering Dynamic and Systems na East African Fossil Co & CMG Construction Co Ltd JV kwa Mkoa wa Singida. Kazi zitakazofanyika katika mwaka 2018/19 ni: ukamilishaji wa Mradi katika Mikoa ya Kilimanjaro na Singida; kumalizia marekebisho madogo-madogo (*snags*) yaliyojitekeza katika miundombinu iliyojengwa; na TANESCO kuendelea kuwaunganisha wateja wanaolipia. Mradi katika Mikoa hii ya Kilimanjaro na Singida unatarajiwa kukamilika Mwezi Agosti 2018.

Mradi Kabambe wa Usambazaji Umeme Vijijini Awamu ya Tatu (*Turnkey Phase III*)

78. ***Mheshimiwa Spika***, Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu (REA III) unalenga: kufikisha umeme katika vijiji 7,873 ambavyo hadi kufikia mwezi Juni, 2016 vilikuwa havijafikiwa na miundombinu ya umeme. Aidha, katika kipindi cha kuanzia mwezi Februari hadi Mei, 2018 jumla ya vijiji 518 kati 7,873 vilivyobaki tayari vimeunganishiwa umeme na hivyo kubaki vijiji 7,355 vinavyoendelea kuunganishiwa umeme. Kazi zinazofanyika ni pamoja na: kujenga miundombinu ya kusambaza umeme na kufunga transfoma katika maeneo mbalimbali ikiwemo Taasisi za Umma, miradi ya maji na shughuli nyingine za kiuchumi, vitongoji na vijiji ambavyo havijafikiwa na umeme (*Turnkey III - Round One*); vijiji vilivyopitiwa na miundombinu ya usafirishajili wa umeme kuititia Mradi wa *Densification*; vijiji vilivyopo pembezoni mwa Mkuza wa njia kuu ya kusafirisha umeme wa msongo wa KV 400 kutoka Iringa hadi Shinyanga. Kazi nyingine zinazofanyika ni pamoja na ujenzi wa miundombinu ya usambazaji na ufungaji wa mifumo ya nishati jadidifu katika maeneo yaliyo mbali na Gridi ya Taifa ambayo yanahusisha visiwa vilivyomo ndani ya Maziwa na Bahari (*Off-Grid Renewable Energy Project*).

79. ***Mheshimiwa Spika***; utekelezaji wa miradi iliyopo katika Mpango wa REA III ni kama ifuatavyo:-

(i) **Mradi wa Usambazaji Umeme katika Maeneo ambayo yameshafikiwa na Miundombinu ya Umeme (*Densification*)**

80. ***Mheshimiwa Spika***, Mradi huu unahusisha kuongeza wigo wa usambazaji umeme katika vijiji, vitongoji na maeneo ambayo tayari yana miundombinu ya umeme katika vijiji 4,395 vilivyounganishwa umeme. Mradi utatekelezwa katika Mikoa yote ya Tanzania Bara na

utahusisha: ujenzi wa kilomita 18,625 za umeme wa msongo wa KV 33; kilomita 35,614 za umeme wa msongo wa KV 0.4; ufungaji wa transfoma 13,622; pamoja na uunganishaji wa wateja wa awali 992,373 kwa kipindi cha miaka mitano (5) kuanzia mwaka 2016/17 hadi mwaka 2020/21 sawa na wateja 300,000 katika utekelezaji wa REA Awamu ya Tatu Mzunguko wa Kwanza.

81. *Mheshimiwa Spika*, Mradi huu unatekelezwa kwa awamu ambapo Awamu ya Kwanza (*Densification – Round I*) ilianza mwezi Aprili, 2017 katika mikoa nane (8) ya Pwani, Tanga, Arusha, Iringa, Njombe, Mbeya, Songwe na Mara na hadi kufikia mwezi Mei, 2018 imekamilika kwa **asilimia 98**. Katika Awamu hii jumla ya vijiji 300 katи ya 305 vimepatiwa umeme pamoja na kuwaunganishia umeme wateja wa awali 12,084 katи ya 53,000. Gharama ya utekelezaji kwa awamu hii ni **Shilingi bilioni 62**. Aidha, Mradi wa *Densification – Round II* utahusisha vitongoji vilivyomo katika vijiji **4,090** vilivyosalia na unakadiriwa kugharimu jumla ya **Shilingi bilioni 1,938**. Awamu hii itaanza kutekelezwa mwezi Julai, 2018.

(ii) Mradi wa Kusambaza Umeme Vijiini Awamu ya Tatu (*Grid Extension*) – Mzunguko wa Kwanza

82. *Mheshimiwa Spika*, Mradi huu unatekelezwa katika vijiji **3,559** vya Mikoa yote ya Tanzania Bara na unahusisha ujenzi wa takriban kilomita **15,600** za njia ya msongo wa **KV 33**; kilomita **16,420** za njia za usambazaji wa msongo wa **KV 0.4**; ufungaji wa transfoma zenyе ukubwa tofauti zipatazo **6,740** na uunganishaji wa wateja wa awali **300,000**. Aidha, maombi ya vijiji **1,541** vilivyorukwa yamepokelewa na yanafanyiwa tathmini kwa ajili ya utekelezaji baada ya kupitia taratibu husika. Ongezeko hilo litafanya jumla ya vijiji vitakavyopelekewa umeme katika Mzunguko huu wa Kwanza kufikia **5,100** na kubaki na vijiji **2,773** vitakavyofikishiwa umeme katika Mzunguko wa Pili. Mradi huu wa REA utaanza mwezi Julai, 2019 na kukamilika mwaka 2020/21.

83. ***Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia mwezi Mei, 2018 katika kipindi cha miezi mitatu (3) ya ujenzi baada ya kukamilika kwa kipindi cha miezi mitatu (3) cha uhakiki wa vijiji na miezi mitatu (3) mingine ya uingizaji wa vifaa na maandalizi ya ujenzi, jumla ya vijiji 502 vinajengwa miundombinu ya umeme ikiwa ni pamoja na kusimikwa nguzo na kufungwa transfoma katika Mikoa yote Tanzania Bara isipokuwa Mikoa ya Kigoma na Katavi. Vijiji hivi vinatarajiwa kuwashwa umeme hivi karibuni na vingine vinaendelea kuwashwa umeme. Mbali na vijiji hivyo vilivyojengwa miundombinu, hadi kufikia mwezi Mei, 2018 vijiji vingine 545 vimewashwa umeme sawa na wastani wa vijiji 182 kwa mwezi ambayo ni **asilimia 92** ya lengo la kuwasha wastani wa vijiji 197 kwa mwezi. Pia, katika vijiji vilivyowashwa umeme wateja 15,073 wameunganishwa sawa na **asilimia 90** ya lengo la kuunganisha umeme wateja 16,666. Utekelezaji wa Mradi huu kwa upande wa Mkoa wa Kigoma Mkandarasi CCC – ETERN-HEI Consortium amepatikana na ataanza kazi mwezi Juni, 2018. Aidha, kwa upande wa Mkoa wa Katavi Mkandarasi atapatikana mwezi Juni, 2018 na kuanza kazi mara moja.

(iii) Mradi wa Kusambaza Umeme katika Vijiji vilivyopo pembezoni mwa Mkusa wa Njia ya Msongo wa KV 400 kutoka Iringa hadi Shinyanga

84. ***Mheshimiwa Spika***: Mradi huu unahuisha usambazaji wa umeme katika vijiji 121 vilivyo pembezoni mwa mkusa wa Mradi wa kusafirisha umeme wa msongo wa **KV 400** kutoka Iringa hadi Shinyanga ambapo jumla ya wateja 25,000 wa awali wanatarajiwa kuunganishiwa umeme. Mradi pia unahuisha upanuzi wa kituo cha kupoza umeme cha Mtera. Hadi kufikia mwezi Mei, 2018, jumla ya vijiji 25 vimefikiwa na umeme na kufanya jumla ya wateja waliounganishiwa umeme kufikia 861. Kwa upande wa upanuzi wa kituo cha kupoza umeme cha Mtera usanifu unatarajiwa kukamilika mwezi Mei, 2018. Shughuli za ujenzi wa kituo zitaanza mwezi

Julai, 2018 na kukamilika mwezi Machi, 2019. Mradi huu unagharimu **Shilingi bilioni 57** ambazo ni msaada kutoka Serikali za Sweden na Norway.

(iv) Miradi ya Uendelezaji wa Nishati Jadidifu (*Off-Grid Renewable Projects*)

85. **Mheshimiwa Spika**, Mradi huu unahusisha uwekaji wa mifumo midogo (*mini grids, micro grids and stand-alone systems*) katika maeneo ambayo yana vyanzo vya nishati mbadala kwa ajili ya kuzalisha umeme. Vilevile, Mradi unahusisha ufungaji wa mifumo ya umeme-jua katika Taasisi za Serikali na maeneo ya huduma za jamii zilizoko vijiji pamoja na kuweshesha ujenzi wa mitambo ya kuzalisha umeme kwa bayogesi katika Taasisi za Umma kwa ajili ya kupikia na kuwashia taa ili kupunguza matumizi ya kuni na mkaa ambavyo vina athari kubwa kwa mazingira.

86. **Mheshimiwa Spika**, Mradi wa Uendelezaji wa Nishati Jadidifu umegawanyika katika makundi mawili ambapo Kundi la Kwanza linahusisha usambazaji wa umeme vijiji kwa maeneo yaliyopo nje ya gridi kwa mfumo wa **Malipo kwa Matokeo (Results Based Financing - RBF)**. Katika Kundi la Kwanza, Mikataba ya miradi 22 yenye uwezo wa kuzalisha jumla ya **MW 24.4** zitakazosambazwa katika vijiji 139 na kuunganisha wateja 33,939 imesainiwa kati ya REA na Waendelezaji wa Miradi na kazi zinaendelea katika maeneo ya Mikoa ya Iringa, Njombe, Tanga, Dodoma, Singida, Lindi, Mtwara, Tabora, Mwanza, Geita na Kagera.

87. **Mheshimiwa Spika**, Kundi la Pili la Mradi huu linahusu kufunga mifumo ya umeme-jua (*solar PV systems*) katika Taasisi za Umma zikiwemo shule za sekondari, vituo vya afya na zahanati zilizopo mbali na gridi pamoja na masoko ili kuboresha huduma zinazotolewa katika taasisi hizo. Mradi huu unatekelezwa katika Wilaya nane (8) za Biharamulo, Bukombe, Chato, Sikonge, Kasulu, Kibondo, Tunduru na Namtumbo. Hadi kufikia mwezi Mei, 2018 utekelezaji wa Mradi umefikia **asilimia 92** na unatarajiwaa kukamilika mwezi Juni, 2019.

(v) **Mradi wa Usambazaji Umeme katika Vijiji vilivyopo Pembezoni mwa Miji** (*Peri-Urban Rural Electrification Program*)

88. **Mheshimiwa Spika**, Mradi huu unalenga kusambaza umeme katika vijiji vilivyopo pembezoni mwa miji ili kuboresha huduma za kijamii na kuhamasisha ujenzi wa viwanda vidogo, vya kati na vikubwa katika maeneo hayo. Wakala wa Nishati Vijijini (REA) umekamilisha usanifu wa mradi wa majaribio utakaotekelawa katika Mkoa wa Pwani na Wilaya ya Kigamboni Mkoani Dar es Salaam. Mradi huu utavinufaisha vijiji/vitongoji zaidi ya 250 na kuwaunga wateja wa awali wapatao 37,000. Mradi huu unafadhiliwa na Serikali ya Norway kwa għarama ya **Shilingi bilioni 83**. Mradi unatarajiwu kukamilika mwezi Aprili, 2019.

89. **Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Aprili, 2018 REA ilikuwa imepokea jumla ya **Shilingi bilioni 313.5** kati ya **Shilingi bilioni 469** zilizopangwa kwa mwaka 2017/18 sawa na **asilimia 67** ya bajeti. Aidha, katika mwaka 2018/19 fedha zilizotengwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya Usambazaji Umeme Vijijini ni jumla ya **Shilingi bilioni 412.08**, kati ya hiso, **Shilingi bilioni 375.38** ni fedha za ndani na **Shilingi bilioni 36.70** ni fedha za nje.

E. SEKTA NDOGO YA NISHATI JADIDIFU

90. **Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kuhamasisha uwekezaji katika vyanzo vya kuzalisha umeme nchini kwa miradi midogo ya nishati jadidifu isiyozidi **MW 10**. Katika mwaka 2017/18 EWURA imekamilisha uandaaji wa Kanuni za Uendelezaji wa Miradi Midogo chini ya MW 10 (*The Electricity (Development of Small Power Projects) Rules, 2018, GN No. 77 of 2018*). Kanuni hizi zinarahisisha uwekezaji katika miradi hiyo ambapo hupunguza muda na għarama za majadiliano ikillinganishwa na miradi mikubwa. Vilevile, EWURA imekamilisha uandaaji wa Kanuni za Kuhamasisha Matumizi Bora ya Umeme Una ozalishwa na Wateja kwa Kutumia Umeme-juu na Upepo chini ya **MW 1** (*Electricity (Net Metering) Rules, 2018, GN No. 76 of 2018*). Kanuni hizi zinatoa

mwongozo kwa wateja wa umeme wanaowekeza katika mitambo ya uzalishaji umeme-jua na upepo katika majengo yao kwa dhumuni la kupunguza matumizi ya umeme kutoka katika gridi.

(i) Nishati inayotokana na Nguvu ya Jua (*Solar Energy*)

91. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2017/18 Serikali iliwasilisha miradi mbalimbali ya umeme-jua katika Fungamano la Kimataifa la Nishati ya Jua (*International Solar Alliance*). Kupitia Fungamano hilo Serikali ya India imetenga jumla ya **Dola za Marekani milioni 385** sawa na takriban **Shilingi bilioni 888.77** kwa ajili ya kuendeleza miradi ya kuzalisha umeme wa jua katika Mikoa ya Shinyanga, Singida, Dodoma, na Kilimanjaro. Katika mwaka 2018/19, Serikali itakamilisha taratibu za kuridhia makubaliano ya *International Solar Alliance* na kuanza maandalizi ya utekelezaji wa Mradi ikiwa ni pamoja na kufanya Upembuzi Yakinifu.

92. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali kupitia TANESCO inashirikiana na Serikali ya Morocco kupitia taasisi yake ya nishati endelevu (*Moroccan Agency for Sustainable Energy -MASEN*) kuendeleza miradi ya kuzalisha umeme-jua nchini yenye jumla ya **MW 300**. Katika mwaka 2017/18 Wizara ya Nishati, TANESCO na MASEN walifanya tathmini ya awali katika maeneo ya Zuzu (Dodoma), Manyoni (Singida) na Same (Kilimanjaro) ili kufahamu ukubwa wa maeneo na kiasi cha umeme unaoweza kuzalishwa. Katika mwaka 2018/19 kazi zitakazofanyika ni kukamilisha Upembuzi Yakinifu, tathmini ya mazingira na kukamilisha taratibu za upatikanaji wa fedha za kutekeleza Mradi.

93. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2017/18 Serikali iliendelea kushirikiana na Sekta Binafsi katika kukuza uzalishaji na matumizi ya teknolojia ya nishati ya jua ambapo hadi sasa kupitia mfumo wa umeme-jua katika kaya na taasisi za huduma za jamii (shule, vituo vya afya n.k) yaani ***Solar Home System***, umeme wa **MW 16** unazalishwa. Aidha, usambazaji wa umeme kwa kutumia gridi ndogo za umeme

katika maeneo ambayo hayajafikiwa na Gridi ya Taifa na maeneo ya visiwani uliongezeka kutoka **MW 1** mwaka 2016/17 na kufikia hadi **MW 2** kwa mwaka 2017/18.

94. ***Mheshimiwa Spika***, kufuatia mafanikio makubwa yaliyopatikana katika utekelezaji wa Mradi wa awali wa majoribio wa *Solar PV Generators* kutokana na fedha za mkopo nafuu kutoka Benki ya Serikali ya Austria, Serikali itaendelea na Utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Mradi katika maeneo mbalimbali nchini. Kupitia Mradi huu jumla ya wateja 2,015 watanufaika. Kazi zitakazotekelawa katika Mwaka 2018/19 ni kuainisha vijiji na maeneo mengine ambayo hayapo katika Gridi ya Taifa ikiwemo visiwa pamoja na kuanza ujenzi. Jumla ya **Shilingi bilioni 2** fedha za nje zimetengwa Mwaka 2018/19 kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo.

(ii) Miradi ya Tungamotaka na Bayogesi

95. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali iliendelea na uhamashajji wa Sekta Binafsi ili kuongeza uzalishajji wa umeme unaotokana na Tungamotaka. Katika kipindi cha mwaka 2017/18, Uzalishajji wa umeme kutokana na chanzo hicho umefikia **MW 42** kutoka **MW 38** za mwaka 2016/17. Aidha, uhamashajji wa matumizi ya bayogesi katika mikoa yote ya Tanzania Bara ulifanyika ambapo mitambo **2,000** ilijengwa. Kwa mwaka 2018/19 miradi hii itatekelezwa kupitia Programu ya Uendelezaji wa Nishati Endelevu kwa wote.

(iii) Maporomoko Madogo ya Maji

96. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2017/18 kiwango cha uzalishajji wa umeme kupitia maporomoko madogo ya maji kiliflikia **MW 42** kutoka **MW 36.99** zilizokuwa zinazalishwa hadi mwaka 2016/17 sawa na ongezeko la **asilimia 13.5**. Ongezeko hili lilitokana na miradi ya Kiliflora (Arusha), Darakuta (Manyara) na Matembwe (Njombe). Aidha, matumizi ya nishati inayotokana na maporomoko madogo ya maji kwa ajili ya kukuza shughuli nyingine za kiuchumi

ikiwemo umwagiliaji yaliongezeka kufutia uhamasishaji wa matumizi ya nishati hiyo.

(iv) Uendelezaji wa Jotoardhi (*Geothermal*)

97. *Mheshimiwa Spika*, rasilimali ya jotoardhi hapa nchini inakadiriwa kuwa na uwezo wa kuzalisha hadi MW 5,000 za umeme. Serikali kupitia Kampuni ya Uendelezaji wa Rasilimali ya Jotoardhi Nchini (TGDC), imekamilisha tafiti nne (4) za kina (*detailed surface studies*) za uendelezaji wa rasilimali hiyo katika maeneo ya Ngozi na Kiejo-Mbaka Mkoani Mbeya, Songwe Mkoani Songwe na Luhoi Mkoani Pwani. Ili kuharakisha uendelezaji wa rasilimali ya jotoardhi, Serikali inatarajia kununua mitambo kwa ajili ya uchorongaji wa visima vya utafiti na uvunaji wa jotoardhi. Jumla ya gharama za ununuzi wa mitambo hiyo ni **Shilingi bilioni 80.50**, kati ya fedha hizo **Shilingi bilioni 66.70** ni gharama za ununuzi wa mtambo mkubwa na **Shilingi bilioni 13.80** ni gharama za ununuzi wa mtambo mdogo.

98. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2018/19 Serikali itaendelea na utekelezaji wa Mradi wa jotoardhi katika eneo la Ngozi. Kazi zitakazofanyika ni pamoja na: kuajiri Mshauri Mwelekezi wa kuandaa Mpango Kazi na kusimamia uchorongaji wa visima vya utafiti; kufanya tathimini ya ardhi hitajika na kulipa fidia; kuajiri Mkandarasi wa uchorongaji; na ujenzi wa miundombinu ya barabara na maji. Aidha, Serikali itakamilisha Upembuzi Yakinifu katika eneo la Songwe kwa ajili ya uzalishaji wa umeme na matumizi mbadala. Jumla ya **Shilingi bilioni 40.20** zimetengwa katika mwaka 2018/19 ili kutekeleza kazi zilizopangwa. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 32.50** ni fedha za ndani na **Shilingi bilioni 7.70** ni fedha za nje.

(v) Matumizi Bora ya Nishati (*Energy Efficiency*)

99. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2017/18 Serikali kupitia ufadhili wa Umoja wa Ulaya (EU) iliandaan Mkakati wa Kitaifa wa Matumizi Bora ya Nishati (*Energy Efficiency Strategy*) pamoja na kukamilisha maandalizi ya Mpango Kazi wa Matumizi Bora ya Nishati (*Energy Efficiency*

Action Plan). Umoja wa Ulaya umetenga **Euro milioni 8** sawa na takriban **Shilingi bilioni 20.14** kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango Kazi huo. Katika mwaka 2018/19 itachaguliwa Taasisi ya Umma ya Mafunzo ambayo itajengewa uwezo (*Centre of Excellence*) kwa ajili ya kutoa mafunzo ya uangalizi wa matumizi ya nishati (*energy management*) na ukaguzi wa upotevu wa nishati (*energy audit*). Aidha, wananchi wataelimishwa ili waweze kufahamu umuhimu na njia za kuepuka upotevu wa nishati kwa lengo la kuokoa fedha na kuipunguzia Serikali għarama za uwekezajji katika miundombinu ya umeme. Fedha za nje **Shilingi bilioni 1.35** zimetengwa katika mwaka 2018/19 kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo.

**(vi) Programu ya Nishati Endelevu kwa Wote
(Sustainable Energy for All - SE4ALL)**

100. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2017/18 Serikali iliingia makubaliano na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) kwa ajili ya ufadhili wa utekelezaji wa Programu ya miaka mitano (5) ya Nishati Endelevu kwa Wote (SE4All) ambapo UNDP itachangia **Dola za Marekani 350,000** sawa na takriban **Shilingi milioni 807.97** na kusaidia upatikanaji wa fedha kutoka vyanzo vingine. Katika kuendeleza vyanzo vyva nishati jadidifu, Programu ya SE4All ilisaidia upatikanaji wa taarifa za vyanzo vyva nishati ya jua na uandaaji wa miradi katika maeneo ya Zuzu (Dodoma); Manyoni (Singida); na Same (Kilimanjaro) ambapo maeneo haya kwa ujumla yana uwezo wa kuzalisha **MW 300**. Taarifa hizo zitasaidia Serikali kutafuta wawekezajji katika miradi hiyo.

101. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/19, kazi zitakazotekelawa kupyitia Programu hiyo ni pamoja na: kuendelea na uboreshaji wa miongozo mbambali itakayosaidia upatikanaji wa nishati endelevu nchini; kuandaa Mkakati wa Tungamotaka na utekelezaji wake; kujenga uwezo kwa watendaji katika kusimamia utekelezaji wa mipango na miradi ya nishati hapa nchini; kuandaa mazingira bora yatakayosaidia kukuza uwekezajji katika miradi ya Nishati Jadidifu na Matumizi Bora ya Nishati; na

kuandaa mfumo wa ukusanyaji na utunzaji wa takwimu za Nishati Jadidifu. Jumla ya **Shilingi bilioni 3** zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi huu katika Mwaka 2018/19, ambapo **Shilingi bilioni 2.5** ni fedha za nje na **Shilingi milioni 500** ni fedha za ndani.

F. SEKTA NDOGO YA MAFUTA NA GESI ASILIA

Shughuli za Utafutaji, Uzalishaji na Usambazaji wa Mafuta na Gesi Asilia Nchini

102. *Mheshimiwa Spika*, Kazi za utafutaji wa mafuta na gesi asilia zinaendelea ambapo jumla ya kampuni nane (8) zinafanya utafutaji wa mafuta na gesi asilia kupitia mikataba kumi na moja (11) ya Uzalishaji na Ugawanaji Mapato (*Production Sharing Agreement -PSA*). Katika mwaka 2017/18 Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) kwa kushirikiana na Kampuni ya Statoil zimechoronga kisima kimoja (Pilipili-1) katika kitalu Na. 2 kilichopo Bahari ya Hindi na hivyo kufanya jumla ya visima vilivyochorongwa kufikia 96. Vilevile, TPDC ikishirikiana na Kampuni ya Ndovu Resources ilifanya uhakiki wa mashapo ya gesi asilia katika kitalu cha Ruvuma, uhakiki huo umeongeza kiasi cha gesi asilia kufikia futi za ujazo bilioni 466 kutoka futi za ujazo bilioni 178 mwaka 2016/17. Hadi kufikia sasa kiasi cha gesi asilia kilichogunduliwa nchini ni Futi za Ujazo Trilioni **57.54**.

103. *Mheshimiwa Spika*, Kampuni za Heritage Rukwa (TZ) Ltd na Swala Oil and Gas Tanzania zimeendelea na maandalizi ya kuchoronga visima vyta utafutaji mafuta katika vitalu vya Rukwa Kusini na Kilosa-Kilombero sawia. Aidha, Kampuni ya Ndovu Resources imeendelea na maandalizi ya Mpango wa Uendelezaji (*Development Plan*) wa gesi asilia iliyogunduliwa katika eneo la Ntorya - Mtwara. Vilevile, Kampuni ya Dodsall Hydrocarbons imeendelea na uchukuaji wa data za mitetemo (*seismic*) katika Kitalu cha Ruvu ili kuhakiki ukubwa wa mashapo ya gesi asilia iliyogunduliwa katika kitalu hicho. Kwa upande mwingine, Kampuni za PanAfrican Energy na Maurel et Prom zimeendelea na uzalishaji wa gesi asilia katika Vitalu vya

Songo Songo na Mnazi Bay kwa wastani wa futi za ujazo milioni 95 na milioni 80 kwa siku sawia. Gesi inayozalishwa inatumika kuzalisha umeme katika mitambo ya TANESCO.

MIRADI YA UTAFITI KATIKA VITALU VYA KIMKAKATI VYA SHIRIKA LA MAENDELEO YA PETROLI NCHINI (TPDC)

(i) Vitalu Namba 4/1B na 4/1C

104. *Mheshimiwa Spika*, TPDC imeendelea na utafiti katika vitalu vyake namba 4/1B na 4/1C sambamba na taratibu za kuwapata Wabia wa Kimkakati (*Strategic Partners*) ili kushirikiana nao katika kuendeleza vitalu hivyo. Katika mwaka 2017/18 kazi zilizotekelizwa ni pamoja na kufanya tathmini ya kifedha na kiuchumi na kukamilisha tathmini ya awali kwa kutumia *data* za mitetemo za 2D ambazo zinaonesha uwepo wa mashapo mazuri ya gesi asilia katika vitalu hivyo. Kazi zitakazotekelizwa kwa mwaka 2018/19 ni ukusanyaji, uchakataji na tathmini ya *data* za mitetemo ya 3D zenye ukubwa wa kilomita za mraba 2,500. Fedha za ndani **Shilingi bilioni 2** zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi.

(ii) Kitalu cha Eyasi – Wembere

105. *Mheshimiwa Spika*, Serikali kupitia TPDC imekusanya *data* za kijiolojia na kijiofizikia kupitia *data* za mgandamizo (*Airbone Gravity Gradiometry-AGG*) na sumaku (*Magnetic*) katika Bonde la Eyasi-Wembere. Lengo la utafiti huu ni kubaini uwepo wa mashapo yenye kuhifadhi mafuta au gesi asilia katika eneo hilo. Katika mwaka 2017/18 wataalam wa Wizara ya Nishati na TPDC wameendelea kufanya mashauriano na wataalam kutoka sekta ya mafuta nchini Uganda. Aidha, mwezi Oktoba, 2017 wataalamu hao walitembelea eneo la utafiti pamoja na kuanda mpango kazi wa kufanya tafiti za kina za kijiolojia na kijiofizikia. Kwa mwaka 2018/19, TPDC imepanga: kutafuta Mbia na kuomba leseni ya utafiti; kufanya Tathmini ya Athari za Mazingira (EIA) kwa ajili ya ukusanyaji wa *data* za mitetemo za 2D; pamoja na kukusanya, kuchakata na kutafsiri *data* za mitetemo zenye

urefu wa kilomita 150 katika eneo la Manonga. Fedha za ndani **Shilingi bilioni 2** zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji kwa shughuli za Mradi.

(iii) Kitalu cha Mnazi Bay Kaskazini

106. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2017/18, shughuli zilizotekelawa katika kitalu hiki ni: kufanya tathmini ya kifedha na kiuchumi; kuomba leseni ya kitalu; kumpata Mshauri Mwelekezi wa kuchakata na kutafsri *data* za mitetemo za 3D; maandalizi ya kuchukua zaidi *data* za mitetemo za 3D; kuandaa Mkataba Kifani wa Ushirikiano (*Model Joint Operating Agreement*) utakaozingatia maboresho ya mikataba inayopitiwa na Serikali ili kuiboresha; na kuanza mchakato wa kumpata Mbia wa Kimkakati wa Mradi. Kwa mwaka 2018/19, shughuli zilizopangwa kufanyika ni pamoja na: kufanya maandalizi ya uchorongaji kwa kushirikiana na Mshauri Mwelekezi; kuanza ununuzi wa vifaa vyta awali vitakavyotumika katika kuchoronga kisima; kutafuta mkandarasi wa kukusanya *data* zaidi za mitetemo za 3D; na kuandaa na kutafsiri *data* zenye ukubwa wa kilomita za mraba 141.63. Fedha za ndani za Shirika **Shilingi bilioni 13.28** zimetengwa kwa ajili ya shughuli hizo.

(iv) Kitalu cha Songo Songo Magharibi

107. ***Mheshimiwa Spika***, Kitalu cha Songo Songo Magharibi kimeonesha kuwa na mategemeo chanya ya uwepo wa gesi asilia. Katika kipindi cha mwaka 2017/18, TPDC imekamilisha kutafsiri *data* za mitetemo za 2D na kubaini maeneo yatakayochorongwa visima. Vilevile, TPDC imeanza taratibu za kumtafuta Mbia wa Kimkakati ambapo Mkataba Kifani wa Ushirikiano (*Model Joint Operating Agreement*) umeandaliwa utakaozingatia maboresho ya mikataba inayoendelea kufanyiwa mapitio na Serikali kwa lengo la kuiboresha. Kwa mwaka 2018/19 shughuli zilizopangwa kufanyika ni pamoja na kumpata Mbia wa Kimkakati wa kukusanya, kuchakata na kutafsiri *data* zaidi za mitetemo za 3D katika eneo la kilomita za mraba 306. Fedha za ndani za

Shirika **Shilingi bilioni 11.3** zimetengwa kwa ajili ya shughuli hizo.

MIRADI YA USAMBAZAJI WA GESI ASILIA NCHINI

108. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali kupyitia TPDC inatekeleza miradi ya usambazaji wa gesi asilia kwa kuunganisha miundombinu ya usambazaji wa gesi hiyo katika matoleo ya bomba linalotoka Madimba Mkoani Mtwara na Songo Songo Mkoani Lindi hadi Dar es Salaam. Uunganishaji wa wateja umeongeza matumizi ya gesi asilia hadi kufikia wastani wa futi za ujazo milioni 175 kwa siku (mwaka 2017/18) kutoka futi za ujazo milioni 145 kwa siku (mwaka 2016/17) sawa na ongezeko la **asilimia 17**.

(i) Miradi ya Kusambaza Gesi Asilia Viwandani

109. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2017/18, TPDC imeendelea kutafuta wateja zaidi wa gesi asilia kwa matumizi ya viwanda pamoja na ujenzi wa miundombinu ya kusambazia gesi hiyo kwa wateja. Shirika limepitia na kuhakiki michoro (*Design Drawings*) ya awali iliyowasilishwa na Mkandarasi kwa ajili ya kuunganisha gesi asilia katika viwanda vya Lodhia Steel, Knauf Gypsum na Bakhressa Food Products vilivyopo Mkuranga. Mkandarasi wa ujenzi wa bomba la kusambaza gesi asilia katika viwanda vya Coca-Cola Kwanza Limited na BIDCO Industry vilivyoko eneo la viwanda Mikocheni ameanza kazi mwezi Aprili, 2018. Kiwanda cha Goodwill Ceramic Tanzania Limited kilichopo Mkuranga kimeendelea kutumia gesi asilia kwa ajili ya shughuli za uzalishaji kiwandani hapo. Aidha, awamu ya kwanza ya ujenzi wa miundombinu ya kupeleka gesi asilia katika kiwanda cha Dangote Cement Tanzania Limited kilichopo Mtwara ulikamilika mwezi Septemba, 2017. Hivi sasa Kampuni ya Dangote inaendelea na maandalizi ya awali ya utumiaji wa gesi asilia (*Testing and Commissioning*).

110. ***Mheshimiwa Spika***, kwa mwaka 2018/19, TPDC itakamilisha majadiliano na kuingia mikataba ya kusambaza gesi asilia katika kiwanda cha Knauf Gypsum kilichopo

Mkuranga Mkoani Pwani. Vilevile, TPDC itafanya majadiliano na wateja wapya wa viwanda walioonesha nia ya kuunganishiwa gesi asilia wakiwemo LN Future Building Materials Co. Ltd na Kings Alluminium vilivyopo Mkuranga-Pwani pamoja na MM-1 Intergrated Steel Mills Ltd kilichopo Mikocheni.

(ii) Miradi ya Kusambaza Gesi Asilia Majumbani

111. *Mheshimiwa Spika*, hadi sasa jumla ya nyumba 70 zilizopo maeneo ya Mikocheni, Dar es Salaam zimeunganishwa na miundombinu ya gesi asilia. Katika mwaka 2017/18, miundombinu ya kuunganisha gesi asilia majumbani imeanza kutandazwa katika Jiji la Dar es Salaam. Maeneo yanayoanza kupelekewa gesi kuititia Mradi huu ulioanza mwezi Aprili, 2018 ni pamoja na Ubungo, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Makongo Juu, Survey, Sinza, Shekilango, Mwenge, Viwanda vya Coca Cola na maeneo ya Mikocheni. Mradi huu ni endelevu kutegemeana na mahitaji yatakavyokuwa yanajitokeza katika maeneo husika. Zaidi ya wateja 1,000 wanatarajiwa kufikiwa na miundombinu ya kuunganisha gesi katika awamu ya kwanza.

112. *Mheshimiwa Spika*, Mradi mwingine unaofanyiwa maandalizi utakaotekelzwa pamoja na Mradi huu ni usambazaji wa gesi asilia katika maeneo ya Magereza, Magomeni, Hospitali Kuu ya Mkoa na Chuo cha Ualimu katika Manispaa ya Mtwara. Kazi inayofanyika sasa hivi ni ukamilishaji wa taratibu za kuunganisha bomba lenye msukumo mdogo (*low pressure*) kwa ajili ya kupeleka gesi asilia katika nyumba. Kazi hizi zitakamilika mwezi Juni, 2018 na kazi ya usambazaji wa gesi asilia itaanza mwanzoni mwa mwezi Julai, 2018 ambapo wateja wa awali wanatarajiwa kuwa zaidi ya 580. Kazi hii itakuwa endelevu ambapo maeneo mengine yataendelea kusambaziwa gesi asilia baadae ikiwemo vijiji vinavyopitiwa na bomba la gesi asilia kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam.

113. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/19, TPDC inatarajia kuweka miundombinu itakayowezesha zaidi ya nyumba 2,000 kuunganishiwa gesi asilia pamoja na kusambaza gesi asilia katika Mgahawa wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Soko la Feri la Jijini Dar es Salaam na Kampuni ya Usimamizi wa Mabasi ya Mwendokasi Jijini Dar es Salaam (UDART). Ili kuweseha uunganishwaji wa wateja hao, uchambuzi wa kifedha pamoja na Tathmini ya Athari za Mazingira na Jamii (*Environmental and Social Impact Assessment-ESIA*) utaendelea kufanyika. Fedha za ndani za TPDC **Shilingi bilioni 20.9** zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi huu.

**Ujenzi wa Miundombinu ya Usambazaji Gesi Asilia
katika Mikoa ya Dar es Salaam, Lindi, Mtwara, Pwani,
Morogoro, Tanga na Dodoma**

114. ***Mheshimiwa Spika***, Mradi huu unajumuisha usambazaji wa gesi asilia kwa njia ya bomba (*Piped Natural Gas-PNG*), ujenzi wa vituo vyta gesi asilia iliyoshindiliwa (*Compressed Natural Gas (CNG) stations*) na miradi midogo ya gesi kimiminika (*Mini-LNG*). Katika mwaka 2017/18, TPDC imeandaa Mkataba wa Ushirikiano wa Ubia (*Joint Venture Agreement*) pamoja na Hati ya Zabuni (*Tender Document*) ili kuwapata wawekezaji kwa njia ya ushindani. Aidha, Mpango wa utekelezaji wa Mradi huu upo katika hatua za mwisho za mapitio kwa kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) pamoja na kitengo cha PPP cha Wizara ya Fedha na Mipango. Awamu ya kwanza ya utekelezaji, inahusisha utafutaji wa Mbia atakayeshirikiana na TPDC kutekeleza Mradi kwa Mkoa wa Dar es Salaam. Mikoa mingine ya Lindi, Mtwara, Morogoro, Tanga na Dodoma iliyoinishwa katika Mpango itafuata baada ya kukamilika kwa Upembuzi Yakinifu. Katika mwaka 2018/19, fedha za ndani **Shilingi bilioni 2** zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi. Mradi unatarajiwa kuanza mwezi Novemba, 2018 baada ya taratibu zote kukamilika na utatekelezwa kwa muda wa miaka mitano (5).

Mradi wa Ujenzi wa Kiwanda cha Mbolea Mkoani Lindi

115. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali kupitia TPDC imeendelea na majadiliano kuhusu Mradi wa kujenga kiwanda kikubwa cha Mbolea katika eneo la Kilwa Masoko, Mkoani Lindi ambacho kitazalisha mbolea ya Amonia tani 2,200 na Urea tani 3,850 kwa siku. Mradi utatekelezwa na Kampuni ya Ubia ya Mradi *Tanzania Mbolea and Petrochemicals Company Limited (TAMPCO)* (inayohusisha kampuni za Ferostaal ya Ujeruman, Fauji ya Pakistani, Haldo Topsøe ya Denmark na TPDC), ambayo imeundwa na kupata hati ya uwekezaji (*Certificate of Incentive*). Mradi huu pamoja na mambo mengine utasaidia upatikanaji wa mbolea kwa urahisi ili kukuza Sekta ya Kilimo na uchumi wa nchi kwa ujumla. Mradi unakadiriwa kugharimu **Dola za Marekani bilioni 1.92** sawa na takriban **Shilingi triliioni 4.43** katika utekelezaji wake.

116. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/19 Serikali itaendelea na majadiliano ya bei ya gesi asilia kwa ajili ya matumizi ya uzalishaji wa mbolea nchini. Serikali kupitia TPDC itasimamia tathmini ya utwaaji ardhi na usanifu wa kihandisi wa upelekaji wa gesi asilia kwa njia ya bomba kuanzia Nangurukuru hadi Kiwandani. Kazi hizi zitatekelezwa kwa kutumia fedha za ndani za Shirika ambapo kiasi cha **Shilingi milioni 266.4** kitatumika.

Mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia (LNG Project)

117. ***Mheshimiwa Spika***, Mradi wa LNG unalenga kusindika gesi asilia iliyogunduliwa katika kina kirefu cha Bahari ili iweze kutumika ndani na kusafirishwa na kuuzwa nje ya nchi. Jumla ya gharama za Mradi zinakadiriwa kuwa **Dola za Marekani bilioni 30** sawa na takriban **Shilingi triliioni 69.25**. Katika mwaka 2017/18 kazi zilizofanya ni pamoja na marudio na ukamilishaji wa uthamini ya eneo la mradi, kukamilisha tafiti za kihandisi na uchaguzi wa teknolojia (*concept selection*) ya uzalishaji na usafirishaji wa gesi asilia kutoka

baharini hadi nchi kavu na kuendelea kwa majadiliano ya kimkataba (*Host Government Agreement - HGA*) kati ya Serikali na wawekezaji. Katika mwaka 2018/19, kazi zinazotekelawa ni pamoja na: kufanya Usanifu wa Awali wa Kihandisi (*Pre-FEED*) kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda cha LNG; kuendelea na majadiliano ya HGA na ulipaji wa fidia kwa wananchi watakaopisha Mradi.

118. ***Mheshimiwa Spika***, faida zinazotarajiwa kutokana na Mradi huo ni pamoja na kuongezeka kwa mapato ya Serikali kupitia mauzo ya gesi asilia katika soko la kimataifa, upatikanaji wa nishati ya uhakika kwa ajili ya matumizi ya ndani, upatikanaji wa ajira kwa wazawa, ukuaji wa Miji ya Lindi na Mtwara ikiwa ni pamoja na upanuzi wa bandari na uwanja wa ndege, upatikanaji wa malighafi za viwanda kama vile mbolea, plastiki na kemikali (Petrochemicals). Fedha za ndani **Shilingi bilioni 6.5** zimetengwa kwa mwaka 2018/19 kwa ajili ya kazi hizo na ujenzi wa Mradi unatarajiwa kuanza mara baada ya kukamilika kwa majadiliano ya HGA.

Mradi wa Kusafirisha Gesi Asilia kutoka Tanzania kwenda Uganda

119. ***Mheshimiwa Spika***, Mradi unahu ujenzi wa bomba la kusafirisha gesi asilia kutoka Dar es Salaam (Tanzania) kwenda nchini Uganda kupitia Mikoa ya Pwani, Tanga, Manyara, Dodoma, Singida, Tabora, Shinyanga, Geita na Kagera. Utekelezaji wa Mradi huu utasaidia upatikanaji wa gesi asilia katika mikoa itakayopitiwa na bomba hilo na mikoa mingine ya jirani. Katika mwaka 2018/19 fedha za ndani **Shilingi bilioni 1.5** zimetengwa kwa ajili ya Upembuzi Yakinifu utakaobainisha gharama za Mradi na namna bora ya utekelezaji wake. Kulingana Mpango Kabambe wa Matumizi ya Gesi Asilia (NGUMP) kiasi cha futi za ujazo triliioni 3.2 kinakadiriwa kusafirishwa kwa njia ya bomba kwenda nchi za jirani ikiwemo Uganda. Serikali za Tanzania na Uganda zinaendelea na majadiliano ili utekelezaji wa mradi huu uende sambamba na ule wa EACOP.

MIRADI YA USAFIRISHAJI WA MAFUTA

Mradi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) kutoka Kabaale (Uganda) hadi Bandari ya Tanga (Tanzania)

120. *Mheshimiwa Spika*, Ujenzi wa Mradi huu utatekelezwa na Kampuni Maalum ya Mradi (*Special Purpose Vehicle*) itakayoundwa na wabia wa Mradi ambao ni Kampuni za Total (Ufaransa), Tullow (Uingereza), CNOOC (China) pamoja na Serikali za Tanzania na Uganda. Gharama za Mradi zinakadiriwa kufikia **Dola za Marekani bilioni 3.5** sawa na takriban **Shilingi trillioni 8.07**.

121. *Mheshimiwa Spika*, Hatua za awali za utekelezaji wa Mradi huu zilianza mwezi Januari, 2018. Kazi zilizotekelzwa ni pamoja na: Usanifu wa Kihandisi wa Mradi (*Front End Engineering Design*); kuridhiwa kwa Mkataba wa *Intergovernmental Agreement (IGA)* na Mabunge ya nchi za Tanzania na Uganda; kulipa fidia ya utwaaji ardhi kwa eneo la Chongoleani, tathmini ya fidia kwa maeneo ya kambi za wafanyakazi na hifadhi ya mabomba; utafiti wa *Geological, Geotechnical* na *Geophysical* katika eneo la Chongoleani; na utafiti wa *Geological* na *Geophysical* kwenye njia ya bomba. Katika kipindi hiki majadiliano ya HGA pamoja na maandalizi ya majadiliano ya mkataba wa Ubia (*Shareholding Agreement - SHA*) yameendelea kufanyika. Kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa mwaka 2018/19 ni pamoja na: kukamilisha majadiliano ya HGA na SHA; kukamilisha Usanifu wa Kina wa Kihandisi (*Detailed Engineering Design*); na kuwalipa fidia wananchi watakaopisha utekelezaji wa Mradi. Kiasi cha **Shilingi bilioni 54.2** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji. Ujenzi wa Mradi unatarajiwa kuanza mwezi Juni, 2018 na kukamilika mwaka 2020.

Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Safi (White Petroleum Products) kutoka Dar es Salaam (Tanzania) hadi Ndola (Zambia)

122. *Mheshimiwa Spika*, Mradi huu upo katika hatua za awali na unahusu ujenzi wa bomba lenye urefu wa kilomita

1,710 litakalojengwa sambasamba na bomba la TAZAMA linalosafirisha Mafuta Ghafi (*Crude Oil*) baada ya kuridhiwa na Serikali za nchi za Tanzania na Zambia. Ili kuleta manufaa katika maeneo yatakayopitiwa na bomba hili, Mradi utahusisha ujenzi wa matoleo ya mafuta (*take-off points*) katika maeneo ya Morogoro, Iringa, Njombe, Mbeya na Songwe. Katika mwaka 2017/18, Andiko la Awali la Mradi (*Project Concept Paper*) kuhusu namna Mradi utakavyotekelawa na faida zake liliandaliwa. Aidha, eneo kwa ajili ya ujenzi wa matenki ya hifadhi ya mafuta Morogoro limepatikana na hatua za utwaaji ardhi zinaendelea. Katika mwaka 2018/19, shughuli iliyopangwa kutekelezwa ni kufanya Upembuzi Yakinifu (*Feasibility Study*) utakaoonesha gharama halisi za Mradi na namna bora ya kutekeleza Mradi. Jumla ya **Shilingi bilioni 1.5** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kugharamia shughuli hizo.

Mradi wa Hifadhi ya Kimkakati ya Mafuta ya Akiba ya Dharura Nchini

123. *Mheshimiwa Spika*, uanzishaji na usimamizi wa Hifadhi ya Kimkakati ya Mafuta ya Akiba ya Dharura (*Strategic Petroleum Reserve - SPR*) ni muhimu kwa nchi ili kujilinda na mabadiliko hasi ya upatikanaji wa mafuta Duniani yanayoweza kutokea. Katika utekelezaji wa Mradi huu, miongozo mbalimbali ikiwemo kanuni (*SPR regulations*), mwongozo wa usimamizi (*SPR manual*) na mfumo wa bei (*price template*) imekamilika. Katika mwaka 2017/18, kazi zilizotekelawa ni pamoja na kumpata Mshauri Mwelekezi na Mkandarasi wa kuondoa mabaki ya mafuta (*sludge*) katika Tenki Na.8 la TPDC liliopo TIPER litakalotumika kutunzia mafuta ya dharura. TPDC imeendelea na taratibu za kupata ardhi kwa ajili ya ujenzi wa matenki mengine ya kuhifadhia mafuta katika Manispaa za Kigamboni na Tanga. Kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa mwaka 2018/19 ni kukarabati Tenki Na. 8 ili kufanikisha uanzishwaji wa hifadhi hiyo nchini. **Shilingi bilioni 14.5** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa shuguli za Mradi.

Mradi wa Usimamizi wa Rasilimali za Mafuta na Gesi Asilia Nchini

124. ***Mheshimiwa Spika***, Mradi huu unalenga kuchochea maendeleo ya tasnia ya uzidua (*extractive industry*) katika sekta ya mafuta na gesi asilia nchini na kuimarisha uendelezaji wa rasilimali hizo zinazotoa mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi. Mradi huu utaiwezesha Serikali kuimarisha uwezo wa kukusanya na kusimamia mapato yanayotokana na rasilimali za mafuta na gesi asilia hususan katika maeneo ya utafutaji, uzalishaji na uendelezaji wa rasilimali hizo. Mradi unatarajiwu kugharimu **Dola za Marekani milioni 29.53** sawa na takriban **Shilingi bilioni 68.17**. Katika Mradi huu Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB) itachangia **Dola za Marekani milioni 26.58** sawa na takriban **Shilingi bilioni 61.35** zikiwa ni mkopo wa masharti nafuu na Serikali itachangia **Dola za Marekani milioni 2.95** sawa na takriban **Shilingi bilioni 6.8**.

125. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/19, Taasisi za Serikali zinazohusika na Mradi huu zitajengewa uwezo katika maeneo ya usimamizi wa rasilimali za mafuta na gesi asilia. Jumla ya **Shilingi bilioni 14** zimetengwa ambapo **Shilingi bilioni 2** ni fedha za ndani na **Shilingi bilioni 12** ni fedha za nje. Mradi unatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu (3) kuanzia mwezi Juni, 2018.

Udhibiti wa Shughuli za Mkondo wa Juu wa Mafuta na Gesi Asilia Nchini

126. ***Mheshimiwa Spika***, kwa mwaka 2017/18, Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli (*Petroleum Upstream Regulatory Authority -PUR*A) imeendelea kusimamia shughuli za utafutaji, uendelezaji na uzalishaji wa gesi asilia katika kampuni nane (8) kuititia PSA 11 zinazofanya shughuli hizo nchini. Katika kutekeleza jukumu hilo kazi zilizotekelizwa ni: kusimamia na kudhibiti uchorongaji wa kisima cha Pilipili-1 katika kitalu Na. 2 unaotekelizwa na Kampuni ya Statoil ikishirikiana na TPDC; kufanya uhakiki na

kuidhinisha Mpango Mkakati na Bajeti kwa PSA 10; na kuanza ukaguzi wa hesabu za PSA ambapo ukaguzi wa PSA ya kitalu Na.2 umekamilika.

127. ***Mheshimiwa Spika***, kwa mwaka 2018/19, Serikali kupitia PURA itasimamia shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi asilia zikiwemo uchorongaji wa kisima cha Hammerkop-1 katika kitalu cha Rukwa kusini na kisima cha Kito-1 katika kitalu cha Kilosa-Kilombero. Mamlaka itasimamia ukusanyaji, uchakataji na tathmini ya *data* za mitetemo za 2D yenye jumla ya urefu wa kilomita za mstari 840 zitakazokusanywa katika vitalu vya Ruvuma na Eyasi-Wembere. PURA itatathmini pia *data* za mitetemo za 3D zenye jumla ya kilometra za mraba 1,357.63 katika vitalu vya Kiliwani Kaskazini, Ruvuma, Songo Songo Magharibi, Mnazi Bay Kaskazini na 4/1B. PURA itaendelea kusimamia uzalishaji wa gesi asilia katika Vitalu vya Songo Songo na Mnazi Bay na kufanya ukaguzi wa hesabu za PSA 10. Fedha za ndani **Shilingi bilioni 1.69** zimetengwa kwa ajili ya kugharamia kazi hizo.

Mfumo wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (*Petroleum Bulk Procurement System*) Nchini

128. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali kupitia Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (*Petroleum Bulk Procurement Agency- PBPA*) imeendelea kusimamia Mfumo wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (*Bulk Procurement System - BPS*). Kwa kipindi cha Mwezi Januari hadi Desemba, 2017 jumla ya lita bilioni 5.36 za mafuta ziliingizwa nchini. Lita bilioni 3.19 sawa na **asilimia 60** za mafuta yaliyoingizwa zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya ndani na lita bilioni 2.17 sawa na **asilimia 40** zilikuwa kwa ajili ya nchi jirani. Mafuta kwa ajili ya matumizi ya ndani yalipungua kwa **asilimia 3.3** kutoka lita bilioni 3.302 mwaka 2016 hadi lita bilioni 3.19 mwaka 2017. Kupungua huko kulitokana na mitambo ya kuzalisha umeme pamoja na baadhi ya viwanda kutumia gesi asilia kuzalisha nishati badala ya mafuta ya Dizeli na Mafuta mazito (HFO). Mafuta yaliyoagizwa kwa ajili ya nchi jirani za Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Rwanda, Uganda na Zambia yalipungua kwa **asilimia 0.8** kutoka lita bilioni 2.185 mwaka

2016 hadi lita bilioni 2.168 mwaka 2017. Upungufu huo ulitokana na baadhi ya kampuni za mafuta kubadili matumizi ya mafuta yaliyoagizwa kwa ajili ya nchi jirani na kutumika hapa nchini (*localization of transit fuel*) **Kielelezo Na 10.**

129. ***Mheshimiwa Spika***, katika kupunguza upotevu wa mafuta na gharama zinazotokana na muda unaotumika kwa meli kupakua mafuta bandarini (*Demurrage Charges*), Serikali inatarajia kuanza upokeaji mafuta sehemu moja (*Single Receiving Terminal - SRT*). Katika kipindi cha mpito utaratibu wa SRT utaanza kwa kutumia miundombinu ya kuhifadhiya mafuta ya TIPER ambayo Serikali inamiliki hisa **asilimia 50** hadi hapo Serikali itakapojenga miundombinu yake. Utaratibu wa SRT utakuwa chini ya usimamizi wa Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA). Katika kufanikisha utaratibu huo, kazi zinazotekelezwa kwa sasa ni pamoja na: uboreshaji wa Kanuni za Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja za Mwaka 2017; uandaaji wa Kanuni za Usimamizi wa SRT; uundaji wa Timu itakayofanya ufuatiliaji na tathmini ya utaratibu wa SRT; na uandaaji wa mikataba itakayotumika katika kutekeleza utaratibu wa SRT.

Matumizi ya Bandari za Tanga na Mtwara katika Upakuaji wa Mafuta

130. ***Mheshimiwa Spika***, kutokana na mafanikio yaliyopatikana kwa kuanza kutumia Bandari ya Tanga kupokea mafuta kwa ajili ya matumizi ya Mikoa ya Tanga, Kilimanjaro, Arusha na Manyara, Serikali itaanza kutumia Bandari ya Mtwara kupokea mafuta kwa ajili ya matumizi ya Mikoa ya Lindi, Mtwara, Ruvuma, Njombe, Mbeya, Songwe, Rukwa, Katavi pamoja na nchi za jirani. Bandari ya Mtwara itaanza rasmi kupokea mafuta kwa kutumika mfumo wa uagizaji kwa pamoja mwezi Juni, 2018. Utaratibu wa kupanga bei ya mafuta yatakayoingizwa kuititia Bandari hiyo utazingatia taratibu zilizotumika katika Bandari ya Tanga. Miundombinu ya kuhifadhiya mafuta ilyopo katika Bandari hiyo ina uwezo wa kutunza lita milioni 26 zinazotosheleza mahitaji ya ukanda huo kwa sasa. Hata hivyo, kutokana na kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi katika maeneo hayo,

Serikali inawakaribisha wawekezaji kuwekeza zaidi katika ujenzi wa miundombinu ya kuhifadhi mafuta katika Bandari za Tanga na Mtwara.

Matumizi ya Gesi inayotokana na Petroli (*Liquified Petroleum Gas - LPG*)

131. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali inaendelea kukamilisha utaratibu wa uagizaji wa LPG kwa mfumo wa pamoja ambapo kwa mwaka 2017/18 Mshauri Mwelekezi anakamilisha utafiti kuhusu viwango vya ubora wa LPG unaohitajika kwa ajili ya matumizi nchini na ujenzi wa miundombinu ya kupokelea na kuhifadhi gesi hiyo. Kwa mwaka 2018/19 EWURA itaandaa mwongozo wa uagizaji wa LPG kwa mfumo wa pamoja baada ya Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kuititia na kuidhinisha viwango vitakavyopendekezwa na Mshauri Mwelekezi. Aidha, Serikali imeendelea kutoa elimu kuhusu matumizi bora ya LPG katika maeneo mbalimbali nchini ili kulinda afya, usalama na mazingira ya watumiaji. Vilevile, Serikali kuititia EWURA imeendelea kusimamia biashara ya LPG ili kubaini wafanyabiashara wasio waaminifu na kuwachukulia hatua stahiki. Kwa mwaka 2017 kumekuwa na ongezeko la uagizaji wa LPG ikilinganishwa na mwaka 2016 ambapo kuanzia mwezi Januari hadi Desemba 2017, gesi iliyoagizwa nchini ilikuwa **tani 107,263** ikilinganishwa na **tani 90,296** za mwaka 2016, sawa na ongezeko la **asilimia 19**.

G. UIMARISHAJI WA MAWASILIANO KATI YA WIZARA NA JAMII

132. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2017/18 Wizara ya Nishati na Taasisi zake imeendelea kuelimisha umma kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu Sekta ya Nishati ili kuongeza uelewa kwa wananchi kuhusu shughuli zinazotekelizwa na Wizara. Njia mbalimbali zimetumika kutoa elimu hiyo zikiwemo magari ya matangazo, redio, magazeti, televisheni, tovuti na mitandao ya kijamii. Aidha, elimu imeendelea kutolewa kuititia Jarida la kila wiki la Wizara (*MEM News Bulletin*) ambapo hadi kufikia mwezi Aprili, 2018 jumla

ya Matoleo 42 yamechapishwa na kusambazwa kwa wadau mbalimbali zikiwemo Ofisi za Balozi za Tanzania. Taarifa zaidi kuhusu Wizara zinapatikana kuititia Tovuti (www.nishati.go.tz), ukurasa wa *Facebook* (Wizara ya Nishati), *Twiter* (Wizara ya Nishati); na *You Tube* (Wizara ya Nishati Tanzania).

133. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka 2017/18 Wizara imeshiriki katika vipindi mbalimbali vya Redio na Televisheni kwa lengo la kuwaelimisha wananchi kuhusu mipango inayotekelzeza na Serikali mathalan kipindi maalum cha 'TUNATEKELEZA' kinachoratibiwa na Idara ya Habari (MAELEZO) kwa kushirikiana na Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC).

H. AJIRA NA MAENDELEO YA RASILIMALIWATU

134. *Mheshimiwa Spika*, katika kuongeza tija na motisha kwa watumishi wa Wizara, kwa mwaka 2017/18 Wizara iliwapandisha madaraja jumla ya watumishi **10** katika kada mbalimbali. Katika kipindi cha mwaka 2018/19 Wizara inatarajia kuwapandisha madaraja watumishi **100** ambao wamepata sifa za kitaaluma na wenyewe utendaji mzuri wa kazi. Aidha, Wizara pamoja na Taasisi zake inatarajia kuajiri jumla ya watumishi **207** katika kada mbalimbali. Kati ya watumishi hao, **43** wataajiriwa na Wizara, **116** TPDC na **48** PURA.

135. *Mheshimiwa Spika*, ili kuhahakikisha kuwa Nchi inakuwa na wataalamu wa Kitanzania wa kutosha katika Sekta ya Nishati, Wizara imeendelea kushirikiana na Washirika wa Maendeleo kutoa ufadhili wa masomo kwa Watanzania wanaokidhi vigezo kwenda kusoma nchi mbalimbali kwa ngazi za Shahada, Uzamili na Uzamivu. Kwa mwaka 2017/18 watanzania **22** walipata ufadhili wa masomo kutoka Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China katika masuala ya mafuta na gesi asilia. Aidha, kuititia Programu za Uendelezaji wa Rasilimaliwatu (*Capacity Building*), *Development in Oil and Gas Industry na Energy Sector Capacity Building Program* watumishi 16 walipata ufadhili katika fani mbalimbali zikiwemo: usimamizi katika masuala ya mafuta na gesi asilia, sheria na uhasibu na fedha. Kwa mwaka 2018/19, watanzania

22 watapatiwa ufadhili wa masomo kutoka Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China.

136. ***Mheshimiwa Spika***, katika kujali afya za watumishi, Wizara imeendelea kutekeleza Waraka wa Utumishi wa Umma Na. 2 wa Mwaka 2006 kwa kuwashudumia watumishi wanaoishi na Virusi vya UKIMWI (VVU) na wenye UKIMWI waliojitokeza kwa kuwapatia lishe na dawa maalum. Aidha, Wizara itaendelea kutoa elimu mahali pa kazi ili kuzuia maambukizi mapya na kuwashudumia waathirika wa UKIMWI kadri watakavyojitokeza. Sambamba na jitihada hizo, Wizara pia itaendelea kuhamasisha watumishi kupima afya hususan kwenye Magonjwa Sugu Yasiyo ambukiza (MSY) ikiwemo shinikizo la damu, kisukari na saratani. Aidha, Wizara imeanzisha utaratibu wa kuhamasisha Watumishi kufanya mazoezi baada ya saa za kazi ili kuimarisha afya zao na kuwawezesha kufanya kazi kwa ufanisi.

137. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kutekeleza agizo la Serikali la kuhamishia shughuli zake Makao Makuu Dodoma ambapo hadi sasa watumishi **50** katи ya **153** wamehamia Dodoma. Wizara inaendelea kukamilisha taratibu husika ili watumishi wote waweze kuhamia Dodoma katika kipindi cha mwaka huu wa fedha.

I. USHIRIKIANO WA KIMATAIFA

138. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara ya Nishati imekuwa ikishirikiana na Washirika wa Maendeleo katika utekelezaji wa Programu, Mikakati na Miradi mbalimbali ya maendeleo. Kwa niaba ya Serikali, napenda kutambua mchango wa: Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya Dunia (WB), Benki ya Exim ya China, Benki ya Ushirikiano wa Kimataifa ya Japan (JBIC), Benki ya Unicredit Austria, *Economic Development Cooperation Fund* (EDCF- Korea), Mfuko wa Uendelezaji Jotoardhi (*Geothermal Risk Mitigation Facility - GRMF*), pamoja na Taasisi na Mashirika ya: JICA (Japan), KfW (Germany), AFD (Ufaransa), OfD (Norway), DFID (Uingereza) Sida (Sweden), Umoja wa Ulaya (EU), Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), na USAID (Marekani). Vilevile,

natoa shukrani kwa Serikali za China, Sweden, Ufaransa, Finland, Ujerumani, Iceland, Norway, Korea ya Kusini, Uganda na Ethiopia. Kwa kipindi cha mwaka 2018/19 Serikali kuitia Wizara ya Nishati itaendelea kushirikiana na Washirika hawa pamoja na wengine katika uendelezaji wa Sekta hii muhimu kwa ukuaji wa uchumi wa Nchi yetu.

J. SHUKRANI

139. ***Mheshimiwa Spika***, kipekee namshukuru kwa dhati Mhe. Subira Khamis Mgusu, Mbunge wa Viti Maalum, na Naibu Waziri wa Nishati kwa namna anavyonisaidia katika kusimamia Sekta ya Nishati. Hakika tangu ameteuliwa kuwa Naibu Waziri amekuwa na mchangano mkubwa katika kusimamia Sekta hii ambayo ina mchangano mkubwa katika ukuaji wa uchumi na ujenzi wa viwanda nchini.

140. ***Mheshimiwa Spika***, usimamizi bora wa Sekta ya Nishati nchini unategemea ushirikiano unaotolewa na watendaji mbalimbali wa Wizara. Hivyo, naomba nitumie nafasi hii kumshukuru Katibu Mkuu wa Wizara Dkt. Hamisi Hassan Mwinyimvua, Wakuu wa Idara na Vitengo pamoja na Watumishi wote wa Wizara kwa ushirikiano wanaonipatia kuniwezesha kuzisimamia shughuli mbalimbali zilizo ndani ya Sekta ya Nishati. Ni matumaini yangu kuwa ushirikiano huu utazidi kuimarika.

141. ***Mheshimiwa Spika***, naomba nitumie nafasi hii kuwashukuru Wenye viti na Wajumbe wa Bodi, Wakuu wa Taasisi na Watumishi wote wa Taasisi zinazosimamiwa na Wizara kwa ushirikiano wanaonipatia. Ni wazi kuwa ushirikiano huo umekua chachu katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu yangu.

142. ***Mheshimiwa Spika***, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, nawapongeza wananchi wa Jimbo la Chato kwa uvumilivu wao hasa wanaponikosa Jimboni nikiwa natekeleza shughuli hizi muhimu. Naipongeza sana familia yangu ikiongozwa na mpendwa wangu mama Kalemani kwa ustahimilivu wao hasa ninapokuwa mbali nao kifamilia nikiwa

katika majukumu haya ya kitaifa, nawaomba waendelee kuwa wavumilivu kwa kuwa kazi hizi ni muhimu kifamilia na kitaifa.

K. HITIMISHO

143. ***Mheshimiwa Spika***, Bajeti ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha wa 2018/19 pamoja na matumizi mengine imeelekezwa katika kutekeleza Miradi Mikubwa ya Nishati ya Kielelezo ambayo itakapokamiliika itasaidia upatikanaji wa umeme wa uhakika nchini.

144. ***Mheshimiwa Spika***, naomba Bunge lako Tukufu sasa likubali kupitisha Makadirio ya Jumla ya **Shilingi 1,692,286,014,000** kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Nishati na Taasisi zake. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama ifuatavyo:

(i) **Shilingi 1,665,141,000,000** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,489,741,000,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 175,400,000,000** ni fedha za nje; na

(ii) **Shilingi 27,145,014,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo **Shilingi 15,025,821,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC). **Shilingi 12,119,193,000** ni kwa ajili ya Mishahara (P.E) ya watumishi wa Wizara na Taasisi zilizo chini yake.

145. ***Mheshimiwa Spika***, naomba tena nitoe shukrani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii pia inapatikana katika Tovuti ya Wizara kwa anuani ya www.nishati.go.tz. Vilevile, Hotuba hii ina vielelezo mbalimbali kwa ajili ya ufanuzi wa masuala muhimu yanayohusu Sekta ya Nishati.

146. ***Mheshimiwa Spika***, naomba sasa kutoa hoja.

MWENYEKITI: Sasa namkaribisha Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini ili aweze kuwasilisha taarifa ya Kamati, Mheshimiwa karibu. (*Makof*)

MHE. DUNSTAN L. KITANDULA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijawasilisha taarifa hii, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingu wa Rehema kwa kunijalia afya njema na hivyo kuweza kuwatumikia Watanznaia na kwa kipekee ndugu zangu wa Mkkinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 na Kanuni ya 117(11) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019. Naomba taarifa yote ya Kamati iingie kwenye *Hansard* kama tulivyoiwasilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka 2017/2018. Kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 98, Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotekelizwa chini ya Wizara ya Nishati katika Mikoa ya Mara, Shinyanga, Tabora na Singida. Lengo la ukaguzi huo lilikuwa ni kujionea hali halisi ya matumizi ya fedha za miradi zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa mwaka husika. Maelezo ya miradi pamoja na matokeo ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo kwa mwaka huo ni kama inavyoonyeshwa kuanzia ukurasa wa 2 hadi 3 wa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya jumla kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Kutokana na ziara hiyo ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo, Kamati inatoa maoni yafuatayo:-

(a) Utekelezaji wa miradi ya umeme vijiji Awamu ya III uzingatie sana ushirikishwaji wa wananchi pamoja na viongozi wa maeneo husika;

(b) Miradi ya umeme vijiji bado inakabiliwa na changamoto kubwa ya upelekaji wa fedha kwa wakati, hali

hiyo inasababisha wakandarasi kuchelewa kutekeleza miradi kikamilifu na kwa wakati. Hivyo, Kamati inaitaka Serikali kupeleka fedha kwa wakati kwa kuwa fedha hizi zina wigo na ni tozo za wananchi. (*Makofi*)

(c) Katika kutekeleza miradi hii ya umeme vijijini, bado maeneo mengi ya vijijini na vitongoji yanarukwa kutokana na *scope* za miradi hiyo kuwa finyu. Aidha, wakandarasi kutoshirikisha viongozi na wananchi wa maeneo husika. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuwa utaratibu wa kuainisha maeneo kwa kuwashirikisha viongozi wa maeneo husika ili wigo wa kazi yaani *scope* unaotolewa kwa wakandarasi wanaotekeleza miradi hii uwe halisi na kukidhi mahitaji.

(d) Miradi ya umeme vijijini bado inakabiliwa na changamoto ya mashine humba (*transformer*) zisizokidhi viwango vya ubora wa mahitaji halisi ya maeneo zinapofungwa. Kamati inaishauri Serikali kufanya ukaguzi wa mashine humba kabla wakandarasi hawajazifunga katika maeneo husika.

(e) Katika maeneo ambayo miradi mbalimbali imetekelvezwa na wananchi wanastahili kulipwa fidia, Kamati inapendekeza wananchi hao kulipwa fidia zao kwa wakati.

Mheshimiwa Mweyekiti, sekta ndogo ya gesi na miradi ya mafuta nchini. Tangu kugundulika kwa gesi asilia nchini tayari jumla ya viwanda 41 vimeunganishwa katika mpango wa matumizi ya gesi asilia. Kati ya viwanda hivyo, viwanda vinne vimesimama uzalishaji na viwanda 37 vinaendelea kutumia gesi asilia. Kamati hairidhishwi na kasi ya ukuzaji wa soko la matumizi ya gesi asilia majumbani na viwandani kwani pamoja na uwepo wa gesi asilia ya kutosha nchini na uwekezaji mkubwa uliofanyika katika ujenzi wa bomba la kusafirisha gesi toka Mtwara hadi Dar es Salaam, idadi ya watumiaji wa gesi asilia waliounganishwa kwa matumizi ya Viwandani na majumbani siyo ya kuridhisha. Ni maoni ya Kamati kuwa, Serikali itoe fedha za kutosha ili kujenga miundombinu ya kusambaza gesi hiyo katika maeneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahusiano ya wadau katika sekta yoyote ile ni jambo la muhimu sana. Wakati wa kupokea taarifa ya utekelezaji wa Shirika la Maendeleo Nchini (*TPDC*) katika kipindi cha robo mwaka kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Kamati haikuridhishwa na mahusiano ya ubia ya kuendeleza miradi ya gesi asilia inayotekelzeza kati ya *TPDC*, *PAN AFRICAN ENERGY*, *SONGAS* pamoja na *TANESCO*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inampongeza sana Mheshimiwa Spika kwa kuchukua hatua za haraka za kuunda Kamati Maalum ya kufanya mapitio ya uwekezaji uliofanyika katika sekta ya gesi nchini ili Kamati hiyo iweze kutoa mapendekezo ya namna bora ya kuendeleza na kunufaika rasilimali ya gesi asilia iliyopo hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na umuhimu wa nchi kuwa na ghala la kuhifadhia mafuta ya dharura yaani *Strategic Petroleum Reserve*, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa mradi wa ghala la kuhifadhia mafuta ya dharura ya Taifa. Mradi huu una manufaa makubwa kwa nchi na utasaidia uwepo wa mafuta ya dharura pindi hali inapokuwa siyo nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua zinazoendelea katika utekelezaji wa mradi wa Bomba la kusafirishia mafuta ghafi kutoka Hoima-Uganga hadi Tanga-Tanzania. Mradi huu una manufaa makubwa kwa Taifa ikiwemo fedha za uwekezaji zitakazoingizwa kwenye uchumi wa Taifa letu, ajira zitakazopatikana na mapato yatokanayo na mauzo ya mafuta pindi mradi utakapokamilika. Pamoja na manufaa makubwa ya mradi huu kwa nchi yetu, Kamati inaishauri Serikali kuangalia kwa umakini matumizi ya fedha za mradi huu kwa kuwa asilimia kubwa ya utekelezaji wa mradi huu ipo upande wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya upatikanaji wa umeme nchini. Pamoja na jitihada mbalimbali zinazofanywa na Wizara ya Nishati katika kuwekeza kwenye miradi mipy ya uzalishaji, usafirishaji, usambazaji wa umeme kama vile

miradi wa kuzalisha umeme kwa nguvu za maji wa Mto Rufiji, miradi ya umeme ya Jotoardhi na miradi mingine, bado maeneo mbalimbali ya nchi yanakabiliwa na tatizo la kukosa umeme wa uhakika, umeme unaokatika mara kwa mara, hali inayosababisha kukwama kwa shughuli mbalimbali za uzalishaji wa kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaendelea kusisitiza kuwa fedha zinazotengwa na kuidhinishwa na Bunge kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ya kusafirishia umeme pamoja na vituo vya kufua umeme nchini zipelekwe zote na kwa wakati kwa shirika la TANESCO ili kuweza kutekeleza jukumu la ukarabati wa miundombinu na vituo hivyo. Hali hii itasaidia sana kuondoa kero kubwa ya kukatika kwa umeme inayosababishwa na uchakavu wa miundombinu katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa bajeti na uzingatiaji wa maoni ya Kamati kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Kamati ilifanya uchambuzi wa bajeti kwa kuzingatia mambo makuu matatu kama yanavyoonekana katika taarifa yetu kwenye ukurasa wa 14 hadi 20.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa kuhusu ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Februari, 2018, Wizara ya Nishati ilikuwa imekusanya jumla ya shilingi bilioni 216 sawa na asilimia 57 ya lengo liliokusudiwa la shilingi bilioni 377.46 hadi kufikia robo tatu ya mwaka 2017/2018. Kamati inaona kuwa mwenendo huo wa ukusanyaji mapato na kwa kuzingatia muda uliobaki kabla ya kufikia mwisho wa mwaka, upo uwezekano mkubwa kwa Wizara kushindwa kufikia lengo la ukusanyaji wa mapato. Hivyo, Kamati inaitaka Wizara kuongeza juhudhi za ukusanyaji katika kipindi kilichobakia. Mchanganuo wa makusanyo ya mapato kuanzia Julai, 2017 hadi mwezi Februari, 2018 unapatikana kwenye kielelezo Na. 01 cha Taarifa yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa fedha kutoka Hazina. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Machi, 2018

Iliyokuwa Wizara ya Nishati na Madini ilikuwa imepokea jumla ya shilingi bilioni 259.8 sawa na asilimia 34.7 tu ya bajeti yote iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Kwa upande wa Miradi ya Maendeleo hadi kufikia Februari, 2018 shilingi bilioni 228.66 zilikuwa zimetolewa, sawa na asilimia 39.94 tu ya fedha za maendeleo. Aidha, hadi kufikia Februari, 2018, Wizara ilikuwa imepokea kiasi cha shilingi bilioni 13.94 kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini kuwepo kwa ucheleweshwaji malipo ya wakandarasi wanaotekeleza Miradi ya *REA*. Hali hii inatokana na uanzishwaji wa utaratibu mpya wa uidhinishaji malipo unaozua *REA* kuidhinisha malipo moja kwa moja kutoka kwenye akaunti ya Mfuko wa Umeme Vijijini. Kwa mujibu wa utaratibu mpya, *REA* inalazimika kuwasilisha maombi Wizara ya Nishati ndipo maombi hayo yapelekwe Wizara ya Fedha. Kamati ilibaini kuwa licha ya wakandarasi kuwasilisha maombi ya malipo ya awali tangu Agosti, 2017, ulipaji wa madai hayo ulichukua takriban miezi minne kwa baadhi ya wakandarasi na wakandarasi wengine hadi Machi, 2018 malipo yao yalikuwa bado hayajaidhinishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilibaini kuwa wakandarasi wanaotekeleza miradi hii waliwasilisha maombi yao ya malipo toka Agosti, 2017. Hata hivyo, hadi kufikia mwezi Machi 2018 takriban miezi 10 tangu kuingiwa kwa mikataba ambayo utekelezaji wake ni wa miaka miwili, bado ufunguaji wa Hati za Muamana (*Letters of Credit*) ambayo ni takwa la kimkataba kuwawezesha wakandarasi kununua vifaa ulikuwa haujafanyika. Ucheleweshaji huu wa ufunguzi wa Hati za Muamana utasababisha kuongezeka kwa gharama za utekelezaji wa miradi pamoja na kutotimia kwa lengo la kuvifikishia umeme vijiji vyote nchini kabla ya mwaka 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya *REA* na *TANESCO* kufanya uhakiki wa kina wa malipo hayo kwa kufuata Kanuni na Sheria ya Nishati Vijijini, utaratibu wa sasa wa uidhinishaji malipo unaitaka Wizara ya Fedha nayo kuyafanya uhakiki

madai ya malipo hayo. Kamati imebaini kuwa mfumo huo mpya wa uhakiki wa malipo umekuwa na changamoto kubwa ya ucheleweshaji wa malipo kwa wakandarasi hivyo *REA* kukiuka makubaliano ya mikataba waliyosaini kati yao na wakandarasi. Kamati inaishauri Serikali kubuni mfumo mzuri utakaofupisha utaratibu huu na kuondoa urasimu ili miradi ya *REA* iweze kutekelezwa kwa wakati na vilevile kuiepusha Serikali na hasara ya kulazimika kulipa fidia kwa wakandarasi kutokana na *REA* kukiuka makubaliano ya mikataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio na utekelezaji na ushauri wa Kamati. Wakati wa uchambuzi wa bajeti kwa mwaka 2017/2018, Kamati ilitoa maoni, ushauri na mapendekezo kadhaa. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa baadhi ya ushauri uliotolewa na Kamati umezingatiwa. Hata hivyo, baadhi haujafanyiwa kazi na Serikali kama ifuatavyo:-

(a) Utekelezaji wa miradi ya *REA* bado unakabiliwa na changamoto kubwa ya maeneo mengi kuachwa au kurukwa katika vijiji na vitongoji pamoja na viongozi wa wananchi kutokushirikishwa vya kutosha katika uanishaji wa maeneo.

(b) Serikali bado haitengi na kupeleka bajeti ya kutosha kuiwezesha *TPDC* kutekeleza majukumu yake ya msingi kama inavyotakiwa.

(c) Serikali bado haliwezeshi vya kutosha Shirika la Ugavi wa Umeme nchini yaani *TANESCO* kwa kulipatia fedha za kutosha kutekeleza majukumu yake, kama vile ukarabati wa miundombinu na vituo vya kufua umeme.

(d) Miradi ya jotoardhi, bado imeshindwa kutekelezwa kutokana na kutokupelekewa fedha. Kwa mfano kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ni asilimia 0.17 tu ya fedha za miradi maendeleo ndiyo iliyopelekwa kwa taasisi ya Jotoardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Mpango na makadirio ya mapato na matumizi Fungu Na. 58 kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Makisio ya makusanyo na maduhuli kwa mwaka 2018/2019 ni Sh.394,450,000,000. Kati ya makusanyo hayo, Sh.394,440,000,000 zitakusanya kuitia shughuli za mafuta ya gesi asilia na Sh.10,000,000 zitakusanya kuitia shughuli za utawala. Kiasi hiki ni pungufu kwa Sh.108,000,000,000 ikilinganishwa na mapato yaliyokusanya kwa mwaka 2017/2018. Kamati inaamini kuwa kadirio hili ni la chini na kwamba Wizara ina uwezo wa kukusanya zaidi endapo itaweka mikakati madhubuti ya kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato kwa vyanzo na rasilimali zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2018/2019, Wizara ya Nishati inakadirisha kutumia jumla ya Sh.1,692,286,014,000 ikilinganishwa na Sh.989,337,759,500 kwa mwaka 2017/2018 kwa ilivokuwa kwa Wizara ya Nishati na Madini na hii ni sawa na ongezeko la asilimia 69.5. Kati ya fedha hizi shilingi bilioni 700 zimetengwa mahsus kwa ajili ya mradi wa kuzalisha umeme wa Mto Rufiji. Kamati inaipongeza Serikali kwa uamuza wa kuanza utekelezaji wa mradi huu muhimu kwa uchumi wa nchi yetu. Hata hivyo, Kamati inatoa angalizo kuwa itakapofika wakati wa utekelezaji, Serikali ihakikishe fedha za mradi huu zinatolewa kwa wakati bila kuwepo kwa urasimu usio wa lazima. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati. Baada ya Kamati kutekeleza majukumu yake ya Kikanuni ambayo ni ukaguzi wa miradi ya maendeleo, uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara kwa mwaka 2017/2018 na makadirio na matumizi ya Wizara ya mwaka 2018/2019, Kamati ina maoni na ushauri ufuatao:-

(i) Kwa kuwa Bunge linaidhinisha fedha za miradi ya maendeleo kama Wizara inavyoomba kila mwaka wa fedha husika, hivyo, Kamati inaishauri Serikali kupeleka fedha za miradi ya maendeleo kwa wakati, kwani fedha kutopatikana kwa wakati kunaathiri utekelezaji wa miradi ya maendeleo. (*Makof*)

(ii) Kwa kuwa kumekuwa na mwenendo wa kusuasua wa utolewaji wa fedha ambapo hadi 5 Mei, 2018 ni vijiji 4730 tu sawa na asilimia 38 ndiyo vimefikiwa na miundombinu ya umeme kati ya vijiji 12,268 vilivyopo hapa nchini. Kamati inaona kuwa hali hii inaweza kuhatarisha azma ya kuvifikishia vijiji vyote miundombinu ya umeme ifikapo mwaka 2021.

(iii) Kamati inaishauri Serikali kutekeleza miradi mipyä ya usafirishaji na usambazaji wa umeme ikiwa ni pamoja na kupeleka fedha za kutekeleza miradi hiyo. Aidha, Serikali ije na mkakati maalum wa kuunganisha Mikoa yote iliyo nje ya gridi ya Taifa hususani Kigoma, Katavi, Lindi, Mtwara na Rukwa. Katika kipindi hiki tunaipongeza Serikali kwa kuhakikisha Mikoa ya Lindi na Mtwara sasa imeunganishwa kwenye *grid* ya Taifa. (*Makof*)

(iv) Upatikanaji wa umeme nchini bado ni changamoto kubwa katika maeneo mengi kutokana na miundombinu chakavu hali inayosababisha kukwama kwa shughuli nyingi za uzalishaji hasa viwandani. Kamati inaishauri Serikali kutoa fedha za kutosha kukarabati miundombinu ya umeme ili kupunguza adha kwa wananchi na kuondokana na tatizo la umeme kukatika mara kwa mara.

(v) Serikali inapaswa kuhakikisha mchakato wa majadiliano ya uwekezaji wa mradi mkubwa wa *LNG* ili kukwepa tishio la kutekwa kwa soko la biashara ya gesi nchini kutokana na uwekezaji unaofanyika katika nchi jirani. (*Makof*)

(vi) Kamati inaendelea kusisitiza kwa Serikali kuwekeza katika vyanzo vingine vya kuzalisha nishati mbadala. Aidha, kuwekeza zaidi katika nishati jadidifu yaani *renewable energy* ambao uzalishaji wake ni nafuu na rafiki kwa mazingira. Mfano uzalishaji wa umeme wa upепo katika maeneo ya Singida, Makambako, Same yenye rasilimali ya kutosha. (*Makof*)

(vii) Serikali ihakikishe *TANESCO* inajielekeza kwenye matumizi ya teknolojia ya kisasa yatakayoiwezesha

kutokuzima umeme pindi inapofanya matengenezo ya mitambo yake. (*Makofî*)

(viii) Kamati inaishauri Serikali kuja na mkakati mahususi wakulipa madeni ya Taasisi inazozisimamia na kuonesha jitihada za dhati katika kulipa wazabuni wanaozidai taasisi hizi. Mfano hadi sasa deni la wazabuni mbalimbali wanaoidai *TANESCO* limefikia takribani bilioni 966.

(ix) Kamati inaendelea kusisitiza na kuishauri Serikali kushirikisha wananchi pamoja na viongozi wakati wa kuainisha maeneo ya kutekeleza miradi ya *REA*. Kwa kufanya hivyo, maeneo mengi ya vijiji na vitongoji hasa yale ya kijamii yatapata huduma ya umeme inavyostahili.

(x) Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuzingatia ubora wa vifaa hasa machine humba (*transformer*) zinazofungwa wakati wa utekelezaji wa miradi ya *REA* Awamu ya III .

(xi) Kamati inaishauri Serikali kuwalipa fidia kwa wakati wananchi wote wanaotoa maeneo yao kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo. Mfano ya miradi ya gesi asilimia, *LNG* Mkoani Lindi pamoja na wananchi waliopisha mradi wa ujenzi wa kusafirisha umeme wa Singida kwenda Arusha. (*Makofî*)

(xii) Kwa kuwa Serikali imeshindwa kuendeleza kampuni yake ya Tanzania *Concrete Poles Manufacturing Company Limited (TSPM)* katika utengenezaji wa nguzo za zege; na kwa kuwa hata dhamira ya kuingia ubia na wawekezaji wengine utekelezaji wake umekuwa wa kusuasua, hivyo basi ili kuharakisha matumizi ya nguzo za zege nchini katika miradi inayoendelea hususani miradi ya *REA*, Kamati inaishauri Serikali kuharakisha utekelezaji wa uendelezaji wa kampuni hiyo kwa kuipatia mtaji wa kutosha na vilevile kutoa fursa ya soko kwa kampuni ambazo zinazalisha nguzo hizo hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho. Nichukue fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kazi nzuri mnayoifanya ya kuliongoza Bunge letu Tukufu. Mungu awajalie afya njema, hekima na busara katika kutekeleza wajibu huu mkubwa tuliowakabidhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda vilevile kutoa shukrani zangu za dhati kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kwa Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Dkt. Merdad Matogolo Kalemani, Mheshimiwa Subira Khamis Mgusu, Naibu Waziri wa Nishati pamoja na watendaji wote wa Wizara hiyo wakiongozwa na Katibu Mkuu, Dkt. Hamisi Mwinyimvua kwa kushirikiano wao mkubwa kwa Kamati yetu kwa wakati wote tulipouhitaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee, nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kwa weledi na umahiri waliounyesha wakati wote wa kutekeleza majukumu ya Kamati hii. Kwa heshima kubwa naomba majina yao katika orodha iliyomo kwenye kitabu chetu yaingizwe katika *Hansard*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndg. Stephen Kagaigai; Mkurugenzi wa Idara ya Kamati ya Bunge, Ndg. Athuman Hussein; Mkurugenzi Msaidizi, Ndg Michael Chikokoto; Makatibu wa Kamati, Ndg. Mwanahamisi Mkunda na Ndg. Felister Mgonja, pamoja na msaidizi wa Kamati ndugu Grace Mwenye, kwa uratibu mzuri wa shughuli zote za Kamati na hatimaye kukamilisha taarifa hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa namna ya kipekee niwashukuru sana wananchi wangu wa Jimbo la Mkinga kwa imani wanayoendelea kunionyesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema haya, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi Fungu 58, Wizara ya Nishati

kwa mwaka wa fedha wa 2018/2019, ambayo ni Sh.1,692,286,014,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA NISHATI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) na Kanuni ya 117(11) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi, kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Fasili ya 6(9) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati inao wajibu wa kusimamia majukumu yote ya kisera yanayotekelizwa na Wizara hii. Aidha, majukumu ya Kamati katika Wizara kuhusiana na Uchambuzi wa bajeti ya kila mwaka yameelekezwa katika Fasili ya 7(1), Kamati imetekeliza ipasavyo majukumu hayo.

Mheshimiwa Spika, Kwa kuzingatia matakwa ya kanuni tajwa, Kamati ilifanya vikao kadhaa kwa lengo la kupokea na kuchambua Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara, kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi, kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

Pia Kamati ilifanya ukaguzi wa baadhi ya Miradi ya Maendeleo iliyoidhinishiwa Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018. Lengo la ukaguzi huo ni kujonea hali halisi ya matumizi ya fedha za miradi zilizoidhinishwa na Bunge kwa mwaka husika.

2.0 UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA 2017/2018

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati ilifanya ziara za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo inayotekelvezwa chini ya Wizara ya Nishati, katika Mikoa ya Mara, Shinyanga, Tabora na Singida.

Aidha, Kamati ilikagua Miradi iliyotengewa fedha na ambayo halkutengewa fedha katika Bajeti ya Maendeleo ya Mwaka 2017/2018. Miradi iliyokaguliwa ni hii ifuatayo:-

- i) Miradi ya Umeme Vijijini, Mkoa wa Mara.
- ii) Mradi wa kusafirisha umeme wa msongo 400kv Iringa – Shinyanga (Backbone), mkoani Shinyanga.
- iii) Miradi ya umeme Vijijini, Mkoa wa Shinyanga.
- iv) Miradi ya Umeme Vijijini, Wilaya ya Nzega na Igunga (Tabora).
- v) Miradi ya Umeme vijijini mkoa wa Singida.
- vi) Mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme 400kv Singida – Arusha, mkoani Singida.

2.1 Maelezo na Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

2.1.1 Miradi iliyokaguliwa na Kamati

i) Miradi ya Umeme Vijijini, Mkoa wa Mara

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Mara ni mionganini mwa mikoa ambayo miradi ya umeme vijijini Awamu ya Tatu inatekelezwa, kuititia Wakala wa Nishati Vijijini (REA). Mradi huu unahusu miradi midogo ya Densification, Uendelezaji wa

Grid ya Taifa (Mizunguko ya I na II) na Mradi mdogo wa maeneo nje ya grid (off-grid).

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitembelea Vijiji viwili vyatilili kwenye wilaya ya Butiama ambavyo ni Busegwe na Muriaza. Vijiji hivi viko katika mradi wa Densification. Kamati ilibaini changamoto kubwa ya ushirikishwaji mdogo wa wananchi pamoja na Viongozi wa maeneo husika na hivyo kusababisha maeneo muhimu na yenye watu wengi kutofikiwa umeme kama inavyotakiwa. Aidha, changamoto hiyo imesababisha maeneo mengi katika vitongoji na vijiji kurukwa wakati wa upelekaji wa umeme huo.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilibaini kuwa mashine Humba zilizofungwa kwaajili ya kusambaza umeme zina uwezo mdogo ikilinganishwa na mahitaji ya eneo husika, hali hiyo inapelekea maeneo hayo kutokuwa na umeme wa uhakika.

**ii) Mradi wa kusafirisha umeme wa msongo 400kv
Iringa – Shinyanga (Backbone), mkoani Shinyanga**

Mheshimiwa Spika, Katika mradi wa REA awamu ya tatu mkoa wa Shinyanga umepata miradi miwili, ambayo ni mradi wa REA – III (grid extension) na mradi wa kuvipatia huduma ya umeme vijiji vilivyo ndani ya mkuza wa njia kuu ya kusafirishia umeme ya msongo wa kilovolti 400 (VEI/BTIP). Aidha, Kamati ilitembelea vijiji viwili vyatilili kwenye Negezi na Bulimba vinavyopatiwa umeme kupitia Mradi huo.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa REA awamu ya tatu kwa mkoa wa Shinyanga unajumuisha ujenzi wa km 669.4 za laini za msongo wa kilovoti 33, ujenzi wa km 453 za laini za msongo wa volti 400, ufungaji wa transformator 201. Gharama ya mradi inakadiriwa kuwa ya jumla ya **shilingi bilioni 33.054**.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Shinyanga pia umepata mradi wa laini kubwa ya kusafirisha umeme ya msongo wa kilovolti 400 yenye urefu wa kilomita 670 kutoka mkoani Iringa kupitia mikoa ya Dodoma na Singida hadi kwenye kituo cha

kupooza umeme cha Ibadakuli. Mradi huu uligharimu jumla ya **dola milioni 120 takribani kiasi cha shilingi 268,800,000,000.**

Mheshimiwa Spika, Changamoto kubwa inayoikabili miradi hii ni Vijiji vingi bado havijapata umeme kwa awamu ya kwanza ya mradi, hasa maeneo mengi yaliyopo ndani ya Halmashauri za miji ya Kahama, Kishapu na Shinyanga vijijini.

iii) Miradi ya Umeme Vijijini, Wilaya ya Nzega na Igunga (Tabora).

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitembelea miradi ya REA, inayotekelawa katika Wilaya ya Nzega, kijiji cha Idala pamoja na kijiji cha Iborogero wilayani, Igunga.

Mheshimiwa Spika, Katika utekelezaji wa miradi ya REA awamu ya tatu pia Mkoa ulipata mradi wa kupeleka umeme kwenye vijiji 12 vilivyoko pembezoni mwa mkuza wa njia kuu ya kusafirisha umeme (400KV) kwa wilaya ya Igunga katika mkoa wa Tabora na wilaya ya Kishapu mkoani Shinyanga.

Pamoja na utekelezaji unaoendelea katika miradi hii, Kamati iliona changamoto ya maeneo mengi ya vijiji na vitongoji kukosa umeme. Aidha, utekelezaji ulionekana ni wa kusuasua, na sababu zikianishwa ni ukosefu wa Fedha. Hata hivyo, bado Viongozi na Wananchi hawashirikishwi katika uainishaji wa maeneo hivyo kuchangia kwa kiasi kikubwa kurukwa kwa maeneo mengi.

iv) Miradi ya Umeme vijijini mkoa wa Singida pamoja na Mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme 400kv Singida – Arusha, mkoani Singida

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Singida unapata umeme kutoka Gridi ya Taifa kupitia njia kuu za kusafirisha umeme za msongo wa Kv 400, katika mradi wa REA awamu ya tatu mkoa Singida umepata miradi 2, ambayo ni mradi wa REA – III (Grid Extension) na mradi wa kuvipitia huduma

ya umeme vijijiini vilivyo ndani ya mkuza wa njia kuu ya kusafirisha umeme ya msongo wa Kv 400.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitembelea ofisi ya Tanesco ya mkoa Singida na kuona kituo cha kupoza umeme cha TANESCO kuititia mradi huu wa msongo wa umeme wa KV400. Aidha, Kamati ilitembelea kijiji cha kisaki na kujionea hali ya upatikanaji wa umeme.

Mheshimiwa Spika, pamoja na miradi inayoendelea kwa mkoa huu bado kuna changamoto ya vijiji kukosa umeme. Aidha, maeneo mengi yaliyopo ndani ya Halmashauri ya Manispaa ya Singida bado hayajafikiwa na huduma ya umeme. Vilevile, kuna maeneo ya miradi ya maendeleo inayotekelawa mkoani hapo hayajapatiwa umeme kama vile mradi wa umwagiliaji maji mkoani hapo.

3.0 MAONI YA JUMLA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

Mheshimiwa Spika, kutokana na ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo Kamati inatoa maoni yafuatayo:-

(a) Utekelezaji wa miradi ya umeme vijijiini awamu ya tatu uzingatie sana ushirikishwaji wa wananchi pamoja na viongozi wa maeneo wanaohusika.

(b) Miradi ya umeme vijijiini bado inakabidiliwa na changamoto kubwa ya upelekaji wa Fedha kwa wakati, hali hiyo inapeleka wakandarasi kuchelewa kutekeleza miradi kikamilifu na kwa wakati. Hivyo basi, kamati inaitaka Serikali kupeleka fedha kwa wakati kwakuwa fedha hizi zina wigo na ni tozo za wananchi

(c) Katika kutekeleza miradi hii ya umeme vijijiini, bado maeneo mengi ya vijiji na vitongoji yanarukwa, Kamati inaishauri Serikali, kuainisha maeneo kwa kuwashirikisha viongozi pamoja na kuongeza wigo (scope) kwa wakandarasi wanaotekeliza miradi hii, ili wigo uwe wa kukidhi maeneo mengi ya vijiji. Mfano kijiji cha Nyabange Wilaya ya

Butiama ni nyumba nne tu zimeunganishwa na umeme na mkandarasi ameshakamilisha kazi yake.

(d) Miradi ya umeme vijijini bado inakabiliwa na changamoto ya mashine Humba zisizo kidhi viwango nya matakwa ya maeneo. Mashine Humba (Transformer) zinazofungwa hazina ubora wenyewe kuaminika. Kamati inashauri Serikali kufanya ukaguzi wa Mashine humba kabla wakandarasi hawajazifunga katika maeneo.

(e) Kamati inapendekeza pia wananchi kulipwa fidia zao kwa wakati katika maeneo ambayo miradi mbalimbali inatekelezwa.

(f) Kamati inaendelea kushauri Serikali kupeleka umeme katika maeneo ya Miji na Halmashauri, Aidha, kipaumbele cha kupeleka umeme kwa kuzingatia zaidi maeneo ya miji ambayo shughuli mbalimbali za uzalishaji na za kiuchumi zinapotekelezwa. Mfano katika Mkoa wa Singida kuna Mradi wa maji /umwagiliaji haujaunganisha na umeme.

4.0 **SEKTA NDOGO YA GESI NA MIRADI YA MAFUTA NCHINI**

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Shirika la maendeleo ya Petroli nchini (TPDC) imeendelea kutekeleza majukumu yake ya kuendeleza sekta ya Mafuta na Gesi. Mnyororo huu wa thamani unahuishwa mkondo wa juu (utafutaji na uzalishaji mafuta na gesi), mkondo wa kati (uchakataji na usafirishaji wa gesi na mafuta) pamoja na mkondo wa chini (usambazaji wa mafuta na gesi kwa watuamiaji).

Mheshimiwa Spika, tangu kugundulika kwa Gesi Asilia nchini jumla ya Viwanda 41 vimeunganishwa tayari katika mpango wa matumizi ya gesi asilia; kati ya hivyo viwanda vinne vimesimamisha uzalishaji na viwanda 37 vinaendelea kutumia gesi asilia.

Aidha, kwa Mwaka wa fedha 2017/18 takwimu za matumizi ya Bomba la gesi asilia kutoka Mtwara hadi Dar Es Salaam kupitia Somanga Fungu linaweza kwa kutoisha wastani wa futi za ujazo milioni 175 kwa siku, ikilinganishwa futi za ujazo milioni 145 kwa siku kwa mwaka 2016/17. Kuongezeka kwa uzalishaji wa Gesi asilia kwa siku imepelekea ongezeko la uzalishaji wa umeme wa MW 697 unaokwenda kwenye gridi ya Taifa kwa mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, Kamati hairidhishwi na kasi ya ukuzaji wa soko la matumizi ya Gesi asilia majumbani na viwandani. Pamoja na uwepo wa Gesi asilia ya kutosha nchini na uwekezaji mkubwa uliofanyika katika ujenzi wa bomba la kusafirisha gesi toka Mtwara hadi Dar es Salaam; Idadi ya watumiaji wa Gesi asilia walionganishwa kwa matumizi ya Viwandani na majumbani nchini siyo ya kuridhisha. **Ni maoni ya Kamati kuwa, Serikali itoe fedha za kutosha ili kujenga miundo mbinu ya kusambaza gesi hiyo.**

Mheshimiwa Spika, mahusiano ya wadau katika sekta yoyote ile ni jambo la muhimu sana, wakati wa kupokea taarifa ya utekelezaji wa shirika la maendeleo ya Petroli nchini (TPDC) katika kipindi cha robo Mwaka kwa Mwaka wa fedha 2017/18, Kamati haikuridhishwa na mahusiano ya ubia ya kuendeleza miradi ya gesi asilia inayotekelizwa kati ya TPDC, PAN AFRICAN ENERGY, SONGAS pamoja na TANESCO. Ili mahusiano hayo yawe na tija kwa Taifa, Kamati iliona ni vema Bunge lako tukufu lifuatilie na kujua maendeleo ya Mikataba na mahusiano baina ya wabia hao katika kuendeleza miradi hii ya Gesi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inakupongeza sana wewe binafsi kwa kuchukua hatua za haraka kuunda kamati Maalum ya kufanya mapitio ya uwekezaji uliofanyika katika sekta ya gesi nchini na kutoa mapendelezo kuhusu namna bora ya kuendeleza miradi ya Gesi asilia nchini.

Mheshimiwa Spika, Kutokana na umuhimu wa nchi kuwa na ghala la kuhifadhi mafuta ya dharura (Strategic Petroleum Reserve), **Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua**

zilizofikiwa katika utekelezaji wa mradi wa ghalia la kuhifadhiya mafuta ya dharura ya Taifa. Mradi huu una manufaa makubwa kwa nchi na utasaidia uwepo wa mafuta ya dharula kwa nchi wakati wote.

Mheshimiwa Spika, Pia Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua zinazoendelea katika utekelezaji wa mradi wa Bomba la kusafirishia mafuta ghafi la kutoka Hoima-Uganga hadi Tanga- Tanzania. Mradi huu una manufaa makubwa kwa Taifa kwakuwa mafuta haya yatauzwa katika masoko ya Kimataifa hivyo kuliongezea Taifa mapato. Pamoja na manufaa makubwa ya mradi huu kwa nchi yetu, Kamati inaishauri Seriakali kuangalia kwa umakini matumizi ya fedha za mradi huu kwa kuwa asilimia kubwa ya utekelezaji wa mradi huu ipo upande wetu.

5.0 HALI YA UPATIKANAJI WA UMEME NCHINI

Mheshimiwa Spika, Hali ya upatikanaji wa umeme nchini inaendelea kuimarika hadi sasa **MW 1,347.51** zimeshaingizwa kwenye gridi ya Taifa, umeme huo unatokana na vyanzo mbalimbali kama vile nguvu za maji **MW 567.70**, Gesi asilia **MW 698.91**, **Mafuta MW 70.4** na Biomass **MW 10.50**.

Matumizi ya juu kabisa yaliyowahi kufikiwa na nchini yetu ni **MW 1,051.27** kimsingi matumizi hayo ni kidogo sana ukilinganisha na mahitaji ya umeme katika maeneo yote yaliyo nje ya gridi, Kamati inaishauri Wizara kuendelea na jitihada za kuhakikisha mikoa yote inaingia kwenye gridi ya Taifa ili umeme wote unaozalishwa kutoka kwenye vyanzo vyote uweze kutumiwa na mikoa yote nchini ili kuondoa dhana ya kuwa nchi yetu ina umeme wa ziada kwenye gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni nchi pekee katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) kuwa na mitambo ya kisasa ya kuzalisha umeme kwa kutumia gesi asilia (combined cycle). Mitambo hii ina uwezo wa kuchoma gesi na kuzalisha umeme pia mitambo hiyo ina uwezo wa kuzalisha megawati nyiningine kwa kutumia mvuke. **Aidha, Ni matarajio ya Kamati**

kuwa uwepo wa Gesi asilia ya kutosha nchini, pamoja na mitambo ya kisasa ni ishara tosha kuwa nchi yetu inapaswa kuwa na umeme wa uhakika na wakutosheleza mahitaji ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada mbalimbali zinazofanywa na Wizara ya Nishati katika kuwekeza kwenye miradi mipyä ya uzalishaji, usafirishaji, usambazaji wa umeme kama vile Stiglers gorge, miradi ya umeme wa jotoardhi na mingine, bado maeneo mbalimbali ya nchi yanakabiliwa na tatizo la kukosa umeme wa uhakika, umeme unaokatika mara kwa mara, hali inayopelekea kukwamisha shughuli mbalimbali za uzalishaji na kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kusisitiza kuwa fedha zinazotengwa na kuidhinishwa na Bunge kwa ajili ya ukarabati wa miundo mbinu ya kusafirishia umeme pamoja na vituo vya kufua umeme nchini zipelekwe zote na kwa wakati kwa shirika la TANESCO ili kuweza kutekeleza jukumu la ukarabati wa miundombinu na vituo hivyo. Hali hii itasaidia sana kuondoa kero kubwa ya ukatikaji wa umeme inayosababishwa na uchakavu wa miundo mbinu katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

6.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya uchambuzi wa Bajeti kwa kuzingatia mambo makuu matatu ambayo ni:-

- a) Makusanyo ya Maduhuli kwa mwaka wa fedha 2017/2018;
- b) Hali ya upatikanaji wa fedha kutoka Hazina na;
- c) Uzingatiaji wa maoni na ushauri uliotolewa na Kamati ya Nishati na Madini wakati huo.

6.1 Uchambuzi wa Taarifa kuhusu Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka wa fedha 2017/2018

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Februari, 2018 Wizara ya Nishati ilikuwa imekusanya jumla ya **Shilingi bilioni 216.20** sawa na **asilimia 57.3** ya lengo lilokusudiwa la **Shilingi bilioni 377.46** hadi kufikia robo tatu ya mwaka 2017/18. Kamati inaona kwa mwenendo huu wa ukusanyaji mapato, na kwakuzingatia muda uliobaki kabla ya kufikia mwisho wa mwaka; upo uwezekano mkubwa kwa Wizara kushindwa kufikia lengo la ukusanyaji wa mapato. Hivyo, Kamati inaitaka Wizara kuongeza juhudi za ukusanyaji katika kipindi kilichobaki.

Mheshimiwa Spika, mchanganuo wa makusanyo ya Mapato kuanzia Julai 2017 hadi mwezi Februari, 2018 unapatikana kwenye kielelezo Na. 01 cha Taarifa hii.

Kielelezo Na. 1

CHANZO CHA MAPATO	BAJETI YA 2017/18	LENGO LA MAKUSANYO HADI ROBO YA TATU YA 2017/18 (SH. BILIONI)	MAKUSANYO HADI MWISHONI MWA MWEZI FEBRUARI, 2018	ASILIMIA %
Mauzo ya Gesi Asilia	477,361,499,6 76	358,021,124,757	188,336,575,69 6	52.6
Mapato mengine	11,725,135,72 4	8,793,851,793	19,787,668,054	225
Ubia	2,864,538,296	2,148,403,722	0	-
Mrabaha na Gawio la Faida ya Gesi	11,339,000,00 0	8,504,250,000	8,084,618,029	95
Jumla (Sh.)	503,290,173,6 96	377,467,630,272	216,208,861,77 9	57.3

6.2 Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 iliyokuwa Wizara ya Nishati na Madini (Fungu 58) iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi bilioni 998.34** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Februari, 2018 iliyokuwa Wizara ya Nishati na Madini ilikuwa imepokea jumla ya **Shilingi Bilioni 259.80**, sawa na **asilimia 34.7** ya Bajeti yote iliyoidhinishwa na Bunge lako tukufu.

Bajeti ya Miradi ya Maendeleo iliyoidhinishwa na Bunge lako ilikuwa ni **Shilingi bilioni 938.63**, sawa na **asilimia 94** ya bajeti yote ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2017/18. Hadi kufikia Februari 2018 **Shilingi Bilioni 228.66** zilikuwa zimetolewa, sawa na **asilimia 39.94 tu** ya fedha za Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kati ya Fedha za maendeleo zilizoidhinishwa **Shilingi bilioni 763.30** sawa na **asilimia 81.3** ya Bajeti yote ya maendeleo ni Fedha za ndani na **Shilingi bilioni 175.33** sawa na **asilimia 18.7** ya bajeti hiyo ni fedha za nje. Aidha, **Shilingi bilioni 756.76** sawa na **asilimia 80.6** ya bajeti yote ya maendeleo zimeelekezwa kwa ajili ya miradi ya kimkakati (Strategic Projects) ambayo ni pamoja na mradi kabambe wa kupeleka umeme vijiji (REA), mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa KV400 wa Singida-Arusha-Namanga utakaounganisha nchi ya Tanzania na Kenya na mradi wa Kinyerezi I Extension MW 85.


Kwa upande wa fedha za Matumizi Mengineyo (OC), fedha iliyoidhinishwa ilikuwa **Shilingi bilioni 28.83** na hadi kufikia Februari, 2018 Wizara ilikuwa imepokea kiasi cha **Shilingi Bilioni 13.94**, sawa na **asilimia 64.52** ya fedha zilizoidhinishwa.

Ufafanuzi zaidi kuhusu uwiano kati ya Bajeti iliyoidhinishwa na fedha zilizopatikana hadi Machi, 2017 ni kama unavyoonekana kuititia Kielelezo Na. 2 katika taarifa hii.

Kielelezo Na. 2

BAJETI ILIYOIDHINISHWA 2017/2018			FEDHA ILIYOPATIKANA HADI MACHI, 2018	
UFAFANUZI	KIASI	ASILIMIA	KIASI	ASILIMIA
JUMLA KUU	Bil 998.34	100	Bil 259.80	34.7
FEDHA MAENDELEO	ZA Bil 938.63	94	Bil 229.50	32.6
MATUMIZI KAWAIDA	YA Bil 59.7	6	Bil 30.30	67.68

CHANZO: Taarifa ya Wizara ya Nishati Fungu 58 kuhusu utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/18.



Kamati ilibaini kuwa licha ya wakandarasi kuwasilisha maombi ya malipo ya awali tangu mwezi Agosti mwaka 2017, ulipaji wa madai hayo ulichukua takriban miezi minne kwa baadhi ya wakandarasi; na wakandarasi wengine hadi mwezi machi 2018 malipo yao yalikuwa bado hayajaidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa Wakandarasi wanaotekeleza miradi hii waliwasilisha maombi yao ya malipo toka mwezi Agosti, 2017, hata hivyo; hadi kufikia mwezi machi 2018 takriban miezi 10 tangu kuingiwa kwa mikataba ambayo utekelezaji wake ni wa miaka miwili, bado ufunguzi wa Hati za Muamana (*Letters of Credit*) ambao ni takwa la kimkataba kuwawezesha wakandarasi kununua vifaa ulikuwa haujafanyika.

Ucheleweshaji huu wa ufunguzi wa Hati za Muamana utasababisha kuongezeka kwa gharama ya utekelezaji wa miradi; pamoja na kutotimia kwa lengo la kuvifikishia umeme vijiji vyote nchini kabla ya mwaka 2020.

Licha ya REA na TANESCO kufanya uhakiki wa kina wa malipo hayo kwa kufuata kanuni na Sheria ya Nishati Vijijini; utaratibu wa sasa wa uidhinishaji malipo unaitaka Wizara ya Fedha nayo kuyafanya uhakiki madai ya malipo hayo.

Kamati imebaini kuwa mfumo huo mpya wa uhakiki wa malipo umekuwa na changamoto kubwa ya ucheleweshaji wa malipo kwa Wakandarasi; hivyo REA kukiuka makubaliano ya mikataba waliosaini kati yao na wakandarasi. Hivyo basi; Kamati inaishauri Serikali kubuni mfumo mzuri utakaofupisha utaratibu huu usio wa lazima ili miradi ya REA iweze kutekelezwa kwa wakati, na vile vile kuiepusha Serikali na hasara ya kulazimika kulipa fidia kwa wakandarasi kutookana na REA kukiuka makubaliano ya mikataba.

6.3 Mapitio ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wa Bajeti ya Mwaka 2017/18, Kamati ilitoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo, kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 7(1) ya Nyongeza ya Nane ya Toleo la Januari, 2016 iliyoelezea majukumu ya Kamati ya kusimamia na kufuatilia utendaji kazi wa shughuli za Wizara. Napenda kiliarifu Bunge lako tukufu kuwa, baadhi ya ushauri uliotolewa na Kamati umezingatiwa na baadhi bado haujafanyiwa kazi na Serikali kama ifuatavyo:-

- a) Utekelezaji wa miradi ya REA bado inakabiliwa na changamoto kubwa ya maeneo mengi kuachwa/kurukwa katika vijiji na vitongoji pamoja na Viongozi na Wananchi kutoshirikishwa vya kutosha katika uainishaji wa maeneo.
- b) Serikali bado haitengi na kupeleka bajeti ya kutosha kuiwezesha TPDC kutekeleza majukumu yake ya msingi kama inavyotakiwa. Mfano dhahiri ni kusuasua katika kutekeleza miradi ya kusambaza gesi katika mikoa ya Dar Es Salaam na mikoa mingine; hususan kuwekeza katika miundombinu ya kusambaza gesi kwa watumiaji.
- c) Serikali bado hailiwezeshi vya kutosha Shirika la Ugavi wa Umeme Nchini (TANESCO) kwa kulipatia Fedha za kutosha kutelekeza majukumu yake. Kama vile ukarabati wa Miundo mbinu na vituo vya kufua umeme.
- d) Miradi ya Joto ardhi bado imeshindwa kutekelezwa kutokana na kutoupelekewa fedha. Kwa mfano kwa mwaka wa fedha 2017/18 ni **asilimia 0.17** tu ya fedha za miradi ya maendeleo ndiyo iliyopelekwa kwa taasisi ya TGDC.

7.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA (FUNGU 58) MWAKA WA FEDHA 2018/2019

7.1 Mapitio ya Malengo ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019

Mheshimiwa Spika, Mwaka wa Fedha 2018/19 Wizara itatekeleza na kusimamia Malengo Makuu Sita (6) yafuatayo:-

- i) Kuongeza uzalishaji na kuboresha mifumo ya usafirishaji na usambazaji wa umeme;
- ii) Kuongeza mchango wa nishati jadidifu katika matumizi mbalimbali ya nishati;
- iii) Kuimarisha shughuli za utafiti na uzalishaji wa mafuta na gesi asilia;
- iv) Kuboresha rasilimali za Wizara ili kutoa huduma bora za nishati;
- v) Kutekeleza kwa ufanisi mkakati wa Taifa wa kupambana na kuzuia rushwa; na
- vi) Kupunguza maambukizi ya VVU na UKIMWI sehemu za kazi na kuboresha utoaji wa huduma kwa waarithika.

Mheshimiwa Spika, malengo haya yakitekelezwa vizuri yatatimiza azma ya Wizara ya kuhakikisha kuwa rasilimali za Nishati zinachangia ipasavyo katika maendeleo ya nchi, kijamii na kiuchumi kwa manufaa ya Watanzania.

7.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato

Mheshimiwa Spika, makisio ya makusanyo ya maduhuli kwa Mwaka 2018/19 ni **shilingi 394,450,860,000**. Kati ya makusanyo hayo, jumla ya **shilingi 394,440,858,600** zitakusanywa kuititia shughuli za mafuta na gesi asilia na **shilingi 10,002,000** zitakusanywa kuititia shughuli za utawala. Kiasi hiki ni pungufu kwa **shilingi 108,839,313,096** ikilinganishwa na mapato yaliyotarajiwा kukusanywa mwaka 2017/18.

Kamati inaamini kuwa kadirio hili ni la chini na kwamba Wizara inao uwezo wa kukusanya zaidi endapo

itaweka mikakati madhubuti kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato kwa vyanzo na rasilimali zilizopo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2018/19, Wizara ya Nishati inakadiriwa kutumia jumla ya **Shilingi Trilioni 1,692,286,014,000** ikilinganishwa na **Shilingi bilioni 998,337,759,500** kwa mwaka 2017/18 kwa iliyokuwa Wizara ya Nishati na Madini, sawa na ongezeko la **asilimia 69.5**.

Mheshimiwa Spika, Bajeti iliyotengwa kwa mwaka 2018/19 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ni **Shilingi 1,665,141,000,000** sawa na **asilimia 98.4** ya bajeti yote ya Wizara. Bajeti ya Fedha za ndani iliyotengwa kwajili ya miradi ya maendeleo ni **shilingi 1,489,741,000,000** sawa na **asilimia 89.5** ya bajeti ya maendeleo sawa na **asilimia 99** ya bajeti yote ya fedha za ndani imetengwa kwa miradi mikubwa ya kimkakati.

7.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi

Mheshimiwa Spika, bajeti ya matumizi ya kawaida iliyotengwa kwa Mwaka 2018/19 ni **shilingi 27,145,014,000** sawa na **asilimia 1.6** ya bajeti yote ya Wizara. Kati ya Fedha hizo **shilingi 15,025,821,000** ni kwajili ya matumizi mengineyo (O.C) na **shilingi 12,119,193,000** ni kwajili ya mishahara (P.E) ya watumishi wa Wizara na Taasisi zilizopo chini ya Wizara.

8.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

Mheshimiwa Spika, baada ya Kamati kutekeleza majukumu yake ya kikanuni ambayo ni ukaguzi wa miradi ya maendeleo, uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara, kwa Mwaka wa fedha 2017/18 na makadirio na matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa fedha 2018/19, Kamati ina maoni na ushauri ufuatao:-

8.1 Bunge linaidhinisha Fedha za miradi ya maendeleo kama Wizara inavyoomba kwa kila Mwaka wa fedha husika , **Hivyo basi Kamati inashauri Serikali kupeleka Fedha za miradi ya maendeleo kwa wakati, Kutopatikana**

kwa wakati kunaathiri utekelezaji wa miradi ya maendeleo hali inayopelekea miradi kuzorota na washauri elekezi kutokulipwa fedha za kutekeleza miradi.

8.2 Kwa mwenendo huu wa utolewaji wa fedha za miradi ya maendeleo wa kususua hususani miradi ya REA; ambapo hadi kufika tarehe 5 Mei, 2018 ni vijiji 4,730 vimefikiwa na miundo mbinu ya umeme kati ya vijiji 12,268 vya Tanzania bara, Kamati inaona kuwa azma ya kuvifikishia vijiji vyote miundo mbinu ya umeme haitatimia ifikipa 2021.

8.3 Kamati inaishauri Serikali kutekeleza miradi mipyä ya usafirishaji na usambazaji umeme ikiwa ni pamoja na kupeleka fedha za kutekeleza miradi hiyo, kuja na mkakati maalum wa kuunganisha mikoa yote iliyo nje ya gridi ya Taifa hususani Kigoma, Katavi, Lindi, Mtwara, Kagera na Rukwa.

8.4 Upatikanaji wa umeme nchini bado ni changamoto kubwa katika maeneo mengi kutokana na miundo mbinu mibovu hali inayopelekea kukwama kwa shughuli nydingi za uzalishaji hasa za viwanda, **Kamati inashauri Serikali kutoa fedha za kutosha kukarabati miundo mbinu ya umeme ili kupunguza adha kwa wananchi na kuondokana na tatizo la umeme kukatika mara kwa mara.**

8.5 Serikali inapaswa kuharakisha mchakato wa majadiliano ya uwekezaji wa mradi wa LNG ili kukwepa tishio la kutekwa kwa soko la biashara ya gesi na nchi nydingine.

8.6 Kamati inaendelea kusisitiza kwa serikali kuwekeza katika vyanzo vingine vya kuzalisha Nishati mbadala, Aidha, **kuwekeza zaidi katika nishati jadidifu (*renewable energy*) ambayo uzalishaji wake ni nafuu na rafiki kwa mazingira, mfano uzalishaji wa umeme wa upепо katika maeneo ya Singida, Makambako na Same yenye upепо wa kutosha.**

8.7 Serikali ihakikishe TANESCO inajielekeza kwenyeb matumizi ya teknolojia ya kisasa yatakayoiwezesha

kutokuzima umeme pindi inapofanya matengenezo ya Mitambo.

8.8 Kamati inaishauri Serikali kuja na mkakati wa kulipa madeni ya Taasisi inazosimamia na kuonesha jithhada za dhati katika kulipa wazabuni wanaozidai taasisi hizi. Mfano Hadi kufikia Februari 2018, Wazabuni mbalimbali walikuwa wanaidai TANESCO jumla ya **Shilingi bilioni 969**.

8.9 Kamati inaishauri Serikali kuendelea Kuimarisha doria katika njia za umeme pamoja na kuhamasisha wananchi kushiriki katika ulinzi wa miundombinu ya usafirishaji na usambazaji wa umeme ili kupunguza tatizo la wizi wa umeme na vishoka ambao wamekua wakiiba umeme.

8.10 Kamati inaendelea kuishauri na kusitiza kwa Serikali kushirikisha wananchi pamoja na viongozi wao wakati wa kuainisha maeneo ya kutekeleza miradi ya REA, kwa kufanya hivyo, maeneo mengi ya vijiji na vitongoji hasa yale ya kijamii yatapata huduma ya Nishati hii muhimu.

8.11 Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuzingatia ubora wa vifaa hasa mashine Humba (*Transformer*) zinazofungwa wakati wa utekelezaji wa miradi ya REA awamu ya tatu.

8.12 Katika kuhamasisha uwazi na uwajibikaji wa rasilimali za mafuta na gesi Asilia, Serikali inapaswa kuendelea kutoa elimu ya kutosha kwa wananchi juu ya manufaa ya rasilimali hizi za mafuta na gesi asilia na faida zake kama taifa katika utumiaji wa rasilimali hizi. Aidha, manufaa yauwepo wa rasilimali hizi yanapaswa kuonekana kwa wananchi.

8.13 Kamati inaiushauri Serikali kulipa fidia kwa wakati wananchi wote wanaotoa maeneo yao kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo, mfano miradi ya Gesi Asilia *LNG* mkoani Lindi, pamoja na wananchi wa Igunga waliopisha mradi wa ujenzi wa kusafirisha umeme Kv400 Singida- Arusha.

8.14 Serikali inapaswa kutafuta fursa zaidi za masomo kwa vijana kwajili ya kuendeleza taaluma mbalimbali kuhusiana na masuala ya uendelezaji ya Nishati kama vile jotoardhi. Kusomesha vijana katika kuendeleza taaluma hizi kutapunguza kwa kiasi kikubwa tatizo la uhaba wa wataalam pamoja na kuongeza soko la ajira nchini tena wenye ujuzi stahiki.

8.15 Kwa kuwa Serikali imeshindwa kuendeleza kampuni yake ya Tanzania Concrete Poles Manufacturing company limited (TCPM) katika utengenezaji wa nguzo za zege. Na kwakuwa hata kuingia ubia na Wawekezaji wengine utekelezaji wake umekuwa wa kusuasua. Hivyo basi, ili kuharakisha matumizi ya nguzo hizo katika miradi inayoendelea hususani Miradi ya REA Kamati inashauri Serikali kuharakisha utekelezaji na uendelezaji wa kampuni hiyo kwa kuipatia mtaji, vilevile kutoa fursa kwa kampuni ambazo zinazalisha nguzo hapa nchini.

9.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyevit i wote wa Bunge, kwa kazi nzuri mnayoifanya ya kuliongoza Bunge hili tukufu. Mungu awajalie afya njema, hekima na busara, katika kutekeleza wajibu huu mkubwa tulio wakabidhi.

Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, kwa Waziri wa Nishati Mhe. Dkt Medard Matogolo Kalemani, (Mb), Mhe. Subira Khamis Mgusu, (Mb)- Naibu Waziri wa Nishati pamoja na Watendaji wote wa Wizara hiyo wakiongozwa na Katibu Mkuu, Dkt. Hamisi Mwinyimvua, kwa ushirikiano wao mkubwa kwa Kamati yetu wakati wote.

Kwa namna ya pekee nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, kwa weledi na umahiri waliounesha wakati wote wa kutekeleza majukumu ya kamati. Kwa heshima kubwa naomba majina yao katika orodha ifuatayo yaingizwe kwenye Hansard:-

1. Mhe. Dustan Luka Kitandula, Mb - **MWENYEKITI**
2. Mhe. Mariam Ditopile Mzuzuri, Mb – **M/MWENYEKITI**
3. Mhe. Hamida Mohamed Abdallah, Mb
4. Mhe. Catherine Valentine Magige, Mb
5. Mhe. Hamoud Abuu Jumaa, Mb
6. Mhe. Vedastus Mathayo Manyinyi, Mb
7. Mhe. Jesca David Kishoa, Mb
8. Mhe. Seif Khamis Said Gulamali, Mb
9. Mhe. Ussi Salim Pondeza, Mb
10. Mhe. Mwantakaje Haji Juma, Mb
11. Mhe. Maryam Salum Msabaha, Mb
12. Mhe. Wilfred Muganyizi Lwakatare, Mb
13. Mhe. Kiza Hussein Mayeye, Mb
14. Mhe. Mohamed Juma Khatib, Mb
15. Mhe. Bahati Ali Abeid, Mb
16. Mhe. Msukuma Joseph Kasheku, Mb
17. Mhe. Ajari Rashid Akbar, Mb
18. Mhe. Yosepher Ferdinandi Komba, Mb
19. Mhe. James Kinyasi Millya, Mb
20. Mhe. Lameck Okambo Airo, Mb
21. Mhe. Suleiman Masoud Nchambi, Mb
22. Mhe. Zubeda Hassan Sakuru, Mb
23. Mhe., Mohamed Ally Kessy, Mb
24. Mhe. John Wegesa Heche, Mb
25. Mhe. Frank George Mwakajoka, Mb

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndg. Stephen Kagaigai, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndg. Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi, Ndg. Michael Chikokoto, Makatibu wa Kamati Ndg. Mwanahamisi Munkunda na Ndg. Felister Mgonja, pamoja na Msaidizi wa Kamati, Ndg. Grace Mwenye, kwa uratibu mzuri wa shughuli zote za Kamati na hatimaye kukamilisha Taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya; sasa naliomba Bunge lako Tukufu, likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya **Fungu 58** Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 ambayo ni **Shilingi 1,692,286,014,000.**

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja,
naomba kuwasilisha.



Dunstan Luka Kitandula, (Mb)

MWENYEKITI
KAMATI YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI
24 Mei, 2018

MWENYEKITI: Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Kitandula. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaanza na michango ya Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Mheshimiwa Ester Bulaya, baadaye Mheshimiwa Maftah Nachuma ajiandae.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia katika Wizara hii nyeti. Naomba nianze na *TANESCO* na muda ukiniruhusu nitaenda maeneo mengine. Wabunge tuliokuwa katika Bunge hili kipindi kilichopita na ripoti mbalimbali za Kamati ikiwepo kamati ya Mashirika ya Umma ambayo mimi nilikuwa mjumbe, Mwenyekiti wangu alikuwa Mheshimiwa Zitto Kabwe, tulizungumzia namna gani *TANESCO* inaijiendesa kwa hasara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya Serikali ya Awamu ya Tano haijaingia madarakani, *TANESCO* ilikuwa ikipata hasara shilingi bilioni 124. Baada ya Serikali ya Awamu ya Tano kuingia madarakani, *TANESCO* inapata hasara shilingi bilioni 346. Hasara hizi zinatokana na upungufu wa maji ya uzalishaji umeme pamoja na gharama za uendeshaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini siyo hapo tu, Mwenyekiti wa Kamati ametoka kuelezea madeni ya *TANESCO* ambayo yamepanda kwa asilimia 23 kabla ya Serikali ya Awamu ya Tano haijaingia madarakani kutoka shilingi bilioni 738 mpaka shilingi bilioni 958. Haya si maneno ya Ester Bulaya, ukisoma ripoti ya *CAG* na imesema kabisa madeni haya hayana uwiano kati ya mali za Shirika la *TANESCO* pamoja na madeni. Kwa namna nyingine *TANESCO* imefilisika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wakati haya yanatokea kulikuwa na ushauri wa Kamati yetu chini ya Mheshimiwa Zitto Kabwe ya Mashirika ya Umma na taarifa mbalimbali ya Serikali kulikuwa na mikakati mbalimbali na ambapo nchi mbalimbali pia zinafanya, kwamba, hili Shirika ni wakati muafaka sasa likagawanywa yakawa mashirika mawili. Likawepo Shirika linalo-deal/na masuala ya uendeshaji na lingine masuala ya uzalishaji, dunia nzima inafanya. Leo hii tusingekuwa tunaendelea kuzungumzia umeme wa kwenye vibaba wakati tuna-*plan* kuwa na nchi ya viwanda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii *Hong Kong* hawasheherekei miaka 50 ya Uhuru wanasherekeia miaka 50 umeme hata siku moja haujukatika kwenye nchi yao. Ni kwa sababu wana mipango mizuri katika uzalishaji na usambazaji. Sisi hatutakuwa wageni, South Africa wanafanya, jirani zetu Kenya wanafanya na hii mikakati ipo kwa nini, Serikali ya Awamu ya Tano hamtaki kufanya? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mambo haya yanafanyika, hapo sijaenda deni la *Standard chartered* la Euro zaidi ya milioni 10 na gharama za kesi takribani bilioni 7.5, hilo naliacha wataongea wengine. Wakati haya yanafanyika na hali ya *TANESCO* ilivyo dhoofu, *TANESCO* pia inashindwa kukusanya madeni makubwa. *TANESCO* inaidai hospitali ya Tumaini dola za kimarekani milioni 9.4 sawa na bilioni 18 za Kitanzania na ni kodi ya pango. Tangu mwaka 1998 hawajawahi kulipa. Kulikuwa na kesi Mahakamani *TANESCO* imeshinda tangu mwaka 2016 na maamuzi ya

Mahakama yanasema hivi, waondoke na kisha walipe *TANESCO* hizi Fedha. Mpaka hivi tunavyozungumza pamoja na maamuzi ya Mahakama *TANESCO* hawajachukua hatua yoyote pamoja na kuwa mfilisi wanahitaji fedha. (*Makof!*)

Mheshimiwa mwenyekiti, lakini kingine *TANESCO* kwa masikitiko makubwa imetoa zabuni kwa mzabuni asiyé na vigezo kinyume na mkataba. Masharti ya mkataba yanasema hivi, mzabuni awe na uzoefu wa miaka mitano, lakini sasa huyo mzabuni mwenyewe ana leseni ya kusambaza pembejeo yaani majembe, mbolea, kazi aliyopewa ni ya kusambaza nguzo ya umeme na keshakula dola milioni moja zaidi ya bilioni 2. Mkataba unasema awe na uzoefu wa miaka mitano na hii ni kinyume cha Sheria Na. 3 ya Mwaka 1972 ya Leseni na Biashara. Serikali ya Awamu ya Tano aibu, *shame, shame*, sasa haya tunayasema kwa sababu tunapenda nchi yetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati haya yanatokea mikakati ya kushindwa kugawanya *TANESCO*, mmeshindwa kulisimamia shirika vizuri, mmeshindwa kufuata ushauri uliotolewa na mikakati ya Serikali inashindwa kutekelezwa mnaenda kwenye mambo mengine ya *Stiegler's Gorge* ambayo mmeitengea bilioni 700, hizo ni fedha zetu za ndani wakati hizo fedha mngepeleka kuboresha Shirika la *TANESCO*, mngeligawa mara mbili na pesa nyingine zingeenda kwenye *REA*. Hapa Mwenyekiti wa Kamati ameeleza wazi, mbali ya kwamba *TANESCO* inadaiwa, bilioni 700 zimetengwa kwenye *Stiegler's Gorge* ambayo hatima yake hatujui. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye *REA* kwa mwaka huu wa fedha, kwenye fedha zote za maendeleo hiyo *Stiegler's Gorge* imetengewa karibia asilimia 40 ya fedha za maendeleo. *REA* ambayo *at least* mbali na changamoto zake imefanya vizuri asilimia 20 na bajeti iliyopita *REA* wamepata asilimia 49. Waheshimiwa Wabunge wote tunajua sheria, fedha zilizowekewa uazio hazipaswi kutumika kwa matumizi mengine. Fedha zinatakiwa zitolewe zote, kufanya hivyo ni kuvunja sheria na ni mfululizo wa Serikali ya Awamu

ya Tano kutokutii sheria, amesema pale Mheshimiwa Nape, mnaendelea tena kufanya hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilitakiwa hizi pesa zitolewe zote, sisi Wabunge tunaotoka mikoani tunajua umuhimu wa umeme wa *REA* kukamilika. Timizeni wajibu wenu, tuache hizi mbwembwe ndogo ndogo halafu hapa mnasema mnataka kuwa na Serikali ya Viwanda, kwa mtindo huu, kweli? Haiwezekani! Mimi niwaambie baada ya kufikiria miradi mipya una uwezo wa kuacha *legacy*kwa kukamilisha miradi uliyokuta ya umeme wa upepo, makaa ya mawe, tukamilishe haya kwanza halafu twende huko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwepo wakati pori la Selou linatangazwa kuwa urithi wa Dunia nchini Qatar na dunia ikakubali kutusaidia kutupa fedha nydingi. Leo tunaenda kukata miti millioni mbili huko kwenye huo mradi halafu nasikia mkiulizwa mnasema ooh, tumechukua eneo dogo, jamani ni kama mwili moyo ni mdogo lakini mwili mkubwa, toa moyo kama binadamu utaishi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi yetu sisi Wabunge ni kushauri na kusimamia Serikali ifanye kazi yake ipasavyo kwa ajili ya vizazi vyetu vijavyo. Tunalipenda Taifa hili, hatuhitaji deni la Taifa lionezeke kwa sababu hakuna mipango thabiti ya kuivusha nchi yetu. Ukiona mpaka wengine tunasema hivi yametuchosha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi, timizeni wajibu wenu, acheni mbwembwe ndogo ndogo. (*Makofi/Vigelegele*)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Ester Bulaya lakini Shirika la Umeme bado halijafilisika na umeme ndio huu tunautumia. Kwa hiyo, tuwaombee Mungu asiwajalie kuafilisika. Tunaendelea na Mheshimiwa Maftah.

MHE. MAFTAH A. NACHUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Namshukuru Mwenyezi Mungu, Subhanahu wa taala, Mwenyezi Mungu ambaye ameendelea kunipa afya

njema. Asiyeshukuru kidogo basi hata akipewa kingi hawesi kushukuru. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi tulikuwa Mtwara na Lindi tukiwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Dkt. Kalemani tumeenda kuzindua umeme, sasa hivi Mtwara na Lindi tumeunganishwa kwenye Gridi ya Taifa, tunashukuru sana. Tunashukuru sana kwa sababu na sisi sasa tumewekwa mionganoni mwa Watanzania maana kwa miaka mingi tumekuwa tukililia suala la Mikoa ya Kusini kuunganishwa na Gridi ya Taifa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru kwamba Mtwara Mjini hivi sasa tumezindua pia mashine mbili mpya ambazo zitaenda kutoa megawati nne za umeme lakini bado mpaka leo hazijaunganishwa sawasawa, tumeenda kuzindua tu. Kwa hiyo, niombe Mheshimiwa Waziri kwamba zile mashine sasa zianze kufanya kazi kwa sababu ile juzi tukiwa pale Mtwara bado umeme usiku ulikatika kwa sababu zile mashine bado hazijaanza kufanya kazi. Kwa hiyo, nikuombe sana Mheshimiwa Waziri Dkt. Kalemani mashine hizi sasa ziunganishwe na mashine zingine zile tisa tuweze kuondoa tatizo la kukatika kwa umeme mikoa hii ya Mtwara na Lindi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze suala hili ambalo nimekuwa nazungumza kwa muda mrefu ndani ya Bunge hili na huu ni mwaka wangu wa tatu nazungumza haya. Kumekuwa na eneo ambalo tunasema ni mkuza wa gesi ambapo bomba la gesi limepita na ikumbukwe Mikoa ya Mtwara na Lindi na hasa Jimbo la Mtwara Mjini, wananchi waliandamana wakapigwa risasi wengine wakauwawa wakidai kujua namna gani hii gesi itaweza kuwanufaisha, tukawa tumeahidiwa sana. Mionganoni mwa ahadi za Serikali zilikuwa ni kupewa umeme wa uhakika. Kwa hiyo, tunashukuru sasa hivi hili linakuja kutekelezwa lakini tunaomba kuwe na kasi ya kusimika zile mashine umeme usikatikekatike. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kwenye haya maeneo ni ule mpango wa Serikali, waliambiwa

wawapelekee wananchi nguzo za umeme lakini walichofanya ni kupeleka nguzo chache sana kwenye huo mkuza wa gesi kwa maana ya maeneo lilitpopita bomba la gesi ambapo Serikali ilisema lazima wale wananchi wapate umeme. Maeneo ya Mtwara Mjini, Lindi na maeneo mengine lakini kilichofanyika Serikali imepeleka nguzo chache sana, wananchi wengi katika maeneo yale hawajapata umeme. Wakitaka kulipia umeme wanalipa kwa bei kubwa sana, nguzo wanunue kwa Sh.500,000, kitu ambacho Serikali ilishasema kwamba wale watu watapelekewa nguzo kwa sababu bomba la gesi limepita mule waweze kuunganisha umeme kwa Sh.27,000 lakini kinachotokea ni kinyume kabisa nguzo zimeenda chache sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maeneo ya Jimbo la Mtwara Mjini, kwa mfano, Mtawanya bomba la gesi limepita mule nguzo za umeme hazijaenda kabisa, maeneo ya Magomeni, pale pale Mtwara Mjini baadhi ya maeneo nguzo hazipo. Kuna maeneo ya Chipuputa hakuna nguzo za umeme, kuna maeneo ya Kiholo, Komoro pale Mtwara Mjini, Mbaye na Mitengo, kote huko bomba la gesi limepita na Serikali iliahidi itapeleka umeme maeneo yale lakini nguzo zimeenda chache sana na wananchi wa wakienda kuomba *TANESCO* wanaambiwa hapa nyie ni mjini, kwa hiyo, mnalipia Sh.500,000 nguzo na ukilipa hiyo Sh.500,000 ndio tutakupeleka umeme. Sasa tunaenda kinyume kidogo na ahadi na nia ya Serikali. Yawezekana wakati mwininge Mheshimiwa Waziri hayajui haya lakini watendaji kule wanafanya haya, wananchi wananiagiza mimi kila siku na ndani ya Bunge hili nimekuwa nazungumza sana. Naomba sana Wizara iangalie maeneo haya ambayo yalikuwa ni ahadi ya Serikali kupeleka umeme kutokana na kupatikana kwa gesi hasa katika maeneo ya ule mkuza wa gesi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna maeneo pia ya pembezoni kwenye miji hii iliyopo Mtwara na Lindi, maeneo yale ambayo mwanzo kabla mji haujatangazwa kuwa Manispaa yalikuwa ni maeneo ya vijijini lakini yale maeneo yakaingizwa kwenye Manispaa lakini kumekuwa na tatizo sana la umeme na tumekuwa tunaongea sana. Ndani ya

Bunge hili nimeongea sana yale maeneo ya pembezoni ambayo sasa hivi ni mitaa mwanzoni yalikuwa ni vijiji wapelekewe huu mpango wa umeme ambao Serikali inasema imeweka mkakati wa kusambaza umeme, tunasema *diversification of electricity* yaani yale maeneo yapelekewe isije ikawa tunatumia sana vyombo nya habari kuzungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwenye hii hotuba leo imetaja sana Mtwara na Kusini, nimekusikia sana Mheshimiwa Waziri Kalemani lakini sasa tunaomba haya maeneo umeme upelekwe kwa sababu unaambiwa na watendaji kwamba huku tunafanya kila nikikuuliza Waziri unaitikia sana unasema bwana nimepewa taarifa kwamba tunapeleka na mwaka jana uliniahidi Mheshimiwa Waziri kwamba utakuja Mtwara nikupeleke kwenye maeneo niende kukuonesha haya ninayozungumza lakini haujafika. Nikuombe mwaka huu baada ya bajeti mguu kwa mguu wewe na Naibu Waziri wako Mheshimiwa Subira anajua sana Mtwara, kakaa sana Mtwara huyo, tunatembea mguu kwa mguu, niite mkutano wa hadhara wananchi wakupe kero hizi ambazo wananiagiza kila siku wananchi wa jimbo la Mtwara Mjini. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, safari hii kama Waziri hautaniahidi kwamba utapeleka umeme nang'ang'ania shilingi yako. Maeneo haya ni maeneo ya Mbawala Chini narudia tena Bunge hili limekuwa linanisikia sana nikiyataja, Mbawala Chini uende umeme, mfanye *diversification* kwenye maeneo haya. Kuna maeneo ya Kijiji Naulongo au Mtaa wa Naulongo pelekeni umeme, kuna eneo la Mkunjanguo mpaka watu sasa wanantania ndani ya Bunge wananiita Mkunjanguo kwa sababu nilikuwa nazungumza sana . (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri haya maeneo yazingatie peleka nguzo za umeme wananchi wanataka umeme, ndio manufaa yenyewe ambayo mmetuambia wananchi wa Mtwara. Kuna maeneo ya Namayanga, Dimbuzi, Mkangala tunaomba umeme

muupeleke kwenye maeneo haya. Nimekuwa nalia sana, naagizwa sana, kila siku nikifanya mukutano wa hadhara wananchi wanalia sana kwenye haya maeneo. Kwa hiyo, niombe sana mlishughulikie suala hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala hili la punguzo la umeme. Tuliahidiwa kwamba pamoja na mambo mengine manufaa ya umeme Mikoa hii ya Kusini Mtwara na Lindi kwamba kuna gesi tutapunguziwa umeme, wananchi wakaacha kuandamana. Wananchi wamenituma kwa mara nydingine nije kuzungumza ndani ya Bunge, kwa kuwa gesi bado ipo Mtwara na Lindi, lile punguzo tunaomba liendelee kuwepo msiliondoe. Kwa sababu sasa hivi wananchi wanavyoenda kuomba kuunganishiwa umeme wanaambiwa walipe Sh.390,000 wakati pale gesi bado ipo na punguzo lilikuwepo. Naomba hili punguzo wananchi wapewe, walikuwa wanaunganisha umeme kwa Sh.97,000 kwenye yale maeneo ambayo sio mkuza wa gesi tunaomba liendelee kwa sababu gesi bado Mtwara na Lindi ipo haijaondolewa katika mikoa hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuunganisha gesi majumbani tunashukuru kwamba Serikali imezungumza kwenye hotuba hapa kwamba Mtwara nayo ipo. Majaribio ya kuunganisha gesi majumbani yameanza Masaki Dar es Salaam wakati gesi yenye we iko Mtwara, tunashangaa sana gesi imetokea Mtwara kwa nini wasingeanza pale kwanza au sisi wana Mtwara hatuna majumba ya kutumia gesi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe sana isije ikawa inazungumzwa sana kwa sababu nilishalionia suala hili kwenye Kamati wakati tunapitia taarifa ya *TPDC* mwaka juzi ndiyo nikaliibua nikawaambia Mikoa ya Kusini ambako inatoka gesi yenye we kumesahaulika kabisa, ilikuwa haipo kabisa. Tunashukuru safari hii mmeweka na unatuambia kwamba tunaenda kupewa hii gesi tuweze kutumia kama nishati. Hii itapunguza matumizi ya mkaa na ukataji wa misitu kule. Kwa hiyo, tunaomba suala hili Mtwara Mjini, Lindi Mheshimiwa Waziri alizingatie kwamba wananchi wanahitaji

gesi majumbani isiwe inazungumzwa tu halafu mnaanza Dar es Salaam, kule kwenyewe inapotoka gesi kunakuwa ni kizungumkuti. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine naomba kuzungumzia suala la viwanda. Serikali ya Awamu ya Tano inasema kwamba ni Serikali ya viwanda. Kusini kuna wawekezaji wanahitaji kujenga viwanda vyta mbolea, *Petrochemical*, wanataka kujenga viwanda vyta mbolea Mtwara na Lindi mpaka leo bado wanapigwa danadana tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Mheshimiwa Waziri mwaka huu hawa watu wape gesi wawezo kujenga viwanda vyta mbolea kwa sababu viwanda vitatoa ajira kwa wananchi wa Mtwara na Lindi na sisi tutaondokana na umaskini kwa sababu gesi hii Mwenyezi Mungu ametupatia imeanzia pale. Wenzetu maeneo mengi ya Tanzania viwanda vimejengwa siku nyingi sisi tuna kiwanda kimoja tu cha Dangote nacho kinasuasua.

MWENYEKITI: Ahsante sana.

MHE. MAFTAH A. NACHUMA: Kwa hiyo, niombe sana Mheshimiwa Waziri safari hii unitekeleze mambo haya, ahsante sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Maftah tunaendelea na Mheshimiwa Jamal Kassim baadaye Mheshimiwa Stephen Ngonyani ajiandae.

MHE. JAMAL KASSIM ALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Awali ya yote niungane na wenzangu kuipongeza Serikali na hususani Wizara yetu hii kwa jitihada kubwa ambayo wanaifanya katika kuhakikisha nchi yetu inapata umeme wa kutosheleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika hotuba leo nitachangia maeneo mawili. Eneo la kwanza nitaanza kuchangia suala la *TAENESCO*. Kusema ukweli kwa takribani

kipindi cha miaka 10 sasa Shirika letu la Umeme la *TANESCO* halifanya vizuri kifedha. Ukiangalia hesabu zake za fedha kwa takribani miaka 10 shirika letu hili lilikuwa linajiendoha kwa hasara. Hii nini maana yake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Tano imedhamiria kwamba tutoke kwenye kuwa Taifa la chini kwenda kuwa Taifa lenye uchumi wa kati na hatuwezi kuwa Taifa la uchumi wa kati kama hatuna viwanda na hatuwezi kuwa na viwanda kama hatuna umeme wenye kutosheleza na uhakika. Hatuwezi kuwa na umeme wa uhakika na wa kutosheleza kama hatuna Shirika la Umeme imara kifedha na kiufanisi. Ukiangalia hesabu zetu hizi za *TANESCO* inaonesha kabisa ipo haja ya kufanya mabadiliko makubwa ya kiutendaji ndani ya shirika letu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hili limeongelewa sana. Mwaka 2002, *Mercado Energético Company* ya Argentina ilifanya stadi ya Shirika la Umeme la *TANESCO* na mapendekezo yake yakawa ili shirika hili liwe la ufanisi lazima *unbundling* ifanyike, tuwe na kampuni ya *generation*, tuwe na kampuni ambayo itasimamia masuala ya *transmission* na tuwe na kampuni ambayo itasimamia masuala ya *distribution*. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, mwaka 2003 *Consultancy Company* ya Marekani nao walifanya utafiti wa Shirika la *TANESCO* wakaja na mapendekezo hayo hayo. Sio hayo tu, mwaka 2005 iliundwa *Presidential Team on Privatization Review of Utility* ikiongozwa na Profesa Chijoriga nao walipendekeza hayo hayo. Mwaka 2014, *Price Waterhouse Coopers* walajiriwa wafanye *study* ya Shirika la *TANESCO* nao walipendekeza hayo hayo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niishauri Serikali baada ya mapendekezo ya *Price Waterhouse Coopers* wakaja na mpango wa miaka 11 wa *Electricity Supply Industry Reform Strategy Roadmap* ambao ulikuwa ni mzuri kabisa ultafsiri mapendekezo yote ambayo washauri elekezi na hizi timu ambazo ziliundwa kuyaingiza katika utekelezaji lakini mpaka

leo hii kimya. Ukiangalia taarifa za *CAG* za hesabu za *TANESCO* kuanzia mwaka 2010 *TANESCO* ilipata hasara ya shilingi bilioni 47, mwaka 2011 ilipata hasara ya shilingi bilioni 43, mwaka 2012 ilipata hasara ya shilingi bilioni 178, mwaka 2013 ilipata hasara ya shilingi bilioni 467, mwaka 2014/2015 ilipata hasara ya shilingi bilioni 124.5, mwaka 2015/2016 imepata hasara ya shilingi bilioni 346. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi *reform* sio sisi wa kwanza wenzetu wa Kenya na Uganda walifanya. Mwaka 1996 Kenya walikabiliwa na changamoto kama zetu, Shirika la Umeme la Kenya lilikuwa moja tu mwaka 1996 wakali-*unbundling* wakawa na shirika ambalo linasimamia masuala ya uzalishaji, shirika linalosimamia *transmission* na shirika ambalo linasimamia masuala ya *distribution*. Nini hatima yake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu Kenya leo hii wanarealize matunda ya *reform* yao. Mwaka 2015 taarifa za ukaguzi wa Shirika la Umeme la Kenya (*KPLC*) zimeripoti faida ya Kenya shilingi 7.56 bilioni, mwaka 2016 faida ya 7.2 bilion Kenya shilingi, mwaka 2017 faida ya 7.27 bilioni Kenya shilingi na miaka yote wamekuwa wanagawa gawio kwa Serikali. Mwaka jana wameweza kugawa gawio la jumla ya shilingi milioni 493 Kenya shilingi kwa Serikali lakini leo hii Shirika letu la Umeme la *TANESCO* bado linategemea lipewe pesa na Serikali kijendesha. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, halikadhalika na Uganda hivyo hivyo. Uganda mwaka 1999 walikuwa na hali mbaya zaidi kuliko ya kwetu lakini wakafanya *reform*. Leo hii ni aibu Uganda walitoka kwenye vita miundombinu yote ya umeme ilikuwa lakini leo hii Shirika lao la Umeme linazalisha faida. Mwaka jana tu waliweza kuzalisha faida shilingi bilioni 100 za Uganda na kugawa gawio bilioni 57.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe Wizara iniambie kwa vile ina mpango, huu mpango upo na ni mpago wa Wizara kabisa ina kugugumizi gani kuifuata? Mwaka huu katika ule mpango ilikuwa Shirika letu la Umeme la *TANESCO* liwe *unbundling* tuanze hizo *reform*. Kwa hiyo, namuomba

Mheshimiwa Waziri atakapokuja ku-*wind up* aje aelete tatizo ni nini, kwa nini hatuendi kwenye mpango ambao tayari Serikali iliukubali na kuupitisha na kwa nini mpaka leo haujatekelezwa? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ambalo nataka kuchangia ni suala la mauziano ya umeme baina ya *TANESCO* na Zanzibar. Kusema ukweli kwa kipindi kirefu sasa hili suala limekuwa vuta nikuvute.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakubaliana nami kwamba kuna tatizo kubwa baina ya biashara hii ya umeme kati ya *TANESCO* na upande wa Zanzibar yaani *ZECO*, muda mrefu sana wamekuwa wakirumbana kuhusu bei stahiki ya kuuziwa umeme na muda mrefu sana hili suala halijapatiwa ufumbuzi. Nimshauri Mheshimiwa Waziri, *theoryzote za upangaji* bei ya umeme zinalekeza kwamba jambo la kwanza bei ya umeme itapangwa kwa kuzingatia gharama za kuufikisha umeme kwa ngazi ya mteja husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zanzibar inachukua umeme katika *level/ya transimision line* 132Kv. Gharama za kuufikisha umeme katika 132Kv ni ndogo kuliko kufikisha umeme katika *medium voltage* na *low voltage*. Ukiangalia bei ya umeme ambayo Zanzibar imekuwa inauziwa haiwiani kabisa, kwanza Zanzibar ni *bulk purchaser* lazima *preferential treatment* ambayo ipo, ukienda *South Africa* kuna *bulk purchaser* ambao wao wanapewa *preferential treatment* na sehemu nyingine mbalimbali duniani ukiachilia mbali suala la kwamba gharama za kuufikisha umeme katika 132Kv ni ndogo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia bei ambayo Zanzibar inanunua umeme, naomba nisome, *unity* moja ya *KVA* Zanzibar inanunua kwa Sh.16,550, wakati wateja ambao wapo katika *media voltage* ambapo gharama ya kupeleka umeme katika *media voltage* ni kubwa wanauziwa na *TANESCO* hiyo hiyo *unity* moja kwa Sh.13,200. Hili si sawa kabisa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukichukua Kenya, nadhani nichukue na Kenya Mheshimiwa Waziri aone mteja wa *high voltage* anachajiwa Sh.4,900 za Kenya wakati mteja wa *low voltage* anachajiwa Sh.6,000, umeona? Kwa hiyo, hapa suala la umeme na bei inayouziwa Zanzibar si sawa na haya madeni hayatokaa yalipike kwa sababu hili tatizo la bei ni kubwa ambalo linaathiri Shirika la Umeme la Zanzibar kulipa madeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nashukuru kwa kunipa nafasi. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Jamal, tunaendelea na Mheshimiwa Stephen Ngonyani.

MHE. STEPHEN H. NGONYANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijachangia, nataka nirudie suala langu la jana naomba nishukuru watu wafuatao. Nimshukuru Mheshimiwa Spika, Katibu wa Bunge, Ofisi ya Uhasibu, Wabunge wote wa Mkoa wa Tanga kwa msaada walionipatia, Wizara ya Afya chini ya Mheshimiwa Waziri Ummy, pamoja na Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na rafiki yangu Ndassa kila wakati alikuwa anakuja kumuona mgonjwa pale Muhimbili. Mungu awabariki sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri kwa kazi kubwa ambayo wanayoifanya. Leo ilikuwa nichangie makubwa sana lakini kufuatana na hotuba na gawiwo walilokuwa wamelipata, Wabunge wenzangu tujaribu kuwaunga mkono hawa mabwana. Kwa sababu tulikuwa tunatarajia kwamba Serikali au Hazina ingetupatia fedha nyingi ili itusaidie katika suala la umeme lakini cha kushangaza ni kwamba hela zile nyingi hazikupatikana na Waziri anafanya kazi katika mazingira magumu na amekuja kwangu mara nyingi na amesema yale aliyokuwa anataka kuyafanya hayafanyiki kwa sababu hana fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tuwashukuru sana wenzetu wa *REA* wanafanya kazi katika mazingira magumu. Hata hivyo, tuna mtihani Wabunge wote tuliokuwa hapa ndani, bila kukaa vizuri na Hazina wakatupa fedha hawa Wabunge hapa wameweka Ubunge wao rehani. Wakati wa mwanzo tulipewa orodha ya vijiji ambavyo vitapata umeme wa *REA* na Wabunge wakafurahia wakapeleka katika majimbo yao na kuonyesha kwamba umeme huu utafika kwa wakati fulani. Cha kusikitisha vijiji ambavyo vilipewa majina na Wabunge tukaenda tukavisemea na Madiwani wakaenda wakavisemea vimematwa vyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, nina kata ishirini na tisa, kuna kata saba ambazo toka Uhuru hazijapata umeme. Mwaka huu ziliingizwa kwenye mpangilio wa kupata umeme, leo hii naambiwa zile kata hazina umeme, nina kwenda kuwaambia nini wapiga kura? Inasikitisha sana, nina Kata za Kizara, Kalalani, Mpale, Mswaha, Mkalamo na Folofolo toka Uhuru umeme wanausikia. Uizingatia Wilaya ya Korogwe ina viongozi wakuu wanatoka pale. Kwa mfano, kata ambayo anatoka Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu, Kata ya Mkomazi haina umeme. Huyo Assad ambaye anawakagua hapa anatoka kwenye jimbo langu lakini kwake hakuna umeme. Ukienda Kata ya Mtindiro, Kijiji cha Mtindiro hakina umeme, ukienda vijiji vingine zilivyoko pale havina umeme. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Askofu Mkuu wa Anglikana anatoka kwenye Jimbo langu, Mheshimiwa Mndolwa lakini leo hii umeme umepita nyumbani kwake, wameruka, wanakwenda kuangalia sehemu nyingine, mnatuweka wapi? Wabunge tutasema nini kwa wapiga kura? Keshokutwa mnataka tuwachague Wenyeviti wa Serikali za Vijiji watakwenda kusema nini kwa wananchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi simlaumu kabisa Mheshimiwa Waziri, wala siwalaumu watu wa *REA*, wanafanya kazi katika mazingira magumu lakini huko Hazina

kuna nini kibaya? Leo mnatuandikia hapa kwamba tunapokwenda kulipa bili *TANESCO*, *REA* wanakata asilimia 3, Ewura wanakata asilimia 1, nani anachukua hela hii? Leo hii kila tukisema hela, makandarasi wanasema hela hawajapewa, unaangalia ukienda kwenye mafuta tunakatwa hela, ukienda kwenye kulipia umeme tunakatwa hela, maji tunakatwa hela ya umeme leo hii tukikulaumu Mheshimiwa Waziri tunafanya makosa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Wabunge wenzangu tuungane tumsaidie hizi fedha ambazo zilikuwa zinazungushwa apatiwe tumaliziwe miradi yetu. Mheshimiwa umezunguka nchi nzima hii unawasha umeme lakini cha kushangaza katika vijiji vyote watu wamerundika nguzo tu ukiuliza wanasema hatujapewa fedha. Sasa tunaipeleka wapi hii nchi, tunapeleka wapi wapiga kura wetu? Mheshimiwa Waziri wa Fedha kama hizi hela zilikuwa haziendi *REA* au *TANESCO*, basi naomba tuondoeni hapa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo wananchi wanatulalamikia wanasema Wabunge wanakwenda kulala, Wabunge wanaonyesha nia kwamba tunatetea umeme, umeme huo tunautetea ni upi? Kama umeme haupatikani, umeme haufiki, Waziri amekuja kwenye Jimbo langu wakati wa kampeni akasema sehemu ambazo zilikuwa hazina umeme upatikane. Kinachoshangaza sana Mheshimiwa Waziri, vile vijiji ambavyo ulisema vipate umeme havipati tena umeme kinapata kijiji kimoja eti hela hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii kwenye Jimbo langu kuna mradi wa maji, kuna nguzo zimebekwa na *TANESCO* toka 2004 mpaka leo waya hazijawekwa. Tumekwenda na viongozi wa *TANESCO* wa Mkoa, viongozi wamekwendwa pale wamenisemea, wananchi wamesikia leo wanakwambia umeme haufiki, mimi mnaniweka wapi na Wabunge wengine tunawaweka wapi? Hii ipo ndani ya llani ya Uchaguzi, kwa nini tusitekeleze haya mambo? Mheshimiwa Dkt. Kalemani ni mchapakazi wa hali ya juu sana, hebu tujaribu Bunge hili

kuhakikisha pale mahali ambapo fedha za *EWURA* na *REA*, zilipokwamia zijaziwe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mweyekiti, suala la pili ni la bomba la mafuta. Tuna kawaida mabomba ya mafuta au kitu chochote kizuri kinapokuja wananchi wanakuwa hawatengewi sehemu badala yake wanachukuliwa watu kutoka nje Watanzania tunabaki hivihivi. Mheshimiwa Waziri bomba la mafuta umekuja, umeliona, umetathmini, umetupa hamasa, watu hawa wote wanaopitiwa na bomba la mafuta naomba Watanzania wawe wa kwanza kupewa kazi. Kuna taratibu watu wanakuja na watu wao, Watanzania ambaa watalilinda bomba lile hawapati kazi. Naomba Mheshimiwa Waziri, wewe ni msikiu sana na ni rafiki yangu sana lakini kwa leo naomba uhakikishe kwamba bomba la mafuta linalopita katika ile Mikoa yote Watanzania wa nchi hii wapate kazi kwanza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, nisisitize katika vijiji ambavyo mlikuwa mna-*support* kwamba vipate umeme Tanzania nzima, kwa kuititia mpango wa *REA* naomba virudishwe kwenye orodha. Mkurugenzi wa *REA* Maganga anakaimu, unafikiri atatoa maamuzi gani? Huyo Bwana Msofe ni mtu mmoja mzuri ukimpigia simu hata saa nane za usiku anakupokea, ukienda Mwenyekiti wa Bodi wa *REA* ni watu wasikivu, wapewe fedha ili hii kazi iishe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya machache, kwa sababu naumwa niliomba tu niwe mtu wa kwanza, naomba niwahi Muhimbili lakini naunga mkono asilimia mia kwa mia Waziri apatiwe fedha afanye kazi. Mungu awabariki sana, ahsanteni sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Stephen Ngonyani. Tunamalizia muda wetu na Mheshimiwa Hasna Mwilima.

MHE. HASNA S. K. MWILIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia Wizara hii muhimu sana kwenye majimbo yetu. Kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na watendaji wao wote ndani ya Wizara hii ya Nishati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo langu lina vijiji 61 lakini vijiji ambavyo vina umeme mpaka sasa ni 6 tu. Wengine wakismama hapa wanasema wamebakisha vijiji 10, 5, tumuombe Mheshimiwa Waziri wakati mnapopanga mradi huu wa Awamu ya III wa REA tukuletea umeme, hebu sisi ambao hatuna umeme kabisa tuwe kipaumbele. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliuliza hapa swalii la nyongeza, kwa bahati mbaya ukachanganya Nguruka na Uvinza, ukasema kwamba mimi na wewe tuliambatana Nguruka kwenda kuwasha umeme. Mheshimiwa Waziri mimi na wewe tuliambata Uvinza kwenda kuwasha umeme. Umenichonganisha na wananchi wangu wa Nguruka. Sasa Mheshimiwa Waziri ili kuninasua na wananchi wangu wa Nguruka, naomba sana tuletewe umeme kwenye Vijiji vya Chagu, Ilalanguru, Mganza, Nyangabo, Nguruka, Itegula, Kasisi, Amriabibi na Mpeta. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataja vijiji hivi kwa sababu kuna sintofahamu huko, kwamba Mheshimiwa Mbunge mbona Waziri amesema mliambatana kuja kutuwashia umeme Nguruka. Sasa hivi vijiji nilivyovitaja viko kwenye Tarafa ya Nguruka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri aniletee umeme kwa sababu, umeme wa Gridi ya Taifa unaotoka Kaliua umekuja mpaka kwenye Kata ya mwisho ya Usinge. Nachomuomba Mheshimiwa Waziri watuongezee pale *substation* ya kutoka Urambo ifungwe Kaliua na

substation nyingine iletwe Uvinza. Kwa kuyafanya haya, ina maana tutarahisisha sasa umeme wa kutoka Kaliua wa Gridi ya Taifa uweze kuingia katika hivi vijiji nilivyovitaja. Kwa kuingiza umeme kupitia Uvinza, itakuwa rahisi kuupeleka kwenye Vijiji vya Basanza na hatimaye kuingia kwenye Jimbo la Kasulu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe pia kuzungumzia REA awamu ya II. Tunavyo Vijiiji vya Kabeba, Mwakizega na Ilagara. Vijiiji hivi umeme umeshamalizika kwa maana ya nguzo, transfoma na kila kitu lakini kutohana na mvutano baina ya Wizara ya Nishati na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi mkandarasi aliyekuwa anatekeleza mradi ule kwa maana ya Mkoa wa Kigoma na Katavi na Rukwa alisimamishwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maswali yangu kwa Waziri atakapokuja hapa kuhitimisha bajeti yake anieleze au awaeleze wananchi wa Jimbo la Kigoma Kusini, hivi Vijiiji vya Mwakizega, Kabeba na Ilagara, mradi wa *REA* mkandarasi ataendelea na taratibu zilizobaki kwenye mradi ule wa *REA* wa Awamu ya II? Kwa sababu tunapata kigugumizi, kama mkandarasi huyu tayari amefutiwa mkataba na hataendelea tena, nani anayeendeleza mradi ule wa *REA* katika Kata zangu hizi mbili za Mwakizega na Ilagara? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nzungumzie umeme kuingia Kata ya Kalia. Nimuombe Mheshimiwa Waziri kwa kuwa kutoka Mwese mpaka Kijiji cha Lugufu kwenda Vijiiji vya Kashaguru, Chambusha, Kalia na hatimaye kumalizia Sibwesa ni karibu sana na Mwese kuliko kutoka kule kuja Ilagara. Sasa nimwombe Mheshimiwa Waziri hebu huu umeme ambao uko Mpanda unaelekea Mwese ndiyo mtuweke kwenye progamu ya *REA* Awamu ya III utoke Mwese, uingie katika hivi vijiji ndani ya Kata ya Kalia. Namuomba kwa unyenyekevu mkubwa na ndiyo maana leo wala siongei kwa jazba, natambua kwamba Waziri ni msikivu, Naibu Waziri ni msikivu

lakini ndugu yangu Maganga naye ni msikivu, atanisikia na kwa faida ya wananchi wa Jimbo langu la Kigoma Kusini, wananchi wa Kalia nao watapata umeme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze kwanza Wizara kwa kuona umuhimu wa kuongeza *megawatts* 45 kutoka Malagarasi hadi Kidahwe. Nipongeze jitihada hizi ni nzuri, najua kwamba mradi huu mkubwa wa Malagarasi ukitekelezwa na njia ile ikijengwa ya kutoka Malagarasi kilomita 53 hadi kufika Kidahwe wananchi watanufaika na kupata umeme wa uhakika. Kwa sasa tunatumia majenereta, uendeshaji wa majenereta jamani ni mkubwa mno na hawa wenzetu *TANESCO* kama walivyooongea Waheshimiwa Wabunge mbalimbali, uwezo wao umekuwa wa chini mno ukilinganisha na siku za nyuma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nzungumzie *TANESCO*. Umeme kwenye vijiji sita kwa maana ya Viji vya Mlela, Kandaga, Uvinza, Kazoramimba na Mwamila umeishia barabarani na ukiwaliza *REA* wanakwambia wenyewe mamlaka ya kuuchukua ule umeme na kuuingiza kwenye vijiji vya ndani ni *TANESCO*. Sasa hao *TANESCO* ambao tunawasema leo tangu mradi wa *REA* wa Awamu ya II umekamilika, hakuna *TANESCO* walichokifanya kutoa nguzo barabarani na kuapelekea wananchi wa Kandaga na Nyanganga. (*Makofi*)

Mheshmiwia Mwenyekiti, nimuombe sana Waziri, hawa *TANESCO* mbona wamebaki tu kama jina? Yaani tumebakia na *TANESCO* kama jina. Kama inaonekana *TANESCO* imefika mahali imekufa kabisa basi Serikali ituambie ili tusiwe tunasimama hapa kupiga kelele za *TANESCO*.

TAARIFA

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa

MWENYEKITI: Mheshimiwa Hasna tusikilize taarifa. Mheshimiwa Heche, haya sema.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampa tarifa dada yangu Mheshimiwa Hasna pale, tatizo la *TANESCO* wala siyo kwamba ni dude kubwa, tatizo ni kwamba *TANESCO* waliingia mikataba mibovu na Songas na Serikali yenu sasa inaleta matatizo *TANESCO* imekuwa mzigo kwa sasabu madeni yanazidi kuongezeka, ndio tatizo hilo. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Heche, Mheshimiwa Hasna taarifa hiyo.

MHE. HASNA S. MWILIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, tuko hapa kuishauri Serikali, hayo mambo ya mikataba na nini mimi sitaki kuijingiza sana huko. Ndiyo maana tunaishauri Serikali ikae chini ione ni jinsi gani ya kuiwezesha *TANESCO*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu, taasisi nyingi ndani ya jimbo langu hazijapata umeme. Kwa mfano, tunayo Shule ya Lugufu Boys na Lugufu Girls lakini tunazo zahanati na vituo vya afya vinashindwa kupata umeme. Mimi niliongea na Meneja wa *TANESCO*, akaniambia nguzo wanazo nadhani mia moja na kitu lakini hawana pesa ya kuwapa mafundi ili waweze kuchukua zile nguzo na vifaa ambavyo wanavyo wawapelekee wananchi umeme kwenye maeneo ambayo hatujapata umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe sana Waziri, Naibu Waziri na Mkurugenzi na pia niungane na wenzangu, huyu Kaimu Mkurugenzi wa *REA*, Ndugu Maganga jamani athhibitishwe kama anaonekane anafaa. Kwa sababu unapokuwa unakaimu, mimi naelewa maana ya kukaimu,

nimefanya kazi Serikalini, ukikaimu unakuwa huna mamlaka, ukikaimu unakuwa huna sauti. Sasa tunabaki kusema mambo mengine akitaka kuyatolea maamuzi anashindwa kwa sababu bado ye ye ni Kaimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nimeona wakati Spika anawatambulisha kila aliyesimamishwa pale ni Kaimu. Sasa mtu anapokuwa Kaimu hapati ile *confidence* ya kufanya kazi yake inavyotakiwa. Kwa hiyo, tuombe Mheshimiwa Waziri umshauri Mheshimiwa Rais ili hawa wanaokaimu kama wamekidhi vigezo waweze kuthibitishwa na hatimaye tuweze kusonga mbele.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa, tumemaliza muda wetu.

MHE. HASNA S. MWILIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na nawapongeza zaidi hawa Mawaziri kwa kweli wanafanya kazi. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yenu, muda wetu kwa mchana huu umefikia mwisho.

Kabla sijasitisha shughuli za Bunge, naomba niwataje kabisa wachangiaji ambao wataanza jioni. Tutaanza na Mheshimiwa Mansoor Shanif, Mheshimiwa Charles Kitwanga, Mheshimiwa Victor Mwambalasa, Mheshimiwa Ussi Kundeza na Mheshimiwa Zuberi Kuchauka.

Baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi jioni.

(Saa 07.00 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 10.00 Jioni)

(Saa 10.00 Jioni Bunge lilirudia)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Tunaendelea na majadiliano yetu. Tunaanza na Mheshimiwa Mansoor Shanif, baadaye Mheshimiwa Ussi Pondeza ajiandae.

MHE. MANSOOR S. HIRAN: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru umenipa nafasi hii ili na mimi nichangie hoja ambayo iko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya njema nisimame mbele ya Bunge lako Tukufu kuwawakilisha wananchi wa Jimbo la Kwimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa bajeti nzuri ambayo ameiwasilisha hapa Bungeni. Mimi nitajielekeza kwenye masuala ya *REA III*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa mpango kabambe wa kupeleka umeme vijiji. Mheshimiwa Waziri, amezindua miradi mingi sana vijiji. Wilaya ya Kwimba tarehe 13 Julai, 2017 alizindua mradi wa umeme vijiji, jana ndiyo kijji cha kwanza kimewasha umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu unasuasua sana, miezi nane kijji kimoja ndiyo kimepata umeme. Tukifuatilia kwa mkandarasi anasema Serikali bado hajasaini mkataba wa kufungua *LC*, mara Hazina hajasaini mkataba. Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Mheshimiwa Waziri wa Fedha, tunawaomba mtusaidie, fedha za umeme za *REA III* ni *ring-fenced* tunaomba zifike kunakotakiwa ili miradi hii ya *REA III* isichelewe.

Mheshimiwa MWenyekiti, pamoja na hayo, wakati wa uzinduzi wa mradi huu tulifanya maboresho, kuna vijiji vingi na taasisi mbalimbali za Serikali na za kidini zilikuwa zimerukwa wakati wa *REA II*. Tulikaa na Mhandisi Msufe,

mkandarasi na wawakilishi wa TANESCO tukaboresha hiyo orodha, Mheshimiwa Waziri naomba mtusaidie hiyo orodha iliyoboreshwa tupatiwe ili tuweze kuiwasilisha kwa wananchi wetu ambao wanasubiri umeme huo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya mwaka huu ambayo inaendelea tuna shilingi bilioni 469, bajeti ya mwaka kesho ambayo tunataka kuitisha hapa tunapitisha shilingi bilioni 375, tunapunguza shilingi bilioni 94 kwenye bajeti ya Nishati. Mimi naomba Serikali isipunguze bajeti ya REA ibaki pale pale au iongezewe zaidi kwa sababu REA ndiyo mkombozi wa wananchi kwa maendeleo. Viwanda vitapatikana kama REA imefika vijijini. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine niende kwenye hotuba ukurasa namba 93 ambapo ameongelea kuhusu *Single Receiving Terminal*, naomba ni-declare Interest mimi ni mdau, naelewa hili suala vizuri. Hotuba hii ni tofauti na uhalisia uliopo. Wiki mbili zilizopita, TPA waliita kikao ambacho wadau wote tulii twa mara ya kwanza, tulikuwa tunasikia fununu kwamba suala hili linakuja lakini killiitwa kikao wiki mbili zilizopita. Kwenye kikao hicho *TIPER* ndiyo walifanya presentation kwamba wao ndiyo wapo tayari kupokea mafuta ya *Single Receiving Terminal*, wakatoa changamoto zilizopo na maandalizi yanayofanyika, lakini kwenye hotuba Mheshimiwa Waziri amesema kwamba hiyo shughuli itafanywa na TPA (*Tanzania Ports Authority*). Sasa ningombaa ufanuzi kwa Mheshimiwa Waziri kwa sababu hiyo ni tofauti na uhalisia uliopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ningependa kusema kwamba katika miaka hii miwili na nusu ya kazi ya Mheshimiwa Waziri nimeona ni Waziri mzuri sana lakini nguvu nyingi ameelekeza kwenye nishati ya umeme, kwenye mafuta amewaachia wasaidizi wamsaidie. Mimi ningeshauri Waziri akee na wadau ambao wanamchangia pesa kwa ajili ya kupeleka kwenye miradi ya REA. Ni muhimu kukaa na wadau, wadau wanaunga mkono hoja hii ya *Single Receiving Terminal* lakini wanassema kuna ukakasi kidogo jinsi mambo yanavyoenda huko kwani hayaendi sawasawa. Kwa hiyo,

naomba na kushauri Waziri akae na wadau, awasikilize, asitume watu, suala hili ni zito sana ni suala la uchumi wa nchi, ni muhimu akae na wadau awasikilize, kuna mambo mengine labda haletewi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningeshauri hata Kamati ya Nishati na Madini ikae na wadau, iwasikilize. Wadau wako tayari kukaa na Kamati ili waeleze changamoto zilizopo na tunawezaje kutoka kwenye hizo changamoto. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo napenda kuliongelea kwenye suala hilo ni kwamba Mheshimiwa Waziri kasema tunaanza biashara hiyo ya *Single Receiving Terminal* kwa sababu tuna ubia na *TIPER* kwa asilimia 50. Mimi nakubaliana kwamba kuna ubia lakini ni vizuri sana kwa sababu kuna gharama ambazo zinahusika kwenye kutoa hiyo huduma, *TIPER* hawatoli huduma bure, kuna gharama kubwa sana ambazo zipo ambazo hajazitaja kwenye hotuba yake, mimi nitaziweka mezani hapa ili Waziri azielewe na awaulize hizo gharama kama zipo ni lazima zishindaniwe, lazima ieleteke wamefikia vipi hiyo gharama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, mafuta yanayoingia ndani ya nchi leo asubuhi Mheshimiwa Waziri kasema kwa mwezi tunapokea karibu takriban milioni 450 ya mafuta. Kwa mwezi ukipokea milioni 450 ya mafuta kwa gharama waliyopanga kwenye kabrasha ya *TIPER* ambayo ninayo hapa wanasema watatoza dola 2.35 kwa siku 10. Kwa hiyo, haya mafuta yote yakipita kwa *TIPER* takriban utakuwa unalipa kwa mwezi bilioni mbili na milioni mia nane na lazima ulipe ili mafuta yapite pale na hiyo ni kwa siku 10. Mafuta hayo yakikaa zaidi ya siku 10, kuna mkataba ambao Serikali hajijahusishwa ambao unaingiza sasa gharama inakuwa shilingi 30 kwa lita moja. Kwa hiyo, ukisema ndani ya milioni 450, kama nusu ya mafuta hayo yamebaki pale kwa siku 11 au 12, utakuwa unalipa karibu bilioni saba zingine kwa mwezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachoomba kwa Mheshimiwa Waziri, huyo mbia wake ni mfanyabiashara,

anafanya biashara ya mafuta, ana-supply mafuta kwenye tender, sasa anapewa nafasi ya kusimamia mafuta katikati na kuingiza ndani ya nchi na kusambaza pia anapewa kazi hiyo yeye na huku chini pia tunashindana naye kwenye biashara. Mheshimiwa Waziri, huyo mtu utashindana naye vipi kwenye biashara? Wengine wote sisi tutashindwa kufanya biashara hiyo kwa sababu huyo mtu mmoja ana-advantage ya kushinda kwenye tenda, anasimamia katikati pale na huku chini pia yumo, unampa *undue advantage*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri ashirikishe hata *Fair Competition Commission* ili waangalie kama utaratibu huu unaendana na sheria zetu. Ningeshauri pia *Attorney General* atusaidie suala hili na aliangalie kwa undani zaidi. Mheshimiwa Waziri ana sifa nzuri sana kwa kazi anazofanya lakini hii inatukumbusha mwaka 2005 wakati nchi illikuwa ina giza, Serikali ikaagiza kwamba tunataka tupate umeme kwa haraka sana, Wizara ya Nishati ikaenda, ikaleta kampuni ya mfukoni inaitwa Richmond, wakaingia mikataba mibovu, imetugharimu mpaka leo, tunarudi huko tulikotoka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkataba huu haueleweki umepita vipi kwa sababu wakati wamefanya *presentation* tukasema tunaomba kujuu makubaliano kati ya Serikali na *TIPER*, hakuna makubaliano. Tukaomba makubaliano kati ya *TPA* na *TIPER*, hakuna makubaliano. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, ningemba hili suala aliangalie kwa ndani sana, nampenda sana na pia Serikali ya Awamu ya Tano haipendi kabisa ihusishwe na mambo ya ufisadi, rushwa na mambo ya hovyo hovyo. Kwa hiyo, ningeshauri Mheshimiwa Waziri, aliangalie hili suala kwa ndani, tusimharibie Rais wetu sifa zake nzuri ambazo anazo za kupambana na ufisadi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine nalopenda kulisema hapa, kwenye hotuba Mheshimiwa Waziri amezungumzia ujenzi wa bomba la kusafirisha mafuta safi, kwenye ukurasa wa 87. Naomba ni-declare interest, mwaka 2014, Wizara ya Nishati na Madini mliletewa andiko, mwekezaji kampuni ya Kitanzania, *Petroleum Logistics*

Tanzania Limited akasema atajenga bomba kutoka Dar es Salaam mpaka Zambia, ghamama iliwekwa pale, akafanya presentation, Wizara ikamuita Katibu Mkuu kutoka Zambia akafika hapa, mwekezaji akafanya presentation mbele ya Katibu Mkuu, Wizara ya Nishati na Maji ya Zambia na Katibu Mkuu Wizara ya Nishati alikuwepo, wataalam walikuwepo na taasisi mbalimbali zilikuwepo. Wamechukua huo mradi, wameugeuza kuwa mradi wa Serikali, sasa wanasema Serikali inaanza mchakato wa kutengeneza mradi. Hiyo kampuni ya Kitanzania, haikuomba mkopo wa Serikali wala haikuomba *guarantee* yoyote ilisema itafanya kwa ghamama zake. Naomba Mheshimiwa Waziri aliangalie hilo pia anasema anaanza mchakato wakati mchakato uko tayari kwenye ofisi zake. (*Makofî*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mansoor.

MHE. MANSOOR S. HIRAN: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Tunaendelea na Mheshimiwa Mussa Sima na baadaye Mheshimiwa Allan Kiula ajiandae.

MHE. MUSSA R. SIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kukushukuru lakini nimshukuru sana Mwenyezi Mungu mwangi wa rehema ambaye ametuwezesha tunaendelea na mjadala wa bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kuwapa pole ndugu zangu wa Ikungi kwa kufiwa na Katibu wao wa Wilaya wa Chama cha Mapinduzi. Mwenyezi Mungu aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii pia kuipongeza Wizara ya Nishati, ama hakika ndugu zetu hawa wa Wizara ya Nishati wanaonesha *vision* na *mission* ya

Tanzania kuwa na umeme wa uhakika, kwa kweli niwapongeze sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejaribu kupitia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri ni dhahiri kabisa na kwa mara ya kwanza naona wameweka fedha za miradi ya maendeleo zaidi ya asilimia 66.7, ni fedha nyingi sana hajjawahi kutoke. Humo ndani wameelekeza vizuri, iko miradi mikubwa ambayo imeelekezwa kupewa fedha nyingi ikiwemo *Stiegler's Gorge* lakini pia na mradi wa *REA*, ni jambo jema sana. Kote huku tunalenga kuwa na umeme wa uhakika. Eneo hili tuna kila sababu ya kumsifu sana na kumtakia kila la kheri Mheshimiwa Waziri na Naibu wake waweweze kufikia malengo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hofu yangu, siku zote lazima tuiweke hofu hili kwamba fedha hili hazifiki kwa wakati. Tunataka tuiombe Serikali tusiwe watu wa kulalamika kila siku fedha hazifiki, mikakati yote iliyowekwa hii haiwezi kutekelezeka kama fedha hazijaenda. Niiombe sana Serikali ihakikishe inawapa fedha ili hii mikakati walioiweka ya kuhakikisha tunapata umeme wa uhakika tuweze kupata huo umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nielezee eneo hili la *Stiegler's Gorge*. Wako watu wametolea mfano kwamba eneo hili wanakata miti ambapo unafananisha sasa ukataji wa eneo lile la miti na kilometa za mraba za Dar es Salaam yaani unafananisha na Jiji la Dar es Salaam. Ndugu zangu, Selous ina kilometa za mraba zaidi ya 50,000, Dar es Salaam ina kilometa za mraba 1,300, maana yake Dar es Salaam pale Selous inaweza ikaingia mara 35 mpaka 40. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nilieleze jambo hili vizuri, Watanzania wanahitaji kuelezwaa vizuri na ukweli. Tukisema zaidi ya Dar es Salaam kwamba tunaangalia ile miti lazima uangalie *value* ya mradi na ile miti inayokatwa, lakini lazima uangalie *multiplying effect* ya ule mradi, tunatarajia huu mradi utusaidie nini. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunajenga reli kwa kiwango cha *standard gauge*, reli hii inatarajiwa kuwa na umeme wa kutosha, utatoka wapi? Malengo haya yaliyowekwa na Wizara ya kuhakikisha kwamba tunapata *megawatt* 2,100 maana yake yatatusaidia sasa hata miradi mingine ambayo inatarajia kuhitaji umeme iweze kutekelezeka, ikiwemo reli. Pia tunahitaji kuwa na viwanda vyaa kutosha vinahitaji umeme, *Stiegler's Gorge* inaweza ikawa ndiyo suluhu ya hiyo miradi ambayo tunatarajia iweze kutekelezeka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wote tunalalamika juu ya kutokuwepo kwa umeme wa uhakika. Pale Singida Mjini tunayo *sub-station* nadhani ina *megawatt* zaidi ya 600 lakini hata pale ilipo kuna mtaa unaitwa Kimpungua, wananchi hawana umeme. Nimuombe Mheshimiwa Waziri, maeneo haya ambayo yako mjini na wako tayari kulipia gharama za umeme, maeneo haya madogo madogo ni vizuri sana Wizara ikawa makini kuhakikisha watu wanapata umeme lakini viko vijiji karibu 13 na mitaa 13 yote haina umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma kitabu cha Mheshimiwa Waziri wameomba fedha kwa ajili ya usambazaji wa umeme mijini, wameomba, hawana fedha. Sasa kama wameomba fedha maana yake sisi tutaendelea kusubiri maombi ya fedha, yanaweza yakakubalia au yakakataliwa ni lazima tuwe na mkakati madhubuti. Hatuhitaji kusubiri fedha zinazokuja sisi tunao umeme wa kutosha ni kuwaongezea tu bajeti ndugu zetu wa TANESCO pale wahakikishe kwamba vijiji vile na mitaa wanaweza kupata ule umeme wala hakutakuwa na tatizo lolote Mheshimiwa Waziri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako maeneo mengine, Singida tumejaaliwa na rasilimali ya umeme wa jua, rasilimali nyingine ya upopo, nashukuru Mheshimiwa Waziri ameeleza vizuri kwenye kitabu chake na ziko fedha wametenga zaidi ya shilingi bilioni 888 kwa ajili ya umeme wa jua, niwaombe sana eneo hili sasa waliangalie na ni vizuri tukaharakisha,

mchakato ufanyike mapema kwani jambo hili halijaanza leo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi, tunao upepo, nashukuru Waziri ametambua. Kwenye kitabu ukurasa wa 32 kama sikosei ametambua kwamba tunao upepo ambapo tunaweza kupata mradi wa umeme wa upepo na ametambua kampuni moja ya *Wind East Africa*, walikuja na kampuni nyingine ya *Power Project*, eneo kubwa sana la Singida ukiacha Kisaki, Mungumaji tunaenda mpaka Unyambo kule Kisasida kote kule kunafaa kwa mradi wa umeme wa upepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niiombe Serikali eneo dogo hapa, kampuni hii tumekuwa nayo zaidi ya miaka 10 sasa lakini hakuna utekelezaji, sijajua kulikuwa na mazingira gani, lakini Waziri ameeleza vizuri kwamba mchakato wa kusaini ile *Power Purchasing Agreement* umefikia hatua ya mwisho, *well and good* lakini muwape *time-frame*, wakimaliza huo mchakato tuwape *time-frame* ni lini wataanza sasa kuhakikisha mradi huu unafanyika. Kama jambo hili linashindikana niiombe Wizara itangaze rasilimali hii hadharani. Wako wawekezaji wengi watatusaidia na watahakikisha tunapata umeme, zaidi ya hii *megawatt* tuliozungumza hapa 100 tunaweza kupata hata *megawatt* 200 na tukaondokana na tatizo la umeme Mkoa wa Singida. Niiombe sana Serikali, tunayo maeneo mengi tunahitaji kuwa na uwekezaji wa viwanda, hatuwezi kuwa na uwekezaji wa viwanda kama hatuna umeme wa kutosha. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejaliwa kuwa na rasilimali kama hii, liwe eneo muhimu sana. Naomba Waziri atakapokuja ku-*wind up* ni vizuri tukawapa *timeframe* hawa wawekezaji tulionao kwa muda mrefu na sasa hivi wananchi wanalamika sana, tufikie mahali tuweke rasilimali hii hadharani kila mtu mwenye uwezo wa kuwekeza kwenye eneo hili aje awekeze. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko eneo lingine, Watanzania hawa tunaowapelekea umeme hasa vijiji

uwezo wao wa ku-afford unit 350 ni mdogo sana. *Unit* moja ina takriban 350, kesho tutakwama kwenye hili. Nataka niiombe Serikali, tunapoweka mkakati wa kuhakisha watu wanapata umeme kwenye vijiji vyote basi tuweke na mkakati wa kupunguza gharama hii, kwa sababu watakuwa watu wengi ambao wanatumia umeme. Tukipunguza gharama hii itatusaidia pia watu waache kutumia mkaa kwa wingi, tutaanza kutumia umeme kwenye shughuli zetu. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Waziri tuweke mkakati wa kupunguza hii gharama. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini watu wanapohitaji kuingiza umeme, tumepongiza gharama za uingizaji umeme. Kwa mjini tumeweka Sh.321,000 bado ni fedha nydingi sana, akiweka nguzo moja tu anaenda Sh.515,000 lakini vijijini tumeweka Sh.177,000, kwa nini tusiwaweke wote sawa kwa sababu wote wanatumia umeme sawa, wote wafanane kwa nini itofautiane? Kama inatofautiana, kwa nini tuweke kipaumbele kwenye REA tukaacha hapa kwenye maeneo ya miji, maeneo ya miji hayana umeme, tumewekeza kwenye maeneo ya vijijini. Niiombe Serikali iliangularie eneo hili itasaidia wananchi wengi kupata umeme na wanaweza kutumia ule umeme kwa gharama nafuu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *vision* hii ya Wizara itatufikisha mahali ambapo lengo ama utekelezaji wa llani yetu ya uwepo wa viwanda vya kutosha na watu kuweza kutumia umeme kwa uhakika itatusaidia sana. Tumepitia bajeti nydingi hapa lakini mkakati kwenye bajeti hii ukiusoma vizuri na watu wakipewa fedha utatufikisha mahali ambapo tunapahitaji. Tuna kila sababu ya kuwaanga mkono watu wa Wizara hii ili waweze kutusaidia sisi kuweza kupata umeme wa uhakika na wa kutosha. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimalizie kwa kuendelea kuishukuru Serikali, mambo mengi tumekuwa tukiyasema hapa, nimuombe Waziri tunaposhauri ni vizuri mkayasema hapahaha msisubiri Rais aseme. Tulishauri kwenye maji hapa kesho Rais akatolea majibu lakini sisi hatukuweza kusema. Sasa niwaombe tuwe tunamaliza humu humu

tusubiri Rais alione hili, Rais wetu anafanya kazi nzuri sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na naiunga mkono bajeti. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mussa Sima. Tunaendelea na Mheshimiwa Allan Kiula baadaye Mheshimiwa Victor Mwambalaswa na Mheshimiwa Jesca Kishoa wajjandae.

MHE. ALLAN J. KIULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami ninashukuru kwa kuweza kupata nafasi ya kuchangia Wizara hii jioni ya leo. Kabla sijaendelea niseme kwamba naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili namshukuru Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wengine wa Wizara hii kwa kazi kubwa wanayofanya na sote tunaiona kazi hiyo. Jambo moja ambalo Waziri inabidi alifahamu ni kwamba kuna hadithi ya uyoga wa porini, ukienda porini ukikuta uyoga haujaguswa hata na ndege ujue huo uyoga ni sumu, kama uyoga umeparuliwa paruliwa ujue basi huo uyoga unaliwa. Sasa mishale anayopata maana yake kwamba anafanya kazi kubwa na watu wanaona kazi hiyo. Wengine tumeshakwenda naye mguu kwa mguu mpaka Majimboni kwetu kwa hiyo tunatambua ufanyaji kazi wake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa ambayo naiona kwenye Wizara hii, yawezekana wewe speed ya Waziri ni kubwa kuliko hao anaofanya nao kazi. Kwa sababu Waziri akitoa maagizo *TANESCO* wenye we wanapumzika wanasubiri tena Waziri aende, sasa tunataka mfumo ufanye kazi. Kwa hiyo, ni jambo la muhimu sana Wizara isimamie mfumo kufanya kazi. Ndiyo maana watu wanasema *TANESCO* inabidi iangaliwe upya, pia *TANESCO* inatakiwe liwe Shirika *vibrant* na liwe *customer focused*. *TANESCO* ikifanya kazi kwa mfumo huo tutapiga hatua kubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa iliyopo katika Jimbo la Mkalama na Mkoa wa Singida kwa ujumla ni kwamba *REA* //ha *REA* ///likuwa haijaanza. Kwenye ukurasa wa 55 tumeambiwa kwamba mkandarasi anaanza, sasa tunaomba mkandarasi afike na afanye kazi kwa ukamilifu. Jambo hili ni muhimu sana kwa sababu kuna maeneo umeme umewaka na maeneo mengine umeme haujawaka na wananchi wanasubiri umeme. Kauli mbiu yetu kwenye llani ya Chama cha Mapinduzi tunasema umeme utawaka vijiji vyote, hata mimi nikienda nawaambia umeme utawaka vijiji vyote. Sasa kama ndiyo kauli mbiu yetu basi umeme unatakiwa uwake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kwamba nguzo zinapelekwa kidogo sana. Pale Ibaga umeme umewaka lakini maeneo mengi hayajapata umeme, kwa hiyo pale manung'uniko mengine yamezaliwa ingawaje kazi kubwa ya kuwasha umeme imefanyika. Ukienda Iyambi, Gumanga, Nkalakala, Kinyangiri, Iguguno umeme umewaka lakini vitongoji vyake au maeneo ya karibu kabisa hayana umeme. *Scope* hiyo inabidi iangaliwe ili watu wengi waweze kupata umeme lakini pia umeme ni biashara *TANESCO* waweze kufanya biashara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua kwamba Serikali inatoa pesa nyingi kujenga vituo vya afya. Wizara ya Afya na TAMISEMI wametoa shilingi milioni 400 kujenga vituo vya afya lakini havina umeme. Nafikiri sasa ni wakati muafaka Waziri atakapo-*wind up* atoe tu agizo kwamba vituo vyote vya afya vilivyojengwa umeme upelekwe, kwa sababu upasuaji na vipimo vitafanyakaje? Jambo hilo naona limesahaulika halafu tunaanza kupeleka maombi *TANESCO* inakuwa ni changamoto. Kama majengo yanakabidhiwa kwamba yamekamilika basi na umeme unatakiwa uwe umefika. Jambo hili pia tutazungumza na Waziri wa Maji ili na maji pia yaweze kufika kwenye vituo hivyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaipongeza Serikali kwa juhudzi zake za kuja na *energy mix*, kwa kuleta vyanzo vya umeme kwenye *Grid* ya Taifa kwa mifumo mbalimbali.

Umeme ulipokuwa unakatika tulikuwa tunalalamika kila siku sasa umekatika na siku hizi tuna mitandao wanasema sasa umeme umekatika, lakini katika kutekeleza azma hiyo huu mradi wa *Stiggler's Gorge* nafikiri umeleta matatizo kidogo kwa baadhi ya watu. Umeleta matatizo kwa sababu tu ya kuwa na fikra mgando kwa sababu ni lazima utumie rasilimali uliyonayo ili uweze kusonga mbele. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya rasilimali tuliyonayo ni hilo bonde na umeme wake unahitajika na kama *study zimeshafanyika* tangu mwaka 1950 na 1960 hakuna jambo jipya ambalo tunafanya sasa hivi. Kwa hiyo, jambo jema ni kushauri mradi huo utekelezwe vipi na hapa tunawashauri wataalam wetu wa mazingira waweze kusimamia kikamilifu jambo hili na mradi utekelezwe lakini tuupokee mradi badala ya kuanza kuuzuia kwamba usiweze kutekelezeka. *After all Serikali imeshaamua kutekeleza nani anatakayezuia tena, kwa hiyo, mradi unaenda kutekelezwa.* (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni ujenzi wa bomba la mafuta kutoka Uganda mpaka Tanga. Bomba hilo litapita katika Mkoa wa Singida na katika Wilaya ya Mkalama ambako mimi ndiye Mbunge wa Jimbo la Iramba Mashariki. Tunaiomba Serikali iangalie na isimamie kwa ukamilifu suala la fidia, pia suala la watu watakaofanya kazi katika bomba hilo katika Wilaya hizo au Mikoa husika waweze kunufaika. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema hivi kwa sababu mara nyingi maandiko huwa yanakuwa mazuri sana, tunapokutana kwenye *presentation*, tunapotaka kuanza mradi mambo yanayozungumzwa yanakuwa *roses*, yote yanakuwa ni maua mazuri lakini mradi unapoanza ndipo changamoto zinakuja. Kwa hiyo, tujifunze kutokana na makosa, hatutarajii kwamba mradi huu utaleta malumbano na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunategemea kutakuwa na *quarters* za wafanyakazi, kwa maana kwamba Wilaya hii au Mkoa huu utaleta wafanyakazi kadhaa na wafanyakazi

hao waandaliwe, ikiwepo hata Mama Ntilie maana yake watapeleka vyakula katika maeneo hayo. Kwa hiyo, jambo hilo tukiliratibu vizuri naflkiri tutapiga hatua kubwa kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ni hili bomba la gesi wanasema linatumika kwa asilimia sita tu. Naona watu wengi tunasimama tunalaumu tu, lakini hayo ndiyo maendeleo na bomba lingekuwa limetumika asilimia 100 ingekuwa *lime-fail*. Sasa hivi tumeona gesi ya majumbani imeanza kutumika na viwanda vinatumia gesi. Kwa hiyo, tunatumai kwamba hili bomba sasa litatumika kikamilifu kulingana na *capacity level*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ni la msingi zaidi ni kwamba Mawaziri tunawahimiza kutembelea maeneo ya vijijini. Mkitembelea maeneo ya vijijini...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Kiula, muda wako umeisha.

MHE. ALLAN J. KIULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Mwambalaswa baadaye Mheshimiwa Jesca Kishoa ajiandae.

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia hoja iliyio mbele yetu hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote. Wizara yenu ni nyeti sana na mzigo mnimapiga kweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi Mheshimiwa Waziri amenishtua, Jumamosi alikuwa Mkoa wa Songwe kwenye Wilaya ya mdogo wangu Mheshimiwa Mulugo na kwa Dada yangu lleje ya Udinde kilometra 300 kutoka Mbeya. Jumatatu namsikia yuko Mtwara anafungua umeme, kwa kweli mnapiga kazi hongereni sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Wizarani kwako kuna watu zaidi ya watano (5) wanakaimu, siyo vizuri. Maana anapokaimu anafanya kazi kukufurahisha wewe ili usije ukamnyima cheo lakini ukim-*confirm* anafanya kazi kwa mujibu wa sheria, kwa hiyo, naomba wawe-*confirmed* haraka. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *REA* / Wilayani kwangu Chunya ilipeleka umeme kwenye viji vingi sana lakini iliruka shule za sekondari zaidi ya saba. Mimi kama Mbunge na kama mzazi nilikopa hela benki nikaenda kulipa *TANESCO* niweze kupeleka umeme kwenye sekondari hizo. Nililipa pale *TANESCO* Chunya, Waziri anaweza ku-*cross check* na Meneja wa Chunya, nililipa pesa ndefu siwezi kuisema hapa kwa sababu sitaki kujisifu, kwa sababu vitabu vya dini vinasema mkono huu ukitoa sadaka huu usijue. Tatizo ni kwamba *REA* //imeruka Kituo cha Afya cha Kata ya Mtanila, cha zamani sana ambacho Mwalimu Nyerere alienda kuweka saini kwenye kitabu cha wageni mwaka 1966. Mheshimiwa Waziri sina uwezo tena wa kwenda kukopa benki kwa sababu bado nalipa ile ambayo nilikopa ya kupeleka umeme katika shule za sekondari. Naomba sana hii *REA* /// inapoenda basi Kituo cha Afya cha Mtanila, Kata ya Mtanila ambacho kinachohudumia Tarafa nzima ya Kipambawe kipelekewe umeme. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru sana Wizara kwa kupelekea hiyo *REA* /// ya sasa hivi, Jimboni kwangu iko kwenye Kata ya Ifumbo, Viji vya Ifumbo, Soweto, Mawelo na viji vingine. Kuna kijiji kinaitwa Itumbi, Wizara ya Nishati inataka kujenga kituo cha kuwahudumia wachimbaji wadogo (*Center of Excellence*) nikamuomba Mheshimiwa Waziri kwamba hii *REA* /// Itumbi wapeleke umeme.

Mheshimiwa Waziri alinikubalia namshukuru sana Mungu ambariki, lakini naona bado Wahandisi wa *REA* hawajapewa hiyo taarifa kutoka kwake. Naomba anapowapelekea taarifa ya ombi langu la Kituo cha Afya cha Mtanila basi awapelekee na hii ya Kijiji cha Itumbi ambako itajengwa *Centre of Excellence*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee kidogo umeme wa maporomoko ya Mto Rufiji, ni wazo zuri sana litaikomboa nchi yetu naliunga mkono sana. Mto Ruaha unakauka, haukauki kwa sababu ya tabianchi hapana unakauka kwa sababu ya matumizi ya maji (*management*), unakauka kwa sababu wakulima wanachukua maji hawayarudishi, unakuka kwa sababu ya wafugaji, unahitaji tu utawala. Ndiyo maana Mheshimiwa Makamu wa Rais alienda Iringa akaliona tatizo hilo akaunda Tume ya kulishughulikia. Mheshimiwa Waziri wa Maliasili alienda Kilombero aliona Mto Kilombero nao unaenda kwenye Mto Rufiji unakauka naye akaunda Tume. Rai yangu ni hii kwa Mheshimiwa Waziri, naomba ye ye ambaye ndiye mwenye dhamana ya Nishati awe ndiyo kinara, achukue Wizara yake ya Nishati, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Maliasili na Wizara zote zinazohusika muweze ku-*manage* mito hii miwili (2); Mto Ruaha na Mto Kilombero ili tupate maji mengi ya kwenda kwenye umeme wetu wa *Stiggler's Gorge*. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeishauri Wizara inasema, Kamati inaendelea kusisitiza Serikali kuwekeza zaidi katika nishati jadilifu (*renewable energy*). Mheshimiwa Waziri wakati anajibu maswali hapa alisema kwamba Tanzania ina-potential ya *megawatt* 5,000 katika *geothermal*, naomba nguvu ambayo Mheshimiwa Waziri ametumia kuunadi mradi wa *Stiggler's Gorge* nguvu hiyo anadi hii *geothermal*, *megawatt* 5,000 ni nydingi mno. Tena hahitaji fedha nydingi Mheshimiwa Waziri, anahitaji tu anunue *rig* moja au mbili azileta hapa nchini na kuikabidhi hiyo Kampuni aliyounda ya *Geothermal Development Company*, yenye we inatoboa mahali ambapo kuna potential/inaleta juu kwenye *well-head* mnatangaza tenda waje wakezaji kuweka mitambo hapo. Kwa hiyo, naomba sana hii *megawatt* 5,000 *potential* ya

Tanzania ni kubwa sana, naomba Mheshimiwa Waziri aishughulikie hii kama alivyoshughulikia *Stiggler's Gorge*. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba niongelee kidogo miradi miwili ya Kiwira *megawatt* 200 na Mchuchuma *megawatt* 600 ya makaa wa mawe. Mheshimiwa Waziri ulipoingia Wizarani ulisikia kuna mradi wa Kiwira *megawatt* 200 Mchuchuma *megawatt* 600. Ulipokuwa Mwanasheria Mkuu wa Wizara, Kiwira *megawatt* 200, Mchuchuma *megawatt* 600. Umekuwa Naibu Waziri Kiwira *megawatt* 200, Mchuchuma *megawatt* 600, sasa umekuwa Waziri bado Kiwira *megawatt* 200, Mchuchuma *megawatt* 600, Mheshimiwa Waziri *do something*, weka alama. Hii historia ya kwamba Kiwira, Mchuchuma iishe, fanya kitu, weka alama ili vizazi vijavyo viseme kwamba Mheshimiwa Dkt. Kalemani allikuwa Waziri wa Nishati alfanya kazi Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, naunga mkono hoja. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mwambalaswa. Tunaendelea na Mheshimiwa Jesca Kishoa, baadaye Mheshimiwa Lathifah Hassan Chande na Mheshimiwa Mwitwa Waitara wajiandae kwa dakika tano, tano.

MHE. JESCA D. KISHOA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwanza kabisa, nianze kwa kusema yapo mambo katika Taifa letu ambayo kiukweli yanatia kichefuchefu sana. Kama Taifa na Bunge endapo mambo haya hayatachukuliwa hatua yoyote sisi Wabunge humu ndani tunakosa sababu ya kuendelea kuwa humu ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nzungumzie picha halisi ya ujisadi mkubwa unaofanyika kwenye mradi wa Songas. Kwenye mradi wa Songas kuna ujisadi mkubwa sana. Ukiangalia *investment* ya mradi wa Songas kwenye upande wa *capital structure*, Songas wali-invest karibu *Euro* milioni

392. Katika *Euro* 392, Serikali ilitoa *Euro* milioni 285 ambayo ni sawasawa na asilimia 73 na Songas wenyewe walitoa karibia asilimia 27 peke yake, shikilia hapo kwanza. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye *shareholding structure* umiliki kwenye mradi wa Songas, Serikali inamiliki *only 46 percent* na Songas inamiliki *54 percent* ya mradi mzima. Swali kwa Serikali ambalo ningependa Mheshimiwa Waziri anapokuja kesho ku-*wind up* hapa aseme. Kama Serikali kwenye *capital structure* im-e-invest kwa asilimia 73 kwa nini kwenye *shareholding structure* inamiliki asilimia 46 peke yake? Serikali kwenye *shareholding structure* inakuwa *minority* wakati kwenye *investment* imekuwa *majority* kwa ku-*invest 73 percent*. Swali la kwanza hilo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kila mwezi *TANESCO* inalipa Dola milioni tano kwenye mradi wa Songas kama *capacity charges*. *Capacity charges* ni kitu gani? *Capacity charges* ni fidia anayopewa mwekezaji kufidia gharama alizowekeza na lengo kubwa ni kutaka baada ya mkataba kuisha ile mali inakuwa chini ya Serikali. Sasa Serikali kuitia *TANESCO* inalipa Songas Dola milioni tano kila mwezi kila mwezi, katika Dola milioni tano kila mwezi wanaacha kutoa Dola milioni 3.6 kwa ajili ya Serikali kama Serikali ambayo imetoa *73 percent* kwenye uwekezekaji. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukipiga mahesabu ya toka mradi huu ulipoanzishwa mwaka 2004 mpaka sasa ni *14 years*, Dola milioni 3.6 kwa miaka 14 tumepeoteza zaidi ya trillioni 1.3. Mkataba huu wa Songas ni wa miaka 20, tafsiri yake ni kwamba huu mkataba unakwenda mpaka mwaka 2024, kama mtapuuza tunakwenda kupoteza zaidi ya trillioni mbili kwenye mradi mmoja peke yake wa Songas. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo ambayo Serikali kuna wakati lazima msikilize na mtii. Mamlaka kubwa kama Bunge inaposhauri ni lazima msikilize, mamlaka kubwa kama *CAG* inaposhauri lazima msikilize. Suala hili la ufisadi kwenye *Songas* limezungumzwa kwenye Kamati ya Kudumu

ya Bunge mwaka 2005, ninayo hapa na mwaka 2006 chini ya Mwenyekiti wake, kipindi hicho alikuwa Mheshimiwa William Shelukindo, katika ukurasa wa 8, anaeleza namna ambavyo mkataba huu una ubadhirifu mkubwa na Serikali inaibiwa pesa nyingi sana, lakini Serikali ikauchuna. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *CAG* akaja mwaka 2009 ninayo hapa taarifa, akaeleza vizuri kuitia ukurasa wa 135 namna ambavyo Serikali inapoteza pesa na mkataba ulivyouwa umekaa kijiji-jiji. *CAG* ameeleza vizuri sana, kwa sababu ya muda nashindwa kusoma, lakini Waheshimiwa Wabunge wakipata nafasi wapitie hii ripoti ya *CAG* ya mwaka 2009, ameeleza vizuri sana. Ufisadi huu Ndugu Ludovick Utouh ameupambanua vizuri sana na huyu ni *CAG* mwingine tofauti na wa sasa hivi lakini mpaka hapo Serikali bado ikaendelea kuuchuna. (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, akaja *CAG* mwingine Profesa Mussa Assad mwaka 2018 na ninyi mnajua ni juzi tu hapa. Ukiangalia ukurasa wa 131 ameeleza vizuri namna gani na amechambua kwa mahesabu, tunapoteza fedha kiasi gani kwenye mkataba wa kijizi ambao tumeingia mwaka 2004, lakini mpaka sasa Serikali hii bado mnauchuna. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naongea hapa, hasira za Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli kwenye mkataba wa *IPTL* nategemea kuziona kwenye mkataba wa *Songas* kwa sababu hawa ni Kulwa na Doto. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Serikali yoyote duniani, hakuna Serikali inayoweza kuingia mkataba wa kijinga namna hii zaidi ya Serikali ya Mfalme Juha. Narudia, hakuna... (Makofii) [Maneno haya siyo sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jesca naomba unyamaze. Mheshimiwa Jenista.

KUHUSU UTARATIBU

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu. Mdogo wangu Mheshimiwa Jesca anajenga hoja, lakini naomba kwa mujibu wa Kanuni ambazo zinatuongoza, Kanuni ya 64(1)(g), hizi lugha anazozitumia nadhani kwa kweli ni lugha za kuudhi siyo lugha nzuri. Anaweza akatumia tu lugha ambazo ujumbe unaweza ukafika vizuri lakini maneno na matamshi hayo anayoyatumia katika mchango wake ningeomba ayaondoe lakini aendelee kuchangia hoja zake ambazo zina msingi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jesca naomba urudi kwenye hoja na hayo maneno ya mwisho yote uyafute.

MHE. JESCA D. KISHOA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashindwa kuelewa ye ye Mfalme Juha ametafsiri ni nani? Kwa sababu nimesema Serikali yoyote duniani ambayo inaweza ikaingia mkataba ambao ime-*invest* kwa asilimia 73 halafu ikawa haipokei chochote kwenye *capacity charge* ni Serikali ambayo katika viwango vyovypote, *any standard* ni Serikali ya Mfalme Juha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jesca ndiyo umeifananisha na Serikali yetu, kwa hiyo, ondoa hiyo lugha. (*Kicheko*)

MHE. JESCA D. KISHOA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeitoa, lakini ujumbe umefika. Naomba niendelee na dakika zangu nilindie. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naliomba Bunge lako Tukufu liunde Kamati. Kama hili jambo limekuwa likipigwa danadana toka mwaka 2004 mpaka sasa na tumeshapoteza *trillions of money*, naomba Kamati iundwe iweze kuchunguza jambo hili. Tetesi zilizopo ni kwamba suala hili limefunkwa na kigogo mkubwa ambaye hagusiki kwa namna yoyote ile na ndiyo maana Serikali inakuwa inasuasua katika kuchukua hatua. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kauli ya Serikali itakuwa hajanyooka vizuri, naahidi kuleta Hoja Binafsi humu ndani, mbivu na mbichi zijulikane. Haiwezekani tukaendelea kuibwa namna hii. Naomba nitangaze rasmi, mwenye masikio asikie, mradi wa *Songas* ni mali ya Serikali, *Songas* ni mali ya wananchi na *Songas* ni mali ya Taifa. Naongea kwa ujasiri huu kwa sababu naamini kwamba Serikali ili-*invest* pesa nyingi sana kwenye mradi huu lakini haipokei chochote kutokana na mradi huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa tabia hizo hizo za kuendelea kupuuza hivyo hivyo, kuna mambo ambayo niliyazungumza hapa mwaka 2016/2017 lakini mpaka leo Serikali hajachukua hatua yoyote. Hizi sheria tumezitunga wenyewe, tumezipitisha wenyewe, pale ambapo tunaona sheria zinavunjwa ni vema hatua ikachukuliwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwenye *transfer of shares* ambayo hata kwenye Kamati Mheshimiwa Waziri nilihoji lakini majibu hamkunipa, nikahoji *FTC* majibu hawakunipa, nikamfuata *Mkurugenzi* wa *TPDC* personally majibu hakunipa, alikuwa anababaika tu. Kulikuwa kuna *transfer of shares* kutoka vitalu vya gesi kutoka Kampuni ya *BG* kwenda Kampuni ya *Shell*. Utaratibu uliopo ni kwamba, kama kuna *transfer of shares* yoyote, ukiangalia *Financial Act* ya mwaka 2012, kipengele cha 29 kinaeleza kwamba...

*(Hapa kengele ililia kuashiria
kwisha kwa muda za mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jesca muda umeisha. Mheshimiwa Lathifah Chande.

MHE. LATHIFAH H. CHANDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi hii ya kuweza kuchangia katika Wizara hii ya Nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri wote tunatambua kwamba kwa muda mrefu sana nchi yetu ilisemekana kukosa chanzo cha uhakika cha kuzalisha umeme baada ya

mabwawa ya Kidatu na Mtera kupungukiwa na maji mara kwa mara, hali iliyosababisha kukosa umeme wa kutosha nchini. Kutohana na hali hii, Serikali iliyokuwa madarakani kwa kipindi hicho iliwekeza nguvu nyingi sana kwenye mradi wa gesi ambaao ndiyo tulitegemea uweze kutuzalishia umeme. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ya Nishati ilituhakikishia kwamba mradi huo ungeweza kutupatia umeme wa kutosha nchi nzima na hata tungeweza kuuza umeme kwenye nchi za jirani. Mradi huu wa gesi uligharimu takribani dola bilioni 1.225, katika dola hizo dola milioni 875.7 zilitumika katika ujenzi wa bomba la gesi ambapo takribani dola milioni 300 zilitumika katika ujenzi wa vinu kwa ajili ya kuchakata gesi. Leo hii Serikali inakuja na mradi mpya wa *Stiegler's Gorge*. Mbali na kwamba mradi huu una madhara mengi yakiwemo yanayoweza kujitokeza kwenye mazingira yetu, lakini Serikali imendelea kupigia debe huu mradi uweze kutekelezwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wa CCM siyo kwamba sisi tuna akili mgando, Wabunge hatukatai maendeleo, miradi ya maendeleo tunaikubali, lakini ikumbukwe kwamba muda mfupi uliopita Serikali iligharamia mabilioni ya fedha ambazo ni fedha za walipa kodi wa Tanzania. Leo hii huu mradi unaenda kutelekezwa tunaingia kwenye mradi mwingine, tunaelekea wapi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia katika mwaka wa fedha 2018/2019, pesa ambayo inaombwa kwa ajili ya Wizara ya Nishati ni Sh.1,665,141,000,000. Katika pesa hizi ambazo zinazelekezwa katika huo mradi ni shilingi bilioni 700 ambayo ni sawa na asilimia 42 ya fedha za miradi ya maendeleo katika Wizara hiyo ya Nishati. Vilevile pesa nyingine inayoenda ambayo ni Sh.112,083,000,000 zinzelekezwa katika mrai wa *REA*, ni asilimia 6 tu ndiyo iliyotengwa kwa ajili ya mradi huu wa gesi ambaao tayari ulishagharimu pesa nyingi za nchi hii, hii maana yake nini? Mnataka kutuaminisha kwamba Serikali ina fedha nyingi au ni *misuse ya zile resources chache tulizonazo?* (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Stiegler's Gorge* itaenda kugharimu fedha hizi zote, wapi tunapoelekea? Tunawaambia nini wananchi wa Lingoko, Mkoa wa Lindi, wananchi wa Songosongo Kilwa, wananchi wa Mtwara Vijiji ambao wameacha makazi yao, wameacha mashamba yao kwa ajili ya kupisha mradi huo wa gesi ambao sasa hivi umeenda kupewa asilimia 6 tu? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni suala ambalo kusema ukweli naishauri Serikali kuliko kuelekeza hii pesa katika mradi mpya huu wa *Stiegler's Gorge* bora hiyo pesa ielekezwe katika mradi ambao tayari umeshaligharimu Taifa mabilioni ya fedha, haiwezekani kila siku tukawa tunaanzisha miradi mipyä ambayo haitekelezeki. Mpaka leo hii fedha zilizotumika hatujaona *returns* zozote, leo hii tunaingia kwenye mradi mwingine? Waziri wa Nishati tunaomba mliangalie tena hili suala. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo napenda kuliongelea ni juu ya usambazaji wa gesi..

*(Hapa kengele ililia kuashiria
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Lathifah muda wako umemalizika. (*Makofii*)

Tunaendelea na Mheshimiwa Waitara, baadaye Mheshimiwa Wilfred Lwakatare ajiandae, dakika tano, tano.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipatia nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wote wangetamani kupata nishati ya umeme popote walipo, wawe wa mjini au vijiji. Kwa hiyo, ushauri wangu kwanza ni kwamba, Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Waziri wa Fedha miradi ya umeme popote ilipo, iwe ya *TANESCO* au *REA*, fedha itoke ikamilike watu watoke gizani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna faida nyingi sana, kwanza kuna usumbufu mkubwa sana mtaani. Watu wa Dar es Salaam na maeneo mengine wanazuiliwa wasitumie mkaa na wanakamatwa sana, wanapigwa, wanateswa na watu wa Maliasili, lakini gesi ni ghali sana, umeme ni ghali na haupatikani. Kwa hiyo, mkitaka ku-save maliasili yetu kwa maana ya misitu lazima umeme upatikane kwa bei ya chini na gesi kwa bei nafuu, ili wananchi wa-opt waone kwamba, kununua gunia Sh.70,000 ni gharama zaidi kuliko kulipia umeme, kwa hiyo, misitu itabaki salama na hali yetu ya maisha itakuwa nzuri zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, Dar es Salaam hasa Ukonga, kuna mitaa haina umeme kabisa. Sasa watu wakiambiwa waende mjini wanafikiri maana yake umeme upo, unafahamu katika mitaa tisa ya Kata ya Msongora ni mitaa miwili ambayo ina umeme, mitaa mingine haina umeme na hata maeneo ya shule. Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri alifika mpaka usiku akaona hakuna umeme pale Ukonga Msongora, Chanika, Kidugalo, Vikongoro, Zavala, mitaa yote sita kati ya mitaa nane, hakuna umeme Buyuni, Kivule, Mvulege, Banguro, tuna mitaa mingi ambayo haina umeme. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu *TANESCO* na hapa ndiyo nasema inatakiwa itengenezewe utaratibu mwingine, wananchi wana fedha mkononi wanalipia umeme zaidi ya miezi sita unaambishiwa nguzo na mita hazipo, hili ni shirika la kibashara, *TANESCO* wameshindwa kufanya biashara. Watu wana pesa zao, wanahitaji umeme, wanalipia, *TANESCO* haipeleki umeme. Ndiyo maana watu wanasema *TANESCO* hii kunatakiwa kuwe na chombo kingine washindane kama ilivyo kwenye mambo ya simu. Kama tungkuwa na shirika lingine ambalo *TANESCO* wakiweka bei Sh.320,000 mwingine aweke Sh.270,000, mwingine Sh.250,000, labda hao wangeamka kutoka usingizini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri alipokee hili. Kwenye taarifa mbalimbali inaonesha kwamba *TANESCO* inajidesha kwa ma-trilioni ya fedha kwa maana

ya hasara. Kwa hiyo, tungependa tupate taarifa halisi kwa nini *TANESCO*, Shirika la Umma kodi yetu, linajiedesha kihasara na nani anasababisha? Tuone tatizo ni nini? Watu wanahitaji umeme, kila mahali ukisoma taarifa za *TANESCO* kuna hasara wanaingia. Tungependa tujue kama Taifa na kama Bunge kwa nini kuna hasara *TANESCO*? Ni muhimu sana hili jambo likafanyiwa kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu gharama ya umeme. Kuna hoja hapa maeneo ya mjini wanalipia Sh.321,000 hata kama huhitaji nguzo, vijijini Sh.170,000. Watu wa mjini siyo kwamba wana uwezo mkubwa, ambacho kingefanyika kuna watu mjini ni maskini kweli, ana kijumba chake anahitaji umeme hapati kwa sababu ya gharama kubwa, kwa hiyo, ninyi mngeangalia watu ambao hawana uwezo, Wenyeeviti wa Mitaa, Wabunge, Madiwani wanajua mtu ambaye hana uwezo apewe bei nafuu, wale wenye uwezo wapewe bei ambayo inawezekana, lakini mjisema mjini na vijijini mtaumiza watu wengine. Mjini wengine wanakaa kwa sababu tu ya majina lakini hawana maisha mazuri, ni maskini, hawasomi na ndiyo maana *TASAF* iko mjini na vijijini na Ukonga kwangu Kivule ipo. Hivyo, hili jambo Mheshimiwa Waziri mliangalie vizuri sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengine ni ya umma. Kuna shule hazina umeme, wana visima vyatya Maji, walimu wanahitaji *photocopy* wachapishe mitihani, hata kufeli mitihani kwa wanafunzi wetu ni mazingira. Kwa hiyo, hili suala la umeme ningekuwa mimi, kama ilivyo Idara ya Maji, Serikali ingekuja na mpango mkakati, wametuambia vijiji vyote watapata umeme, Wabunge wanatarajia, wananchi wanasubiri lakini umeme haupatikani, hili jambo lingeisha. Huwezi kwenda kwenye viwanda kama hata umeme majumbani hauna, haiwezekani. Hauwezi kwenda kwenye viwanda vikubwa umeme wa majumbani hauna, lazima mpango uwekwe mahsusumumeme upatikane mijini na vijijini, anayehitaji umeme awekewe ambaye hahitaji abaki kwenye giza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo mngeyafanya na Serikali ya Chama cha Mapinduzi ndio mngepata sifa. Kuna watu wanashauri hapa mahali ambapo kuna hasara watu washughulikiwe. Kuna mafisadi wengi, kuna mikataba mingi *IPTL* iko miaka nenda miaka rudi, ishughulikiwe, haya ndio maeneo Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli amulike atu wenye mikataba mikubwa. Watu wanaacha kutumia umeme wa bei nafuu wanatumia jenereta katika ofisi zao matokeo yake tunashindwa kujiedesha tunapata hasara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Fedha ni muhimu, hayumo humu Bungeni lakini taarifa anazo. Hii miradi ya *REA*, miradi ya umeme, Mheshimiwa Mpango kama kuna mahali umekwamisha bajeti yako inakuja hapa watu wanakusubiri. Kwa hiyo, tunaomba fedha itoke, kama fedha haipo mtuamble fedha haipo tupange mipango ya kupata fedha, umeme upatikane, tunataka umeme mjini na vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa. Tunaendelea na Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, baadaye Mheshimiwa Zuberi Kuchauka na Mheshimiwa Mussa Mbarouk wajiandae wote kwa dakika tano, tano.

MHE. WILFRED M. RWAKATARE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe ushauri kwa Mheshimiwa Waziri, wataalam na Serikali nzima ya Chama cha Mapinduzi kwamba wanapopanga miradi ya kutekelezwa ni vema wakaanza kuchukua dira tofauti na kuangalia dira ya uchaguzi. Miradi mingi inapangwa kwa *ku-focus uchaguzi 2020, 2019* kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa, matokeo yake wanakuwa *over ambitious*, wanapanga miradi ambayo kiukweli haiwezi kutekelezeka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Nishati na Madini nimezunguka katika miradi mbalimbali. Ukimsikiliza Mheshimiwa Waziri humu ndani, lugha anazoongea na wakati akijibu maswali wanazungumzia lugha ya kwamba kila kijiji lazima kiwekewe umeme kwa sera ya *REA* lakini kwa watu tuliotembea, tuliokwenda kwenye maeneo kukagua miradi unakuta kwenye kijiji ni kitongoji kimoja ndiyo kina umeme na kitongoji chenyewe unakuta ni watu watatu, ni kaya nne au tano. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningemuomba Mheshimiwa Waziri, ili kutowaweka Wabunge katika sakata baya sana ifikapo wakati wa uchaguzi, wataulizwa maswali huo umeme uko wapi kwa kila kaya, badala yake ningemshauri hii lugha ya kila kijiji ibadilike na kuwa kwamba mahali ambako kutapitishwa umeme au kwenye *centrey* maeneo fulani, ili wananchi tuanze kuchukua sera mpya, wananchi waanze kuwekewa mpango wa kuvuta wao wenyewe umeme kutoka sehemu mnazoweka umeme. Hii lugha ya kila kijiji haipo, haitekelezeki, kutokana na kutolewa mafungu machache hiki kitu hakitekelezeki, ni uwongo uliokubuhu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni suala la ulipaji wa wakandarasi. Naipongeza taarifa ya Kamati ya Bunge imezungumza ukweli kwamba, wakandarasi kwa mfano wa *Phase III*, tangu mwezi Oktoba mpaka leo watu hawajalipwa pesa. Matokeo yake hawa watu wamesaini mikataba ambayo kimsingi baada ya miaka miwili wanapaswa wawe wamemaliza mikataba hii. Tutaomba Mheshimiwa Waziri atueleze ukweli kutokana na ucheleweshwaji wa hawa wakandarasi Serikali inaingia hasara kiasi gani ili tujue upande wa pili wa shilingi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kuna mdudu huyu ambaye ameingia, mimi namuona kama mdudu. Hili suala linaloitwa uhakiki, malipo mengi ndani ya Serikali yanachelewa kutokana na kuambiwa kuna suala la uhakiki. Hili suala la uhakiki linaanza *REA* wanahakiki kivyao, inakuja

Wizara inahakiki na Hazina wanahakiki, hivi Serikali gani ambayo hamuaminiani? Kwa nini hamuaminiani? Kwa nini kusiwe na *centre* moja, kama ni uhakiki ufanyakie katika *centre* moja badala ya *centre* tatu, matokeo yake miradi inachelewa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni *compensation* kwa wananchi. Kwa mfano, katika mradi wa KV 400 wa Singida - Arusha mpaka Namanga, wananchi wamezuiwa kuendeleza maeneo yao kwa sababu pale kutapitishwa mradi, tunajua sheria inazungumzia miezi sita, hawa wananchi sasa hivi ni miaka miwili. Mheshimiwa Waziri tutaomba uwaelezee Wabunge na wananchi wasikie hatima yao ya kulipwa *compensation* ni nini? Kama miaka imepita, miezi sita imepita, je, watalipwa *interest* kwa kucheleweshwa au vinginevyo izungumzwe wazi hapa, wananchi waruhusiwe kuendeleza maeneo yao kwa sababu Serikali imeshindwa kufanya *compensation* na hawajui hatima yao. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho ni umeme katika vijiji mji. Nashukuru huu mradi umeanza uko Kigamboni na unategemewa kutekelezwa. Naomba kujua katika Vijiji vya Ijuganyondo, Buhembe, Kahororo, Kibeta nini hatima yeke katika suala hili. Mnajua sisi wananchi wa Mjini (Bukoba Town) umeme ni *deal*, hatuulizi stakabadhi ghalani, hatuulizi pembejeo sisi umeme ndiyo mahala pake. (*Makof!*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Lwakatare.

MHE. WILFRED M. LWAKATARE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makof!*)

MWENYEKITI: Tunaendelea na Mheshimiwa na Zuberi Kuchauka, Mheshimiwa Mussa Mbarouk na Mheshimiwa Bobali wajiandae kwa dakika tano, tano.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi nichangie jioni hii ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitoe shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri anayehudumu kwenye Wizara hii, kwa kuiweka Mikoa ya Lindi na Mtwara kwenye Gridi ya Taifa. Tunashukuru sana kwa jambo hili kwa sababu mara nydingi sisi watu wa Kusini tulikuwa tunalalamika mara nydingi mnatusahau sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile na suala la kupeleka meli ya mafuta katika Bandari ya Mtwara na Lindi, tunashukuru mmeefanya jambo zuri sana. Hata hivyo, mradi huu nina wasiwasi nao kwa sababu Mikoa mingi ambayo imepitiwa na hii Gridi ya Taifa nimeona nguzo kubwa za chuma ipo lakini kuanzia Mbagala mpaka Mtwara sijaona nguzo ya chuma. Isiye tukapigwa changa la macho kwa hizi nguzo za magogo, kama ndio hivyo basi tutashukuru. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili nataka niongelee *REA*. *REA* awamu ya I na II hajifanya vizuri katika nchi hii, kwa sababu sehemu nydingi za taasisi za umma umeme huu haukizingatiwa lakini kwenye hii awamu ya III naona imezingatiwa. Je, zile sehemu ambazo zilipitiwa na awamu ya I na II kuna utaratibu gani sasa wa kufikisha umeme kwenye hizi taasisi za umma? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, awamu ya III ya *REA* nayo ina ukakasi wake. Mkoaa mzima wa Lindi tumepata mkandarasi mmoja. Mpaka leo mkandarasi wa *REA* Mkoaa wa Lindi bado yuko Ruangwa hajui Liwale ataenda lini, hajui Nachingwea ataenda lini na awamu ya III sehemu ya kwanza mnasema inakamilika mwezi Juni mwakani, lakini hatuelewi awamu hii ya kwanza huyu mkandarasi atafikia wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile walituambia kwamba maeneo ambayo yako mbali na vyanzo vyta umeme yatapatiwa na umeme juu. Katika Halmashauri yangu ya Wilaya ya Liwale kuna vijiji ambavyo viko umbali mfupi,

kutoka Halmashauri ya Wilaya ni kama kilomita 70 au kilomita 50 kutoka kwenye vyanzo vya umeme, Vijiji kama vya Ndapata, Mpigamiti, Kimambi, Mdunyungu, Milui, Kikuyungu, Lilombe, Mlombwe, Ngongowele, Kipelele, Naujombo, najua kwamba hakuna uwezekano wa kujenga nguzo za umeme kutoka Liwale mjini mpaka kufikia vijiji hivi, naomba nipate ufanuzi umeme jua katika vijiji hivi utakuja lini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachogomba hapa mambo ya *Stiegler's Gorge* hii ni kwa sababu ya falsafa moja kwamba ukiwa muongo lazima usiwe msahaulifu. Serikali hii mlishtuaminisha kwamba gesi ya Mtware ndiyo muarobaini wa umeme nchi hii, matokeo yake haikuwa hivyo, ndiyo maana watu wanavyoingia kwenye *Stigler's Gorge* pamoja na madhara yote haya ambayo tunaenda kuyapata, je, haitakuwa sawa na yale yaliyokuwa kwenye gesi? Maana tuliamiwa kwamba gesi itashusha bei ya umeme, bei ya umeme bado iko juu. Tuliamiwa gesi itakuwa mwarubani wa umeme nchi hii na kuuza nchi za nje, lakini mpaka leo pesa nyingi zimepotea, hatujui hatima ya mradi ule. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana sasa tunapoingia kwenye *Stiegler's Gorge* ambako tunajua madhara ni makubwa, kwa madhara haya kama kweli hili jambo lillilokusudiwa litakwenda kufanyika tunaweza tukavumili haya madhara, lakini kwa kuona matatizo yale yaliyojitokeza kwenye mradi wa gesi ndiyo maana leo hii wananchi wengi na Wabunge wengi wanalilalamikia suala hili. Wanakuwa waoga kwa sababu tusije tukatumrukia kwenye tope kama tulivyotumbukia kwenye gesi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee suala la gharama za umeme nchini. Suala hili Mheshimiwa Waziri inabidi alitupie macho sana kwa sababu linatugharimu kwa kiwango kikubwa sana. Ndiyo maana hata viwanda vyetu vinazalisha bidhaa ambazo zinashindwa kuingia kwenye soko la Kimataifa kwa sababu gharama ya uzalishaji nchini ni kubwa. Leo hii mtu aki-*import* sukari kutoka nje ya nchi inauzwa rahisi kuliko ya ndani ya nchi. Kwa hiyo, suala la

gharama ya umeme linatakiwa liangaliwe kwa makini sana.
(*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Zuberi. Tunaendelea na Mheshimiwa Mussa Mbarouk, Mheshimiwa Bobali na Mheshimiwa Simbachawene wajiandae.

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi lakini kwanza niwashukuru sana wapiga kura wangu wa Jiji la Tanga ambao nitaanza kwanza kwa kuwazungumzia katika suala zima la bomba la mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza hilo nisije nikasahau kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ameniwezesha kunipa afya njema na kuweza kuzungumza katika Bunge lako hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanga itakuwa ndiyo *last destination* ya bomba la mafuta na patakuwa na *refinery* nyingi ambapo itakuwa ndiyo mitambo ya kuingiza kwenye meli, mitambo ya kusafisha *crude oil* na mambo mengine. Kwa hiyo, kama walivyosema wasemaji wengine niishauri Serikali kwamba pale ambapo mradi utakuwa umepita kipaumbele cha kwanza katika ajira wapewe watu wa eneo hilo. Kwa hiyo, nawaombea watu wa Tanga wale ambao wana taaluma mbalimbali wapewe kipaumbele cha kwanza katika ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, nizungumzie suala zima la umeme wa *REA*. Sisi ambao tuko kwenye Majiji umeme wa *REA* sasa umekuwa kama unatugeuka kwa sababu tuliambiwa kwanza hakutarukwa kijiji hata kimoja lakini pia shule zote za msingi na sekondari ambazo hazina umeme watawekewa umeme wa *REA*. Nitaomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha atueleze mpaka sasa hivi ni shule ngapi za msingi

zimewekewa umeme wa *REA* na shule ngapi za sekondari zimewekewa umeme wa *REA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hilo halitoshi, kwenye umeme wa *REA*, kuna baadhi ya vijiji waliomba umeme wa *TANESCO* baada ya kuja hii neema ya *MCC* ambayo ililetia *REA I*, *II* na *III* wakaomba sasa waingizwe katika mradi ule ambaao utakapokuwa umefanya *wiring* unalipa Sh.27,000. Hata hivyo, *TANESCO* inawalazimisha walipe gharama ile ile ya *TANESCO* ya Sh.370,000. Mfano upo katika Jiji langu la Tanga kwenye Kata za Kiomoni kwa maeneo ya Pande Mavumbi, Pande Muheza, Pande Marembwe, vilevile katika Kata ya Pongwe maeneo ya Kinangwe na Kisimatui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hilo halitoshi, hata kwenye Kata ya Kirare kule kunakozalishwa sana muhogo, maeneo ya Mapojoni na maeneo ya Mtakuja, bado umeme wa *REA* huko haujafika lakini wananchi pia wamekuwa na huko wanakizungumkuti wakiuliza wanaambiwa kwa sababu mmekuwa Jiji ninyi hampaswi kupata umeme wa *REA*. Kuna kitu kipyaa sasa hivi pia nimeambiwa kinaitwa *para urban*, kwamba kuna kitengo kipyaa kinaanzishwa, huu itakuwa kama ni ujanja wa kuwakwepa wananchi. Kama tumeamua kuwasaidia wananchi tusianze kuleta visingizio vidogo vidogo tuwapelekeeni umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukiambiana hapa kwamba asilimia 75 ya Watanzania wanaishi vijijini lakini tangu tupate Uhuru mpaka leo ni asilimia 10 tu ya Watanzania wanaofaidi umeme. Sasa kwa nini tunataka wazalishaji wawe wa vijijini lakini tukifika kwenye umeme tunaanza kupanga mipango tofauti. Naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa atuhakikishie ni kweli vijiji havitarukwa au lah! (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna baadhi ya vijiji walipelekewa nguzo chache. Wanakijiji wako 1,000 wanaomba nguzo 1,000 wanapelekewa nguzo 500 au nguzo 400, wengine wanakosa kupelekewa huduma ya umeme. Wako tayari kulipia kama vile ambavyo unalipa umeme

TANESCO lakini unashubiri miezi sita, hata kwenye *REA* watu wapo tayari kulipia lakini hawapatiwi umeme. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali ichukue utaratibu wa kuandaa kampuni ya *TANESCO* iwe kama vile kampuni za simu, pawe na ushindani kwa sababu *disadvantage of monopoly* kwa *TANESCO* ndiyo inawafanya wajione kwamba wao zaidi. Tuanzishe kampuni za umeme kama kampuni za simu iwe mwananchi ana uhuru wa kuchagua kampuni anayotaka. Simu leo wanashindana kupunguza bei ya muda wa maongezi kusudi wapate wateja. Kama kungekuwa na shirika lingine la umeme Tanzania, Waziri nakuhakikisha *TANESCO* labda ingebaki na Taasisi za Serikali, kwa sababu kuna usumbufu, kuna urasimu, na rushwa imejaa huko. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyoju, ujisadi wote unaopita Tanzania *TANESCO* hawatoki. Mheshimiwa Waziri tunaomba hili uliweke sawa. Kwenye umeme wa *REA* tunataka wananchi wetu wapate umeme wa vijiji na kama ni Sh.27,000 mtu akishafanya *wiring* iwe Sh.27,000 kweli, siyo Serikali inatangaza Sh.27,000 akifika *TANESCO* anaambiwa aaah, hizo ni kauli za wanasiasa tu, hili jambo linaichafua Serikali. (*Makoff*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la bei ya umeme. Bei ya umeme ndiyo inayosababisha watu watumie mkaa kwa wingi, ndiyo inayosababisha watu watafute vishoka kwa ajili ya kuwaunganishia umeme. Sasa tushushe bei ya umeme ili wananchi wetu wafaidi umeme. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Afrika Mashariki na Kati ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mussa Mbarouk. Tunaendelea na Mheshimiwa Hamidu Bobali, Mheshimiwa Simbachawene na Ussi Pondeza wajlandae.

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Waziri, Naibu Waziri na Mkurugenzi wa *TPDC* kwa kukubali ushauri wangu wakati tunapitisha bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Kuna ushauri niliutoa nawashukuru mmetusaidia hususani kwa wananchi wangu pale Kilangala kuweza kunufaika na mkuza. Mheshimiwa Waziri nakuomba tu kwamba yale tuliyoyaanza na Mkurugenzi wa *TPDC* nafikiri ananisikia basi tuyamalizie ili kile tulichokubaliana wananchi sasa wakione ili wapate moyo ule ambao walikuwa nao siku ile tulipokuwa tunakubaliana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina hoja mbili ama tatu, kwanza nataka nihoji Wizara. Mwaka 2013, Rais wa Marekani Barack Obama alikuja Tanzania na kuzindua *Initiative ilioitwa Power Africa*. Sababu iliyofanya aje kuzindua *Power Africa*, Tanzania ni mionganini mwa nchi ambazo wananchi wengi hawapati huduma za umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi ambazo ziko *Sub-Saharan Africa*, asilimia 76 ya wananchi tunaoishi katika Jangwa la Sahara hatupati umeme na *Power Africa* ilikuja kuzinduliwa Tanzania, ilikuwa ni mpango wa miaka mitano chini ya ufadhili wa *African Development Bank* na *partners wengine*. Sasa miaka mitano imefika, tunaomba ndani ya Bunge iletwe tathmini ama Waziri wakati anajibu atuambie tathmini ya programu ya *Power Africa* imeishia wapi? Je, fedha ambazo ziliikuwa zimeahidiwa zimepatikana ama hazijapatikana? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu taarifa tulizonazo Mheshimiwa Waziri *Power Africa* alipoondoka Rais Kikwete na *Power Africa* imeondoka Tanzania. Ndiyo taarifa tulizo nazo na imeondoka kwa sababu tumefeli kwenye

Diplomasia ya Kiuchumi. Wafadhili waliokuwa wanafadhili miradi ile ya *Power Africa* wengi wao wame-withdrawfedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hili siyo sahihi wakati Waziri anakuja kuhitimisha aje atueleze kwa sababu takwimu tunazo. Wamarekani ndiyo walikuwa wachangiaji pamoja na *partners* wao, wao sasa hivi hawatoi fedha na tunajua sababu kubwa na ugomvi mkubwa wa Marekani na Serikali iliyopo sasa madarakani ni hii Sheria ya Mtandao, sheria hizi ambazo zinakinzana kabisa na demokrasia ya wakati huu. Sasa fedha hizi kama kweli zilikuwa zinakwenda au zimetolewa basi tunahitaji tathmini ya *Power Africa* imeishia wapi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichangie suala la gesi. Gesi imegundulika maeneo ya Kusini mwa Tanzania lakin kiwango ambacho kimepatikana ni kikubwa mno. Nashauri kama inawezekana hatuna hata sababu ya kwenda kwenye *Stiegler's Gorge*, hatuna. Kwa kiwango cha gesi tulichonacho unaweza kupatikana umeme wa kutosha tukatumia kwenye viwanda na kwenye majumba yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi ya *Qatarinatumia* gesi. Rasilimali kubwa iliyofanya Qatar leo wafike pale walipofikia ni gesi. Mheshimiwa Rais Kikwete wakati yuko Mtwara anatushawishi wananchi wa Kusini tukubali mradi wa bomba la gesi alisema Tanzania itabadilika itakuwa Qatar ya Afrika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais Kikwete alikuwa Rais aliyetokana na Chama cha Mapinduzi ambaye ndiye aliyetuahidi kwamba tutakuwa Qatar ya Afrika. Rais John Magufuli naye ni Rais anayetokana na Chama cha Mapinduzi amekuja anaachana na ule mradi wa bomba la gesi, anaachana na miradi yote ya gesi, je, mmeshatufikisha kwenye Qatar ya Afrika? Kama tumefika kwenye ile *level/ya kuitwa* Qatar ya Afrika basi tuelezeni. Tunachokishuhudia ni umeme shida na kiwango cha upatikanaji wa umeme vijijini bado ni tatizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna biashara ya gesi ambayo nimemwona Waziri juzi anaizungumzia kwamba inataka kuanza Mtwara na Dar es Salaam, ni biashara nzuri sana. Mwaka jana hapa tulitenga fedha kwenye bajeti kwamba pamoja na maeneo mengine ambayo gesi itasambazwa majumbani ni Lindi. Nakumbuka ilitengwa shilingi bilioni moja kwenye bajeti iliyopita kwa ajili ya kutengeneza miundombinu Lindi. Leo Waziri anakwenda kuzindua anaanza kusema kwamba Dar es Salaam na Mtwara wataanza kutumia gesi majumbani mbona Lindi haipo? Lindi tuna gesi ya kutosha lakini sijaona imetajwa. Sasa Waziri hebu atueleze kwamba wametutoa au sisi tutakuwa watu wa kufuatia baadaye? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kuhusu suala la *REA*. Mheshimiwa Waziri wakandarasi wengi wa *REA* wanalamika kwamba Waziri amekuwa kama anawafanya *harassment*. Leo Waziri anasema mnakwenda kuzindua mradi, vifaa wanatakiwa waende wakavichukue *TANESCO*, wakaviazime, wakati mwngine kuna miradi mnaizindua haijakamili ili mradi tu ionekane kwamba *REA* inafanya kazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna tatizo Wizara ya Fedha ambako Bunge zima tunajua kwamba mambo ya nchi hii hayaendi kwa sababu tatizo liko Hazina na Wizara ya Fedha. Hakuna Mbunge ambaye hajui, hakuna mwananchi ambaye hajui kwamba kama Waziri Mpango ndiyo Waziri wa Fedha na ataendelea kuwepo katika miaka mitano yote ya Rais Magufuli, nchi hii haitakwenda kwa sababu ameshindwa kumshauri Rais. Mimi leo ukiniambia nitaje Waziri aliyefeli zaidi nchi hii ni Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Philip Mpango, hili halifichiki. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Wizara ya Kilimo wamelalamika fedha, kwenye Wizara ya Maji wamelalamika fedha, TAMISEMI wamelalamika fedha, kwenye umeme tunajua Waziri hasemi tu kwa sababu ya uwajibikaji wa pamoja lakini naye pia shida yake ni fedha. Ndiyo maana

wakandarasi wamesaini mikataba zaidi ya miezi tisa mpaka sasa hamjawapa fedha. (*Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Bobali.

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, zilikuwa dakika kumi.

MWENYEKITI: Zimemalizika Mheshimiwa.

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Aaah! Ndiyo nilikuwa naanza.

MWENYEKITI: Tunaendelea na Mheshimiwa Simbachawene baadaye Mheshimiwa Ussi Pondeza na Mheshimiwa Sulemani Zedi wajiandae.

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nianze kwa kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Dkt. Kalemani mdogo wangu, Naibu wake Mheshimiwa Subira Mgusu, Katibu Mkuu, Ndugu Mwinyimvua na watumishi wote wa Wizara ya Nishati, hongera sana kwa kazi nzuri mnayoifanya na napenda nianze kwa kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, dunia sasa inapima uwezo wa uchumi wa nchi kwa kuangalia uwezo wake wa kuzalisha na kutumia umeme. Kwa hiyo, ukitaka kupata kipimo kizuri cha kujua nguvu ya uchumi wa Taifa fulani, unaangalia wana uwezo gani wa kuzalisha nishati na wana uwezo gani wa ku-*consume* nishati hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitoe takwimu, nchi ya kwanza kwa kuzalisha umeme yaani *energy per capita*/ni Iceland, nchi ya 73 ni China, nchi ya 137 ni Tanzania, nchi ya mwisho ni Eritrea. Katika *grouping* walizozifanya kwa *clusters* sisi ni wa 137 na uwezo wetu wa kuzalisha umeme ni

megawatt 1,500. Ukiangalia kwa kiwango hiki utaona kwamba tunapozungumzia kupeleka umeme vijiji vyote zaidi ya 12,000, tunapozungumzia uchumi wa viwanda na kwamba mpaka mwaka 2020 tufike uchumi wa kati ni ndoto kama hatuna *energy* ya kutosha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha wakati Serikali inafanya juhudini kubwa sana ya kuzalisha umeme na sera ya dunia ya nishati, *The World Energy Policy is power mixing*. Lazima uwe na vyanzo vya aina zote ili hiki kikitetereka unakitumia hiki, hiki kikitetereka unakitumia hiki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwelekeo huu tunaokwenda wa kwenda uchumi wa viwanda ambapo pande zote mbili za Bunge tunakubaliana, hatuwezi kufika huko kama bado suala la uzalishaji wa umeme kwa nchi yetu siyo suala la kufa na kupona. Ni lazima liwe suala la kufa na kupona, ni lazima tuzalishe umeme wa aina yoyote ili tuweze ku-fit kwenye hicho tunachokitaka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi siyo Mchumi na wakati mwiningine napenda kusikiliza hotuba ili nijifunze kwa sababu kujifunza hakuna mwisho. Inanisumbua napoona hata wabobezi wa uchumi waliopo humu wana-*undermine* jitihada hizi zinazofanyika. Sababu zenyewe zinazotolewa, nimesikiliza sana wasemaji wengi wanasema tuache *Stiegler's Gorge*, tuzalishe umeme huu mradi ulioanza kufanyiwa *study* mwaka 1972 mpaka leo haujatekelezwa, tuachane nao na sababu wanazozitoa ni kwamba kwa kuwa tuna gesi hatuna haja ya kuzalisha umeme huu kwa sababu gesi tunayo tuzalishe umeme wa gesi. Wakati wanajua kabisa kwa sasa hivi *the leading generation* katika nchi ya *energy* ni gesi ambayo ina *megawatt* zaidi ya mia saba na arobaini na kitu, inayofuatia ni *hydro* ambayo ina mia nne themanini na kitu karibu 500, zinazofuatia ni ndiyo *biomass* na vitu vingine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa sisi suala la kuzalisha umeme wa *hydro* ni la kufa na kupona. Miradi mingi ya *hydro* duniani huwa inapata upinzani mkubwa na hupata upinzani

mkubwa kwa sababu tu umeme wake ni wa bei rahisi na unaweza ukaiibua nchi hiyo kutoka kwenye umaskini na kuwa nchi yenyé uchumi *stable*. (*Makofí*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Waganda wanajenga Bujagali upinzani ulikuwa mkubwa, wakasema tunajenga kwa pesa zetu na wakajenga kwa pesa zao. Vyanzo vya maji yanayozalisha umeme ule wa Bujagali, Kabahale ni vyanzo vya Mto Nile ambapo kuna siasa nyngi na *international affairs* nyngi lakini bado wame-generate umeme. (*Makofí*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *installed capacity* Ethiopia ni *megawatt* zaidi ya 4,000 na wamezi-*tap* kwenye Mto Nile wakajenga mradi, unazalisha umeme na walikataa kusaidiwa na mtu yeoyote wakaamua kuzalisha kwa pesa yao. Hivi sasa Ethiopia wana mradi unaoitwa *The Grand Ethiopian Renaissance Dam* ambao utazalisha *megawatt* 6,450 na wanachukua Mto Nile. Sisi tunazuiwa na Watanzania wenzetu wanaosema ni wazalendo, kukata miti *square kilometer* 1,400. (*Makofí*)

TAARIFA

MHE. JAMES K. MILLYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa, dakika moja.

MHE. JAMES K. MILLYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Simbachawene ni mtu nayemheshimu sana ni rafiki yangu na Wakili msomi, lakini ikumbukwe kwenye Bunge hili kwamba Mheshimiwa Simbachawene ameshakuwa Waziri wa Nishati na Madini wa nchi hii. (*Makofí*)

MWENYEKITI: Mpe taarifa, hiyo siyo taarifa.

MHE. JAMES K. MILLYA: Ni taarifa, lakini hajawahi kuleta suala hili kwenye Bunge hili, maana yake ni mtu anaye-

support jambo ambalo yeye mwenyewe hakuliamini alipokuwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Simbachawene naomba uendelee. Mheshimiwa Zitto mbona unaongea bila hata sijasema.

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa mbili kwa pamoja haiwezekani, Mheshimiwa Simbachawene naomba uendelee.

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE: Mheshimiwa Mwenyekiti, mzungumzaji ni mdogo wangu na nampenda sana rafiki yangu, alipokuwa anagombea Urais Chuo Kikuu nilimsaidia pia. (*Kicheko/Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tunapaswa kulichukua jambo hili kwamba siyo la kisiasa, ni jambo letu sote na ushindi wa kujengwa kwa chanzo hiki cha umeme iwe ni wa kwetu sote. Ili tuweze kufika kwenye uchumi wa viwanda, kwanza ili tuweze kupeleka umeme kwenye vijiji vyetu vyote zaidi ya 12,000 tunahitaji zaidi ya megawatt 2,500 ambazo hatuna. Sasa anayesema anataka umeme wa REA kijijini kwake ndiyo huyo anayekataa chanzo chenye bei nafuu kuzalisha umeme. (*Makof*)

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE: Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania katika ukanda huu wa *East Africa*...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Mbunge muda wako umemalizika. (*Makofii*)

Tunaendelea na Mheshimiwa Ussi Pondeza, Mheshimiwa Selemani Zedi ajiandae.

MHE. USSI SALUM PONDEZA AMJADI: Mheshimiwa Mwenyezekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyezekiti, napenda nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Waziri kwa jinsi ambavyo amewasilisha hotuba yake hii ya Wizara ya Nishati na Madini. Pia niwapongeze Watendaji Wakuu wa Wizara hii ya Nishati akiwemo Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi wa *REA*, *TPDC* kwa jinsi ambavyo wanafanya kazi vizuri na wanaweza kufikia yale malengo ambayo sote matarajio yetu ni kuiona Tanzania ya viwanda inakuja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyezekiti, nasema maneno haya kwa sababu tunaposema Tanzania ya viwanda tunaitaka bila umeme wa uhakika basi hatuwezi kuipata, lakini kwa kasi ambayo wanakwenda nayo Mawaziri hawa na Watendaji wao, tuna uhakika *vision* yetu ya 2020 tunao uwezo wa kufikia malengo haya. Tunachotakiwa ni sote humu ndani kama Wabunge kuishauri Serikali na kuwasaidia hawa katika juhudhi zao ambazo wanaziendeleza katika kufanikisha upatikanaji wa umeme wa kutosha na wa uhakika ili tuweze kufikia malengo yetu yale ambayo tunayakusudia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyezekiti, jambo lingine nishauri Wizara na Mheshimiwa Waziri kwa upande wa *REA*. Mimi ni Mjumbe wa Kamati tumetembelea miradi na tumekutana na matatizo mengi ikiwepo *scope of work* kwa maana kwamba maelekezo yanatolewa kwenye vitabu lakini mkienda *field* sivyo ilivyo. Hili ni tatizo kubwa ambapo wakandarasi wengi ambaao tumewahoji hawana majibu mazuri, wanakwambia mimi *scope* yangu mwisho hapa, lakini wananchi wanalalamika wanasesma katika kijiji chetu mradi umekuja lakini waliopata ni watu wanne, watano hawazidi 10. Kwa

maana, hiyo upatikanaji au ile dhana kamili ya kusema wananchi wote watapata umeme wa *REA* inakuwa haifikiwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo lingine nataka nilzungumzie nalo ni kuhusu *REA* kupewa pesa kwa wakati. Sehemu zote ambazo tumetembelea, miradi tunaikuta imesimama au inasuasua tatizo kubwa ni fedha. Ukiwaliza kwa nini fedha hampati, tumejaribu kuwahoji *REA* na Wizarani, tatizo kubwa ni Wizara ya Fedha kutotoa fedha kwa wakati. Hili suala linazungumzwa karibu katika kila Wizara kwamba Wizara ya Fedha imekuwa kila pesa ambayo inatengwa lazima iwe inafanyiwa uhakiki, hatukatai kufanya uhakiki, lakini kuna mambo mengine ambayo kama hii *REA* ambayo iko *ring fenced* inachukua muda. Kuna *time* watu hawajalipwa imefika mpaka miezi nane, watu wanasubiri lini watalipwa ili waweze kupata *material*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaposema sasa tuna matarajio ya kufika mpaka mwaka 2020...

TAARIFA

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ussi subiri taarifa moja. Mheshimiwa Kuchauka, nusu dakika.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa muongeaji kwamba kwenye utawala wa Awamu ya Tano hakuna fedha ambayo iko *ring fenced*.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ussi Pondeza, endelea.

MHE. USSI SALUM PONDEZA AMJADI: Mheshimiwa Mwenyekiti, sikubaliani naye na taarifa siipokei, hii tunajua ipo na akitaka ushahidi nafikiri kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri ameeleza, hiyo taarifa yake siipokei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maana kuwa *REA* lazima wapewe pesa kwa wakati ili tuweze kufikia malengo yetu yale ambayo tumekusudia ya kuhakikisha uchumi wetu unatoka uchumi wa chini na kuwa uchumi wa kat. Hapa kila Mjumbe ambaye amesimama, jambo kubwa ambalo tunalizungumzia ni jinsi gani pesa zitatoka Wizara ya Fedha kuja *REA* ili wakandarasi waweze kulipwa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa nilizungumzie kwa ruhusa yako ni kuhusu tatizo la deni la Zanzibar. Kuna taarifa ambayo mazungumzo yameanza na yanaendelea kwa sababu imetuwa kuna sintofahamu katika suala la deni la *TANESCO*, katika taarifa zao wanasema wanadai hivi lakini *reality* haiko hivyo. Kwa sababu mazungumzo yameanza kufanyika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri atakopofanya majumuisho naomba hili aliweke wazi limefikia hatua gani na kuna nini ambacho kinaendelea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, imetuwa ni tatizo kubwa sana kwetu Wazanzibar kila mwaka linajirejea hili na inafika pahali watu tunaonekana labda kama vile tunapata kitu cha bure au hatulipi, tunasaidiwa. Kwa sababu sisi tunajiamini na tuna uwezo wa kulipa *current bill* kabisa kama tunavyolipa sasa hivi, nakutaka Mheshimiwa Waziri anapokuja hapa aje atoe taarifa hii ya kuhusu Zanzibar tunavyolipa umeme, deni na *current bill* ambayo tunatumia kila mwaka. Kuhusu suala la bei tutalizungumza baadaye. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haya machache, sitaki niendelee sana maana nitatoa utamu wa haya maneno yangu ambayo nimemalizia, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Ussi Pondeza. Tunaendelea na Mheshimiwa Selemani Zedi na Mheshimiwa Charles Kitwanga ajiandae.

MHE. SELEMANI J. ZEDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia hoja hii muhimu sana ya Wizara ya Nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Nishati Dkt. Kalemani na Naibu wake Mheshimiwa Subira Mgali kwa utayari wao wakati wote kuwasikiliza Wabunge na kupokea ushauri wao na kuufanya kazi. Kiukweli Mheshimiwa Dkt. Kalemani na Mheshimiwa Subira Mgali ni mfano mzuri wa Mawaziri ambao wanasiliza Wabunge na kufanya kazi kero za Waheshimiwa Wabunge. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati *REA* awamu ya III inaanza, Waheshimiwa Wabunge tuliombwa tutoe mapendeleko katika maeneo yetu kwamba ni vijiji gani ambavyo tunadhani ni muhimu vipatiwe umeme. Waheshimiwa wote tulitoa mapendeleko yetu lakini orodha ya *REA* awamu ya III ilipokuja kulikuwa na mkanganyiko mkubwa sana, vijiji vingi vilikuwa vimerukwa, vimeachwa na vingine ambavyo siyo muhimu ndio vilikuwa vimewekwa. Niwapongeze tena Mheshimiwa Dkt. Kalemani alikuwa *very flexible*, alizingatia kwa umakini hoja za Wabunge na marekebisho makubwa yalifanyika karibu Wabunge wengi maeneo mengi ya vijiji ambayo yalikuwa yamerukwa au yameachwa yakawa *incorporated* kwenye *REA* awamu ya III. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwangu kwa mfano vijiji muhimu kama Vijiji vya Mwamala, Lububu, Kayombo, Sekondari ya Kili, Karitu na vingine vilikuwa vimeachwa kimakosa lakini baada ya kumfuata Mheshimiwa Waziri na kumuelezea umuhimu wa vijiji hivi alikuwa *very flexible*, aliwasiliana na *REA* na pia niwapongeze *REA* kwa sababu nao walitikia kwa uharaka na sasa hivi tunavyoongea vijiji hivi vimo kwenye *REA* awamu ya III na kazi nzuri inaendelea. Mheshimiwa Dkt. Kalemani na Mheshimiwa Subira Mgali hongera sana na naomba muendelee na ari hiyo hiyo ya kusikiliza Wabunge na kufanya kazi hoja zao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wengi wameongelea suala la uwezo mdogo wa *TANESCO* kukidhi mahitaji. Hili jambo ni *very serious*, inabidi jitihada za makusudi zifanyike ili kuisaidia *TANESCO* iweze kukidhi mahitaji ya wateja. Hali ilivyo sasa hivi kwa *TANESCO* kwa kweli siyo ya kuridhisha kabisa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya yangu ya Nzega, Ofisi ya *TANESCO* Nzega, leo hii kuna malalamiko makubwa sana. Wateja ambao wamelipia ili wapatiwe umeme tangu mwezi Januari mpaka leo hawajaweza kupatiwa umeme, tunakaribia miezi sita (6) sasa. *Speed* hii ni ndogo mno na kwa *standard* na *level* yoyote ile haikubaliki. Haiwezekani mteja alipie kupata huduma tangu Januari mpaka leo tunakaribia Juni hajaweza kupata huduma. Ni kipindi kirefu sana na wananchi wanakata tamaa na huduma ya namna hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba hiki kilio cha uwezo wa *TANESCO*, Serikali ikifanyie kazi. Kwa kweli *TANESCO* wamechoka na uwezo wao ni mdogo sana. Nitakupa mfano, Jimbo langu kuna Kata inaitwa Mambali ni kilometra 40 kutoka Nzega Mjini kina huduma ya umeme, ikitokea *technical fault* pale *TANESCO* Mjini Nzega hawana hata uwezo wa kufika kilometra 40, hawana hata gari lolote la kubeba nguzo, kubeba vifaa vyaa kujengea, hivyo, hawawezi ku-*attend technical fault* yoyote ambayo iko nje ya Mji wa Nzega na *TANESCO* Nzega inahudumia *radius* kama ya kilometra 40 ama 60 hivi. Kwa hiyo, hali *TANESCO* ni mbaya, hawawezi kukidhi mahitaji ya wateja. Haiwezekani mtu asubiri nguzo miezi sita wakati ameshalipia, hili kwa kweli lifanyiwe kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema *REA* awamu ya III, tatizo ninaloliona hapa ni *speed* ndogo sana. Nikubaliane kwa sababu *REA* inachofanya ni kusambaza umeme, kinachotakiwa sasa hizi jitihada kubwa za kusambaza umeme vijijini lazima ziendane na ongezeko la uzalishaji wa umeme kwa sababu huwezi kusambaza bidhaa ambayo hujaizalisha, huwezi kusambaza kitu ambacho huna. Kwa

hiyo, niunge mkono hoja aliyozungumza Mheshimiwa Simbachawene kwamba kuna umuhimu mkubwa sana wa kuwa na uzalishaji wa uhakika wa umeme wa kutosha ndipo tuusambaze. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu *REA* wanachofanya ni kusambaza lakini huwezi kusambaza kitu ambacho hakijazalishwa. Kwa hiyo, jitihada kubwa bado nashauri kwamba Serikali iendelee na miradi yake ya kuzalisha umeme kwa wingi ikiwemo *Stiegler's Gorge* ili tupate umeme wa kutosha ambao ndiyo sasa utasambazwa kwenye vijiji. Hatuwezi kukazania usambazaji wakati hatujui sasa utasambaza nini kama umeme huo haujazalishwa. Kwa hiyo hilo, naomba lizingatiwe. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie bomba la mafuta...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Zedi. Tunaendelea na Mheshimiwa Charles Kitwanga.

MHE. SELEMAN J. ZEDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makof*)

MHE. CHARLES M. KITWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze tu kwa kusema kwamba unapozungumzia Serikali ya viwanda halafu huna umeme ni sawasawa na binadamu anayeishi halafu hakuna hewa. Hilo ni wazi, kwa hivyo niipongeze sana Serikali ya Mheshimiwa Rais John Joseph Pombe Magufuli kwa juhudhi wanazozifanya za kuhakikisha kwamba tunajenga Serikali ya viwanda na umeme upo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa ambacho nitakizungumzia na nitatoa ushauri, kwanza ni namna gani

tuwe na umeme wa kutosha. Huu mlolongo wa kusema *megawatt* 20, *megawatt* 40 *forget about it*, zungumzia *megawatt* 2,000 za *Stiegler's Gorge*, sasa hivi tuanze mpango mkakati wa kuweka umeme wa makaa ya mawe *megawatt* 5,000. Haya mambo tunayoambiwa eti tukienda kwenye makaa ya mawe tutachafua hewa, nenda Marekani, Uingereza umeme wanaotumia *percentage* kubwa ni upi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, teknolojia imebadilika, tuwe na mpango mkakati wa *ku-generate* umeme mkubwa wa makaa ya mawe na tutajenga teknolojia inayoweza *ku-absorb* zile *fusion* ili zichukue zile *fumes* zote kusiwe na matatizo. Faida kubwa tutakayopata, wananchi wengi watapata kazi katika maeneo hayo, miji iliyo poto karibu na pale itakuwa imeendelea na umeme tutakaokuwa *tuna-generate* ni wa bei nafuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, duniani umeme wa bei nafuu ni maji na mkaa. Halafu hao Wazungu wanao-*generate* umeme wa mkaa wanatudanganyadanganya hapa, danganyweni ninyi siyo Kitwanga. Ni lazima tufikirie, tuwe na uwezo wa kujua teknolojia hii tutaipataje lakini kila siku tunalalamika hapa, ninyi mmekuwa watalaam sana kuliko Wazungu ambao wana umeme wa makaa ya mawe miaka nenda rudi na bado wanaishi tu na wana afya nzuri hata wakati mwengine kuliko hata sisi? (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamani lazima mje hapa na mpango mkakati, hatutaki hizi *megawatt* 200 ama 300, tunataka *big*. Tume panya kutoka *megawatt* 1,450 mpaka 1,517, hilo Mheshimiwa Waziri mdogo wangu usilitaje, hilo siwezi kukusifia nalo. *Come with big kama ulivyo big, you are a good person and you are doing wonderful job* na hii miradi midogo mingi, *it is costing us a lot kui-manage*. Yaani una-*manage* mradi wa *megawatt* 20, una Afisa Utumishi, *Engineer* na mambo mengine mengi. (*Makofi/Kicheko*)

MBUNGE FULANI: Ongea na Mwenyekiti.

MHE. CHARLES M. KITWANGA: Ninaongea na Mwenyekiti, tatizo kubwa la watu wa huku wanapenda kusifia vinavyofanywa na CCM wao wamelala tu. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi *REA* kila mtu anasifia lakini nazungumza *with this feeling because I love my country. I am ready to die for it and there is nobody can change me on that.* Kama ulikuwa hujui kwamba najua Kizungu njoo nikufundishe Kisukuma. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nzungumzie suala ambalo lipo hapa kila mtu analisema, ukosefu wa pesa, hivi kwa nini unakosa pesa?

MBUNGE FULANI: Shangaa.

MHE. CHARLES M. KITWANGA: Wewe kama ni Waziri wa Fedha halafu unasema hatuna pesa, ondoka hapo. Wewe kama ni Mbunge wa Jimbo fulani wananchi wako wanasesma unajua kuna matatizo, ondoka hapo. *You are been a human being and you are given that opportunity to save that place, because people trust you and you must think. No thinking, get out of that place.* (*Makofi/Kicheko/Vigelegele*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, niwaombe ndugu zangu Wabunge jambo la kwanza ambalo litatufanya tuisaidie nchi yetu ni ku-*think and implement. Work hard, be ready to die for what you requested for.* (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakuwa na shida mno mimi... (*Makofi*)

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

WABUNGE FULANI: Aaaaaaaaa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waitara naomba ukae, Mheshimiwa Kitwanga naomba uendelee.

MHE. CHARLES M. KITWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, niwaombe ndugu zangu wa REA, we are here and we have brain. Mkiwa na upungufu wa mawazo tupo. Watanzania lazima tuweze kusaidia mahali popote, tuache kulalamika. Unalalamika kwa nini, hujala? Kula, shiba, fanya kazi. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata mimi asubuhi sikuwa na hela, nimekwenda kufanya kazi nimepata. (*Makofi/Kicheko*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa, natamani nikuongeze muda lakini muda umekwisha.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Muongeze dakika tano.

MHE. CHARLES M. KITWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Kitwanga, muda wetu hauruhusu sana, naomba nimpe dakika tatu tu Mheshimiwa Richard Mbogo ili tuweze kukamilisha mjadala wetu kwa leo.

MBUNGE FULANI: Mbona muda bado, bado dakika 20 nzima.

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi. Kwanza nianze kuunga mkono hotuba ya bajeti ya Wizara ya Nishati. Naomba niende moja kwa moja kwenye jambo ambalo lina manufaa makubwa kwa nchi yetu lakini baadhi ya wachangiaji wamekuwa kidogo wanapotosha wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia miundombinu, tukianza na reli, mkoloni alivyojenga reli kuanzia Dar es Salaam mpaka Kigoma na Mwanza alisafisha miti na walivyojenga barabara walisafisha miti. Kwa hiyo, unavyotengeneza miundombinu yoyote kwa manufaa ya wananchi lazima utagusa mazingira. Kwa misingi hiyo, ujenzi wa Bwawa la *Stiegler's Gorge* linagusa mazingira lakini kwa asilimia tatu ya eneo lote la Selous. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia kwenda kwenye nchi ya viwanda kama wenzangu ambavyo wameweza kuzungumza, lazima tuwe na umeme wa uhakika na vyanzo mbadala ambavyo ni zaidi ya kimoja. Nitaomba nijikite kidogo kwenye faida za kuwa na hili bwawa. Jambo la kwanza, Wabunge wengi wamezungumzia kuhusu *TANESCO* kufanya biashara kwa hasara, lakini hawajajiuliza kwa nini imefanya kwa hasara. Kwanza, ni nafuu ambayo imewekwa kwa wananchi kwa bei ambayo haiendani na soko na gharama za uzalishaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kitabu cha Waziri ukiangalia upande wa kuzalisha *unit* za umeme kwa kutumia maji ndiyo wenye bei nafuu, kwa shilingi za Kitanzania 36 kwa *unit*, kwa dola ni dola 1.63. Katika umeme tunaoutumia kwa sasa hivi wa *megawatt* 1,517 ni asilimia 37 tu inatokana na maji. Kwa hiyo, niombe Serikali huu mpango tunauunga mkono endeleeni, msiangalie nini watu wanasema, angalieni matakwa ambayo yalianzishwa na Baba wa Taifa tangu mwaka 1972. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna faida ya ajira, maji hayo pia yatatumika kwa ajili ya matumizi ya majumbani. Wananchi na Wabunge wengi wa Mtwara na Lindi walikuwa wanazungumzia kutoa maji kutoka Mto Rufiji kupeleka Mtwara na Lindi, hii itakuwa ni suluhisho. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakuwa na uvuvi na sasa hivi tuna teknolojia ya kuwa na zile *cage* za uvuvi. Ziwa Victoria ipo, watu wanaotoka Musoma na Mwanza wanajua

na wavuvi hapa waupo, itakuwepo. Tutakuwa na utalii, katika ujenzi watu wanaenda China wanatembea kwenye ule mlima wanaangalia lakini hapa pia tutakuwa na utalii wa ndani na nje tutaweza kuvutia na tutaongeza mapato ya ndani na *GDP* yetu itapanda. (*Makofii*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mbogo, umeeleweka vizuri nashukuru sana kwa mchango wako.

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, nafunga mjadala, sasa namkaribisha Mheshimiwa James Mbaitia aweze kuleta maelezo yake binafsi.

MAELEZO BINAFSI YA MBUNGE

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi niweze kutoa maelezo binafsi ndani ya Bunge hili kuhusu kuitaka Serikali kuwakinga, kuwalinda na kuokoa raia wake dhidi ya majanga yanayosababishwa na binadamu kwa takribani asilimia 96 na yanayosababishwa na nguvu asilia (*acts of God*) kwa asilimia 4.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo haya nayatoa kwa mujibu wa Kanuni ya 50(1) na (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakumbukwa kwamba mnamo mwaka 2015, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilipitisha Sheria ya Wakala wa Usimamizi wa Maafa Namba 7 ya Mwaka 2015 (*The Disaster Management Act, 2015*) ambapo moja ya malengo na madhumuni ya sheria hiyo ilikuwa ni kuwakinga, kuwalinda na kuokoa wananchi dhidi ya majanga ya aina mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa nilizonazo mpaka sasa, Wakala wa Usimamizi wa Majanga haijaundwa na badala yake kazi zake zinafanywa chini ya Kitengo cha Maafa katika Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika siku za hivi karibuni, kumekuwepo na mvua nyingi ambazo kimsingi bado zinaendelea kunyesha katika baadhi ya maeneo mbalimbali nchini na zinaendelea kuleta maafa ya aina mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ni karibu nchi nzima lakini Halmashauri ya Wilaya ya Moshi ni sehemu mojawapo ilioyathirika na maafa yaliyosababishwa na mafuriko kufuatia mvua kubwa zinazoendelea kunyesha. Mafuriko haya yamesababisha madhara ya aina mbalimbali kama ifuatavyo:-

(a) Kwanza uharibifu wa barabara katika Kata za Kindi – Old Moshi Magharibi, Mabogini – Arusha Chini, Kirua Vunjo Kusini, Kahe, Kirua Mashariki, Kilema Kaskazini, Kilema Kati na Kirua Vunjo Magharibi;

(b) Mafuriko kwenye mashamba, taasisi na makazi ya watu ambayo yameleta athari kubwa kwa wananchi na taasisi nyingi hasa shule ambazo baadhi yake imebidi zifungwe;

(c) Kudidimia kwa miundombinu ya vyoo kwenye baadhi ya makazi ya watu na shule;

(d) Kuathirika kwa mazao kwenye mashamba mfano mashamba ya shule za msingi na pia ekari 150 za mpunga katika Kijiji cha Mandaka Mnono;

(e) Vifo vyta mifugo ikiwemo ng'ombe, mbuzi, kuku na mifugo mingineyo katika Vijiji cha Kuchakindo, Soko, Mawala, Mangaria na Ngaseni nikitaja kwa uchache; na

(f) Kutokea kwa magonjwa ya mlipuko na yanaendelea kutokea na kichaa cha mbwa ambapo inasadikika mpaka sasa watu watatu wamefariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa cha kusikitisha katika matukio yote haya, Serikali haijaweza kutoa msaada wa aina yoyote kwa wananchi isipokuwa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) ambapo limejitahidi kusaidia wananchi katika baadhi ya maeneo yaliyoathirika na mvua hizo na siku ya leo Ofisi ya Mbunge wa Vunjo imewasaidia shilingi milioni tano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo maeneo mengine mbalimbali nchini yaliyoathirika na mvua hizi na hali za watu siyo nzuri ikiwemo Jiji la Dar es Salaam, Mkoa wa Tabora na Rukwa. Kwa mfano, Rukwa kipindupindu kimetokea Sumbawanga na watu saba wameshafariki dunia nikitaja kwa uchache. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hali hiyo inayotokana na madhara makubwa ambayo ni mojawapo ya majanga yanayoweza kutokea wakati wowote katika jamii, naiomba Serikali izingatie mambo yafuatayo:-

(a) Kwa kuwa wajibu namba moja wa Serikali ni kulinda uhai wa raia wake, Serikali ijitahidi kulinda uhai huo hasa huduma muhimu za kukuza utu wao mfano huduma ya chakula, majisafi na salama, afya, makazi yaliyo mazuri na huduma nyinginezmo muhimu zinazokuza utu wa binadamu;

(b) Serikali iboreshe miundombinu ya shule za msingi na sekondari;

(c) Serikali irudishe miundombinu ya mawasiliano hususan barabara ziweze kuitika muda wote; na

(d) Serikali ianzishe Wakala wa Usimamizi wa Majanga mara moja kama inavyotakiwa na kwa mujibu wa Sheria ya Wakala wa Usimamizi wa Maafa Namba 7 ya Mwaka 2015 (*The Disaster Management Act, 2015*) iliyosainiwa na Rais Jakaya Mrisho Kikwete tarehe 11 Mei, 2015 siku ya Jumatatu ili ifanye jukumu lake la kuwakinga, kuwalinda na kuwaokoa raia wake dhidi ya majanga ya aina mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya, napenda tena kukushukuru kwa kunipa nafasi hii, naiomba Serikali ifanyie kazi haya niliyoyaeleza kwa kuwa hili tatizo la majanga lipo nchi nzima na hasa Jimbo la Vunjo, Halmashauri ya Wilaya ya Moshi na Taifa lote kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.
(*Makofî*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa James Mbatia kwa Maelezo yako hayo Binafsi. Serikali imeyasikia na naamini itayafanya kazi kama iwezekanavyo kwa wakati muafaka.

Waheshimiwa Wabunge, shughuli zetu za leo zimeisha lakini naomba Makatibu wale wa Vyama, kwa wale ambao hawakuweza kupata nafasi leo na walikuwa kwenye orodha waweze kurudisha majina yao kesho ili waweze kupata nafasi hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijaahirisha shughuli za Bunge, nina tangazo moja hapa, nawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote Wanawake na Wanaume kuwa siku ya Jumatatu tarehe 28 Mei, 2018, saa 7.00 mchana, mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge, kipindi cha asubuhi kutakuwa na mazoezi ya miondoko ya wanamitindo (*cat walk*) kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliojisajili katika fomu maalum iliyopo katika meza ya mapokezi lango kuu la kuingia Bungeni. Mazoezi hayo yataendeshwa na Mwanamitindo Bibi Khadija Mwanamboka, Waheshimiwa

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Wabunge mnaombwa kuendelea kujiorodhesha kwa ajili ya tukio hilo. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nitumie fursa hii kuwatakiwa heri wote ambao mmechangia leo, baada ya hapo naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 12.00 Jioni Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa,
Tarehe 25 Mei, 2018, Saa Tatu Asubuhi)*